# Majibu Yatolewayo Na Islam Juu Ya Matatizo Ya Zama Hizi

Na

Hadhrat Mirza Tahir Ahmad
Khalifa Mtukufu wa Nne[rh]

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LTD

**Majibu Yatolewayo Na Islam**

**Juu Ya Matatizo Ya Zama Hizi**

Tafsiri ya Kiswahili ya:
***Islam's Response to Contemporary Issues*** (Kiengereza)

Mwandishi:
Hadhrat Mirza Tahir Ahmad Khalifa Mtukufu wa Nne[rh]

Wafasiri:

1. Bw. Mussa A. Mpinga
2. Bw. Amiri A. Kaluta
3. Sheikh Shahab Ahmad
4. Bw. Seif Hassan Nakuchima
5. Bw. Mahmood Hamsin Mubiru
6. Dkt. Saleh Kitabu Pazi

Chapa ya Kwanza (Kiengereza): 1992
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2020

© Islam International Publications Ltd.

Kwa Maelezo Zaidi:
Tanzania:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

Kenya:
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

ISBN: 978-1-84880-542-2
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# FAHARISI


**MAELEZO YA MWENEZI** .................................................. i
**UTANGULIZI** .................................................. I
Ukosefu wa Amani .................................................. I
Mchango wa Islam kwa Amani ya Dunia .................... II
**SURA YA KWANZA** .................................................. 3
**AMANI BAINA YA DINI MBALIMBALI** ...................... 3
Desturi Njema za Kidini Zimepoteza Thamani ............ 3
Unabii ni kwa Walimwengu Wote ................................ 6
Manabii Wote ni Sawa .................................................. 7
Je Kwaweza Kuwapo Tofauti ya Cheo ikiwa Usahihi ni Sawa? .................................................. 9
Wokovu Hauwezi Kubinafsishwa na Dini Moja Yoyote Iwayo .................................................. 18
Uhamasishaji wa Maelewano na Kuheshi-miana Baina ya Dini Mbalimbali .................................................. 23
Dhana ya Dini kuwa Jambo la Ulimwengu Wote ....... 24
Islam ni Dini ya Dunia Nzima .................................... 27
Nyenzo za Jitihada — Hakuna Karaha ........................ 33
Uzima wa Kinachojimudu Zaidi .................................. 36
Uhuru wa Kuongea .................................................. 38
Uhuru na Ukombozi Katika Muktadha wa Dunia ya Leo .................................................. 39
Kejeli .................................................. 40
Ushirikiano Baina ya Dini Mbalimbali ........................ 48
Hitimisho .................................................. 50
Marejeo .................................................. 57

**SURA YA PILI** ........ **61**
**AMANI YA KIJAMII** ........ **61**
Utangamano wa Jamii ya Kisasa ........ 61
Hali Mbili za Utaratibu wa Kijamii ........ 67
Upuuzi wa Jamii Yenye Kupenda Mali na Mwisho Wake ........ 68
Kukataliwa kwa Maisha Yajayo ........ 70
Sifa Nne Bainifu za Jamii Yakinifu ........ 75
Uwajibikaji ........ 77
Hali ya Mazingira ya Jamii ya Kiislamu ........ 93
Misingi ya Jamii ya Kiislamu ........ 98
Usafikhulka ........ 100
Kutenganisha Jinsia ........ 105
Mapambazuko ya Zama Mpya kuhusu Haki za Wanawake ........ 107
Haki Sawa kwa Wanawake ........ 112
Mitala ........ 113
Kuwatunza Wazee ........ 125
Kizazi Kijacho ........ 130
Mambo ya Ufujaji na ya Kipuuzi Yamekatazwa ........ 134
Udhibiti Tamaa ........ 136
Kujenga Uaminifu na Kutokiuka Amana na Mikataba ........ 138
Kuondoa Maovu — Jukumu la Wote ........ 138
Mahimizo na Makatazo ........ 142
Mahimizo ........ 143
Makatazo ........ 144
Kupinga Ubaguzi wa Kimbari ........ 145
Marejeo ........ 163

**SURA YA TATU ..................................................... 167**
**AMANI YA KIJAMII NA KIUCHUMI ..................... 167**
Uadilifu wa Kiuchumi katika Ubepari, Ujamaa na Uislamu ............................................................ 167
Kutoa katika njia nzuri hata kwa dhiki ..................... 171
Kutoa katika kuwasaidia maskini ............................ 171
Shukurani ................................................................. 172
Fadhila Hazizawadiwi na Binadamu ......................... 176
Kuombaomba ............................................................ 178
Nini kinachotakiwa kutolewa kama sadaka? ............ 181
Kutoa kwa Dhahiri na kwa Siri ................................. 181
Wajibu wa Kijamii ..................................................... 182
Mfano katika historia ya mwanzo ya Islam .............. 183
Mipaka mipana ya utoaji .......................................... 185
Kuwatumikia Wengine .............................................. 186
Uharamu wa kunywa pombe na kucheza kamari .... 187
Marejeo ..................................................................... 197
**SURA YA NNE .......................................................... 201**
**AMANI YA KIUCHUMI ............................................ 201**
Falsafa za Uchumi wa Kibepari, Kijamaa na Kiislam ......................................................................... 201
Ubepari ..................................................................... 201
Ujamaa ..................................................................... 202
Dhana ya Kiislamu .................................................... 204
Sifa Nne za Jamii ya Kibepari .................................... 205
Hatima ya Ubepari ni Maangamio ............................ 206
Mpangilio wa Kiuchumi wenye Mabadiliko ............ 206
Mfumo wa Kiuchumi wa Kiislamu ........................... 211
Zaka .......................................................................... 213
Makatazo Ya Riba ..................................................... 217

Viwango vya juu vya Riba nchini Uingereza ............ 218
Madhara Mengine ya Riba .......................................... 224
Riba Inavyohatarisha Amani ....................................... 232
Makatazo ya Kujilimbikizia Mali ................................ 234
Kuishi Maisha Rahisi na ya Kawaida .......................... 237
Matumizi Kwenye Sherehe ya Ndoa .......................... 237
Ulaji Chakula kwa Kiasi ............................................. 240
Ukopaji wa Fedha ....................................................... 240
Tofauti za Matabaka ya Kiuchumi ............................. 245
Sheria ya Mirathi ya Kiislam ...................................... 246
Makatazo ya Hongo .................................................... 247
Maadili ya Kibiashara ................................................. 248
Mahitaji ya Msingi ..................................................... 251
Ibada Kama Njia ya Umoja wa Kiuchumi .................. 256
Majukumu ya Kimataifa ............................................ 258
Marejeo ...................................................................... 266
**SURA YA TANO ........................................................ 269**
**AMANI YA KISIASA ................................................. 269**
Amani ya Kisiasa Inabidi Ichunguzwe Katika Kiwango cha Taifa na Kimataifa ............................................... 269
Hakuna kukataa moja kwa moja kwa mfumo wowote wa kisiasa ............................................................... 270
Kuainisha Dhana ya Demokrasia ............................... 274
Islam Inavyoainisha Demokrasia ............................... 277
Nguzo mbili za Demokrasia sawa na Islam ............... 278
Kushauriana Kunapewa Kipaumbele ......................... 278
Mkanganyiko kuhusu Mfumo halisi wa Serikali ya Kiislam ....................................................................... 282
Mamlaka ya Kimbingu ............................................... 282
Umullah ...................................................................... 283

Utii Uliogawanyika Baina ya Dola na Dini ................ 287
Je, Dini ndio iwe na Haki Pekee ya Utengenezaji wa Sheria? ................ 289
Ujuzi wa Kuongoza Serikali Katika Islam ................ 294
Mahusiano ya Kimataifa – Kanuni ya Uadilifu Inawahusu Wote Kwa Usawa. ................ 299
Wajibu wa Umoja wa Mataifa ................ 300
Marejeo ................ 308
**SURA YA SITA ................ 311**
**AMANI YA NAFSI ................ 311**
Mtu kuwa na Amani na Nafsi yake Mwenyewe ................ 311
Kushindana katika Matendo Mema ................ 311
Upendo kwa Jamaa na Ndugu ................ 315
Kuwatumikia Wengine ................ 315
Kutafuta Radhi ya Mungu ................ 318
Kuwajali Daima Binadamu Wengine ................ 320
Mawanda Mapana ya Upendo ................ 320
Dhamira ya Uumbaji wa Binadamu ................ 321
Hakuna Amani bila Mungu ................ 326
Marejeo ................ 329

# MAELEZO YA MWENEZI

Mkononi mwenu mna tafsiri ya Kiswahili ya hotuba aliyowahi kutoa Hadhrat Mirza Tahir Ahmad mnamo 24 Februari 1990 huko Queen Elizabeth II Conference Centre mjini London. Hadhrat Mirza Tahir Ahmad[rh] baadaye mnamo mwaka 1982 akachaguliwa kuwa Khalifa wa Nne wa Masihi Mau'udi[as].

Hotuba hii ilisikilizwa kwa makini sana na wageni mia nane mashuhuri, kati yao walikuwapo wanasiasa, wataalamu wa lugha ya Kiarabu, waandishi wa habari, maprofesa, walimu, wanaume kwa wanawake waliobobea katika utaalamu wa aina mbalimbali. Mwenyekiti wa kikao hiki alikuwa mheshimiwa Edward Mortimer. Amiri wa Jumuiya Ahmadiyya ya UK, mheshimiwa Aftab Ahmad Khan aliwakaribisha wageni. Baada ya hotuba, kulikuwa na kikao kifupi cha maulizo na majibu. Hotuba yenyewe ilikuwa kwa lugha ya Kiingereza.

Baadaye hotuba hii ya kusisimua, ilitolewa kwa sura ya kitabu kiitwacho Isam's Responce to Contemporary Issues. Na sasa inatolewa tafsiri yake kwa Kiswahili iliyofanywa na jopo la wasomi sita ambao kati yao watano ni Watanzania kindakindaki. Wote hao walijibidiisha kweli kweli kutekeleza jukumu lao. Majina yao ndiyo yafuatayo:

1. Bw. Mussa A. Mpinga
2. Bw. Amiri A. Kaluta
3. Sheikh Shahab Ahmad
4. Bw. Seif Hassan Nakuchima
5. Bw. Mahmood Hamsin Mubiru
6. Dkt. Saleh Kitabu Pazi

Kabla ya kupelekwa mtamboni, niliidurusu kwa uangalifu. Sheikh Ansar Hussain akasaidia hasa katika kazi ya fometi.

Mwenyezi Mungu Awapatie wote hao malipo bora sana hapa na kule Akhera.

Mola wetu akifanye kitabu hiki kiwe chenye manufaa ya kielimu na kiroho. Amin.

Jamil R. Rafiq

Wakilut Tasnif, Tahrike Jadid

Rabwah, Pakistan 1 Desemba 2019

# UTANGULIZI

Baada ya kutoa shahada mbili na kusoma Sura Al-Fatiha (Sura ya kwanza ya Kurani Tukufu) sawa na desturi, Kiongozi Mkuu wa Jumuiyya ya Waislamu Waahmadiyya alianza kusema kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Bwana Edward Mortimer (Mwenyekiti), wageni waalikwa, mabibi na mabwana!

Nawashukuruni nyote wasomi kwamba mmehudhuria alasiri ya leo. Mada ya hotuba yangu ya leo ni changamoto kwangu. Mada hii ni pana sana, nahofia kwamba nisiweze kutoa haki yake katika muda huu mfupi.

Kwa vyovyote naanza kwa kutaja maswali mawili ya msingi: Zipo changamoto gani za zama hizi? Dini yoyote yawezaje kuishughulikia hali hii ya kisasa?

## Ukosefu wa Amani

Ndwele ya pekee ya muhimu sana kabisa ya zama hizi ni ukosefu wa amani. Katika ulimwengu wa kisasa, binadamu kwa ujumla ameishafika kiwango cha juu sana cha mafanikio katika maendeleo ya mambo ya kidunia, yaliyowezekana kwa sababu ya sayansi na teknolojia kupiga hatua kubwa mbele katika kila uwanja wa mahitaji ya mtu kwa mwendo wa kushangaza.

Hakuna shaka kuwa sehemu ya jamii ya binadamu iliyo na bahti njema ijulikanayo kwa Ulimwengu wa Kwanza na Ulimwengu wa Pili, imepata sehemu kubwa zaidi ya matunda ya maendeleo ya kisayansi katika zama hizi,

lakini Ulimwngu wa Tatu nao pia umenufaika kiasi fulani. Miali ya maendeleo imepenya hata ndani sana mafichoni kwenye maeneo ya kiza totoro ambako jamii ya watu bado inaishi katika zamani za kale.

Hata hivyo, mtu hana furaha wala utulivu. Unaendelea kuzidi utukutu, hofu, wasiwasi, kukosa itibari kuhusu mustakbali na kutoridhika na aliyorithi. Haya ni baadhi ya mambo ya msingi yaliyo changamoto kwa hali ya ulimwengu wa sasa. Hiyo kwa upande wake inazalisha kutoridhika kabisa kwa mtu kuhusu maisha ya nyuma au ya hivi sasa; hususan inaathiri mno katika mchakato wa kujenga fikira ya kizazi kipya. Mwanadamu yumo katika kuisaka amani.

## Mchango wa Islam kwa Amani ya Dunia

Tafsiri sisisi ya Islam ni amani. Katika neno hili moja tu mafundisho yote ya Islam yanaakisiwa vizuri sana na kwa muhtasari. Islam ndiyo dini ya amani. Mafundisho yake yanatoa dhamana ya amani katika duara zote za shauku na matamanio ya kibinadamu.

Kwa hotuba ya leo, nimechagua baadhi ya maeneo yanayohitajika sana kuyaelezea kuongoza ulimwengu wa sasa:

1. Amani na maelewano baina ya dini.
2. Amai ya jamii kwa jumla.
3. Amani ya kijamii na kiuchumi.
4. Amani ya kiuchumi.
5. Amani ya kisiasa ya taifa na baina ya mataifa.
6. Amani ya kila mtu.

Bila shaka Sisi Tumekutuma kwa haki ili ubashiri na kuonya, na hakuna taifa lolote ila alipita humo Mwonyaji.

- Kurani Tukufu, 13:29

Hakika wale walioamini na Mayahudi na Masabii na Wakristo - atakayemwamini Allah na siku ya Mwisho na kufanya vitendo vizuri - basi hao hawatakuwa na hofu wala hawatahuzunika.

- Kurani Tukufu, 5:70

# SURA YA KWANZA

# AMANI BAINA YA DINI MBALIMBALI

## Desturi Njema za Kidini Zimepoteza Thamani

Mtu aangaliapo taswira nzima ya hali ya dini, hawezi kushindwa kubaini kwamba inaelekea kuna hali isiyoyumkinika inayoshamiri katika dini hivi leo. Kwa ujumla, Dini inapoteza hatamu yake na bado kwa wakati huo huo ikiikaza hatamu katika maeneo tofauti. Katika baadhi ya makundi ya jamii, takriban kwenye dini zote, inaelekea kuna mrejeo wa nguvu kwenye mwelekeo wa mawazo mgando unaofanywa kwa ubishi wa kikale na kutovumilia hoja mbadala.

Kwa upande wa maadili, dini imeufyata mkia; uhalifu umeenea; ukweli unapotea haraka; usawa na utoaji wa haki vyakaribia kutoweka; uwajibikaji katika kusimamia ustawi wa jamii unapuuzwa; badala ya yote hayo ubinafsi wa mtu mmoja mmoja unapata nguvu hata katika nchi zile duniani ambazo zingependa kudai kuwa ni za kidini. Haya na maovu mengine katika jamii, ambayo ni alama za wazi za jamii inayoporomoka kimaadili, yamekuwa ndio hali ya kawaida. Ikiwa desturi njema za kimaadili katika dini yoyote ndio uhai na roho ya dini yenyewe, basi kuendelea kuzinyonga desturi hizi kwaweza kutuelekeza kwenye hitimisho lisilokwepeka kwamba wakati mwili wa dini unaendelea kuhuishwa, roho inaondoka haraka kwenye mwili.

Hivyo tunachokiona kwenye dini leo, kile kinachoitwa kuhuishwa kwa dini inakuwa sawa na kuamsha miili iliyokufa itembee kama mazezeta.

Katika maeneo mengine kusimama kwa muda mrefu na kukosekana shughuli mpya zenye kuleta hamasa kunapelekea kupoa kwa hamu miongoni mwa watu wenye fikra za kidini. Matukio ya kimiujiza, ambayo wanayatazamia kutokea, hayatokei. Matukio ya kimaajabu ya kuingilia kati kusiko kwa kawaida kwenye masuala ya ulimwengu ili kubadilisha ulimwengu sawa na matakwa yao hayatokei. Wanataka kuona tabiri za kinabii za ajabu zikitendeka kuzipa hadhi imani zao. Lakini wapi, hakuna kinachotokea. Hao ndio wale watu ambao huwa ni chanzo cha kuzuka kwa madhehebu mapya ambayo hustawi kwa mbolea ya kukata kwao tamaa. Haja ya kuachana na yaliyopita inazaa jazba ya kuziba ombwe linalojitokeza kwa kitu kipya.

Mbali na mienendo hii haribifu, jambo jingine linalosumbua sana akili, ambalo, labda, linahusikana na kuzuka upya kwa imani kali katika dini, linatishia amani ya dunia. Kutokana na kuzuka kwa itikadi hizo kali mazingira yenye sumu huzalika ambayo matokeo yake ni kuua moyo mwema wa majadiliano na mabadilishano huria ya mawazo. Kama vile haya hayatoshi, jitihada makusudi za wanasiasa wasio wanyofu ambao daima wako tayari kujinufaisha na hali tete, zinafanyika kupaka matope muonekano wa dini yenyewe. Vile vile

upinzani na ugomvi wa kihistoria baina ya dini mbali mbali unayo nafasi yake ya kuhusika.

Juu ya hayo kile kinachoitwa 'vyombo huru vya habari' vinatawaliwa na mikono isiyoonekana badala ya kuwa huru kushika nafasi isiyofungamana kabisa na upande wowote katika masuala ya ulimwengu.

Kwa hiyo pale vyombo vya habari vya nchi ambayo watu wake walio wengi ni wa dini fulani vinajiunga katika vita ya kudhalilisha muonekano wa dini pinzani, mandhari inayojitokeza inakuwa tatanishi sana. Mhanga wa kwanza wa kivumbi hiki, bila shaka ni dini yenyewe.

Kwa kweli nahuzunishwa sana na kufadhaishwa na kile kinachotokea katika ulimwengu wa Dini leo hii. Kuna haja ya haraka sana kwa Dini mbalimbali kufanya juhudi ya kweli na ya dhati ya kuondoa tofauti baina yao. Ninaamini kwamba Islam inaweza kuleta matokeo hayo kwa ubora wa hali ya juu kwa namna ambayo itatosheleza kikamilifu mahitaji na haja zetu.

Ili kufanikisha uelewa bora, nimeligawa tena somo hili kwenye mafungu tofauti.

Kwa mfano, naamini kwamba ili dini iweze kusaidia katika kuleta amani duniani, ni muhimu kwamba dini ambayo kimsingi ina uwezo wa kuwaunganisha watu ulimwenguni kote, ni lazima yenyewe ikubali dhana ya upana wa dini kwa maana ya kwamba wanadamu wa rangi yoyote, kabila lolote na mahala popote wote ni

viumbe wa Muumbaji yule yule. Kwa hivyo, watu wanastahiki sawa katika kupata mafundisho kutoka kwa Mungu — ikiwa imewahi kutokea mafunzo kutoka kwa Mungu wakapatiwa kundi lolote la jamii ya wanadamu. Wazo hili linakinzana na dhana ya kwamba kuna dini fulani moja tu iliyo ya kweli minghairi ya zingine zote.

Dini zile, bila kujali majina yao au imani, popote zinapopatikana na ziwe za zama zozote, zinayo haki ya kudai kuwa zinao ukweli kiasi fulani wa ki-Ungu. Kadhalika, mtu inabidi akubali kwamba, pamoja na tofauti zilizopo katika imani na mafundisho ya dini mbali mbali, dini zimeelekea kwamba zina chanzo kimoja. Adhama ile ile ya Ki-Ungu, ambayo ilileteza kuzaliwa kwa dini yoyote katika sehemu moja ya dunia, lazima vile vile iliangalia mahitaji ya kidini na kiroho ya wanadamu wengine katika sehemu nyinginezo za ulimwengu na katika zama tofauti.

Huu hasa ndio ujumbe wa Kurani Tukufu, kitabu kitakatifu cha Islam.

## Unabii ni kwa Walimwengu Wote

Kurani Tukufu inayo yafuatayo ya kusema juu ya jambo hili:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِيْ كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُوْلًا أَنِ اعْبُدُوا اللّٰهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوْتَ ۚ

*Na bila shaka Tulimwinua Mtume katika kila umati ya kwamba Mwabuduni Allah na mwepukeni Mwovu.*[1]

Pili, Kurani Tukufu inanadi kwamba: Ewe Nabii wa Mungu, wewe sio nabii pekee duniani:

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا مِّن قَبْلِكَ مِنْهُم مَّن قَصَصْنَا عَلَيْكَ وَمِنْهُم مَّن لَّمْ نَقْصُصْ عَلَيْكَ

*Na kwa yakini Tuliwatuma Mitume kabla yako, wengine wao Tumekusimulia na wengine wao Hatukukusimulia.*[2]

Kurani Tukufu inamkumbusha Mtume wa Islam

إِنْ أَنتَ إِلَّا نَذِيرٌ ﴿٢٣﴾ إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ بِالْحَقِّ بَشِيرًا وَنَذِيرًا وَإِن مِّنْ أُمَّةٍ إِلَّا خَلَا فِيهَا نَذِيرٌ ﴿٢٥﴾

*Wewe siye ila ni Mwonyaji tu. Bila shaka Sisi Tumekutuma kwa haki ili ubashiri na kuonya, na hakuna taifa lolote ila alipita humo Mwonyaji.*[3]

Kwa kuangalia hayo hapo juu, ni dhahiri shahiri kwamba Islam haijibinafsishii ukweli na kuziondoa katika ukweli dini nyingine zote, bali inanadi wazi wazi kwamba katika zama zote na katika sehemu zote za dunia Mungu Amekuwa akiangalia mahitaji ya kiroho na ya kidini ya wanadamu kwa kuwatuma Mitume ambao walifikisha ujumbe wa Mungu kwa watu waliotumwa kwao na kupewa mamlaka juu yao.

## Manabii Wote ni Sawa

Swali linazuka ya kwamba ikiwa kuna Manabii wengi wa Mungu waliotumwa kwa watu wote duniani, katika sehemu mbalimbali za dunia na katika zama mbali mbali, je wote wanayo mamlaka sawa kutoka kwa Mungu? Kwa mujibu wa Kurani Tukufu, Manabii wote ni wa Mungu, na kwa hiyo kadri mamlaka waliyopewa

na Mungu yanavyohusika, wanatekeleza dhima zao kwa nguvu na juhudi sawa. Hakuna mtu aliye na haki ya kubagua baina ya Nabii mmoja na mwingine. Kwa kadri usahihi wa ujumbe wao unavyohusika, Manabii wote ni lazima wawe sawa. Mtazamo huu wa Islam juu ya dini zingine na Waanzilishi wake pamoja na Manabii wafuasi, waweza kuwa njia muhimu kabisa ya kuziunganisha na kuzipatanisha dini mbali mbali. Msingi kwamba usahihi wa ufunuo wa kila Nabii unafaidi hadhi sawa unaweza kutumika kama kani unganishi yenye nguvu sana, ya kuzileta pamoja dini mbali mbali. Hii inapindua mtazamo wa kuzichukia funuo za Manabii wa dini zingine kuwa ule wa heshima na nyenyekeo. Huu hapa tena ndio msimamo wa dhahiri na busara uliochukuliwa na Kurani Tukufu.

اٰمَنَ الرَّسُوْلُ بِمَآ اُنْزِلَ اِلَيْهِ مِنْ رَّبِّهٖ وَ الْمُؤْمِنُوْنَ ؕ كُلٌّ اٰمَنَ بِاللّٰهِ وَ مَلٰٓئِكَتِهٖ وَ كُتُبِهٖ وَ
رُسُلِهٖ ۫ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ اَحَدٍ مِّنْ رُّسُلِهٖ ۫ وَ قَالُوْا سَمِعْنَا وَ اَطَعْنَا

*Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola wake, na waaminio (pia): wote wamemwamini Allah, na Malaika Wake, na Vitabu Vyake, na Mitume Wake; (nao husema), hatutofautishi baina ya mmoja wa Mitume Wake; na husema, Tumesikia na tumetii.*[4]

Somo hili limerudiwa katika aya zingine za Kurani Tukufu. Kwa mfano:

اِنَّ الَّذِيْنَ يَكْفُرُوْنَ بِاللّٰهِ وَ رُسُلِهٖ وَ يُرِيْدُوْنَ اَنْ يُّفَرِّقُوْا بَيْنَ اللّٰهِ وَ رُسُلِهٖ وَ يَقُوْلُوْنَ نُؤْمِنُ
بِبَعْضٍ وَّ نَكْفُرُ بِبَعْضٍ ۙ وَّ يُرِيْدُوْنَ اَنْ يَّتَّخِذُوْا بَيْنَ ذٰلِكَ سَبِيْلًا ﴿١٥٠﴾ اُولٰٓئِكَ هُمُ الْكٰفِرُوْنَ حَقًّا ۚ وَ

أَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُّهِينًا ﴿١٥١﴾ وَالَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ وَلَمْ يُفَرِّقُوا بَيْنَ أَحَدٍ مِّنْهُمْ
أُولَٰئِكَ سَوْفَ يُؤْتِيهِمْ أُجُورَهُمْ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿١٥٢﴾

*Hakika wale wanaomkataa Allah na Mitume Wake, na wanataka kutenga baina ya Allah na Mitume Wake, na husema: Wengine tunawaamini na wengine tunawakataa, na wanataka kushika njia iliyo kati ya haya. Hao ndio makafiri kweli, na Tumewaandalia makafiri adhabu ifedheheshayo. Na waliomwamini Allah na Mitume Wake, wala hawakumfarikisha mmojawapo kati yao, hao ndio karibuni Atawapa ujira wao. Na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.*[5]

## Je Kwaweza Kuwapo Tofauti ya Cheo ikiwa Usahihi ni Sawa?

Ikiwa Manabii wote ni sawa katika usahihi wao, je ni lazima wawe pia sawa katika vyeo? Jibu kwa swali hili ni kwamba katika jiha nyingi, Manabii waweza kutofautiana katika sifa binafsi na namna wanavyotekeleza wajibu wao. Kadiri unavyohusika ukaribu wao na Mungu na hadhi aliyonayo kila mmoja mbele ya Mungu, Mitume na Manabii waweza kutofautiana wao kwa wao. Uchunguzi wa Historia ya Manabii kutoka kwenye maelezo ya Biblia takatifu, Kurani Tukufu na vitabu vingine unakubaliana pia na hoja hii.

Kurani Tukufu inakiri kwamba zipo tofauti za hadhi kwa namna ambayo haipaswi kuhangaisha amani ya

watu. Kurani Tukufu ile ile ambayo inatangaza kwamba hakuna tofauti kwa kadri ya usahihi wa Jumbe kutoka kwa Mungu zinavyohusika baina ya Nabii mmoja na mwingine, inatangaza:

تِلْكَ الرُّسُلُ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلٰى بَعْضٍ ۘ مِنْهُمْ مَّنْ كَلَّمَ اللّٰهُ وَ رَفَعَ بَعْضَهُمْ دَرَجٰتٍ ؕ

*Hao Mitume Tumewafadhili baadhi yao zaidi kuliko wengine; miongoni mwao wako ambao Allah alisema nao, na wengine wao akawapandisha daraja.*[6]

Baada ya kukubalii hoja hii, mtu aweza kujiuliza, ni yupi anastahili kujulikana kuwa ni mbora kwa daraja baina ya manabii. Hili ni swala nyeti, lakini bado mtu hawezi kulifumbia macho kutokana na umuhimu wake.

Waumini wa dini karibu zote duniani hudai kwamba mwanzilishi wa dini yao ndiye kinara wa wote na hakuna mwingine awezaye kuwa sawa naye katika utukufu, heshima, uchamungu, adhama na kwa kifupi sifa zote zihusikanazo na Unabii. Baada ya hayo, je Islam nayo inadai kwamba Muhammad[saw], Mtume mtukufu wa Islam, ndiye mbora kabisa wa Mitume wote? Ndio, Islam hufanya madai hayo bila kumung'unya maneno juu ya utukufu mkamilifu na ubora wa sifa wa Mtume mtukufu[saw] juu ya manabii wengine wote wa ulimwengu. Lakini bado, kuna tofauti ya wazi kati ya Islam na dini nyingine katika mtazamo wao juu ya dai hili.

Kwanza kabisa, yapasa itiliwe maanani kwamba hakuna dini minghairi ya Islam inayotambua kuwa unabii ni kwa walimwengu wote. Wayahudi wanapodai, kama wanafanya hivyo, kuwa Musa[as] alikuwa ndiye nabii mkubwa kuliko wote, hawamlinganishi Musa[as] na Buddha[as], Krishna[as],Yesu[as] au Muhammad[saw] kwa kuwa wanayakataa madai ya waanzilishi watukufu wengine wote wa dini zilizotajwa hapo juu kuwa ni ya kweli na yanayostahili kukubaliwa. Kwa hivyo, katika orodha ya Kiyahudi ya Manabii, hakuna manabii wengine wanaotajwa isipokuwa wale waliomo katika Agano la Kale; hata uwezekano wa kuwapo Manabii mahali pengine duniani unakataliwa mbali. Kwa kutumia uono huu, madai yao kuhusiana na ubora wa Nabii yeyote wa Kiyahudi hayawiani na madai kama hayo yafanywayo na Islam; kwa vile sawa na dini ya Kiyahudi, Manabii wasiokuwamo ndani ya Biblia ni yumkini hawapo. Sawa kabisa na msingi huu ndio msingi wa madai kama hayo ya Wabuddha, Wazoroarista, Wahindu na kadhalika.

Zaidi ya hayo ipo pia tofauti nyingine ya kuzingatiwa. Tunapowazungumzia manabii tunafahamu kwamba wao hawawatambui kwa kawaida watakatifu wa dini zao kama Manabii. Dhana ya manabii na mitume kama inavyoeleweka katika Uyahudi, Ukristo na Uislamu haichukuliwi namna hiyo hiyo na dini nyingine nyingi. Badala yake, wanawachukulia waanzilishi wa dini zao na watu watakatifu kuwa watu watakatifu, au madhihirisho ya Mungu, au Mungu Mwenyewe, au kitu

karibu na hicho. Labda kwa hali hii, Yesu Kristo[as] pia apaswa kutambulika kuwa ni tofauti kwa mtazamo wa Ukristo.

Lakini kwa mujibu wa Islam, wote hawa wanaodaiwa kuwa miungu au miungu katika miili ya binadamu au wadaiwao wana wa Mungu au watoto wa Mungu ni Manabii tu na mitume ambao walitwikwa uungu na wafuasi wao baadae sana. Kwa hakika ili kuainisha zaidi jambo hili, kwa mujibu wa Islam, kutwikwa uungu kwa watu watakatifu katika dini mbali mbali ni jambo lililotokea pole pole na sio la kizazi kilichokuwepo wakati wa uhai wa Nabii[as]. Lakini kuhusiana na jambo hili, tutaongea baadae.

Kwa vyovyote, pale Islam inapodai kwamba mwanzilishi wake mtukufu ni mbora wa manabii, inawahusisha watu watakatifu wa dini zote duniani katika maana inayoeleweka sawa na dhana ya Kiyahudi na Islam kuhusu Manabii. Yafaa kurudia hapa kwamba Islam inawatambua waanzilishi watakatifu wa dini zote zilizofunuliwa kuwa ni wanandamu tu ambao waliinuliwa na Mungu kuwa na hadhi ya manabii. Hakuna utofauti katika jambo hili la ulimwengu wote. Kwa mfano Kurani Tukufu inatangaza:

فَكَيْفَ إِذَا جِئْنَا مِن كُلِّ أُمَّةٍ بِشَهِيدٍ وَجِئْنَا بِكَ عَلَىٰ هَٰؤُلَاءِ شَهِيدًا ﴿٤٢﴾

*Basi itakuwaje tutakapoleta shahidi katika kila umati, na Tukakuleta wewe uwe shahidi juu ya hawa?*[7]

Baada ya kufanya upambanuzi huu wa msingi, sasa tunasonga mbele kuchunguza hadhi ya Mtume Mtukufu[saw] wa Islam, kwa mujibu wa Kurani Tukufu. Madai bayana zaidi na yasiyopingika kumhusu Mtume Mtukufu[saw] wa Islam yamefanywa katika aya maarufu na inayojadiliwa sana ya Kurani Tukufu.

مَا كَانَ مُحَمَّدٌ اَبَآ اَحَدٍ مِّنْ رِّجَالِكُمْ وَ لٰكِنْ رَّسُوْلَ اللّٰهِ وَ خَاتَمَ النَّبِيّٖنَ ؕ وَ كَانَ اللّٰهُ
بِكُلِّ شَیْءٍ عَلِیْمًا ﴿٤١﴾ ع

*Muhammad si baba ya ye yote katika wanaume wenu, bali yeye ni Mtume wa Mungu na Muhuri wa Manabii. Na Allah ndiye Ajuaye kila kitu.*[8]

Neno la Kirabu *Khatam* katika aya hii lina maana nyingi lakini tafsiri halisi ya cheo *Khaatamun Nabiyyiin* bila shaka yoyote iwayo, ni kuwa mbora kabisa, mkuu wa wote, neno la Mwisho, mamlaka ya mwisho, yule anayewazunguka wote na atoae ushahidi juu ya ukweli wa wengine.[9]

Aya nyingine inayozungumzia ubora wa mwanzilishi mtukufu wa Islam inasema kwamba mafundisho ya Mtume mtukufu[saw] wa Islam ni kamilifu na ya mwisho. Aya hii inakwenda ifuatavyo:

اَلْيَوْمَ اَكْمَلْتُ لَكُمْ دِيْنَكُمْ وَ اَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِيْ وَ رَضِيْتُ لَكُمُ الْاِسْلَامَ دِيْنًا

*Leo Nimewakamilishieni dini yenu, na kuwatimizieni neema Yangu, na Nimewapendeleeni Islamu iwe dini yenu.*[10]

Kusudio dhahiri la dai hili litakuwa kwamba kati ya manabii wote walioleta sheria duniani na katika kuipa dunia mafundisho yaliyokamilika kabisa, yeye (s.a.w) anashika nafasi ya juu kabisa miongoni mwao.

Kuendeleza somo hili mbele Mtume Mtukufu[saw] anahakikishiwa kwa kauli thabiti kwamba kitabu kilichofunuliwa kwake kitalindwa na kuhifadhiwa yasiingizwe ndani yake maneno ya watu. Kwa jinsi hii, sio tu mafundisho yanaelezwa kuwa ni makamilifu, lakini pia, yanatangazwa kuwa ni ya kudumu milele — yatahifadhiwa katika hali yake ya uhalisi bila kuingizwa ndani yake maneno ya watu na kubakia katika maneno yale yale yaliyofunuliwa kwa mwanzilishi mtukufu[saw] wa Islam.

Historia ya karne kumi na nne zilizopita imebeba ushahidi mwingi juu ya ukweli wa dai hili.

Zifuatazo ni baadhi ya aya zenye ujumbe huu:

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿١٠﴾

*Hakika Sisi Tumeteremsha mawaidha na hakika Sisi ndio Tuyalindao.*[11]

بَلْ هُوَ قُرْآنٌ مَّجِيدٌ ﴿٢٢﴾ فِي لَوْحٍ مَّحْفُوظٍ ﴿٢٣﴾

*Bali hii ni Kurani Tukufu, katika ubao uliohifadhiwa.*[12]

Kwa kuzingatia hayo hapo juu, mwanzilishi mtukufu wa Islam[saw] ni dhahiri sio tu anadaiwa kuwa mbora bali pia

mtume wa mwisho wa kuleta sheria ambaye mamlaka yake yataendelea mpaka wakati wa mwisho.

Baada ya kusema hayo, mtu anaanza kuwaza kwamba katika macho ya baadhi, haya madai juu ya ubora wa mwanzilishi mtukufu wa Islam[saw] yaweza kumaanisha kuanzisha chuki na mtafaruku na wafuasi wa dini zingine. Kwa hivyo, kwa vipi twaweza kupatanisha mada ya maelezo haya, isemayo ya kwamba Islam inatoa dhamana ya amani katika nyanja zote zinazogusa maisha ya watu, dini ikiwa sio ya mwisho kwa umuhimu katika nyanja hizo.

Nilikuwa na swali hili moyoni ndio maana nikalazimika kuielezea hoja hii kwa urefu kiasi. Swali hili laweza kujibiwa vya kutosha kwa mwenye moyo safi na atafutae ukweli kwa njia zaidi ya moja.

Kama ambavyo imeshaelezwa kabla, madai kama hayo yanafanywa pia na wafuasi wa dini zingine nyingi. Ni jambo la busara kwa mtu kuchunguza usahihi wa madai hayo bila kujazibika na madai yenyewe. Madai yenyewe kama yalivyo hayapaswi kuzikwaza hisia za wafuasi wa dini nyingine wanaofanya madai kama hayo.

Lakini Islam inakwenda mbali zaidi na kufundisha upole wa moyo na uungwana wa kimatendo kwa wafuasi wake hivi kwamba imani juu ya ubora wa Mwanzilishi mtukufu[saw] wa Islam haitamkwi bila staha, ikapelekea kuwakwaza wengine.

Hadithi mbili zifuataza za Mwanzilishi mtukufu[saw] wa Islam zinasimama kipekee kama nguzo kuthibitisha hoja ya nukta hii.

1) Mmoja wa Masahaba wa Mwanzilishi mtukufu[saw] wa Islam alikuwamo katika mjadala mkali sana na mfuasi mwenye msimamo mkali wa Nabii Yunus wa kisa cha samaki (Nyangumi). Pande zote katika mjadala zilidai Nabii wao amemzidi mwingine kwa ubora. Inaelekea mbishani wa Kiislam alileta madai yake kwa namna ambayo iliumiza hisia za mfuasi wa Yunus[as] ambaye alimwendea Mtume Mtukufu Muhammad[saw] na kufikisha malalamiko dhidi ya Mwislamu aliyekuwa akibishana naye. Akiuasa umma wote wa Kiislam, Mtume[saw] alisema maneno haya ya mwongozo:

لَا تُفَضِّلُوْنِيْ عَلٰى يُوْنُسَ بْنِ مَتّٰى

*Yaani msitangaze ubora wangu juu ya Nabii Yunus bin Matta.*[13]

Baadhi ya wanazuoni wa Hadithi wa Kiislam wanapigwa na butwaa na Hadithi hii kwa kuwa yaelekea kwenda kinyume na madai ya Kurani kwamba Muhammad[saw] ni mbora sio tu kwa Yunus[as] bali manabii wote[as]. Lakini inaonekana kuwa hawakuelewa kuwa alichokisema sio kwamba yeye ni wa chini mbele ya Yunus[as] (wala si mbora kwa Yunus[as]) bali hivi tu kwamba wafuasi wake hawapaswi kutangaza ubora wake kwa namna itakayopelekea kuzikwaza hisia za

wengine. Kwa muktadha wa yaliyokwisha semwa kabla maana pekee inayoweza kuchukuliwa hapa ni kwamba Mtume[saw] alikuwa akiwafundisha Waislamu somo katika adabu njema. Alikuwa akiwaongoza wasijiingize katika masemezano mabaya. Yawapasa wawe waangalifu kuepuka kujadili hadhi yake kwa namna ambayo yaweza kusababisha kwaziko. Mtazamo kama huo kwa hakika utakuwa unaharibu mwendeleo wa Islam kwa sababu badala ya kuzivutia nyoyo na fikra kwenye ujumbe wa Islam, matokeo ya kinyume chake kabisa yatapatikana.

2) Mtazamo huu wa Mtume Mtukufu[saw], unashadidishwa zaidi na Hadithi nyingine ambapo Mwislamu alikuwamo katika mjadala unaofanana na huo na Myahudi. Kila mmoja alidai ubora wa kiongozi wake wa kiroho. Tena alikuwa ni yule asiyekuwa Mwislam ndiye aliyeona inafaa kupeleka malalamiko juu ya mpinzani wake Mwislam. Mtume Mtukufu[saw], alijibu kwa upole wake wa kawaida na akamfundisha yule Mwislam somo lile lile katika adabu na wema kwa kusema:

لَا تُفَضِّلُوْنِيْ عَلٰى مُوْسٰى

*Yaani msieleze ubora wangu juu ya Musa[as].[14]*

Maana halisi ya habari hii ni kwamba ni juu ya Mungu kuamua na kutangaza daraja la kila mmoja wa Mitume[as] katika ukaribu nae. Inawezekana kabisa kwamba katika

zama fulani, kwa muktadha wa dini fulani, Mungu huenda akaeleza kuridhishwa kwake na Nabii wa zama kwa lugha sisitizi kiasi cha kutangaza kwamba Nabii huyo alikuwa ni mbora wa wote. Sifa kuu zaweza, pamoja na yote, kutumika pia kwa maana linganishi kwa muradi wa matumizi yaliyo ndani ya mipaka ya muda na mahala fulani.

Hilo laweza kirahisi kusababisha wafuasi wa mtu huyo mtakatifu kuamini kwamba alikuwa ni mbora na mtakatifu zaidi ya wote kwa zama zilizopita na nyakati zote zitakazokuja. Kuamini jambo hili kwa uaminifu hakupaswi kuchukuliwa kuwa ni uchokozi dhidi ya wengine. Mtazamo wa kistaarabu utahitajia kwamba mambo kama haya yasitumike vibaya kuleta chokochoko mioyoni mwa wafuasi wa dini mbali mbali. Hiyo hasa ndio maana ya nasaha ya Mtume Mtukufu[saw] iliyonukiliwa hapo juu. Ikiwa mshikamano na msingi huu wa upole na ustaarabu utafuatwa na dini zote, mifarakano mingi baina ya dini mbali mbali itaepukwa.

## Wokovu Hauwezi Kubinafsishwa na Dini Moja Yoyote Iwayo

Suala la wokovu, hata lionekane halina madhara namna gani, ni nyeti kwa hatari yake kwa amani katika ulimwengu wa dini.

Ni jambo moja kwa dini kutangaza kwamba wale wanaotafuta kukombolewa kutoka kwa shetani na kuupata wokovu wakimbilie kwenye hifadhi salama ya

dini hiyo, ni humo ndimo watakamokuta wokovu na ukombozi wa kuondokana na dhambi. Lakini ni jambo jingine kabisa kwa dini hiyo hiyo kutangaza papo hapo kwamba wale wasiokuja kwake kutafuta hifadhi watalaaniwa milele hao wote. Chochote wafanyacho kumpendeza Mungu, kwa kiasi chochote wampendacho Muumba wao na viumbe wake, kiasi gani wanaishi maisha ya utawa na uchaji Mungu, bila kujali hayo kwa uhakika kabisa watahukumiwa kuingia kwenye Moto wa milele.

Wakati mtazamo mgando wenye fikra finyu na usio na ustahamilivu kama huu unapoelezwa kwa lugha ya kichokozi kama ilivyo kawaida ya wafuasi ng'ang'anizi wa dini mbali mbali, inajulikana kusababisha machafuko mabaya.

Watu huwa wa aina mbali mbali. Wapo walioelimika, wastaarabu na watulivu, na ndivyo kunavyokuwa kuchokozeka kwao wanapochokozwa. Lakini wengi wa watu wenye kushika dini, wawe wenye elimu au mbumbumbu, uwezekano mkubwa ni kughadhibika kwa fujo zinapoumizwa hisia zao za kidini.

Kwa bahati mbaya huu huelekea kuwa ndio msimamo wa viongozi wa takriban dini zote duniani dhidi ya wale ambao hawafuati imani zao. Hata Islam inaelezwa na wanazuoni wa zama za kati kama mlango wa pekee wa wokovu, ili imaanishe kwamba baada ya kuja kwa Islam, wana wote wa Adamu[as] walioishi na kufariki wakiwa nje

ya Islam wamenyimwa wokovu. Ukristo hautoi dhana tofauti na hii kwa kadri nijuavyo mimi.

Lakini ngoja niwahakikishie wasikilizaji wangu kwamba kunasibishwa kwa mtazamo huu wa kijahili kufanywako na wenye fikra finyu na Islam hakuna msingi. Kurani Tukufu ina hadithi tofauti kabisa ya kutusimulia juu ya jambo hili.

Kwa mujibu wa Kurani Tukufu, wokovu hauwezi kubinafsishwa na dini yoyote moja iwayo duniani. Hata kama kweli mpya zinafunuliwa, na zama mpya za mwangaza zimewadia, wale wanaoishi maisha ya ujingani kwa sababu zisizokuwa za makosa yao na wale wanaojitahidi kuishi maisha ya ukweli hata kama walirithi imani potofu, hawatanyimwa wokovu na Mungu.

Aya zifuatazo kutoka kwenye Kurani Tukufu zinaelezea nukta hii kwa kina zaidi.

لِكُلِّ اُمَّةٍ جَعَلۡنَا مَنۡسَكًا هُمۡ نَاسِكُوۡهُ فَلَا يُنَازِعُنَّكَ فِى الۡاَمۡرِ وَ ادۡعُ اِلٰى رَبِّكَ ؕ اِنَّكَ لَعَلٰى هُدًى مُّسۡتَقِيۡمٍ ﴿۶۸﴾

*Kila umati Tumewajaalia kawaida ya ibada wanayoishikilia, basi wasikugombeze katika jambo hili; na uite kwa Mola wako; bila shaka wewe uko juu ya mwongozo ulio sawa.*[15]

Katika Aya nyingine Kurani Tukufu inadai kwa muktadha huo huo.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَالَّذِينَ هَادُوا وَالصَّابِئُونَ وَالنَّصَارَىٰ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَعَمِلَ صَالِحًا
فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ○

*Hakika wale walioamini na Mayahudi na Masabii na Wakristo - atakayemwamini Allah na siku ya Mwisho na kufanya vitendo vizuri - basi hao hawatakuwa na hofu wala hawatahuzunika.*[16]

Niruhusu nikukumbusheni kwamba ingawa istilahi ya *Ahlulkitaab,* "Watu wa kitabu", inatumika kwa Wayahudi na Wakristo, kwa dhamiri inayo matumizi mapana zaidi.

Kwa muktadha wa msisitizo wa Kurani Tukufu kwamba "Hakuna watu duniani ila Tumemtuma mwonyaji kwao" na aya kama hizo zilizorejewa hapo kabla, hatubakiwi na nafasi ya kutia shaka, kwamba watu hawa hawakuwa watu wa Agano la Kale na Agano Jipya (au Torati na Injili) ambao walipewa kitabu, lakini ni hakika kabisa kwamba vipo vitabu vingine vilivyofunuliwa kwa ajili ya wanadamu. Kwa hiyo dini zote, ambazo zinayo madai ya kuwa zipo juu ya msingi wa ufunuo kutoka kwa Mungu zitaingia katika "*Watu wa Kitabu.*"

Tena Kurani Tukufu hutumia neno *Sabii* ambalo huelezea zaidi jambo hili na kuondoa shaka. *Sabii* ni neno litumiwalo na Waarabu kumaanisha wafuasi wa dini zote zisizokuwa za Kiarabu au za Mashariki ya Kati ambazo zinavyo vitabu vyake vilivyofunuliwa. Kwa

namna hii, wafuasi wa dini zote zilizotokana na ufunuo kutoka kwa Mungu wamehakikishiwa kwamba sharti wameshindwa kutambua ukweli wa dini mpya (juu ya juhudi zao za dhati kuutambua) na wamebakia kwa uaminifu na ukweli kwenye mafundisho ya dini ya mababu zao, hawana cha kuogopa kutoka kwa Mungu na hawatanyimwa wokovu.

Kurani Tukufu, ikilizungumzia kundi mojawapo kati ya makundi ya waaminio: Wayahudi, Wakristo na Wasabii, inaahidi:

أَجْرُهُمْ عِندَ رَبِّهِمْ ۚ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦٢﴾

*Watapata ujira wao kwa Mola wao, wala haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika.*[17]

Na:

وَلَوْ أَنَّهُمْ أَقَامُوا التَّوْرَاةَ وَالْإِنجِيلَ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْهِم مِّن رَّبِّهِمْ لَأَكَلُوا مِن فَوْقِهِمْ وَمِن تَحْتِ
أَرْجُلِهِم ۚ مِّنْهُمْ أُمَّةٌ مُّقْتَصِدَةٌ ۖ وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ سَاءَ مَا يَعْمَلُونَ ﴿٦٦﴾

*Na kama wangalisimamisha Taurati na Injili na yale yaliyoteremshwa kwao kutoka kwa Mola wao, kwa yakini wangalikula vya juu yao na vya chini ya miguu yao; wako watu miongoni mwao washikao njia ya katikati, lakini wengi wao wanayoyafanya ni mabaya.*[18]

Kuwazuia Waislamu kuwalaumu kiholela watu wote wasiokuwa Waislamu, Kurani Tukufu inasema hivi:

لَيْسُوْا سَوَآءً ؕ مِنْ اَهْلِ الْكِتٰبِ اُمَّةٌ قَآئِمَةٌ يَّتْلُوْنَ اٰيٰتِ اللّٰهِ اٰنَآءَ الَّيْلِ وَهُمْ يَسْجُدُوْنَ ۝١١٤ يُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ
وَ الْيَوْمِ الْاٰخِرِ وَ يَاْمُرُوْنَ بِالْمَعْرُوْفِ وَ يَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَ يُسَارِعُوْنَ فِى الْخَيْرٰتِ ؕ وَ اُولٰٓئِكَ مِنَ
الصّٰلِحِيْنَ ۝١١٥ وَمَا يَفْعَلُوْا مِنْ خَيْرٍ فَلَنْ يُّكْفَرُوْهُ ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌۢ بِالْمُتَّقِيْنَ ۝١١٦

*Wao wote si sawa. Miongoni mwa watu wa Kitabu lipo kundi la watu wanaosimama imara katika ahadi zao; wanasoma Aya za Allah nyakati za usiku na wanamsujudia. Wanamwamini Allah na siku ya Mwisho na wanaamrisha mema na wanakataza maovu na wanaharakia mambo mema; na hao ndiyo miongoni mwa watendao mema. Na heri yo yote watakayoifanya hawataikataliwa; na Allah anawajua wamchao.*[19]

Kuna mkanganyiko mkubwa hivi leo, utokanao na uadui wa kisiasa, kati ya Wayahudi na Waislamu, ambapo kwa mujibu wa Waislamu, Wayahudi wote wataingia motoni. Dai hili sio la kweli kabisa kwa muongozo wa kile nilichokisema mbele yenu kutoka Kurani Tukufu, na kwa mwongozo wa Aya ifuatayo.

وَ مِنْ قَوْمِ مُوْسٰى اُمَّةٌ يَّهْدُوْنَ بِالْحَقِّ وَ بِهٖ يَعْدِلُوْنَ ۝١٦٠

*Na katika kaumu ya Musa wako watu wanaoongoza kwa haki na papo hapo wakifanya adili.*[20]

## Uhamasishaji wa Maelewano na Kuheshi-miana Baina ya Dini Mbalimbali

Imetangazwa kwa lugha fasaha katika Kurani Tukufu kwamba sio tu Waislamu wasimamao thabiti sambamba na ukweli na kutimiza na kutoa haki kwa kumuogopa

Mungu, kati ya wafuasi wa dini nyinginezo, pia wapo watu wengine wafanyao kama hivyo.

Huu ndio mtazamo, ambao ulimwengu wote wa dini ni lazima waufuate leo ili kukuza ubora wa mahusiano na dini zingine. Amani ya kidini haiwezi kupatikana bila kupandikiza aina hii ya fikra pana, upendo na mtazamo wa maelewano ya kiutu na watu wa imani zingine. Ikimaanisha dini zote duniani, kwa ujumla, Kurani Tukufu inasema.

وَمِمَّنْ خَلَقْنَآ أُمَّةٌ يَهْدُونَ بِٱلْحَقِّ وَبِهِۦ يَعْدِلُونَ ۝١٨١

*Na katika wale Tuliowaumba wako watu wanaoongoza kwa haki na papo wanafanya uadilifu.*[21]

## Dhana ya Dini kuwa Jambo la Ulimwengu Wote

Tangu azali wanafalsafa wengi wamekuwa wakiuota wakati ambao wanadamu wataweza kukusanyika wote pamoja kama familia moja kubwa ya wanadamu chini ya bendera moja. Dhana hii ya muungano wa wanadamu imeendelea kubebwa sio tu na wanafalsafa wa kisiasa bali pia na wachumi na wanajamii hali kadhalika. Lakini hakuna mahala ambapo wazo hili limefuatiliwa kwa hamu kubwa zaidi kama katika ulingo wa dini.

Ingawaje Islam nayo inalo wazo hili kama zilivyo dini zingine (baadhi zikiwa na mikakati ya tamaa kubwa juu ya kujieneza duniani), ndani ya mfanano huu unaoonekana, Islam inasimama na tofauti ya pekee katika mtazamo wake juu ya madai ya kitamaa

yaliyotajwa hapo awali. Hapa si mahala pa kuelezea mada hii tata kwa kirefu na kuingia katika mdahalo wa ipi hasa ndio dini iliyopewa mamlaka na Mungu kuwakusanya watu wote chini ya bendera moja ya Mungu. Ni muhimu sana kwetu kuelewa matokeo ya madai kama hayo yafanywayo na dini zaidi ya moja duniani.

Ikiwa dini mbili, tatu au nne zenye nguvu zilizo na desturi za kihistoria, zinazojulikana kwa muda mrefu, kwa pamoja zikidai kuwa ni dini za dunia nzima, je hii haitaleta mkanganyiko wa kutisha na wasiwasi katika vichwa vya wanadamu wote? Je uadui baina yao na mapambano ya kuwa juu ya zingine havitaleta tishio la kweli na kubwa vya kutosha juu ya amani ya dunia?

Vuguvugu kama hizi zinazoienea dunia nzima zifanywazo na dini mbali mbali zenyewe ni jambo la kutia hofu kubwa. Lakini kwa kuongezea hapo hatari ya vuguvugu hizo kuangukia kwenye mikono ya viongozi wasiojali kitu, wakorofi na waliokosa ustahamilivu inamaanisha kwamba tishio kwa amani litakuwa kubwa sana na lenye uwezekano mkubwa wa kutokea kuliko kuwa nadharia tu.

Kwa upande wa Islam, kwa bahati mbaya, kuna propaganda iliyoenea sana kwamba Islam inahamasisha matumizi ya nguvu kila iwezekanavyo kwa ajili ya kueneza mafundisho yake. Maneno kama haya yanasemwa sio tu na wapinzani wa Islam bali pia na

wanazuoni wenye mawazo ya kizamani ambao ni viongozi wa Islam.

Ni ukweli wa wazi, ikiwa dini moja itachagua kushambulia, zingine zitakuwa na haki ya kujitetea kwa kutumia silaha zile zile. Bila shaka sikubaliani na napinga kwa nguvu zote fikra kwamba Islam inahimiza matumizi ya nguvu katika kueneza mafundisho yake - lakini juu ya somo hili nitarejea hapo baadae.

Kwanza hebu tutazame usahihi wa madai kama haya kwa dini yoyote duniani. Je yawezekana dini yoyote — Islam, Ukristo au yoyote nyingine — kuwa ya dunia nzima katika ujumbe wake? Kwa maana kwamba ujumbe uweze kutumika na watu wote wa dunia, wa rangi yoyote, kabila lolote na Taifa lolote? Vipi kuhusu tofauti nyingi za jamii, kikabila, mila za kitaifa, tabia za kijamii na tamaduni zilizojengeka?

Dhana ya dini ya dunia nzima kama inavyopendekezwa na dini mbalimbali, yapasa sio tu kuvuka mipaka ya kijiografia na mipaka ya kitaifa bali yapasa pia kuvuka mipaka ya wakati. Hivyo swali litakuwa: Je dini yaweza kuwa haina mpaka wa wakati, yaani mafundisho ya dini hiyo yafae kutumika na yawe yanawatosha watu wa zama hizi kadhalika na wale wa miaka elfu iliyopita na miaka elfu ijayo? Hata kama dini ikubaliwe duniani kote na watu wote wa dunia nzima, itawezaje kuwa inamudu vya kutosha kutimiza mahitajio ya vizazi vijavyo?

Ni juu ya wafuasi wa kila dini kuonyesha kwa namna gani mafundisho ya dini yao yanapendekeza kutanzua masuala yaliyoelezwa hapo juu. Kwa hivyo kwa niaba ya Islam, nitapenda kueleza kwa muhtasari na kwa kifupi kabisa jibu la Islam kwa maswali haya.

## Islam ni Dini ya Dunia Nzima

Kurani Tukufu kwa kurudia rudia inaweka wazi kwamba Islam ni dini ambayo mafundisho yake yana uhusiano na silika ya mwanadamu. Islam inasisitiza kwamba dini yoyote, ambayo mizizi yake inashikiliwa na silika ya mwanadamu inavuka mipaka ya wakati na eneo. Silika ya binadamu haibadilishiki. Kwa hiyo dini ambayo kweli mizizi yake imo kwenye silika ya binadamu inakuwa haibadilishiki kwa sababu hiyo hiyo ilimradi kwamba haijiingizi sana katika maswala ya mpito ya mwanadamu, katika zama zozote asongavyo mbele. Ikiwa dini hiyo itabakia kwenye misingi hiyo ambayo inatokana na silika ya binadamu, dini kama hiyo inao uwezekano unaoyamkinika wa kuwa dini ya ulimwengu mzima.

Islam inaenda hatua moja mbele. Katika mtazamo wake wa kipekee wenye kuleta maelewano, Islam inazitambua dini zote za dunia kuwa zinayo sifa hii ya kuwa za dunia nzima kwa kiwango fulani. Kwa hivi, katika kila dini iliyofunuliwa na Mungu, siku zote kunakutikana kiini cha kati cha mafundisho, ambacho kinashabihiana na silika ya binadamu na ukweli wa milele. Kiini hiki cha

dini zote kinabaki bila badiliko, isipokuwa bila shaka wafuasi wake wafisidi dini hiyo katika kipindi cha baadae cha wakati.

Aya zifuatazo zinafafanua hoja ya nukta hii:

وَ مَآ أُمِرُوْٓا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللهَ مُخْلِصِيْنَ لَهُ الدِّيْنَ ۙ حُنَفَآءَ وَ يُقِيْمُوا الصَّلٰوةَ وَ يُؤْتُوا الزَّكٰوةَ وَ ذٰلِكَ دِيْنُ الْقَيِّمَةِ ﴿٦﴾

*Wala hawakuamrishwa ila kumwabudu Allah kwa kumhalisishia dini kwa haki na kusimamisha Sala na kutoa Zaka: na hii ndiyo dini madhubuti.*[22]

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّيْنِ حَنِيْفًا ۚ فِطْرَتَ اللهِ الَّتِيْ فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا ۚ لَا تَبْدِيْلَ لِخَلْقِ اللهِ ۚ ذٰلِكَ الدِّيْنُ الْقَيِّمُ ۙ وَلٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٣١﴾

*Basi uelekeze uso wako kwenye dini ukiwa daima umeegemea kwenye haki - na fuata hali asilia ya Allah ambayo kwayo Aliwaumba binadamu wote. Hakuna mabadiliko katika uumbaji wa Allah. Bila shaka hiyo ndiyo dini iliyosimama madhubuti na inazisaidia zingine kusimama wima. Lakini watu wengi hawajui.*[23]

Kwa kuangalia hayo hapo juu, swali laweza kuzuka juu ya hekima hasa ya kutumwa dini moja baada ya nyingine zikiwa na mafundisho yale yale. Zaidi ya hayo, mtu aweza kujiuliza kwa nini Islam inadai kwa maana linganifu kuwa ya dunia nzima zaidi na kamilifu zaidi kuliko dini zile za kabla yake ikiwa zote zilikuwa na mafundisho yale yale yasiyobadilishika kwa wanadamu kwa nyakati zote.

1. Katika kujibu swali la kwanza Kurani Tukufu inaelekeza umakini wa wanadamu kwenye ukweli wa kihistoria usiopingika kwamba vitabu na maandiko yaliyofunuliwa mapema kabla ya Kurani Tukufu vimechezewa (kwa mkono wa watu). Mafundisho yake yamefisidiwa kwa mchakato wa masahihisho ya pole pole au mambo mapya yaliongezwa kwa njia ya kutona maneno mpaka usahihi na uhalisia wa vitabu hivi na maandiko ukawa wa kutiliwa shaka na usioaminika.

Kwa hivyo, dhima ya kuthibitisha kwamba hakuna mabadiliko yoyote yawayo yaliyofanywa, bila shaka, inabebwa na wafuasi wa dini hizo. Kurani Tukufu kwa upande wake, imejiweka katika sehemu ya kipekee na tofauti kabisa kati ya vitabu vya dini zote na maandiko. Hata baadhi ya maadui wabaya kabisa wa Islam, ambao hawaiamini Kurani kuwa ni neno la Mungu, wamelazimika kukiri kwamba Kurani Tukufu, bila ya chembe ya shaka, imebakia kitabu kile kile bila mabadiliko au nyongeza yoyote ambacho kilidaiwa na Muhammad[saw] kuwa ni neno la Mungu.

Kwa mfano:

> *There is otherwise every security, internal and external, that we possess the text which Mohamet himself gave forth and used.*[24]

"Vinginevyo kuna kila uthibitisho, wa ndani na nje, kwamba tunayo maandiko ambayo Muhammad mwenyewe aliyatoa na kuyatumia."

> *We may, upon the strongest assumption, affirm that every verse in the Qur'an is the genuine and unaltered composition of Mohamet himself.* [25]

Tunaweza kwa kutumia hoja thabiti kabisa kuthibitisha kwamba kila aya katika Kurani ni ile ile asilia na utungo usiobadilishwa wa Muhammad mwenyewe."

> *Slight clerical errors there may have been, but the Qur'an of Uthman contains none but genuine elements, though sometimes in very strange order. The efforts of European scholars to prove the existence of later interpolations in the Qur'an have failed.*[26]

"Makosa madogo ya uandishi yaweza kuwapo, lakini Qura'n ya Uthman haina lolote ndani yake isipokuwa maneno asilia, ingawa wakati mwingine katika mpangilio wa kushangaza sana. Jitihada zilizofanywa na wasomi wa Ulaya kutafuta uwepo wa maingizo ya baadaye katika Kurani zimeshindwa."

Ni eneo jingine kabisa la malumbano kwamba ni kitabu kipi kilitungwa na nani. Lakini kitabu kile kile ambacho utungwaji wake na Mungu unabishaniwa na watu wengine wa Kitabu ni ushahidi wa ukweli wake kwamba, sio tu Torati na Injili (kwa pamoja Agano la Kale na Agano Jipya) vilitungwa kwa kiasi fulani na Mungu Mwenyewe, lakini pia vitabu vingine vya dini zingine mbali mbali katika maeneo mengine ya dunia, navyo bila shaka, vilitungwa na Mungu yule yule - hitilafu zionekanazo ndani ya vitabu hivyo hivi sasa

zimesababishwa na watu. Je bado ipo haja ya kusemwa kwamba mtazamo wa Kurani Tukufu ndio wenye busara zaidi na wenye kuleta amani miongoni mwa dini mbali mbali?

2. Kuhusu swali la pili, Kurani Tukufu inaelekeza umakini wetu kwenye mchakatao wa mabadiliko katika kila eneo la jamii ya watu. Dini mpya zilihitajika sio tu kwa ajili ya kurudisha tena mafundisho ya msingi ya dini za zamani ambayo yalikuwa yameharibiwa kwa mikono ya binadamu, bali pia, kadri jamii ilivyokua, mafundisho mapya ilibidi yaongezwe kwenye yale ya zamani ili kuendana na hatua ya maendeleo ya watu.

3. Sio hivyo tu, sababu nyingine katika mchakato huu wa mabadiliko ilikuwa ni suala la mafundisho ya nyongeza yaliyohusiana na wakati ambayo yalifunuliwa kukidhi haja za watu wa wakati maalum. Hii yamaanisha kwamba dini sio tu zilijengwa na viini kati vya misingi isiyobadilishika, bali pia ilivikwa na mafundisho ya pembeni, ziada na hata mafundisho ya mpito.

4. La mwisho lakini sio kwa umuhimu, mwanadamu hakuelimishwa na kufundishwa katika miongozo ya Mungu katika hatua moja, bali alipelekwa mbele hatua kwa hatua kwenye daraja la ukomavu wa akili ambapo alionekana anatosha na amekomaa kupokea mafundisho yote ya msingi ambayo yalihitajika kwa ajili ya mwongozo wake. Kwa mujibu wa madai ya

Kurani Tukufu, mafundisho ya nyongeza yasiyotenganishika kufuatana na kanuni za msingi za milele, yalifunuliwa pia kama sehemu ya dini ya mwisho, kamilifu na timilifu yaani Islam. Kile ambacho kilihusu sehemu fulani tu au muda fulani tu kimeondolewa na kufutwa; kile ambacho kilikuwa bado kinahitajika baadae, kiliwekwa na kubakizwa.[27]

Hii kwa kifupi ndio dhana ya Islam ya dini kuwa ya ulimwengu mzima, ambayo Islam inadai kuwa ndio hali yake. Ni juu ya kila mtu kuchunguza na kuamua uzito wa hoja za kila mdai.

Sasa, kwa mara nyingine, tunaligeukia suala la dini zile, ambazo zimejiwekea zenyewe lengo la kuienea dunia. Ni dhahiri, Islam inashikilia tamaa kama hiyo. Kwa namna ya bishara, Kurani Tukufu inatangaza kwamba Islam hatimae itatokezea siku moja kuwa dini pekee ya wanadamu:

هُوَ الَّذِيٓ اَرۡسَلَ رَسُوۡلَهٗ بِالۡهُدٰی وَ دِیۡنِ الۡحَقِّ لِیُظۡهِرَهٗ عَلَی الدِّیۡنِ کُلِّهٖ وَ لَوۡ کَرِهَ الۡمُشۡرِکُوۡنَ ﴿۱۰﴾

*Yeye ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa mwongozo na kwa dini ya haki ili kuifanya ishinde dini zote ijapokuwa washirikina wachukie.*[28]

Pamoja na kusudio lake la dhati katika kuhamasisha amani na mtangamano miongoni mwa dini mbalimbali, Islam haizuii ushindani katika kueneza ujumbe wa dini mbalimbali pamoja na mafundisho yao kwa zenye nia ya kuzipiku dini zingine. Kwa kweli inaweka ushindi wa

Islam hatimae juu ya dini zingine zote kuwa ni lengo adhimu, ambalo kila Mwislam anawajibika kulifuatilia.

Ikimuongelea mwanzilishi mtukufu[saw] wa Islam, Kurani Tukufu inasema:

قُلْ يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ اِنِّىْ رَسُوْلُ اللّٰهِ اِلَيْكُمْ جَمِيْعَا ۨالَّذِىْ لَهٗ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَ الْاَرْضِ ۚ لَاۤ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ يُحْىٖ وَ يُمِيْتُ ۠ فَاٰمِنُوْا بِاللّٰهِ وَ رَسُوْلِهِ النَّبِىِّ الْاُمِّىِّ الَّذِىْ يُؤْمِنُ بِاللّٰهِ وَ كَلِمٰتِهٖ وَ اتَّبِعُوْهُ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُوْنَ ﴿١٥٩﴾

*Sema: Enyi watu, hakika mimi ni Mtume wa Allah kwenu nyote, Ambaye Anao ufalme wa mbingu na ardhi, hapana aabudiwaye ila Yeye, Ahuishaye na Afishaye. Basi Mwaminini Allah na Mtume Wake, aliye Nabii Ummi, ambaye humwamini Allah na maneno Yake; na mfuateni yeye ili mpate kuongoka.*[29]

Hata hivyo, ili kuepuka misuguano na magomvi, Islam inaweka kundi la kanuni bayana za kuenendea zinazohakikisha ustaarabu, haki kabisa, uhuru wa kuongea, haki ya kujieleza na haki ya kutokukubaliana zilizo sawa kwa wote.

## Nyenzo za Jitihada — Hakuna Karaha

Dini inawezaje kujidaia kuwa ni ya ulimwengu mzima, ya kimataifa au ya duniani kote na bado isisababishe misuguano? Hakuna dini yenye ujumbe kwa ulimwengu mzima na malengo ya kuunganisha watu wa dunia nzima chini ya bendera moja yanaweza hata kwa muda

mdogo kulipendelea wazo la kutumia nguvu katika kueneza ujumbe wake.

*"Mapanga yaweza kushinda himaya lakini sio nyoyo"*

*"Mabavu yaweza kuinamisha vichwa sio fikra"*

Islam hairuhusu matumizi ya nguvu kama nyenzo ya kueneza ujumbe wake. Inatangaza:

لَآ إِكْرَاهَ فِى ٱلدِّينِ ۖ قَد تَّبَيَّنَ ٱلرُّشْدُ مِنَ ٱلْغَىِّ ۚ

*Hakuna karaha katika dini; hakika uongofu umekwisha pambanuka katika upotevu ...* [30]

Kwa hiyo hakuna haja ya kulazimishana. Mwachie mtu mwenyewe kupima ukweli uko wapi. Akimwambia mwanzilishi mtukufu[saw] wa Islam, Mungu wazi wazi anamuonya asifikirie wazo lolote la kutumia nguvu katika jitahada za kuirekebisha jamii. Hadhi yake kama mwonyaji inadhihirishwa katika aya ifuatayo:

فَذَكِّرْ إِنَّمَآ أَنتَ مُذَكِّرٌ ﴿٢١﴾ لَّسْتَ عَلَيْهِم بِمُصَيْطِرٍ ﴿٢٢﴾

*Basi kumbusha, hakika wewe ni Mkumbushaji tu. Wewe si mlinzi wao.*[31]

Kwa kendeleza zaidi mada hiyo, Mtume Mtukufu[saw] anakumbushwa:

فَإِنْ أَعْرَضُوا۟ فَمَآ أَرْسَلْنَٰكَ عَلَيْهِمْ حَفِيظًا ۖ إِنْ عَلَيْكَ إِلَّا ٱلْبَلَٰغُ ۗ

*Na kama wakigeuka, basi Hatukukupeleka uwe mhifadhi wao, si juu yako ila kufikisha.*[32]

Hata kama mapambano yanazuka katika mchakato wa kueneza mafundisho mapya na upinzani mkali unajitokeza, hapo Islam inawaasa kwa dhati wafuasi wake kuonyesha subira na uvumilivu na kuepuka faraka kadri iwezekanavyo. Hii ndio maana kila Mwislamu alipotakiwa kufikisha ujumbe wa Islam kwa dunia nzima; taratibu maalum ya kufuata imewekwa kwa ajili yake. Miongoni mwa aya nyingi zihusianazo na somo hili, tunanukuu aya chache zifuatazo kufafanua jambo hili:

ادْعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحِكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ ۖ وَجَادِلْهُم بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ ۚ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ
أَعْلَمُ بِمَن ضَلَّ عَن سَبِيلِهِ ۖ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿١٢٦﴾

*Uite (watu) kwenye njia ya Mola wako kwa hekima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola wako ndiye Humjua sana aliyepotea katika njia Yake, naye ndiye Awajuaye sana walioongoka.*[33]

Na:

ادْفَعْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ السَّيِّئَةَ ۚ نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَا يَصِفُونَ ﴿٩٧﴾

*Uzuie ubaya kwa yaliyo bora; Sisi Tunajua wanayoyaeleza.*[34]

Hapa, *ahsan* maana yake ni bora kabisa, kinachovutia zaidi na kitu kinachopendeza.

Ikieleza taratibu za mwenedo ambazo hufuatwa na waaminio katika kufikisha ujumbe, Kurani Tukufu inayo maelezo yafautayo:

وَ الْعَصْرِ ۙ﴿۲﴾ اِنَّ الْاِنْسَانَ لَفِیْ خُسْرٍ ۙ﴿۳﴾ اِلَّا الَّذِیْنَ اٰمَنُوْا وَ عَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ وَ تَوَاصَوْا بِالْحَقِّ ۬ۙ وَ تَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ ﴿۴﴾

*Naapa kwa ushahidi wa wakati. Kwa hakika mtu yumo hasarani. Isipokuwa wale walioamini na wakafanya vitendo vizuri, na wakausiana (kushika) haki na wakausiana (kushika) subira.*[35]

Tena:

ثُمَّ كَانَ مِنَ الَّذِیْنَ اٰمَنُوْا وَ تَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ وَ تَوَاصَوْا بِالْمَرْحَمَةِ ﴿۱۸﴾

*Kisha awe miongoni mwa waaminio na wanaousiana kusubiri na wanaousiana kuhurumiana.*[36]

## Uzima wa Kinachojimudu Zaidi

Kwa mujibu wa Kurani Tukufu, uzima na hatimae kushinda kwa ujumbe hutegemea tu nguvu ya hoja zake, sio nguvu ya kimwili inayoweza kuitumia. Kurani Tukufu iko dhahiri shahiri na mahsusi katika somo hili. Inaeleza kwamba hata kama nguvu kubwa kabisa zitumike kutaka kuzuia ukweli na kusaidia uongo, jitihada kama hizo daima zitashindwa na kufadhaika. Akili wakati wote itashinda juu ya nguvu tupu ya silaha shikika. Kwa mfano imesemwa katika Kurani Tukufu:

قَالَ الَّذِيْنَ يَظُنُّوْنَ اَنَّهُمْ مُّلٰقُوا اللّٰهِ ۙ كَمْ مِّنْ فِئَةٍ قَلِيْلَةٍ غَلَبَتْ فِئَةً كَثِيْرَةًۢ بِاِذْنِ اللّٰهِ ؕ وَ اللّٰهُ مَعَ الصّٰبِرِيْنَ ۝٢٥٠

*Wakasema wale wenye yakini ya kukutana na Mola wao: Makundi mangapi madogo yameyashinda makundi makubwa kwa idhini ya Allah! Na Allah Yu pamoja na wafanyao subira.*[37]

Dhana ya ushindi wa Islam yapaswa kueleweka katika muktadha wa amri ya Mungu iliyotajwa hapo juu.

Katika sehemu nyingine ya aya ya Kurani Tukufu, inasemwa:

رَضِيَ اللّٰهُ عَنْهُمْ وَ رَضُوْا عَنْهُ ؕ اُولٰٓئِكَ حِزْبُ اللّٰهِ ؕ اَلَاۤ اِنَّ حِزْبَ اللّٰهِ هُمُ الْمُفْلِحُوْنَ ۝٢٣

*Allah Amekuwa radhi nao, na wao wamekuwa radhi naye; hao ndio kundi la Allah. Sikilizeni! Hakika kundi la Allah ndio wanaofaulu.*[38]

Wakati wa vita vya Badri (Vita vya kwanza katika historia ya Islam) jeshi kubwa la makafiri wa Makka lilikutanishwa vitani dhidi ya idadi ndogo ya Waislamu - waliozidiwa kabisa kiidadi, kiujuzi, kisilaha na vifaa, na waliolazimishwa kupigana vita vya kujihami kwa ajili ya kulinda mafundisho yao na sio kwa ajili ya maisha yao binafsi. Ikielezea tukio hili Kurani Tukufu inasema:

لِّيَهْلِكَ مَنْ هَلَكَ عَنْۢ بَيِّنَةٍ وَّ يَحْيٰى مَنْ حَيَّ عَنْۢ بَيِّنَةٍ ؕ وَ اِنَّ اللّٰهَ لَسَمِيْعٌ عَلِيْمٌ ۝٤٣

*Ili aangamie aangamiaye kwa dalili dhahiri, na aishi aishiye kwa dalili dhahiri. Na hakika Allah ndiye Asikiaye Ajuaye.*[39]

Hii ndiyo kanuni ya kudumu, ambayo inachukua nafasi ya muhimu katika muendeleo wa kimaumbile ya binadamu. Uzima kwa kinachojimudu zaidi ndio maana ya ujumbe huu. Hiyo, kwa hakika, ndio njia fanyizi ya muendeleo wa maisha.

## Uhuru wa Kuongea

Uhuru wa kuongea na kujieleza ni muhimu katika kueneza ujumbe halikadhalika katika kurejesha heshima ya binadamu. Hakuna dini inayostahili kuthaminiwa hata kidogo mpaka iwe imejikita katika kurejesha na kulinda utu wa mtu.

Kwa kuzingatia hayo, itaonekana wazi kwamba haiwezekani kwa dini kama Islam kukataza uhuru wa kuongea na kujieleza. Tofauti na hivyo, Islam inathamini kanuni hii kwa namna ambayo na kwa kiasi cha ujasiri ambacho ni nadra kuonekana katika mafundisho au dini nyingine duniani. Kwa mfano Kurani Tukufu inasema:

وَقَالُوا لَنْ يَدْخُلَ الْجَنَّةَ إِلَّا مَنْ كَانَ هُودًا أَوْ نَصَارَىٰ ۗ تِلْكَ أَمَانِيُّهُمْ ۗ قُلْ هَاتُوا
بُرْهَانَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١١١﴾

*Nao husema: Hataingia Peponi ila aliye Myahudi au Mkristo! Hayo ndiyo matamanio yao. Sema: Leteni dalili yenu kama ninyi ni wakweli.*[40]

Tena:

أَمِ اتَّخَذُوا مِن دُونِهِ آلِهَةً ۖ قُلْ هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ ۖ هَٰذَا ذِكْرُ مَن مَّعِيَ وَذِكْرُ مَن قَبْلِي ۗ بَلْ
أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ الْحَقَّ ۖ فَهُم مُّعْرِضُونَ ﴿٢٥﴾

*Au je, wameshika badala Yake miungu? Sema: Leteni dalili zenu. Huu ni ukumbusho wa wale walio pamoja nami, na ukumbusho wa wale wa kabla yangu; lakini wengi wao hawajui ukweli, kwa hiyo wanapuuza.*[41]

Na:

وَنَزَعْنَا مِن كُلِّ أُمَّةٍ شَهِيدًا فَقُلْنَا هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ فَعَلِمُوا أَنَّ الْحَقَّ لِلَّهِ وَضَلَّ عَنْهُم
مَّا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٧٦﴾

*Na Tutatoa katika kila uamti shahidi na Tutasema: Leteni dalili zenu; ndipo watajua ya kwamba kweli ina Mungu na yatawapotea yale waliyokuwa wakiyazusha.*[42]

Na:

أَمْ لَكُمْ سُلْطَانٌ مُّبِينٌ ﴿١٥٧﴾ فَأْتُوا بِكِتَابِكُمْ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٥٨﴾

*Au mmepata dalili iliyo wazi? Basi leteni Kitabu chenu kama mnasema kweli.*[43]

## Uhuru na Ukombozi Katika Muktadha wa Dunia ya Leo

Uhuru na ukombozi ni miito miwili ambayo inaiathiri dunia nzima kwa kiwango tofauti na maana tofauti katika sehemu mbalimbali za dunia. Hakuna shaka yoyote iwayo, kwamba binadamu anapata utambuzi

mpana zaidi na ufahamu juu ya umuhimu na thamani ya uhuru. Kuna haja kubwa inayosikika kila mahala duniani ya ukombozi, lakini kutoka kwenye nini? Je ni kutoka kwenye kamato la utawala wa kigeni; udikteta; ufashisti; utawala wa makasisi au aina nyingine za utawala wenye falsafa za kiimla; demokrasia kandamizi na ukiritimba fisadi; ukandamizaji wa kiuchumi wa nchi maskini na nchi tajiri; ujinga; itikadi za kidhana au umasanamu?"

Islam inaleta jitihada za kujikomboa kutoka kwenye madhila haya yote lakini sio kwa namna ya kuleta machafuko, fujo na kisasi kisicho mipaka, kiasi cha kuleta mateso kwa wasio na hatia. 'Na Mungu hapendi machafuko () ndio ujumbe wa Islam.[44]

Islam kama ilivyo kwa dini nyingine yoyote, inasisitiza nafasi ya uhuru wenye mipaka katika roho ya mpeano kila upande upate na utoe. Dhana ya uhuru bila mipaka haina mashiko, ni tupu, na haina ukweli kwa muktadha wa jamii.

Wakati mwingine dhana ya uhuru inaeleweka vibaya mno kiasi kwamba uzuri wa msingi unaopendwa kama uhuru wa kuongea unapata kubadilishwa kuwa ubaya wa uhuru wa kuongea vibaya, kutoa matusi na kejeli.

## Kejeli

Islam inaenda hatua mbele kuliko dini yoyote ile katika kumpatia mwanadamu uhuru wa kuongea na kujieleza.

Kejeli inakatazwa kwa misingi ya kimaadili na ustaarabu, bila shaka, lakini hakuna adhabu ya kimwili imetolewa katika Islam kwa kejeli kinyume na dhana ya watu wengi katika ulimwemengu wa sasa.

Baada ya kuisoma Kurani Tukufu kwa mapana na marefu na kuirudia rudia kwa umakini wa kina, nimeshindwa kuona Aya hata moja ambayo inaeleza kejeli kuwa ni kosa linaloweza kuadhibiwa na wanadamu.

Ingawa Kurani Tukufu inakataza kwa nguvu tabia isiyokuwa ya kistaarabu na maongezi ya kipuuzi au kuumiza hisia za wengine kukiweko au bila kuweko sababu, Islam haielekezi kuadhibiwa kejeli katika dunia hii au kumpa mamlaka ya kufanya hivyo mtu yeyote.

Kejeli kumetajwa mara tano katika Kurani Tukufu.

1) Kwa mfano, somo hili limetajwa kwa ujumla wake.

وَقَدْ نَزَّلَ عَلَيْكُمْ فِي الْكِتٰبِ اَنْ اِذَا سَمِعْتُمْ اٰيٰتِ اللّٰهِ يُكْفَرُ بِهَا وَيُسْتَهْزَاُ بِهَا فَلَا تَقْعُدُوْا مَعَهُمْ حَتّٰى يَخُوْضُوْا فِيْ حَدِيْثٍ غَيْرِهٖٓ ۖ اِنَّكُمْ اِذًا مِّثْلُهُمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ جَامِعُ الْمُنٰفِقِيْنَ وَ الْكٰفِرِيْنَ فِيْ جَهَنَّمَ جَمِيْعًا ۙ﴿١٤١﴾

*Naye Amekwisha wateremshieni katika Kitabu ya kwamba mnaposikia Aya za Allah zinakataliwa na kufanyiwa mzaha, basi msikae pamoja nao, mpaka waingie katika mazungumzo ghairi ya hayo; (maana mtakapokaa) hakika ndipo mtakuwa kama wao. Hakika*

*Allah Atawakusanya wanafiki na makafiri wote katika Jahanamu.*[45]

وَ اِذَا رَاَيۡتَ الَّذِيۡنَ يَخُوۡضُوۡنَ فِىۡۤ اٰيٰتِنَا فَاَعۡرِضۡ عَنۡهُمۡ حَتّٰى يَخُوۡضُوۡا فِىۡ حَدِيۡثٍ غَيۡرِهٖ‌ؕ وَ اِمَّا يُنۡسِيَنَّكَ الشَّيۡطٰنُ فَلَا تَقۡعُدۡ بَعۡدَ الذِّكۡرٰى مَعَ الۡقَوۡمِ الظّٰلِمِيۡنَ ﴿۶۹﴾

*Na unapowaona wale wanaozifanyia mzaha Aya Zetu, basi ujitenge nao mpaka wazungumze maneno mengine; na kama Shetani akikusahaulisha, basi usikae baada ya kukumbuka pamoja na watu wadhalimu.*[46]

Jibu zuri lilioje kwa sura isiyopendeza kabisa ya kejeli. Sio tu Islam haimruhusu mwanadamu yeyote kutoa adhabu kwa mtukanaji kwa mikono yake mwenyewe, lakini inatangaza kwamba watu wanapaswa kuonyesha kutokubaliana kwao na kejeli kwa kutoka nje kutoka kwenye mkusanyiko wa watu ambapo desturi njema za kidini zinafanyiwa mzaha na kudharauliwa. Hakuna mapendekezo ya hatua zozote za adhabu, na hakuna hata pendekezo la kumtenga kwa kudumu mtukanaji lililotolewa na Kurani Tukufu. Kinyume chake, Kurani Tukufu inabainisha wazi kabisa kwamba kumtenga kuendelee kwa kipindi kile tu ambapo tendo la kejeli litakuwa linaendelea.

2) Tena, kejeli imetajwa katika surah Al-An'am ambapo kinadharia, suala la kejeli limejadiliwa sio tu kumhusu Mwenyezi Mungu lakini kuwahusu masanamu na vitu vya kufikirika vinavyoabudiwa kinyume cha Mwenyezi Mungu.

Mtu anaelemewa na uzuri wa mafundiso ya Kurani Tukufu pale inaposema:

وَ لَا تَسُبُّوا الَّذِيۡنَ يَدۡعُوۡنَ مِنۡ دُوۡنِ اللّٰهِ فَيَسُبُّوا اللّٰهَ عَدۡوًۢا بِغَيۡرِ عِلۡمٍ ؕ كَذٰلِكَ زَيَّنَّا لِكُلِّ
اُمَّةٍ عَمَلَهُمۡ ۪ ثُمَّ اِلٰى رَبِّهِمۡ مَّرۡجِعُهُمۡ فَيُنَبِّئُهُمۡ بِمَا كَانُوۡا يَعۡمَلُوۡنَ ﴿۱۰۹﴾

*Wala msiwatukane wale ambao wanawaita kinyume cha Allah wasije wakamtukana Allah kupita kiasi bila kujua. Hivyo Tumewapambia kila watu vitendo vyao, kisha marejeo yao yatakuwa kwa Mola wao, naye Atawaambia waliyokuwa wakitenda.*[47]

Ni Waislamu ambao wanaambiwa na aya hii. Wanakatazwa katakata kuyatusi masanamu na miungu wa kufikirika wa makafiri. Imetajwa pia kwamba ikiwa mtu atafanya hivyo, wengine wanaweza kwa kulipiza kisasi, kujihusisha na matusi dhidi ya Mwenyezi Mungu. Katika maelezo haya ya kinadharia ya kejeli dhidi ya Mwenyezi Mungu na masanamu kwa namna ilivyo sawa, hakuna adhabu ya kimwili iliyowekwa kwa upande wowote.

Adili ya fundisho hili imejaa hekima kubwa. Ikiwa mtu atazikosea hisia za kiroho za mwingine au wengine, upande uliokosewa unayo haki ya kulipiza kwa namna ile ile bila kujali aina ya imani na kama imani hiyo ni sahihi au ni potovu. Na hairuhusiwi kulipiza kwa namna nyingine. Mtu anaweza kuhitimisha uelewa kutokana na hayo ya kwamba makosa ya kiroho yapaswa kulipizwa kwa njia za kiroho kama ambavyo

makosa ya kimwili hulipizwa kwa njia za kimwili — lakini bila kuruka mipaka.

3) Kuleta matusi kumetajwa katika Kurani Tukufu kuhusiana na Mariamu na Yesu[as].

وَّ بِكُفۡرِهِمۡ وَ قَوۡلِهِمۡ عَلٰی مَرۡیَمَ بُهۡتَانًا عَظِیۡمًا ﴿۱۵۷﴾

*Na kwa sababu ya kufuru zao na kusema kwao juu ya Mariamu masingizio makubwa.*[48]

Aya hii inaelezea msimamo wa kihistoria wa Wayahudi waliokuwepo nyakati za Yesu Kristo[as]. Kwa mujibu wa aya hii, Wayahudi walileta matusi makubwa kwa kumtangaza Mariam kuwa muasherati na kumshuku Yesu, kuwa ni mtoto wa haramu *Mungu apishe mbali*.

Neno la Kirabu '*Buhtanan Adhiima*' (lililofasiriwa hapo juu kuwa 'masingizio makubwa') linaelezea kulaani ujinga huu uliofanywa na Wayahudi kwa kauli ya sisitizo zito kabisa. Bado kwa mshangao hakuna adhabu ya kimwili iliyowekwa kwa kosa hili.

4) Inavutia kuona kwamba wakati Wayahudi wamelaaniwa na Kurani Tukufu kwa kufanya kosa la kejeli dhidi ya Mariam na Yesu, wakati huo huo Wakristo, kwa upande wao, wanakaripiwa kwa kuleta matusi dhidi ya Mungu kwa kudai kwamba mwana alizaliwa na Mungu kupitia mwanadamu. Katika Aya ifuatayo Kurani Tukufu inalitangaza hili kuwa ni kosa kubwa. Hata hivyo hakuna adhabu ya kimwili ya aina yoyote imependekezwa wala mamlaka hayakukasimiwa

kwa mwanadamu yeyote kuadhibu matusi hayo dhidi ya Mungu.

مَا لَهُمْ بِهٖ مِنْ عِلْمٍ وَّلَا لِاٰبَآئِهِمْ ؕ كَبُرَتْ كَلِمَةً تَخْرُجُ مِنْ اَفْوَاهِهِمْ ؕ اِنْ يَّقُوْلُوْنَ اِلَّا كَذِبًا ۝٦

*Wao hawana elimu ya jambo hili, wala baba zao. Ni neno kubwa litokalo katika vinywa vyao; hawasemi ila uwongo tu.*[49]

Mwishowe hebu sasa nije kwenye eneo nyeti — nyeti zaidi kwa maana kwamba Waislamu wa leo wanaguswa zaidi na kejeli dhidi ya Mwanzilishi mtukufu[saw] wa Islam kuliko kejeli dhidi ya kingine chochote - hata Mungu.

Hata hivyo kuna tukio la kejeli nzito kiasi hiki kwamba limeandikwa katika Kurani Tukufu yenyewe, ambalo linamzungumzia ʻAbdullah bin Ubayy bin Saluul, ajulikanaye katika historia ya Islam kuwa ni kiongozi wa wanafiki. Siku moja wakirejea kutoka vitani, Abdullah bin Ubayy alitangaza mbele ya watu kwamba wafikapo Madina mbora zaidi wa watu atamfukuza mdhalilifu zaidi miongoni mwa watu wa Madina.

يَقُوْلُوْنَ لَئِنْ رَّجَعْنَآ اِلَى الْمَدِيْنَةِ لَيُخْرِجَنَّ الْاَعَزُّ مِنْهَا الْاَذَلَّ ؕ وَ لِلّٰهِ الْعِزَّةُ وَ لِرَسُوْلِهٖ وَ لِلْمُؤْمِنِيْنَ وَ لٰكِنَّ الْمُنٰفِقِيْنَ لَا يَعْلَمُوْنَ ۝٩

*Wanasema: Tukirudi Madina, mwenye heshima atamfukuza mnyonge; na heshima hasa ni kwa Allah na kwa Mtume Wake na kwa waaminio; lakini wanafiki hawajui.*[50]

Kila mmoja alielewa tusi lililokusudiwa kwa Mtume Mtukufu[saw]. Walikuwa wanatatarika kwa jazba na hasira kiasi kwamba, kama wangeliruhusiwa wangelimpiga mapanga Abdullah bin Ubayy. Imeripotiwa kwa usahihi wa kutegemewa kwamba jazba zilikuwa juu sana katika tukio hili kiasi hiki si mtu mwingine bali mwana wa Abdullah bin Ubayy mwenyewe alimwendea mwanzilishi Mtukufu[saw] wa Islam kuomba ruhusa ya kumuua baba yake kwa mikono yake. Mwana huyu alitoa hoja kwamba ikiwa mtu mwingine yeyote angefanya hivyo, baadae kwa ujinga, yeye angeweza kujenga wazo la kujilipiza kisasi dhidi ya muuwaji wa baba yake. Kwa karne nyingi Waarabu walizoea kulipa kisasi hata kwa tusi dogo kabisa dhidi yao au ndugu zao wa karibu. Labda desturi hii ndiyo aliyokuwa nayo kichwani mwana huyo. Lakini Mtume Mtukufu[saw] alikataa kumpa ruhusa hiyo wala hakumruhusu yeyote mwingine miongoni mwa masahaba wake kumwadhibu mnafiki yule, Abdullah bin Ubayy, kwa namna yoyote ile iwayo.[51]

Baada ya kurejea Madina baada ya vita, Abdullah bin Ubayy aliendelea kuishi kwa amani. Alipofariki hatimaye, kifo cha kawaida, bila shaka, kwa mshangao wa kila mtu, Mtume Mtukufu[saw] alimpa mwana wa Abdullah shati lake mwenyewe ili aukafini mwili wa baba yake kwa ajili ya maziko - kitendo cha kipekee cha urehemevu, kwa hakika, ambacho ni lazima kiliwaacha masahaba wengine wakitamani kulinunua tendo hilo

kutoka kwa mwana huyo kwa gharama ya vitu vyote walivyokuwa navyo. Si hivyo tu, Mtume Mtukufu[saw] aliamua kuongoza sala yake ya jeneza. Tendo hili lazima liliwaumiza wengi wa masahaba zake ambao hawakuweza kamwe kumsamehe Abdullah bin Ubayy kwa kosa hilo kubwa lililotajwa hapo juu. Tena jukumu likamwangukia Umar[ra] ambaye baada ya Mtume[saw] akawa Khalifa wake wa Pili kutoa kauli kwa fadhaa yao waliyoizua nafsini.

Imeripotiwa kwamba Mtume Mtukufu[saw] alipokuwa akielekea kwenye mazishi, Umar[ra] ghafla alimpita mbele na kusimama njiani akimwomba Mtume[saw] kubadili uamuzi wake. Katika kufanya hivyo, Umar[ra] alimkumbusha Mtume[saw] juu ya aya ya Kurani Tukufu ambamo maelezo yametolewa juu ya mnafiki anayejulikana ambaye juu yake uombezi hautakubaliwa hata kama Mtume Mtukufu[saw] angemuombea mara sabini. Kusemwa hapa idadi ya sabini isichukuliwe kihalisi mno kwa sababu, kwa mujibu wa matumizi ya Waarabu, lilitumika tu kumaanisha idadi kubwa.

Hata hivyo, Mtume Mtukufu[saw] alitabasamu na akajibu: Kaa kando Umar. Najua vyema zaidi. Kama nikijua Mungu hatamsamehe hata niombe mara sabini, nitamuombea zaidi ya mara sabini. Kisha Mtume Mtukufu[saw] aliongoza sala ya jeneza.[52]

Hili ni karipio la kutosha kwa wale wanaolia mpaka sauti zinawakauka katika kudai kifo kwa mdhalilishaji

anaediriki kumtusi Mwanzilishi Mtukufu[saw] wa Islam na sio kingine chochote bali kifo. Dini kama hiyo lazima iwe na nafasi katika kuleta amani baina ya dini mbalimbali duniani.

## Ushirikiano Baina ya Dini Mbalimbali

Kuhusu ushirikiano baina ya dini mbalimbali, Islam inaenda hatua moja mbele zaidi kwa kutangaza:

وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَاٰنُ قَوْمٍ اَنْ صَدُّوْكُمْ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ اَنْ تَعْتَدُوْا ۘ وَ تَعَاوَنُوْا عَلَى الْبِرِّ وَ
التَّقْوٰى ۖ وَلَا تَعَاوَنُوْا عَلَى الْاِثْمِ وَ الْعُدْوَانِ ۖ وَاتَّقُوا اللّٰهَ ۗ اِنَّ اللّٰهَ شَدِيْدُ الْعِقَابِ ③

*Na uadui wa watu usiwashawishini kwa sababu waliwazuilieni Msikiti uliotukuzwa, ya kwamba mruke mipaka. Na saidianeni katika wema na utawa, wala msisaidiane katika dhambi na uasi. Na mcheni Allah; hakika Allah ni mkali wa kuadhibu.*[53]

Kurani Tukufu haiwaruhusu waislamu kuwatendea vibaya hata maadui wale ambao wamewahi kuwashambulia Waislamu kwa sababu ya chuki ya kidini.

Sasa tunageukia kundi la makafiri wale ambao hawakuwahi kushiriki katika mapambano dhidi ya Waislamu. Kuwahusu wao, waaminio wanaambiwa katika Kurani Tukufu:

عَسَى اللّٰهُ اَنْ يَّجْعَلَ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَ الَّذِيْنَ عَادَيْتُمْ مِّنْهُمْ مَّوَدَّةً ؕ وَاللّٰهُ قَدِيْرٌ ؕ وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ۝٨ لَا يَنْهٰىكُمُ اللّٰهُ عَنِ الَّذِيْنَ لَمْ يُقَاتِلُوْكُمْ فِى الدِّيْنِ وَلَمْ يُخْرِجُوْكُمْ مِّنْ دِيَارِكُمْ اَنْ تَبَرُّوْهُمْ وَتُقْسِطُوْۤا اِلَيْهِمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِيْنَ ۝٩

*Asaa Allah Akaweka mapenzi baina yenu na wale ambao mnawaona kuwa maadui miongoni mwao; na Allah ni Mwenye kudra; na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu. Allah Hawakatazeni wale ambao hawakupigana nanyi kwa ajili ya dini wala hawakuwafukuzeni katika nyumba zenu ya kwamba mwafanyie hisani na adili. Hakika Allah Huwapenda wafanyao uadilifu.*[54]

Waislamu wamefundishwa pia kuwaalika Watu wa Kitabu na kushirikiana nao katika kueneza ujumbe wa umoja wa Mungu - imani inayoshikiliwa na wao pia. Lengo la Aya ifuatayo hapa chini ni kutilia mkazo nukta ya mfanano na kuunda programu ya pamoja kwa faida ya binadamu badala ya kusisitiza maeneo ya tofauti za kiimani — jambo ambalo matokeo yake ni kuzua mizozo.

قُلْ يٰۤاَهْلَ الْكِتٰبِ تَعَالَوْا اِلٰى كَلِمَةٍ سَوَآءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ اَلَّا نَعْبُدَ اِلَّا اللّٰهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهٖ شَيْئًا وَّلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا اَرْبَابًا مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ ؕ فَاِنْ تَوَلَّوْا فَقُوْلُوا اشْهَدُوْا بِاَنَّا مُسْلِمُوْنَ ۝٦٥

*Sema: Enyi watu wa Kitabu, njooni kwenye neno lililo sawa baina yetu na baina yenu, ya kwamba tusimwabudu ye yote ila Allah, wala tusimshirikishe na cho chote, wala baadhi yetu isifanye wengine kuwa*

*waungu badala ya Allah; lakini wakigeuka, basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu.*[55]

## Hitimisho

Kabla ya kuangazia wajibu wowote wa maana ambao dini maarufu duniani zaweza kutimiza katika kumpatia amani mwanadamu katika maeneo yote ya shughuli za kibinadamu, ni muhimu sana kuchambua kiyakinifu nafasi ya dini (kwa ujumla wake) katika kuleta amani ndani ya madhehebu mbalimbali ya wafuasi wa dini hizo na vile vile kupima iwapo dini hizo — kwa kadiri zinavyobaki hai — zinaweza daima kujifunza kuishi kwa amani baina yao. Ikikadiriwa kutokana na ongezeko la athari ya hali ya kupenda mali na mhimili wa fikra katika jamii kuhama kutoka kuwa wa kiroho kuelekea kwenye matamanio na anasa za kimwili, mtu aweza kuelekezwa kuamini kwamba dini yapaswa kutupiliwa mbali na kupuuzwa kama jambo lisilo na maana.

Nasikitika kutokubaliana na hitimisho kama hilo kwa sababu kama hatukurekebisha mitazamo ya dini, kwa ndani na kwa nje, dini itaendelea kuchukua nafasi kubwa katika kuleta athari mbaya, badala ya njema, katika jitihada zetu za kufikia amani ya dunia. Dini ambayo ilipaswa kushika nafasi ya uongozi katika kuleta amani, kuondoa mizozo baina ya wafuasi wa madhehebu na dini mbalimbali, kustawisha ustaarabu, na kuhamasisha kanuni ya kuwa mvumilivu, kwa bahati mbaya katika zama hizi, imefanya juhudi kidogo mno,

na isiyoleta athari ya maana, kama imefanya chochote, katika kuhamasisha amani popote duniani. Lakini katika kuleta machafuko na umwagaji damu na kusababisha mateso na taabu, bado dini ni nguvu yenye makali na wepesi, ambayo haipaswi kubezwa. Amani duniani haiwezi kufikirika bila kutatua tatizo hili muhimu na kuziba mianya yake.

Kwa ndani, jazba za kidini zaweza kuamshwa kwa nguvu na kutiwa makali ya kueneza mateso na taabu dhidi ya dhehebu ndani ya dini hiyo hiyo, ambalo kwa bahati mbaya, ni dhehebu lenye wafuasi wachache ndani ya dini hiyo.

Historia yote ya Waislamu imejaa matukio mabaya na yasiyopendeza kama hayo ambamo Islam, dini ya amani, yenyewe ilitumika kuzima amani ya waaminio wasio na hatia, ambao, bila shaka waliamini Islam, lakini sio kwa namna na mtindo ambao wengine wangeutaka. Kwa hakika, utafiti wa historia ya Islam unathibitisha bila ya wingu la shaka kwamba Islam imetumika 'vibaya' katika kuwatesa Waislamu wenyewe. Vita vitakatifu ambavyo Waislamu wamepigana dhidi ya Wapiganaji wa Kikristo vimepitwa kwa mbali ki-idadi na kiuzito na 'vita vitakatifu' ambavyo Waislamu wamepigana dhidi ya Waislamu katika karne kumi na nne zilizopita.

Somo hilo bado halijafungwa. Kile kinachoendelea Pakistan dhidi ya Waislamu Waahmadiyya na sio mara

chache dhidi ya Washia walio wachache kinatosha kuleta jicho la umakini kwenye ukweli kwamba tatizo hili la 'kimbuai' ambalo lilipaswa kufa siku nyingi zilizopita bado linaishi hadi leo.

Katika Ukristo, mateso dhidi ya Wakristo kwa mikono ya Wakristo yaweza kuonekana ni kilio cha mbali kilichozikwa katika vumbi la historia ya Ulaya na Amerika, lakini utafiti wa magomvi ya kidini na kisiasa huko Ireland waonekana kuthibitisha vinginevyo. Vile vile kuna hatari zilizofichika za magomvi ya kimadhehebu ndani ya Ukristo wenyewe katika maeneo mengine ya dunia, ambayo kwa sasa yanashughulishwa na magomvi mengine na vita.

Katika mahusiano baina ya dini mbalimbali, machafuko baina ya Wahindu na Waislamu huko India, au Waislamu na Wakristo huko Nigeria au chuki baina ya Wayahudi na Waislamu huko Mashariki ya Kati na penginepo, na pia wimbi la chini kwa chini la uhusiano tete wa kisiasa na kiuchumi kati ya Wayahudi na Wakristo, ni alama chache za hatari zilizolala ambazo zipo kama volkano zilizolala ndani ya ardhi ya ulimwengu wa dini.

Umuhimu wa kurekebisha mitazamo juu ya matatizo kama haya hauwezi kupita kiasi katika kusisitizwa.

Kwa kuweka pamoja jawabu la Islam kuhusu namna gani matatizo kama haya yapaswa kutatuliwa, tunahitimisha kwa kuainisha kwamba:

1) Dini zote za ulimwengu, kama zinaamini Islam au la, lazima zikubaliane na kanuni ya msingi ya Islam ya kutotumia nguvu au msukosuko kwa namna yoyote kama nyenzo ya kutatua migogoro baina ya madhehebu na baina ya dini mbalimbali. Uchaguzi wa dini, uhuru wa kuhubiri, kueneza, kuabudu na kufuata, au kukataa au kuacha kuamini au kubadilisha imani ya mtu ni lazima ulindwe kabisa.

2) Hata kama dini nyingine haziwezi kukubaliana na dhana ya Islam ya kwamba ukweli ni wa ulimwengu mzima na hata kama kwa mfano, kwa mtazamo wa Uyahudi, Ukristo, Ubuddha, Ukonfusi, Uhindu, Uzoroarista, n.k., dini nyingine zote ni za uongo na hazina uhusiano wowote na Mungu, basi bila kujali kukataa huku kwa ukweli kwingineko, dini zote ni lazima zikubaliane na kanuni ya Islam ya kuonyesha heshima na unyenyekevu kwa waanzilishi na watu watakatifu wa dini zingine. Kwa kutekeleza hili, hawahitaji kuchujisha misingi ya imani zao. Ni suala tu la haki za msingi za binadamu. Haki ya kila mwanadamu kwamba hisia zake za kidini na mafungamano yake yasikiukwe na kukwazwa ni lazima itambuliwe.

3) Yapaswa ikumbukwe kwamba kanuni hiyo hapo juu haiwezi kusimamiwa na sheria za kitaifa au kimataifa. Yapaswa kueleweka kwa mfuatano na kanuni kwamba kukejeli hakuhitaji adhabu iliyoundwa na

binadamu lakini kwapaswa kupingwa na kukatazwa kwa kuhamasisha maoni ya watu dhidi yake kwa kulaani vitendo kama hivyo kwamba sio vya kistaarabu, vimekosa busara na vinachukiza.

4) Mikutano baina ya dini mbalimbali kwa utaratibu ulioletwa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya katika sehemu ya mwanzo mwa karne hii yapaswa kuhimizwa kwa mapana na kuhamasishwa. Roho na lengo la mikutano kama hiyo yaweza kuelezewa kwa sifa zifuatazo:

a) Wazungumzaji wote wahimizwe kuainisha nukta njema za sifa za kuvutia na za kipekee za dini zao bila kuzilaumu dini zingine.

b) Kwa dhati wazungumzaji wa dini fulani wanapaswa kwa uaminifu kujaribu kuona ubora wa sifa wa dini zingine, kuziongelea sifa hizo na kueleza kwa nini wamevutiwa nazo.

c) Wazungumzaji kutoka dini tofauti wapaswa kuusifu utukufu na sifa njema za viongozi wa dini nyingine. Kwa mfano, mzungumzaji wa Kiyahudi aweze kuongelea sifa maalum za Mtume Mtukufu Muhammad[saw] ambazo zaweza kukubalika na wanadamu wote bila kuchujisha imani za dini zao. Halikadhalika mzungumzaji Mwislamu aweza kumuongelea Krishna, mzungumzaji wa Kihindu akamuongelea Yesu Kristo, mzungumzaji Mbuddha akamuongelea Musa na kadhalika na kadhalika. Katika

muongo wa tatu wa karne hii mikutano kama hiyo ilifanywa na Jumuiya Ahmadiyya kwa faida kubwa na ikaendelea kupendwa katika kuboresha mahusiano baina ya wahindu na Waahmadiyya huko India.

d) Bila kutengua kilichopendekezwa katika (c) hapo juu, heshima ya majadiliano ya kidini lazima ilindwe baina ya madhehebu na baina ya dini mbali mbali. Kubadilishana maoni baina ya dini mbalimbali kusionekane kuwa ni majaribio ya kuhujumu amani ya kidini. Ni namna yanavyofanywa majadiliano, ambapo ikiwa potofu, yapaswa kulaaniwa na sio majadiliano yenyewe. Mtiririko huru wa mawazo ndio muhimu zaidi kati ya haki za msingi za binadamu, muhimu kwa ajili ya uzima kwa kilicho bora zaidi. Haitakiwi ihafifishwe kwa gharama yoyote ile.

e) Kupunguza maeneo ya tofauti na kupanua uwezekano wa makubaliano, ni muhimu sana kwamba dini zote zikubali kanuni ya kubakisha mijadala yao na wafuasi wa dini nyingine ndani ya mipaka ya vyanzo vya dini zao. Tangazo la Kurani kwamba dini zote ni sawa katika vyanzo vyao halipaswi kuchukuliwa kiwepesi. Ndani mwake kuna ulimwengu wa hekima, ambao wapaswa kuangaliwa na kutafitiwa na dini zote kwa faida zao wenyewe, vile vile kwa faida ya wanadamu wote kwa ujumla.

5) Ushirikiano katika mipango yote mizuri na mikakati kwa faida ya wanadamu wote lazima

uhamasishwe na kuhimizwa. Kwa mfano miradi ya kusaidia jamii yaweza kufanywa kwa ushirika baina ya Waislamu na Wakristo na Wahindu na Wayahudi, n.k.

Ni hapo tu ndipo tunaweza kuwa na tumaini la kufanikisha ndoto ya tangu kale ya watawa na wanafalsafa waliopita, yaani ndoto ya kuwaunganisha wanadamu wote chini ya bendera moja katika maeneo yote ya harakati za binadamu kama ziwe harakati za kidini, kijamii, kiuchumi na kisiasa na yote yale yenye umuhimu.

## Marejeo

[1] Sura 16: Al-Nahl: 37
[2] Sura 40: Al-Mu'min: 79
[3] Sura 35: Al-Fatir: 24–25
[4] Sura 2: Al-Baqarah: 286
[5] Sura 4: Al-Nisa': 151–153
[6] Sura 2: Al-Baqarah: 254
[7] Sura 4: Al-Nisa': 42
[8] Sura 33: Al-Ahzab: 41
[9] Lexicons of the Arabic language E.W. Lane, Aqrab al-Mawarid, Mufradat cha Imam Raghib, Fath na Zarqani
[10] Sura 5: Al-Ma'idah: 4
[11] Sura 15: Al-Hijr: 10
[12] Sura 85: Al-Buruj: 22–23
[13] Al-Bidaya wan Nihaya Libni Kathir, jal.1 uk.171
[14] Ibid. jal.1 uk.237, pia angalia Bukhari
[15] Sura 22: Al-Hajj: 68
[16] Sura 5: Al-Ma'idah: 70
[17] Sura 2: Al-Baqarah: 63
[18] Sura 5: Al-Ma'idah: 67
[19] Sura 3: Al-'Imran: 114–116
[20] Sura 7: Al-A'raf: 160
[21] Sura 7: Al-A'raf: 182
[22] Sura 98: Al-Bayyinah: 6
[23] Sura 30: Al-Rum: 31
[24] uk. xxvii Life of Mohamet cha Sir William Muir London, 1878
[25] Cha juu. uk. xxviii
[26] Prof. Noldeke in Encyclopaedia Britannica; toleao la 9 chini ya Kurani.
[27] Angalia Kurani Tukufu Sura 5:14–16

[28] Sura 61: Al-Saff: 10
[29] Sura 7: Al-A'raf: 159
[30] Sura 2: Al-Baqarah: 257
[31] Sura 88: Al-Ghashiyah: 22–23
[32] Sura 42: Al-Shura: 49
[33] Sura 16: Al-Nahl: 126
[34] Sura 23: Al-Mu'minun: 97
[35] Sura 103: Al-'Asr: 2–4
[36] Sura 90: Al-Balad: 18
[37] Sura 2: Al-Baqarah: 250
[38] Sura 58: Al-Mujadalah: 23
[39] Sura 8: Al-Anfal: 43
[40] Sura 2: Al-Baqarah: 112
[41] Sura 21: Al-Anbiya': 25
[42] Sura 28: Al-Qasas: 76
[43] Sura 37: Al-Saffat: 157–158
[44] Sura 2: Al-Baqarah: 206
[45] Sura 4: Al-Nisa': 141
[46] Sura 6: Al-An'am: 69
[47] Sura 6: Al-An'am: 109
[48] Sura 4: Al-Nisa': 157
[49] Sura 18: Al-Kahf: 6
[50] Sura 63: Al-Munafiqun: 9
[51] Imesimulia na Ibn Ishaq: Al-Sira tun Nabawiyya cha Ibn Hisham, jal. III; uk. 155
[52] Bukhari, Kitabul Jana'iz, Babul Kafani fil Kamisilladhi Yukaffu 'au la Yukaffu
[53] Sura 5: Al-Ma'idah: 3
[54] Sura 60: Al-Mumtahinah: 8–9
[55] Sura 3: Al-'Imran: 65

Kwa hakika Allah Anaamuru uadilifu, na hisani, na kuwapa (watu kama uwapavyo) ndugu; na Anakataza upujufu, na uovu, na uasi. Anawanasihini ili mpate kufahamu.

- Kurani Tukufu, 16:91

א

Jueni ya kwamba maisha ya dunia ni mchezo na upuuzi na pambo na kujifurahisha baina yenu, na tamaa ya kuzidiana katika mali na watoto. Mfano wake ni kama mvua ambayo huwafurahisha makafiri maotesho yake, kisha yanakauka na unayaona yenye rangi ya manjano, kisha yanakuwa yenye kuvunjika-vunjika; na katika Akhera ni adhabu kali na (pia) msamaha wa Allah na radhi (Yake); na maisha ya dunia siyo ila ni starehe idanganyayo.

- Kurani Tukufu, 57:21

# SURA YA PILI

# AMANI YA KIJAMII

SASA HEBU TULIGEUKIE SWALA LA DHIMA YA ISLAM katika kuleta amani ya kijamii katika jamii ya kisasa

**Utangamano wa Jamii ya Kisasa**

Kwa bahati mbaya dini inapoteza kwa kasi mashiko yake ya kimaadili katika jamii. Kufanya hali kuwa mbaya zaidi, harakati zinaendelea za kudai kwa nguvu uhuru dhidi ya faradhi za kidini, na zinapata msukumo kutoka karibu kila pembe ya dunia ya sasa. Ingawa, pia ipo khofu, inayotokana na hali inayoshamiri ya ukosefu wa amani na ufisadi katika mienendo ya kijamii, inayokwenda sambamba na mitindo ya kudharau amri za kidini na kimaadili. Imani juu ya Mungu Aliye Hai, Ambaye sio tu kwamba Ameandaa marejeo ya binadamu lakini pia Ambaye Ana Haki ya kuyapanga maisha yao ya kila siku yakaeje, imani hiyo inapotea kwa kasi.

Kurani Tukufu imetoa majumuisho ya hali hii kwa kusema:

ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ

*Ufisadi umedhihirika barani na baharini.*[1]

Ukristo, ikiwa ndio dini yenye nguvu katika nchi za Magharibi, ilikuwa na udhibiti na mashiko yenye ufanisi mpaka mwanzo mwanzo mwa karne hii, ikidhibiti maadili ya waumini wake katika nchi za Magharibi. Ni sikitiko, hali si hivyo tena kwa sasa.

Badala yake umeibuka ustaarabu unaotokana na athari za Ukomunisti, maendeleo ya kasi ya sayansi na ya kidunia kwa ujumla, yaliyoulazimisha Ukristo kurudi nyuma, hatua kwa hatua, na ukashika dhima ififiayo katika kujenga khulka za kijamii.

Kwa hiyo leo hii, maadili katika nchi za Magharibi kidogo au zaidi ni ya Kikristo kwa tabia yake kama ambavyo maadili katika nchi nyingi za Kiislamu ni ya Kiislamu. Kwa bahati mbaya hii ndiyo hali ya tabia za kijamii na kimaadili iliyopo sehemu zingine za dunia.

Kuna Wabudha, Wakomfusi na Wahindu wengi duniani leo hii, lakini kwa bahati mbaya ni kiasi kidogo sana kinachoweza kudhihirika cha Ubudha, Ukomfusi na Uhindu.

*Maji maji kotekote lakini hakuna hata tone la kunywa.*

Kama maadili ya kidini au kimila yanakosekana katika jamii, uadilifu utakuwa si kitu chenye maana kwa kizazi, ambacho si tena chenye kukubali kwa moyo mkunjufu urithi wa kimila kuwa ni mantiki na halali. Kizazi kama hicho ni lazima kitapitia katika kipindi nyeti cha mpito kisicho na kitu. Hii itapelekea kuzalika kwa haja ya

uchunguzi wa awali. Harakati za uchunguzi wa awali zinaweza au zisiweze kupelekea katika kuvumbua kanuni za kimaadili zilizo bora na zenye kuridhisha zaidi. Harakati hizo kwa upande mwingine zinaweza kuishia kwenye vurugu moja kwa moja au hali ya kuwa na utitiri wa maadili. Kwa bahati mbaya, kwa namna ninavyoyaona mambo, ni hali ya pili, inayoonekana kuwa ndiyo chaguo la jamii ya kisasa.

Upepo wa mabadiliko unavuma katika jamii zote za dunia, ziwe za Mashariki au Magharibi, za kidini au za kisekula. Ni upepo mchafu, unaochafua hali ya hewa ya dunia nzima.

Dunia ya sasa inaonekana kuwa inashika tahadhari na iko makini zaidi juu ya ongezeko la kiwango cha uchafuzi wa mazingira ya kidunia kuliko ongezeko la kasi la kiwango cha uchafuzi wa mazingira yetu ya kijamii.

Kurani Tukufu, bila shaka ikizungumzia kuhusu zama hizo, inatamka:

وَ الْعَصْرِ ۙ﴿۲﴾ اِنَّ الْاِنْسَانَ لَفِیْ خُسْرٍ ۙ﴿۳﴾ اِلَّا الَّذِیْنَ اٰمَنُوْا وَ عَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ وَ تَوَاصَوْا بِالْحَقِّ ۙ۬ وَ تَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ ﴿۴﴾

*Tunaleta ushahidi wa zama zile ambapo binadamu watakuwa katika hasara, isipokuwa wale wachache walioamini na kufanya matendo mema na kwa ukweli wakahimiza wengine kuukubali ukweli na kwa subira wakahimiza wengine kuwa na subira.*[2]

Unyonyaji, undumakuwili, unafiki, ubinafsi, ukandamizaji, uchoyo, wehu wa kutafuta starehe, utovu wa adabu, rushwa, wizi, ujambazi, uvunjaji wa haki za binadamu, ulaghai, udanganyifu, ukosefu wa uwajibikaji na ukosefu wa kuheshimiana na kuaminiana vimekuwa ndio chapa ya jamii ya kisasa. Kibao vene cha uzunguzungu hakiwezi tena kuficha uhunde unaozidi na kuzidi kuwa bayana. Lakini hata hivyo itakuwa ni kosa kusema kwamba ishara hizi za kutisha za kushindwa ubinadamu zilikuwa hazipo katika zama zilizopita. Kwa kweli, staarabu nyingi za zamani pia ziliugua uele wa aina hiyo hiyo kabla enzi zao katika kitabu cha historia ya binadamu hatimaye kufungwa. Itakuwa ni kosa kunyooshea kidole eneo lolote makhususi la dunia, kwamba ndilo limezongwa na maadili maovu.

Jamii zinaanza kumong'onyoka kwa namna moja kila pahali. Kinyume na nchi zinazotawaliwa na falsafa za kiimla, katika zile zinazoitwa dunia huru kuongezeka kwenyewe kwa utambuzi wa uhuru binafsi kunakuwa ni mwelekeo unaokengeuka, ambao kwa kiasi kikubwa unahusika na kukua kwa tabia mbaya katika jamii.

Katika nchi zinazotawaliwa na falsafa za kiimla, kukua huku endelevu kwa utambuzi wa uhuru wa mtu binafsi kwa sasa kunakabiliana na mapambano makali ya ukombozi wa mtu binafsi kutoka kwenye udhibiti kamili wa kiimla. Isipokuwa tu kama kutakuwa na muinuko

mkali wa kupinga mapinduzi kutoka kwa majeshi yenye nguvu ya mrengo wa kushoto, mwelekeo huu wa kudai uhuru zaidi una kila uwezekano wa kushinda vita hivi punde. Kinachoweza kutokea baada ya hapo hakibashiri mazuri kwa matarajio ya maadili ya vijana waliokombolewa wa nchi zilizokuwa za kikomunisti.

Karibu vizazi viwili vimefikia utu uzima vikiwa katika upweke wa jamii isiyomhamu Mungu, wakiwa hawana chochote cha kuwaongoza na kuadabisha mwenendo wa kimaadili. Mbali na ukosefu wa maadili yaliyojengwa kutoka kwenye itikadi za kidini, kuna hatari ya mienendo ya mwelekeo wa ovyo, kupenda michezo ya starehe na kutowajibika inayofurika kutoka nchi za Magharibi ikiwakumba vijana wa USSR na Ulaya Mashariki, inayoweza kuleta matokeo ya kuteketeza mienendo yao ya kimaadili kwa miaka mingi ijayo.

Wakati huo huo, mtu hawezi kushindwa kuona kuwa tajriba ya kuishi bila ya dini kwa miongo mingi sio tu kwamba imerithisha ubaya kwenye jamii ya kisasa lakini pia imebainisha baadhi ya faida. Mapinduzi ya kisoshalisti ya Urusi yalikata maungano ya dunia ya kisoshalisti sio tu na dini bali pia na imani za kidini na mitazamo iliyogeuzwa na kupotoshwa. Uwe Ukristo au Uislamu, liwe dhehebu lolote la Wakristo au Waislamu, kuliingizwa fikra za karne zilizopita falsafa za mafundisho ya dini zao, fikra ambazo zilileta katika maeneo mengi ya imani, kupingana kati ya itikadi za

kidini na uhalisia wa kimaumbile. Itikadi za kidini na uhalisia wa kimaumbile havingeweza vyote kuwa sahihi kwa wakati mmoja. Ilichukua kipindi maalum cha mafunzo ya kiakili ili kuweza kuona mapungufu ya mawazo ya kidini na uhalisia wa kimaumbile lakini bado mtu akawa katika hali ya utulivu. Pengine kuishi na mafumbo sio rahisi isipokuwa kama mafumbo hayo yamezalika kizazi baada ya kizazi.

Kidogokidogo, unafikia wakati ambapo jumuiya za kidini kwa namna fulani zinaweza kuishi na mafumbo hayo bila kujua kama yapo.

Pamoja na mambo mengine, kilichofanywa na mapinduzi ya kisoshalisti kwa watu wao ni kuwatakasa dhidi ya mafumbo ya kiitikadi na kuwaponya na makengeza na mayopia.

Matokeo yake, hili limewapa aina fulani ya umaasumu, ambao unaweza kupatikana tu kama hakuna hata chembe ya unafiki. Ni mapema mno kusema kwamba hali hii ya umaasumu inaweza kuwa ni yenye faida kimaadili katika kipindi kigumu kijacho cha mapambano. Lakini jambo moja ni la uhakika kwamba watu hawa ni wasikivu na wanaweza kupokea ujumbe wa haki na kuukubali bila ya chuki kuliko watu wengine wowote duniani leo hii.

Nasikitika kwamba hayo hayawezi kusemwa kuhusu kuongezeka kwa mienendo ya ubinafsi katika wale wanaoitwa watu "huru" wanaoishi duniani leo hii.

Kimsingi mtu anaweza kufanya chochote kwa kujihalalishia uhuru kujiamulia atakavyo. Wakiwa viongozi katika mwenendo huu, Marekani kwa kiasi kikubwa inaathiri sio tu nchi za Dunia ya Kwanza za Ulaya bali hata jamii za watu wa Dunia ya Pili na ya Tatu. Mwangwi wa dhana iliyoharibiwa ya uhuru binafsi inayomfanya mtu atoke nje ya nidhamu ya maisha ya kimaadili unasikika kutoka mbali ukikatiza mapazia ya itikadi za kijamaa.

Mashoga, wasagaji, mateja, wanyoa vipara, wanyoao mapanki, na wahalifu wa aina zote, wote wanazidi kuongezeka kwa idadi na nguvu. Ujasiri wa kutetea tabia zao kwa kumuuliza tu awaonyaye, "Kwa nini isiwe hivyo" imekuwa ni changamoto mbaya katika jamii ya kisasa.

## Hali Mbili za Utaratibu wa Kijamii

Kurani Tukufu inaelezea hali mbili za jamii:

1. Ya kwanza ni ile ambayo uovu uko huru kuenea, na
2. Nyingine ni ambayo kukua kwa uovu kume-zuiliwa kabisa.

Kama vichukuliwe vipande vipande vya mafundisho ya maadili ya Kiislam, itakuwa vigumu sana kwa fikra za ki-Magharibi kuelewa falsafa za Ujumbe wake. Hii ni kwa sababu mafundisho ya maadili ni lazima yatizamwe kama sehemu za mazingira ya kijamii. Mtu ayatizame

kwa ujumla. Huwezi kuuelewa msimu wa kupukutika majani kwa kuyaangalia tu majani makavu yaliyoanguka au baadhi ya majani yakibadilika rangi. Mtu ni lazima achunguze kwa makini na ahisi hali yote ya hewa na mwenendo wa majira hayo ili aweze kujua majira ya kupukutika majani yako vipi na ni kwa namna gani yanaathiri maisha ya mimea. Halikadhalika, si busara kuamua jambo kutokana na tukio moja. Wakati ambapo majira ya kupukutika majani yanakatisha tamaa, majira ya kuchipua majani yanaleta matumaini ya maisha. Siyo tu swala la kubadilika kwa hali ya joto bali ni mabadiliko mazima ya hali ya hewa ambapo hata upepo peke yake unapuliza kuleta maisha. Mifumo ya kijamii nayo pia ni kama majira mbalimbali ya mwaka yakiambatana na sifa na athari zake.

## Upuuzi wa Jamii Yenye Kupenda Mali na Mwisho Wake

Islam inaelezea somo hili kwa namna hiyo hiyo kabisa. Kwanza, acha nielezee jamii, ambayo kwa mujibu wa Kurani, siyo ya Kiislam.

اِعْلَمُوْٓا اَنَّمَا الْحَيٰوةُ الدُّنْيَا لَعِبٌ وَّ لَهْوٌ وَّ زِيْنَةٌ وَّ تَفَاخُرٌۢ بَيْنَكُمْ وَ تَكَاثُرٌ فِى الْاَمْوَالِ وَالْاَوْلَادِ ؕ
كَمَثَلِ غَيْثٍ اَعْجَبَ الْكُفَّارَ نَبَاتُهٗ ثُمَّ يَهِيْجُ فَتَرٰىهُ مُصْفَرًّا ثُمَّ يَكُوْنُ حُطَامًا ؕ وَ فِى الْاٰخِرَةِ
عَذَابٌ شَدِيْدٌ ۙ وَّ مَغْفِرَةٌ مِّنَ اللّٰهِ وَ رِضْوَانٌ ؕ وَ مَا الْحَيٰوةُ الدُّنْيَآ اِلَّا مَتَاعُ الْغُرُوْرِ ﴿٢١﴾

*Jueni ya kwamba maisha ya dunia ni mchezo na upuuzi na pambo na kujifurahisha baina yenu, na tamaa ya kuzidiana katika mali na watoto. Mfano wake ni kama*

*mvua ambayo huwafurahisha wakulima maotesho yake, kisha yanakauka na unayaona yenye rangi ya manjano, kisha yanakuwa yenye kuvunjika-vunjika; na katika Akhera ni adhabu kali na (pia) msamaha wa Mwenyezi Mungu na radhi (Yake); na maisha ya dunia siyo ila ni starehe idanganyayo.*[3]

Tena, ikirejea upuuzi wa maisha ya kidunia, Kurani Tukufu inalo hili la kusema:

وَالَّذِينَ كَفَرُوٓا أَعْمَالُهُمْ كَسَرَابٍۭ بِقِيعَةٍ يَحْسَبُهُ الظَّمْـَٔانُ مَآءً حَتّٰىٓ إِذَا جَآءَهُۥ لَمْ يَجِدْهُ شَيْـًٔا وَّ
وَجَدَ اللّٰهَ عِنْدَهُۥ فَوَفّٰىهُ حِسَابَهُۥ ۗ وَاللّٰهُ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٣٩﴾

*Na wale waliokufuru, vitendo vyao ni kama mazigazi jangwani, mwenye kiu huyadhani ni maji; hata ayafikiapo hapati cho chote, na humkuta Mwenyezi Mungu hapo, naye Humpa hesabu yake sawasawa; na Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhesabu.*[4]

Kurani Tukufu inalisawiri hili kama mazigazi ambayo yanamtamanisha bure mtu mwenye kiu kwa kuendelea kwenda mbali mpaka anakuwa amechoka kabisa kiasi kwamba hawezi tena kuyafuatilia. Hapo ndipo anapopata adhabu. Anafanywa atambue kuwa hilo ni lengo batili lisilo na chochote, alilokuwa akilifuatilia njia yote. Ghafla, mazigazi yanasimama ili kumpa fursa ya kuzoea hali ile kwa ajili tu ya kumfanya aelewe maana chungu ya kufuatilia kisichokuwepo. Hiyo ndiyo adhabu waliyopimiwa wale wanaofuata upuuzi katika

maisha, na kwamba sawa na Kurani Tukufu, ndivyo jamii zote za aina hiyo zinapoishia.

Kinyume na hivi, dini inafundisha itikadi inayosema kwamba maisha katika dunia hii sio lengo kuu la kila kitu bali kuna maisha yajayo huko akhera.

Kama hatufi kifo cha moja kwa moja hapa bali tunaendelea kuishi kwa namna moja au nyingine, kama ambavyo Islam na dini nyingi nyingine zinavyotuaminisha; kama maisha duniani hayawezi kuchukuliwa peke yake kwa kuacha maisha ya Akhera; na kama maisha yote yanatakiwa yaeleweke kuwa ni muendelezo wa maisha yaliyopita kwa yajayo, basi itakuwa si busara kabisa kupuuzia mchango wa athari za kijamii kwa mtu hapa duniani. Uovu, ushetani na mivuto isiyo na afya ni lazima itazaa roho isiyo na afya katika maisha yajayo.

## Kukataliwa kwa Maisha Yajayo

Hii sio sehemu ya kujadili kwa kina falsafa ya Islam kuhusu maisha baada ya kifo lakini itoshe tu hapa kutaja kwamba, kwa mujibu wa Islam, jinsi tunavyoishi hapa duniani inaathiri roho zetu kama vile wakati mwingine, baadhi ya magonjwa ya mama mjamzito yanavyomuathiri mtoto wake angali tumboni. Mtoto anaweza kuwa na ulemavu wa kuzaliwa nao kiasi kwamba unakuwa ni jahanamu kwake kuishi na ulemavu wake akiwa miongoni mwa watoto wenye afya akiwa katika hali ya kutojiweza. Uchungu utakuwa

mkali zaidi na wa kina kadiri hisia zake zinavyobaleghe. Kwa ufupi, hivi ndivyo tunavyojijengea pepo au jahanam yetu kwa mujibu wa Islam.

Kwa muktadha huu, ni bayana kwamba mfumo wowote wa kijamii, unaojenga tabia za kutowajibika, vurugu na ushetani ni lazima ukataliwe bila kujali una mvuto au ushawishi kiasi gani kwa mtazamaji wa juu juu.

Ni sawa kwa waaminio kuyasema mambo haya na kuyatolea madai kama walivyo wengine wenye mtazamo wa kidunia. Hata hivyo, ni nani aliyerudi kutoka huko kunakoitwa akhera ili kuthibitisha au kuyapinga madai hayo? Kwa nini usiridhike na ndege uliye naye mkononi utake kubadilisha na wawili walioko porini? Hili ndilo jibu la watu wa kidunia kwa falsafa ya Islam kuhusu ni jinsi gani jamii itengenezwe na upi uwe msingi wa kanuni zake.

Falsafa ya Islam inayazunguka maisha katika dunia hii na maisha ya Akhera kuwa ni mtiririko wa maisha endelevu uliokatizwa kwa muda tu na kifo, ambacho, kwa hakika, ni kipindi tu cha mabadiliko kutoka maisha ya aina moja kwenda nyingine. Kwa kupingana na hilo, falsafa ya watu wa kidunia inayaona maisha kuwa ni fahamu tu ya muda mfupi iliyokuja bila utaratibu, ambayo inatoweka wakati wa kifo. Kwa hiyo, mfumo wa kijamii unahitaji tu kutosheleza mahitaji yanayohusiana na kipindi hiki kifupi cha maisha. Mtu anawajibika kwa jamii wakati tu akiwa hai na kwa kile kipengele tu cha

maisha kionekanacho na kung'amulika; kile ambacho kimefichika kwa namna ya mawazo yake, nia, mipango, njama na makosa ya kijinai yanayotendeka bila kugundulika kirahisi, vinabaki having'amuliwi na haviulizwi.

Tena, makosa ya jinai humtia mtu hatiani pale tu kunapokuwepo na ushahidi usio na shaka yoyote kwamba kosa limetendeka. Kuna uwezekano wa haki kutotendeka. Katika taratibu kama hiyo ya kijamii utoaji wa haki sio tu ni wa kubabiababia na wenye mapungufu bali unatengeneza mazingira ya kusaidia utendekaji wa makosa kwa jamii. Unahimiza matendo yenye maslahi binafsi, kuhamasisha uchoyo wa hali ya juu kwa mtu husika.

Inavutia pia kuona kwamba katika jamii isiyomjua Mungu au inayomjua kinusunusu ambapo dhana ya kuwajibika baada ya kifo inakataliwa kabisa au inachukuliwa kiwepesiwepesi na kimashakamashaka kiasi cha kuifanya ionekane haina maana, ni vigumu sana kupata fasili ya jinai, ambayo inaungwa mkono kikamilifu katika falsafa thabiti za kimaadili. Ni vigumu sana kuwaza kwamba watu wa jamii isiyomwamini Mungu wataridhika kwa dhati kuhusu makosa wanayoyafanya wakati wanavunja sheria fulani. Kwani, sheria ni nini? Je, ni neno la mtawala dikteta mwenye amri zote, ni uamuzi wa serikali ya chama kimoja au ni amri za kidemokrasia za walio wengi? Kwa mtu wa

kawaida, ni ipi kati ya hizo itakayokuwa ni sheria ya haki kwa msingi wa falsafa thabiti za kimaadili? Ni aina gani hii ya falsafa ya kimaadili?

Kama hamuoni yeyote kuwa ndiye aliyemuumba, au kama hana khofu yoyote ya kuulizwa huko Akhera kuhusu matendo yake ya hapa duniani, kwa kuwa, sawa na anavyoona, hakuna maisha ya Akhera, basi majibu kwa maswali yaliyoulizwa hapo juu, kwa kuangalia faida yake, yatakuwa tofauti kabisa na mahitajio ya jamii inayowajibika. Kwake yeye maisha ni haya mafupi tu na anaihitaji jamii kwa ajili ya faida yake binafsi tu. Anatii viongozi wa juu wa jamii kwa kulazimika tu. Kama anaweza kutoroka akiwa amejipatia faida fulani na akapata muda kidogo wa kujistarehesha hapa na pale huku akitumia ujanja wake asijulikane, kwa nini asifanye hivyo? Ni katazo lipi la 'kimaadili' litakalozuia mkono wake?

Mtizamo huu wa kisaikolojia kuhusu makosa ya jinai unaanza kujengeka na unakuwa na nguvu kadiri muda unavyopita katika jamii zisizoamini Mungu na za kiyakinifu.

Hili limetajwa hasa kwenye Kurani Tukufu kuwa ndio kiini cha jamii yakinifu.

Makafiri wanadai:

إِنْ هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا نَمُوتُ وَنَحْيَا وَمَا نَحْنُ بِمَبْعُوثِينَ ﴿٣٧﴾

*Ni hapa hapa tu ndipo tunapoishi maisha yetu. Tunakufa hapa hapa na tunaishi hapa hapa, na kamwe hatutafufuliwa tena.*[5]

(yaani tunakataa dhana ya maisha baada ya kifo au maisha sehemu nyingine).

Kisha, tena, makafiri kwa dhihaka waliwaambia Mitume[as] wa zamani kwa kuwauliza:

وَقَالُوٓا۟ ءَإِذَا كُنَّا عِظَـٰمًا وَرُفَـٰتًا أَءِنَّا لَمَبْعُوثُونَ خَلْقًا جَدِيدًا ﴿٥٠﴾

*Na wakasema: Je, tutakapokuwa mifupa na chembe zilizosagika, je, tutafufuliwa kuwa viumbe wapya?*[6]

قَالُوٓا۟ أَءِذَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا وَعِظَـٰمًا أَءِنَّا لَمَبْعُوثُونَ ﴿٨٣﴾

*Wanasema: Je, Tutakapokufa na tukawa udongo na mifupa, je, tutafufuliwa?*[7]

Hii, sawa na Kurani Tukufu, ndio sababu kuu ya uovu wote katika jamii yakinifu. Na ndio sababu msisitizo mkubwa umewekwa kwa maisha ya Akhera na kwa siku ya Hesabu.

Katika moja ya Hadithi, Ibn Mas'uud[ra] anasimulia kwamba Mtume Mtukufu[saw] alichora mstatili na katikati yake akachora msitari sambamba na urefu wa mstatili na sehemu yake ya juu ikazidi mstatili. Akachora mistari kadhaa mifupifupi inayokata ule wa katikati. Akaonyesa kwamba mchoro huo unawakilisha mtu, mstatili unawakilisha kifo, mstari wa kati unawakilisha tamaa zake na mistari mifupi inayoukata inawakilisha mitihani

na majonzi maishani. Akasema: Kama mmoja kati ya hii ukimkosa, mwingine utampata,"[8]. Katika Hadithi nyingine, kifo kimeelezwa kuwa ndicho kinachokatiza starehe.[9]

## Sifa Nne Bainifu za Jamii Yakinifu

مَا سَلَكَكُمْ فِي سَقَرَ ﴿٤٢﴾ قَالُوا لَمْ نَكُ مِنَ الْمُصَلِّينَ ﴿٤٣﴾ وَلَمْ نَكُ نُطْعِمُ الْمِسْكِينَ ﴿٤٤﴾ وَكُنَّا نَخُوضُ
مَعَ الْخَائِضِينَ ﴿٤٥﴾ وَكُنَّا نُكَذِّبُ بِيَوْمِ الدِّينِ ﴿٤٦﴾

*Na nini kilichowapelekeni katika 'saqar'? Watasema: Hatukuwa miongoni mwa wanaosali, wala hatukuwa tukilisha maskini, na tulikuwa tukipiga porojo pamoja na wapigao porojo, na tulikuwa tukikadhibisha Siku ya hukumu,*[10]

Sifa za jamii isiyomwamini Mungu na yakinifu zisingeweza kujumuishwa kwa usahihi zaidi na kwa kueleweka zaidi. Hizo ni:

1. Kushindwa kufanya ibada
2. Kushindwa kulisha maskini
3. Kujikita katika kusaka mambo yasiyofaa
4. Kukataa Siku ya Hesabu ya kuwajibika.

Kabla ya kuendelea zaidi, acha tuondoe mkanganyiko mmoja, ambao unaifanya iwe vigumu kuiagua hali ya jamii. Hata katika jamii ambako imani ya Mungu inaonekana kuwa yenye nguvu na maarufu na imani ya Akhera ni sehemu muhimu ya imani yao, maovu

yanashamiri ambayo kimantiki hayawezi kufikiriwa kuwepo miongoni mwa wanaomuamini Mungu na maisha ya Akhera wakiwa wanawajibika kikamilifu.

Hapo swali linazuka kwamba kwa nini jamii kama hizo zinamuamini Mungu na Akhera, lakini bado sifa zao nyingine zinabaki kuwa ni jamii zinazopenda mali kwa kila hali? Jibu la swali hili siyo gumu kulipata pale tunapochunguza kwa kina asili ya imani. Kwa hakika, kuwa tu na imani ya mbali ya kuwepo kwa Mungu hakuwezi kuathiri tabia ya kijamii ya muaminio wa aina hiyo. Hii ni kutokana na ukweli kwamba imani za aina hiyo kiasili ni za kinadharia tu na kamwe haziwezi kumbadilisha mtu awe na tabia ya kuwajibika ya kiuchamungu. Inawezekanaje imani ya kweli ya Mungu ichanganyikane na uwongo, udanganyifu, uchoyo uliokithiri, kupora haki za wengine, rushwa na ukatili? Dhana ya Mungu katika jamii za aina hiyo ni kama urembo tu, haina uhalisia kabisa na haiwezi kusaidia chochote huko Akhera, na uwajibikaji unakuwa ni jambo lililopakazwa tu lisilowezekana kutendeka. Kila mara chaguo linapokuja, utaona matamanio aliyonayo mtu daima ndiyo yanayopewa kipaumbele yakisogeza mbali khofu yoyote ya Akhera.

Tunapozungumzia jamii yakinifu, hatumaanishi tu jamii ambazo kwa uwazi kabisa zinakana uwepo wa Mungu na maisha baada ya kifo. Jamii nyingi zinazoamini Mungu na zisizoamini Mungu zinaweza kuonekana

kutofautiana kabisa kiitikadi, lakini, matendo yao yote yakawa yanafanana sana.

**Uwajibikaji**

Kurani Tukufu, kwa upande mwingine, inasema:

لِّلَّهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَإِن تُبْدُوا مَا فِي أَنفُسِكُمْ أَوْ تُخْفُوهُ يُحَاسِبْكُم بِهِ اللَّهُ ۖ
فَيَغْفِرُ لِمَن يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَن يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٨٥﴾

*Vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini ni vya Allah; na kama mkidhihirisha yaliyomo katika mioyo yenu, au mkiyaficha, Allah Atawatakeni hesabu ya hayo; kisha Amsamehe Amtakaye, na Amwadhibu Amtakaye; na Allah ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.*[11]

Kurani Tukufu inaongezea:

وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ ۚ إِنَّ السَّمْعَ وَالْبَصَرَ وَالْفُؤَادَ كُلُّ أُولَٰئِكَ كَانَ عَنْهُ مَسْئُولًا ﴿٣٧﴾

*Wala usifuate usiyo na elimu nayo. Hakika masikio na macho na moyo - hivyo vyote vitaulizwa.*[12]

Hapa, kwa kutaja moyo, Kurani Tukufu inamaanisha msukumo wa msingi wa maisha ambao unasababisha kila tendo alifanyalo mtu. *Fu'aad*, katika Kurani Tukufu, ina maana ya ule utashi wa mtu wa msingi uamuao ambao unauendesha ubongo kama vile mtu aiendeshavyo kompyuta. Kwa maana kwamba utashi wa msingi ndio chanzo cha uovu wote na wema wote na ni utashi huo katika sura ya maisha mapya baada ya kifo ambao, kwa pamoja na sikio na macho, vitawajibika.

Hebu sasa tuzichunguze kimakini zaidi sifa bainifu za jamii zisizoamini Mungu. Huwa inatokea kwamba kukana uwepo wa Mungu na kutoamini Akhera vinabaki visivyo wazi, si dhahiri na visivyogundulika katika hali ya kujitambua nusunusu. Kiimani, mtu anaweza kuendelea kidhahiri kuamini uwepo wa Mungu na Akhera, lakini kwa hali zote za kimatendo, inaonekana imani hizo hazipo. Wakati mwingine inakuwa ni vigumu kuleta uhalisia huu uliojificha kwenye ufahamu wa akili ya mtu. Wakati mwingine hata vizazi na vizazi vinaweza kuishi bila kutambua kikweli ugeugeu na wepesi wa imani zao. Ni katika nyakati hizo, ambapo ukanaji Mungu na kutoamini Akhera, ambako kulibaki hakugunduliki wala hakudadiswi, kunaanza kuibuka. Katika jamii ambazo tayari zimo katika utafutaji wa starehe bila kuchagua kwa busara wala kuweza kujizuia, ukanaji Mungu na Akhera wa makusudi unasababisha mmong'onyoko wa kimaadili na kupotoka ki khulka kwa kasi kubwa.

Muelekeo wa ustaarabu, haijalishi sehemu ipi ya dunia au zama gani katika historia ya binadamu, daima ni kutoka uduni kuelekea uungwana. Haja za msingi za nafsi, ambazo zinafanya kazi kama nguvu ya msingi iendeshayo tabia ya mtu, hizo zinabaki zilivyo, zisizoweza kubadilishwa. Kinachobadilika ni jinsi ya kuitikia haja hizo. Kwa mfano, njaa ya mtu inaweza kuitikiwa kwa kula nyama au mbogamboga. Ubora na ubichi wa nyama na mbogamboga unatofautiana. Mtu

anaweza akavila vikiwa vimepikwa na kuungwa kwa namna tofautitofauti au akavila vikiwa vibichi ikiwa amependa hivyo.

Kadri jamii inavyopata maendeleo, miitikio kwa haja za msingi inaanza kutokea na inakuwa ya kiungwana zaidi na ya kisasa. Hali hiyo inaendelea kusonga mbele, ingawa kasi yake inategemea kwa kiasi kikubwa hali za kiuchumi na kisiasa za watu. Lakini viongozi wa jamii daima wanaendelea mbele, wakati mwingine polepole, wakati mwingine kwa mwendo wa kasi.

Ustaarabu unapopevuka, usasa uliopindukia na baadhi ya hali zingine zenye kuleta hasara vinaanza kurudisha nyuma wimbi la muelekeo huu wa kupiga hatua. Katika jamii zinazoshuka kiwango, muelekeo huwa unarudi kinyume kutoka kwenye uungwana na kuwa duni. Hili ni somo lenye maana pana na linahitaji uchunguzi wa kina. Nasikitika kwamba ni nje ya uwanda wa hotuba ya leo lakini ningependa kuelezea kwa undani zaidi nukta chache.

Jamii zinapoanza kusawijika au kuhemewa au kwenda upande kutokana na usasa uliopindukia, wanaanza kuanguka chini na kurejea kwenye ile ile miitikio duni ya kihayawani ya haja zao. Hili linaweza likawa si lenye kuonekana katika kila shughuli ya kijamii na kiutamaduni, lakini daima linaonekana katika mahusiano ya watu na mitindo wakati wa kutafuta starehe. Uchunguzi mfupi wa binadamu katika muitikio

wake wa kujamiiana utabainisha suala linalozungumziwa. Kuhusu silika ya msingi ya kuzaana kwa njia ya kujamiiana, raha imewekwa kiasili kwa wanyama wote. Tunachokiona tofauti katika jamii ya mwanadamu ni kule kuhama taratibu kutoka kwenye kujitosheleza kwa haja hii tu na kuelekea kidogokidogo kwenye fikra za kistaarabu zaidi katika kutosheleza haja ya mwili. Asili kamwe haikuhitaji kujamiiana kuwa ndio lengo la msingi. Lengo la msingi daima limekuwa ni kuzaliana na kendeleza kizazi. Kujamiiana ilikuwa ni jambo lake la pili. Jamii zinapoharibika, dhima ni kama imegeuzwa kabisa.

Maendeleo ya hatua kwa hatua ya taratibu za ndoa, ada zihusikazo katika taratibu hii, na miiko kuhusu mahusiano kati ya wanawake na wanaume, inaweza kuchukuliwa na mwanasaikolojia kuwa hali zilizotokana na kukua kwa asili kwa jamii na hazihusiani na dini. Lakini, vyovyote iwavyo, kukua huko kuwe kumeongozwa kutokea juu au ni hali ya kibahati ijiendeshayo yenyewe, ukweli haupingiki kwamba polepole miitikio ya kukidhi haja ya msingi imekuwa ya kisasa zaidi na zaidi na migumu.

Kuwa na wenzi wengi wa kujamiana kunakoongezeka katika mahusiano ya wanaume na wanawake ni ishara tena ya maradhi hayo hayo. Si tu kwamba eti ni fikra huru za kimaendeleo kuhusiana na mahusiano ya kujamiiana lakini bila shaka kuna mengi zaidi

yanayokwenda na hilo ili kubadilisha mazingira ya eneo hili muhimu sana kwa shughuli na shauku ya mwanadamu. Majadiliano kuhusu uhalali au uharamu wa mahusiano ya aina hiyo yanapuuzwa kwa kuona ni mambo ya zamani. Bila shaka, yapo makundi mengi ya waaminifu yenye mrengo wa kidini ambayo bado yanaendelea kulijadili swala hili. Lakini wakati wa majadiliano yao kwenye vyombo vya habari mtu hawezi kushindwa kuona ya kwamba watu wa aina hiyo wa mitindo ya kizamani ambao mawazo yao yameng'ang'ania dini wanashushuliwa kuwa ni wachache wasio na maana.

Inakuwa zaidi katika nchi za Magharibi kwamba ni kwenda na wakati kulichukulia suala la kujamiiana kuwa ni haja ya kimaumbile ambayo ni lazima iitikiwe bila vizuizi. Utamaduni wa kuona haya unaombatana na mazungumzo miongoni mwa wanawake unakuwa ni kitu cha zamani. Kutembea uchi, kujidhihirisha, kujionyesha, mazungumzo yasiyo na aibu na kukiri maovu yanahesabiwa tu kuwa ni kuonyesha ukweli hadharani.

Hakuna mtu anayeonekana kubeba jukumu la kutumia hoja hiyo hiyo kwa ajili ya haja zingine za kimaumbile za mwanadamu. Je siyo haja ile ile ya kimaumbile aliyonayo mnyama, ambayo iko pia kwa binadamu ya kukipata kitu anachokipenda? Tena, siyo haja ya kimaumbile ya mnyama kukasirika na kuhamaki na

kuitema mihemuko hii kinyama kadiri iwezekanavyo? Mbwa dhaifu atasukumwa na haja zilezile kama za aliye na nguvu zaidi lakini wakati ambapo mbwa mwenye nguvu zaidi atang'ata, mbwa aliye dhaifu ataonesha hisia zake hizo angalau kwa kubweka.

Vipi kuhusu miiko mingine kwenye jamii — kanuni za tabia kuhusu raia, dhana ya adabu, nk, ambazo daima zinaingilia uonyeshaji wa haja za asili? Kwa nini ni lazima kujamiiana tu kuwe ndio msukumo ambao upewe leseni ya bure ya kujionyesha bila kujali utamaduni, kaida, adabu, kufaa na swala la udugu au vinginevyo? Tunachokiona leo ni tukio, ambalo ni lazima litambuliwe na kuchunguzwa kwa umakini. Tunachokiita rukhsa katika mahusiano ya kujamiiana kinafanyika kwa namna ya muelekeo unaokua wa kuiba na kupora kutoka maeneo mengine ya shughuli za binadamu, na kuumiza na kujeruhi wengine. Utafutaji wa raha usio na mipaka, wenye upotoshaji unaotokana na mielekeo ileile iliyooza ambayo inabomoa misingi imara tena sharifu ya ustaarabu na kurudisha taratibu za maisha kulekule zilikotoka.

Sio tu kwamba tunaona kuongezeka kwa wingi kwa ada, miiko na masharti wanayowekewa watu na jamii, lakini pia tunakuta kwamba hali za kujiingiza katika mapenzi na uchumba vinachangia dhima muhimu katika eneo hili. Ushairi, matangazo, sanaa, muziki, mitindo, fasheni, maonyesho, kupenda manukato, na kukua kwa tabia

njema zilizopatikana kwa malezi mazuri, yote hayo ni mazao ya haja hiyo hiyo ya msingi, kama sio yote basi angalau kwa kiasi fulani, zikiwa ndio miitikio ya jamii (kwa haja hiyo). Muda utafika ambapo kizazi kijacho kitaanza kuasi na kukataa mafanikio ya jamii yaliyopatikana baada ya maelfu ya miaka ya maendeleo. Uasi huu unaweza usichukue sura ya kukataa kabisa kila kitu. Lakini jicho lenye kumaizi haliwezi kushindwa kuona mwendo uelekeao huko. Kuasi mila na tamaduni, kutofuata desturi, ubakaji na kuongezeka kwa vurugu zinazonasibishwa na mapenzi na kurejea kwa tabia za kimapenzi kwenye hali yake ya asili, kihayawani na ovyo ovyo ni mifano michache ya kurudi nyuma kwa mitindo tulikokusema hapo kabla.

Mtu anaweza kufanya ujasiri wa kuangalia kundi la vijana waasi na wachafu wanavyoishi katika maskani zao ndipo atatambua nini kinachoendelea kwa kizazi kipya. Uchafu na harufu mbaya vinaonekana kuwa mbadala wa usafi na manukato. Mavazi nadhifu yameondoka na kufungua njia kwa nguo za midabwada zisizo na staha. Zama zimepita ambapo kukodolea macho mavazi ya mtu kwa dakika moja kulikuwa kunasababisha tahayari kubwa. Majinzi (suruali ngumu) yaliyochakaa, yaliyochanwa makusudi ili kuonyesha sehemu za mwili, yanakuwa na thamani kubwa zaidi kuliko suruali mpya. Bila shaka, sio jamii yote inayoonyesha kipeo cha ishara aina hiyo za kutoridhika na mambo ya zamani au urithi wa utamaduni, lakini

ugonjwa unapoingia, sio siku zote ambapo mwili mzima unapata madonda. Madonda machache yanatokea hapa na pale na haya ndiyo yanayodhihirisha ugonjwa au maradhi yaliyopo. Uzembe unaanza kushamiri. Utovu wa nidhamu na vurugu vinaanza kuwa matukio ya kila siku. Dalili nyingi za ukosefu wa maadili zinaanza kuibuka katika maeneo tofauti yanayopendwa na binadamu.

Utafutaji wa anasa katika nyanja zote za maisha unahitaji mabadiliko na ubunifu mpya ili kuleta msisimko mkubwa zaidi. Mambo yaliyokuwa yanawafanya watu waridhike hapo zamani, hayafanyi hivyo tena. Uvutaji wa sigara na vileo vya asili vinashindwa kuleta msisimko unaotakiwa na jamii yenye wahaka uongezekao. Madawa ya kulevya ya kila aina yanaanza kutokea na hakuna hatua yoyote iwayo inayochukuliwa kuzuia mwelekeo wa kutisha wa mateja inayoonekana kufaa. Na bado teja anataka msisimko mkubwa zaidi. Hivyo kitia wazimu, kilicho kama dawa ya kulevya chenye nguvu zaidi, chenye kumfanya mtu awe teja zaidi, na chenye kuua kimevumbuliwa kama vile kokeini iliyosafishwa iliyo na nguvu sana ya kulevya.

Katika nyanja za muziki, mielekeo ya aina hiyo hiyo aste aste imejengeka katika kipindi cha miongo michache iliyopita ya karne hii. Uchunguzi wa maendeleo ya muziki katika karne za hivi karibuni, sambamba na mapinduzi ya ghafla yaliyopatikana katika miongo

michache iliyopita ya karne hii, unatupatia takwimu za kufurahisha na za kuvutia sana kwa ajili ya malinganisho.

Binafsi, sijui sana kuhusu muziki na nisamehewe kama baadhi ya maoni yangu yataonekana ni mageni juu ya ukweli wa ulimwengu wa muziki. Hata hivyo hisia zangu zinanifanya niamini kwamba katika karne chache zilizopita maendeleo ya hatua kwa hatua ya muziki, katika nchi za Magharibi, yalikuwa katika muelekeo adhimu, mzuri sana na wenye heshima. Miziki ya aina hiyo ilileta utulivu wa moyo na akili kwa pamoja. Muziki bora kabisa ulikuwa ni ule uliojitambulisha na ukajizamisha kabisa kwenye muziki uliojificha ndani ya akili na roho ya binadamu. Utulivu na amani yalikuwa ndio malengo ya msingi yaliyosakwa katika ukuzaji wa muziki. Naam, kulikuwa na sehemu kadhaa katika kazi za watungaji na wasanii wakubwa wakubwa ambazo ziliumba taswira ya milipuko ya volkeno, vimbunga, radi na hisia za ghasia, ambavyo vililingana na hali za nje za asili. Kumbukumbu zake zilihifadhiwa na kutunzwa kwenye mitambo ya asili ya kuhifadhia zisiweze kufutika. Baadhi ya wakati, kilele chake kilifikia kelele kali kana kwamba ulimwengu mzima unataka kupasuka. Lakini hata hivyo wasikilizaji walikuwa hawachezi, wakijizamisha katika gharika ya muziki, bila kuchezesha hata msuli mmoja au kugongagonga kope za macho, mpaka ghafla ukimya kabisa unatokea. Ni hapo tu ndipo ukumbi mzima unalipuka kwa makofi mengi.

Hata muziki mkali namna gani, wenye hisia kali, ulikuwa haumfanyi msikilizaji kuwa na fujo, kulipuka na kuwa muasi. Ujumbe wa miziki yote ulikuwa na shani, amani na utananishi. Mazuri kabisa ya mtu yaliibuliwa na kuamshwa; mabaya yalifukuzwa.

Ni masikitiko kuwa katika kipindi cha miongo miwili iliyopita, tumeona hali tofauti kabisa. Masikio ya kizazi cha sasa yametiwa uziwi na muziki unaoweza kuleta hisia za maisha za kishenzi zisizoendelezwa. Kizazi kilichochanganyikiwa na kukosa utulivu kinajikuta kimeoanishwa tu na miziki ya aina hiyo inayowafanya wawe wehu. Muziki wa fujo zaidi ndio upendwao zaidi. Tena, ninaomba nisamehewe kwa jambo lolote ninaloliona linalotokana na kutokuwa kwangu na ujuzi wa ulimwengu wa muziki dhati na inayopendwa, lakini kwa kitu kimoja nina uhakika nacho ambacho ni kwamba vurugu, uasi, uchizi na uharabu n.k kwa kasi vinapotosha hisia adilifu za binadamu.

Profesa Bloom, ambaye anapaswa kuheshimiwa kwa elimu yake ya muziki wa Kimagharibi, anaonekana kukubaliana nami katika kitabu chake *The closing of the American Minds (Kufungwa kwa akili za Kimarekani)* pale aliposikitikia mmong'onyoko wa hisia za vijana wa kisasa ambao, kwa maneno yake mwenyewe, wanageuzwa kuwa mahayawani kwa kusikilizishwa daima miziki ya kurukaruka ambayo ameipuuza kuwa ni chakula kichafu kwa roho.

Kuna dalili zinazojionyesha dhahiri za hali hii ya ugonjwa katika jamii, ambayo hatua kwa hatua inayafanya maisha ya binadamu yachanganyikiwe zaidi na yasipate kinai, kutosheka, amani na utulivu. Mtu anaweza kukataa uwepo wa Mungu anavyopenda lakini hawezi kukataa uwepo wa asili yenye nguvu zote ambayo inajua vizuri sana jinsi ya kuadhibu makosa yanayotendwa dhidi yake.

Katika jamii zote yakinifu, vipengele vikuu vinavyohusika na makuzi endelevu na kuzaliana kwa maovu ni kama vinafanana. Baadhi ya mijadala imeshapita; hivyo tutaorodhesha kwa kifupi vipengele vinavyohusika kwa ajili ya ukumbusho. Vipengele hivi ni:

1. Kukua kwa imani ya kukana uwepo wa Mungu;

2. Kudhoofishwa kwa imani ya kweli ya Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu hasa Ambaye Ana shauku isiyokwisha juu ya masuala ya binadamu na namna watu wanavyojenga khulka zao.

3. Udhaifu endelevu katika kuamini utamaduni na maadili; na

4. Kuendelea kwa mwelekeo wa kuusahau mwisho na kuifanya njia ya kufikia mwisho kuwa ndio mwisho wenyewe.

Hii ndiyo hali inayopatikana katika hizo zinazoitwa jamii ‘zilizostaarabika’ au ‘zilizoendelea’ za duniani.

Taratibu, kadiri khulka na maadili yanavyoendelea kudidimia, wanaanza kuathiri utungaji wa sheria na utendaji wa serikali. Kama hakuna sheria zilizowekwa na Mungu zinazoweza kukubaliwa, na maadili na tamaduni sharifu zinapingwa na kukataliwa kila siku, sheria yoyote itakayowekwa kulinda nidhamu ya mienendo ya kimaadili nayo pia inakuwa sio kali na yenye kuendana nayo zaidi. Jukwaa ambalo linatumika kutunga sheria za kimaadili, linaanza kutelezea mbali.

Utafiti unaolinganisha hali ya utungaji sheria katika eneo hili kwa kipindi cha karne chache zilizopita utathibitisha kikamilifu suala linalozungumziwa. Zimeshapita zama za Oscar Wilde ambapo ushoga ulichukuliwa na jamii kuwa ni kosa, ambalo liliadhibiwa vikali bila huruma yoyote. Zimeishapita zama ambapo ubikira haukuwa tu ni jambo jema bali imani ya jamii, ambayo kama ikivunjwa, inakuwa ni kesi ya kujibu. Ulaini huu kwenye makosa hauonekani tena kuwa tishio. Hilo ndio tatizo.

Tafsiri ya kosa nayo inapata mabadiliko ya msingi. Lile lililoonekana kosa jana siyo hivyo tena. Lile lililokuwa linafunikwa kwa khofu ya aibu au kukemewa linafunuliwa na kuonyeshwa kwa ufahari mkubwa. Kama falsafa hii ingekuwa timamu na yenye kustahili kudumishwa basi falsafa zote za kidini, kimaadili na kikhulka zinaweza kuonekana kuwa zimepitwa na wakati na zisizotakiwa kwa kuwa hazisaidii chochote katika zama za sasa.

Msukumo wa kiasili, ambao unapatikana katika viumbe hai na visivyo hai, ni ile kanuni ya kilimwengu yenye nguvu ya kosa na adhabu na wema na tuzo. Katika viumbe visivyo na uhai, kanuni hii inaweza kutambulika kuwa inafanya kazi katika utendaji wa kanuni za asili zisizotambulika. Katika viumbe hai, mabadiliko ya polepole kabla ya kuumbwa mtu yalisukumwa na kanuni hiyo hiyo ambayo ilipata hali ya utambuzi nusu au ubwete nusu. Kadiri mtu anavyopanda vidato vya awali vya hatua za mabadiliko mpaka kuwa mtu, safari hiyo inaonekana kuwa ni kutoka utambuzi mdogo kuelekea utambuzi mkubwa. Katika istilahi ya mabadiliko, kanuni ya kosa na adhabu na wema na zawadi inaelezwa kuwa 'ataishi anayestahili.' Katika mwenendo mzima wa mabadiliko, huu ndio unabaki msukumo ambao daima unasukuma mabadiliko mbele na kuyapandisha juu.

Ni jambo la kushangaza kwamba wakati muendeleo huu umefikia ukamilifu wake kwa binadamu, ambaye ndiye kiumbe bora kuliko viumbe vyote, na uelewa na utambuzi umefikia nyanja za juu zaidi kuliko fikra shenzi na za kinyama; mara kanuni ya kosa na adhabu inatakiwa iondolewe na kuonekana imepitwa na wakati. Kama kuna lengo la juu zaidi ya uumbaji, lazima kuwe na uwajibikaji kiasi fulani ambapo bila huo zoezi zima litakuwa halina maana.

Inashangaza sana kwamba wakati mwingine wasomi wakubwa kabisa na wenye uwezo wa kuona mbali wanashindwa kuona ukweli wa wazi wenye ushahidi kama huu. Hiyo ndio hali ya Albert Einstein, muasisi wa nadharia ya uwiano wa mwendo, umbali na muda, anayesema:

> *Siwezi kumtafakari Mungu Ambaye Anatunuku na kuadhibu kitu alichokiumba yeye mwenyewe, ambaye matilaba yake ni mfano wetu — kwa kifupi, Mungu Ambaye siye ila ni akisio la udhaifu wa binadamu.*[13]

Kama kuna Mungu, Bwana Muumbaji Ambaye Uwepo wake Albert Einstein asingeweza kuukataa, na kama kanuni zote za kisayansi zinazofanya kazi kwa uumbaji Wake, zimebuniwa, kuumbwa na kutawaliwa na huyo huyo Mwenyezi, haiwaziki Kwake kuacha matlaba ya msingi ya uumbaji Wake kwa kuondoa kanuni ya kosa na adhabu na kumuacha binadamu atangetange katika vurumai za tabia zisizo na adabu na zisizowajibika.

Kuhusiana na sehemu ya pili ya wazo lake, ni dhahiri kwamba ameshindwa kuelewa sio tu dhima ya kosa na adhabu katika maendeleo endelevu ya uumbaji, lakini pia hakuelewa kabisa maana ya mtu kuwa *ameumbwa katika sura ya Mungu*.

Binadamu *ameumbwa katika sura ya Mungu* sio muradi wake kuwa ni umbo kamili la Mungu ardhini. Kama ingekuwa hivyo, dunia ingekuwa zaidi ya pepo ardhini na binadamu wote wangekuwa wanafanana kabisa. Ni

jambo la mjadala, bila shaka, kama sehemu hiyo ingestahili kuitwa pepo au choshi, ambapo hakuna mbadala, badiliko au tofauti kati ya harufu, maono na rangi — badala yake bahari iliyotulia iliyojaa tele yenye matone yanayofanana yasiyo na rangi. Huo sio mradi na madhumuni ya mtu kuwa *ameumbwa katika sura ya Mungu*.

Kirai hiki kimejaa busara ya kina na kinazungumzia kipawa ambacho kwacho binadamu amejaaliwa. kinazungumzia lengo lililo bora kabisa na la msingi ambalo binadamu ni lazima daima ajaribu kulipata. Lengo hilo ni kuwa safi kabisa kama mtu awezavyo kuwa, kwa kushika sifa za kiungu na kuibuka zaidi kama Mungu. Sio lengo lenye ukomo, ambalo mtu anaweza kulifikia na kisha kufurahia adhama ya kuwa sura ya Mungu, akiwa amebaki hapo. Kwa kuwa sifa za Mungu hazikomi au hazina mipaka, hivyo kila safari kumuelekea Yeye inabaki isiyo na kikomo. Ukamilifu katika muktadha huu una maana tu kusogea kutoka ukamilifu wa ngazi ya chini wa vitu kuelekea ukamilifu wa ngazi ya juu ya vitu.

Mungu ni Mkamilifu na Mwenye Haki kuliko wote, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu, Aonaye vyote, Ajuae kila kitu, Bwana Muumbaji na Mmiliki wa Siku ya Hukumu. Sifa zote njema zinamhusu Mungu. Kurani Tukufu inasema:

هُوَ اللّٰهُ الَّذِيْ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۚ عٰلِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ ۚ هُوَ الرَّحْمٰنُ الرَّحِيْمُ ﴿٢٣﴾ هُوَ اللّٰهُ الَّذِيْ لَآ اِلٰهَ
اِلَّا هُوَ ۚ اَلْمَلِكُ الْقُدُّوْسُ السَّلٰمُ الْمُؤْمِنُ الْمُهَيْمِنُ الْعَزِيْزُ الْجَبَّارُ الْمُتَكَبِّرُ ۗ سُبْحٰنَ اللّٰهِ عَمَّا
يُشْرِكُوْنَ ﴿٢٤﴾ هُوَ اللّٰهُ الْخَالِقُ الْبَارِئُ الْمُصَوِّرُ لَهُ الْاَسْمَآءُ الْحُسْنٰى ۗ يُسَبِّحُ لَهٗ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَ
الْاَرْضِ ۚ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ﴿٢٥﴾

*Yeye ndiye Allah Ambaye hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Yeye; Ajuaye yasiyoonekana na yanayoonekana; Yeye ndiye Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu. Yeye ndiye Allah, Ambaye hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Yeye; Mfalme, Mtakatifu, Mwenye salama, Mtoaji wa amani, Mwangaliaji, Mwenye shani, Jabbari, Mkubwa. Allah Yu mbali na hao wanaomshirikisha naye. Yeye ndiye Allah, Mwumbaji, Mtengenezaji, Mfanyaji wa sura; Mwenye majina mazuri; kinamtukuza kilichomo mbinguni na ardhini; naye ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.*[14]

Ni Mungu Huyo Ambaye ameumba ulimwengu huu. Hana madhaifu ya kibinadamu. Kurani Tukufu inawahimiza waaminio kutafakari Ishara Zake. Kwa mfano:

تَبٰرَكَ الَّذِيْ بِيَدِهِ الْمُلْكُ ۖ وَهُوَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرُ ﴿٢﴾ الَّذِيْ خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيٰوةَ لِيَبْلُوَكُمْ
اَيُّكُمْ اَحْسَنُ عَمَلًا ۗ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْغَفُوْرُ ﴿٣﴾ الَّذِيْ خَلَقَ سَبْعَ سَمٰوٰتٍ طِبَاقًا ۗ مَا تَرٰى فِيْ خَلْقِ
الرَّحْمٰنِ مِنْ تَفٰوُتٍ ۗ فَارْجِعِ الْبَصَرَ ۙ هَلْ تَرٰى مِنْ فُطُوْرٍ ﴿٤﴾ ثُمَّ ارْجِعِ الْبَصَرَ كَرَّتَيْنِ يَنْقَلِبْ
اِلَيْكَ الْبَصَرُ خَاسِئًا وَّهُوَ حَسِيْرٌ ﴿٥﴾

> *Mwenye mibaraka ni Yule Ambaye Mkononi Mwake umo ufalme, naye ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu, Ambaye Aliumba kifo na uzima ili kuwajaribuni, ni nani miongoni mwenu aliye bora kwa vitendo; naye ni Mwenye heshima, Mwenye kusamehe; Ambaye Aliumba mbingu saba zilizo tabaka-tabaka, huoni tofauti yo yote katika uumbaji wa Rahmani; basi rudisha macho, je unaona kosa? Tena rudisha macho mara kwa mara; mtazamo wako utakurudia hali ya mahangaiko na mchoko.*[15]

Baada ya kuelewa maana ya maneno *sura ya Mungu,* wakati mtu anapotafakari nguvu yote ya uumbaji wa ulimwengu — kutokea wakati wa Big Bang (*mlipuko mkubwa angani unaoaminika kuwa ndio chanzo cha ulimwengu- mfasiri*) mpaka leo hii — safari nzima ya uumbaji kutokea hali ya kutojitambua hadi kujitambua, kwa kweli, ni safari ya kuja kuwa *sura ya Mungu* na kuzalisha katika mtu sifa za kiungu.

## Hali ya Mazingira ya Jamii ya Kiislamu

Islam, kwa upande mwingine, inanuia kujenga hali ya mazingira ambayo ni tofauti na hiyo iliyoelezwa hapo juu, kama vile majira ya kuchipua yalivyo tofauti na majira ya kupukutika kwa majani. Katika dhana ya Kiislamu ya jamii, Islam inayawekea taratibu, nidhamu na kuyapunguza matamanio ya asili ambayo, yakiachwa bila kudhibitiwa, yanaweza kuleta maangamizi pale jazba ya binadamu inapofikia upeo. Islam inakataza au

kupiga marufuku kukidhi haja ambazo zinaweza, hatimae kuleta taabu kuliko raha katika jamii.

Wakati huo huo, Islam inakuza ladha mpya na kujenga uwezo wa kupata raha na utoshelevu kutokana na matendo ambayo yanaweza kuonekana yaso rangi, chapwa na yaso ladha kwa asostaarabika na asofunzwa. Ladha zinabadilishwa kidogo na tamaa ya anasa za kishenzi inapata mafunzo na kutakaswa na kugeuzwa kuwa kupata utawa.

Lakini swali ni jinsi gani tunaweza kupambanua kwamba mielekeo ya jamii iliyoenea na ya kisasa ina madhara kwa jamii? Binafsi yangu, jibu linaonekana kuwa ni jepesi. Afya ya jamii ni lazima itanzuliwe kwa dalili zile zile zenye ishara kwa afya ya mtu. Kama mtu akiwa na maumivu, mahangaiko, mwenye mjibisho usio wa kawaida au nusu kawaida au kama wasiwasi unaonekana umeondoa utulivu wake na amani ya moyo na fikra, haihitaji mtu mwenye busara kubwa au daktari bingwa kumtanzua au kumgundua mtu asiye na afya kiasi hicho kuwa yu mgonjwa taabani. Dalili zote hizi zi bayana katika jamii ya kisasa.

Yalikuwa ni ya kweli kiasi gani maneno ya Yesu[as] aliposema:

> *Utawatambua kwa matunda yao. Kamwe watu hawavuni zabibu kutoka kwenye miba au tini kutoka kwenye mbaruti, wanafanya hivyo? Halikadhalika kila mti mzuri unazaa matunda mazuri, lakini kila mti*

*mbaya unazaa matunda yasiyofaa; mti mzuri hauwezi kuzaa matunda yasiyofaa wala mti mbaya hauwezi kuzaa tunda zuri.*[16]

Watu wanalia madende kutokana na uchungu wa tunda leo hii, lakini kwa namna fulani hawataki kuubadilisha kwa mti ulio bora zaidi. Wanashindwa kuona kwamba sio mti ulio na makosa wala tunda unalozaa. Utangamano wa jamii ya Islamu unajikita katika kung'oa mti mbaya na badala yake kupanda ulio na afya zaidi.

Sawa na Kurani Tukufu, Adam[as] alipokatazwa kula tunda la mti hiki ndicho hasa kilichomaanishwa:

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا كَلِمَةً طَيِّبَةً كَشَجَرَةٍ طَيِّبَةٍ أَصْلُهَا ثَابِتٌ وَفَرْعُهَا فِي السَّمَاءِ ﴿٢٥﴾ تُؤْتِي
أُكُلَهَا كُلَّ حِينٍ بِإِذْنِ رَبِّهَا ۗ وَيَضْرِبُ اللَّهُ الْأَمْثَالَ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٢٦﴾

*Je, hukuona jinsi Allah Alivyopiga mfano wa neno zuri? Ni kama mti mzuri (ambao) mzizi wake ni imara na (kila) tawi lake lafika mbinguni. Hutoa matunda yake kila wakati kwa idhini ya Mola wake. Na Allah Huwapigia watu mifano ili wapate kudhukuru.*[17]

Hapa, mti ni mfano tu. Kwa uwazi kabisa Kurani Tukufu inazungumzia falsafa isiyo na afya ikiilinganisha na falsafa yenye afya kwa lugha hiyo hiyo ya mfano. Mti mbaya na hali ya makafiri vinaelezwa katika aya mbili zifuatazo:

وَمَثَلُ كَلِمَةٍ خَبِيثَةٍ كَشَجَرَةٍ خَبِيثَةٍ اجْتُثَّتْ مِنْ فَوْقِ الْأَرْضِ مَا لَهَا مِنْ قَرَارٍ ﴿٢٧﴾ يُثَبِّتُ اللَّهُ الَّذِينَ
آمَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ ۖ وَيُضِلُّ اللَّهُ الظَّالِمِينَ ۚ وَيَفْعَلُ اللَّهُ مَا يَشَاءُ ﴿٢٨﴾

*Na mfano wa neno baya ni kama mti mbaya ambao umeng'olewa ardhini, hauna imara. Allah Huwaimarisha wale walioamini kwa kauli thabiti, katika maisha ya dunia na katika Akhera; na Allah Huwaangamiza wadhalimu. Na Allah Hufanya Apendavyo.*[18]

*Neno* limetumika katika muktadha huu kwa maana ya falsafa, mfumo na utaratibu kama ambavyo neno hilo hilo limetumika katika maana yake pana zaidi katika aya ya kwanza ya Yohana:

*Hapo mwanzo kulikuweko Neno na Neno lilikuwa kwa Mungu na Neno lilikuwa Mungu.*[19]

Falsafa na taratibu mbovu ni lazima zitakumbana na jaala ya mti mbaya unaoshindwa kuhimili jaribio la falsafa ya "wanaoweza kuishi ni wenye kufaa zaidi" na hatimaye utang'olewa na kutupwa huku na huko na dhuruba kali.

Kwa upande mwingine, mfano wa mfumo na utaratibu wa mambo wenye afya ni kama mti wenye afya ambao mizizi yake imeshika vizuri katika ardhi hii lakini ambao mashina na matawi yake marefu yanafika kwenye angahewa halisi la kimbingu. Unastawishwa kwa nuru ya kimbingu na unazaa matunda mazuri yaletayo afya

katika kila majira. Kurani Tukufu inawaelezea waaminio kuwa wenye imani thabiti kwa Mungu; muundo wao mzima wa kimaadili na unyoofu umejengwa ukiwa imara na kuyakinika katika imani hii. Hili linaleta sifa ya uhalisi wa dhana ya Islamu ya unyoofu na maadili, ambayo hairuhusu ubaguzi kwenye uwanda wowote ujulikanao wa tofauti za kijamii, kidini au kimbari.

Kanuni elekezi itumikayo kwa shughuli zote za binadamu inaelezwa katika aya ifuatayo ya Kurani Tukufu:

وَلِلّٰهِ غَيْبُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَاِلَيْهِ يُرْجَعُ الْاَمْرُ كُلُّهٗ فَاعْبُدْهُ وَتَوَكَّلْ عَلَيْهِ ؕ وَمَا رَبُّكَ بِغَافِلٍ
عَمَّا تَعْمَلُوْنَ ﴿١٢٣﴾

*Na siri za mbingu na ardhi ni za Allah, na habari yote itarudishwa Kwake. Basi Mwabudu Yeye na kumtegemea. Na Mola wako Haghafiliki na yale mnayoyatenda.*[20]

Halikadhalika:

اَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْاَمْرُ ؕ تَبٰرَكَ اللّٰهُ رَبُّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٥٥﴾

*Fahamuni! uumbaji na amri ni Vyake. Mwenye baraka ni Allah, Mola wa walimwengu.*[21]

Falsafa zote za Islam zinaanza na kumalizia kwa mamlaka kamili ya Mungu, Mola Muumba wa ulimwengu.

## Misingi ya Jamii ya Kiislamu

Aya ya Kurani, ambayo inahusika sana na swala hili, ni kama ifuatavyo: [*][22]

إِنَّ ٱللَّهَ يَأْمُرُ بِٱلْعَدْلِ وَٱلْإِحْسَـٰنِ وَإِيتَآئِ ذِى ٱلْقُرْبَىٰ وَيَنْهَىٰ عَنِ ٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنكَرِ وَٱلْبَغْىِ ۚ
يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٩٠﴾

Hakika, Mungu Anaamuru uadilifu, na zaidi ya uadilifu; kuwapa watu zaidi ya wanachokistahili na kuwahudumia watu kwa ukarimu kana kwamba wanakuhusu (kama vile jamaa, ndugu na marafiki) na Mungu Anakataza kuonyesha uovu, kama ambavyo inaonekana leo mara nyingi kwenye runinga, redio na mitaani katika jamii nyingi duniani — na Anakataza yote yale yanayotambulika kuwa makosa, sio kidini ila kwa dhamira ya kibinadamu, na kila kitu kinachopelekea kwenye uasi na vurugu. Mungu Anawaadhi — asaa mtafaidika na mawaidha haya.

Sehemu ya kwanza ya aya hii inatumika zaidi kwenye nyanda za kiuchumi kuliko tangamano la kijamii. Inaleta sura iliyo bayana ya dhana ya Islam juu ya haki, kutopendelea na ukarimu katika kuwahudumia hohehahe kwenye jamii. Sehemu ya pili inatumika

* Tafsiri: 'Kwa hakika Allah Anaamuru uadilifu, na hisani, na kuwapa (watu kama uwapavyo) ndugu; na Anakataza upujufu, na uovu, na uasi. Anawanasihini ili mpate kufahamu.' [Mwenezi]

kwenye taswira ya jamii katika nchi, ambayo Islam imekamia kuijenga. Katika sehemu hii, Mungu Anakataza yote yale yanayoonekana mabaya kwa viwango vya kimataifa, kama vile tabia mbaya, kuadhiri, kutukana na bila shaka maovu yote katika jamii ambayo, bila hata kurejelea kwenye fundisho la dini yoyote, jamii ya binadamu kwa ujumla wake inakubaliana kuyalaani.

Halikadhalika, Islam inatupilia mbali kabisa na kulaani kila muelekeo, tabia na mkao ambao unaweza kupelekea fujo, uasi na vurugu. Neno *uasi* ni lazima lieleweke kwa maana ya jaribio lolote lisilo la haki la kupindua utaratibu uliowekwa. Lakini hilo halitoshi. Kila mara neno la kiarabu *baghyi* likitumika katika Kurani Tukufu, linatumika sio tu kwenye tukio la jeshi au la kisiasa lakini pia katika uasi kwenye jamii dhidi ya tamaduni zake sharifu, maadili na viwango, mafundisho ya dini na unyoofu.

Mwishoni, jamii inaonywa waziwazi kwamba amri hii ni kwa ajili ya faida ya watu wenyewe. Hii inakamilisha picha ya sifa muhimu za mfumo wa jamii ya Kiislam. Inaweza kuongezwa kusema kwamba sehemu ya kwanza ya aya hii pia inapotana kwa kina na mafundisho ya jamii ya kiislamu. Jamii ambayo haijali mateso ya watu wengine na daima haiko katika kuwahudumia binadamu, haiwezi kusemwa kuwa ni jamii ya kiislamu hata kama inafuata kiasi gani

vipengele vingine vya mafundisho ya Islam kuhusu jamii.

Hebu sasa tugeukie baadhi ya sifa zingine za jamii ya Kiislam zinazotajwa na Kurani Tukufu. Islamu inasisitiza uaminifu, utiifu, imani na inahamasisha hatua zote zile zitakazoleta utulivu wa moyo na mawazo. Inachukua hatua za kukinga dhidi ya kukengeuka kwa jamii katika kutafuta starehe. Hivyo, tabia yoyote, hata ikionekana haina madhara yoyote mwanzoni, ambayo inaweza kupelekea jamii kuwa na uhuru usio na mipaka, inakataliwa. Dhara kwa jamii ni kubwa sana na la namna nyingi. Jamii za aina hiyo ni lazima zitaishia katika hali za hovyo hovyo tunazoziona duniani leo hii. Katika jamii za aina hiyo, mielekeo isiyo na mipaka ya kutafuta starehe inapelekea, pamoja na mambo mengine, kwenye mmong’onyoko na hatimaye kuvunjika kwa mafungamano ya kifamilia. Kinyume na hili, inahifadhi kwa upendo mkubwa na kwa raghba mahusiano yote ya kibaba, kimama, kikaka, kidada na ya mtoto. Islam inataka kujenga urafiki, ambao ni wa kitaamuli zaidi kuliko wa kingoa, ashiki wala tamaa.

## Usafikhulka

Kwa kuanzia na mpango kwa wanawake katika jamii, ni lazima, sawa na Islam, kuchukua hatua zote zile za kuhamasisha usafikhulka, uaminifu, kujizuia na maisha safi. Msisitizo juu ya kuishi kwa khulka safi, zilizohamiwa vizuri dhidi ya hatari za mkato wa haja za

kingono ni sifa muhimu ya jamii ya Kiislamu. Kipengele hiki cha mafundisho ya Islam kuhusu jamii ni cha muhimu mno kwa ajili ya kulinda na kudumisha mfumo wa kifamilia. Hii ndio haja kuu ya sasa. Islam inatafuta kupanua idara ya familia badala ya kuiminya ionekane iko chini kabisa; familia ambamo njaa ya binadamu ya pendo na haja ya kupendwa inashibishwa sio kwa kukidhi haja za kujamiaana tu, bali kwa urafiki wa kistaarabu zaidi na kiungwana na uhusiano kama ambao unaenea kiasili baina ya ndugu wa damu wa karibu na wa mbali. Inashangaza jinsi watu wenye busara wa jamii ya leo wanavyoshindwa kuona udhaifu wa mwanadamu pale starehe zihusikanazo na ngono zinaporuhusiwa kushika dhima isiyodhibitiwa katika jamii. Kwa kweli, zinashamiri kwa kuua maadili yaliyotakaswa na kunywa damu yao kama kupe. Sigmund Freud, bila shaka, alikuwa ni zao la jamii kama hiyo. Alianza kuchunguza kila motisha ya binadamu kwa kutumia miwani yenye rangi ya kujamiiana. Kwake yeye, ule uhusiano wa utii wa hali ya juu uliopo kati ya mtoto na mama msingi wake ni tendo la kujamiiana. Hata uhusiano kati ya baba na binti hauna utakatifu bali una muelekeo wa kujamiiana au unatokana na kujamiiana. Takriban kila kitu ambacho mtu anakifanya iwe anajijua au hajijui, ni kwa ajili ya haja kubwa iliyofichika mwilini ya kujamiiana. Nashangaa kama katika zama za Freud jamii ilikuwa imefikia daraja la ushaghalabaghala, ambalo liko leo hii, lakini ilikuwa inatosha kuzaa uelewa wa akili ya

binadamu ambao kabisa umetawaliwa na kujamiiana. Lakini kama Freud alikuwa yuko sahihi, ni lazima zaidi kutokuruhusu jamii kuchezea bila kujijua nguvu hizo za hatari kwani zinaweza kusababisha mkato.

Ni masikitiko kwamba mazingira ya jamii za kisasa yasingeweza hata kutaka kujaribu kuelewa asili na sifa za mazingira ya jamii ya Kiislamu. Ikiwa mtu anakubali au kukataa dhana ya Mungu kutawala shughuli za binadamu na kuziwekea mipango, na ikiwa mtu yuko tayari au la kurekebisha tabia zake za kijamii ili ziendane na neno lililofunuliwa la Mungu, jambo moja ni uhakika kabisa kwamba mtu hawezi kulishinda Tendo la Mungu (yaani Asili) wala Neno la Mungu (yaani ukweli uliofunuliwa). Vyote hivi viwili; Tendo na Neno lazima viwe vinapatana ili viweze kuleta maana. Tabia yoyote ile ya kijamii ambayo mtu anaishika yenye kupingana moja kwa moja na Neno la Mungu ni lazima itaishia kwenye madhara.

Mtu, hata atake namna gani, hawezi kuwa na starehe isiyo na mipaka na isiyodhibitiwa. Anachoweza kufanya ni kubadili tu baadhi ya manufaa kwa kuyachagulia mbadala. Jamii inayotafuta kukwepa kuwajibika au kweli za maisha kwa msaada wa dawa za usingizi na za kulevya; jamii iliyoshikwa na tamaa ya ngono, misisimko ya ovyo na chereko; jamii ambapo ladha zinapotoshwa kwa makusudi ili zikidhi haja ya kimasoko iliyopandikizwa ya kutaka vipya, vifaa na vitu

vya kuchezea watoto kwa ajili ya anasa ambavyo havisaidii ila kuleta msisimko na kusababisha kiu ya kutaka zaidi; haja za kimasoko zilizobuniwa na mashirika yenye nguvu ambayo lengo lao ni kujilimbikizia mali; jamii ya aina hiyo inachagua yote haya kwa gharama ya maadili mema ya kibinadamu, utulivu wa mawazo na usalama katika jamii kwa ujumla. Hauwezi kuwa navyo vyote kwa wakati mmoja; amua kimojawapo.

Msisitizo wa Islam ni kinyume kabisa na huo. Starehe sawa — lakini siyo kwa gharama ya kuteketeza utulivu wa mawazo na usalama wa jamii kwa ujumla. Islam inazuia kwa nguvu zote mielekeo yote ya aina hiyo, ambayo kama haitadhibitiwa, inaweza kupelekea kubomoka taratibu taratibu kwa maisha ya kifamilia na kuhamasisha uchoyo, kutokuwajibika, upujufu, uhalifu na vurugu.

Mazingira yaliyozalishwa kutokana na falsafa hizi mbili yanatofautiana kwa mbali sana.

Inanishangaza jinsi baadhi ya watu wanavyoamini kwamba kwa kukuza tamaa au kuacha tamaa itawale inavyotaka katika jamii, wanaweza siku yoyote labda wakaahidi kuleta utulivu wa mawazo. Hakuna jamii duniani, hata kama iwe na uchumi mzuri kiasi gani, inayoweza kukumbatia uzalishwaji wa tamaa isiyokuwa na mipaka wala kudhibitiwa.

Hata katika jamii tajiri kuliko zote za dunia, daima kuna matajiri na maskini. Wale wasioweza kujipatia mahitaji ya msingi ya maisha ndio walio wengi katika jamii ikilinganishwa na idadi ndogo ya wale wanaomudu kulipia wanachokipenda. Hata hilo bado lina swali la kujiuliza kwa sababu inaonekana kwamba kadiri utajiri unavyoongezeka, tamaa nazo huongezeka na pengine huenda hata matajiri wakubwa hawawezi kutimiza ndoto zao kikamilifu. Lakini hali ya masikini walio wengi ni mbaya zaidi. Hawawezi hata kupata mahitaji ya msingi ya maisha, achilia mbali anasa ambazo zinaweza kufikiwa na sehemu ya jamii ya wenye ukwasi. Ni kwa hao masikini ambao mihemuko na haja zao hutoneshwa na vyombo vya habari. Kila kukicha wanaletewa kwenye nyumba zao kuukuu, picha za kutia mshawasha wa maisha ya kifahari za majumba makubwa, yenye bustani nzuri sana, utitiri wa magari ya kianasa, helikopta, ndege binafsi na jeshi la wapambe. Mtindo wa maisha huko Hollywood na kwenye Vilima vya Beverly ambako kuna matamasha, madensi, dhifa za kufurahi, au maisha kwenye makasino, nyumba za kamari, au yote yale ambayo mifululizo ya michezo ya kuigiza ya mivutano ya kijamii inaweza kuvuta taswira za matamanio ambayo kwamba hata watu masikini kabisa wanaweza kupata. Lakini ni wachache, hata miongoni mwa matajiri wakubwa, wanaoweza kuwaza kupata pepo hii ya dunia. Watu wa aina hiyo bila shaka hawatajali mazingira yao duni ya kimasikini. Raha ya

kuwa na nyumba na familia haitakuwa tena na mvuto kwao. Ukosefu wa utamaduni na ustaarabu unakuwa sambamba na matarajio haya ya kutamanisha, na, katika muktadha huu, ukweli wa maisha yao wenyewe unaanza kupoteza maana zote. Kama haya ndiyo yangekuwa kilele cha maendeleo ya jamii yanayotokana na starehe za kipuuzi na matarajio yasiyokuwepo, ukarimu na amani ya nyumbani na raha ya nyumba na familia yote yanazidi kuwa ndoto. Hapo basi kusingekuwa na chochote kilichobaki kwao kukitarajia kwa siku za usoni.

Itahitajika kuchukua hatua zaidi ya moja kurudisha famila ya asili iliyo ya muhimu sana kuunganisha wanafamilia pamoja wakiaminiana, wakitegemeana na amani inayoleta upendo. Lakini, pengine, tumeisha chelewa kabisa kulizungumzia hili.

Islam ina ujumbe wa wazi. Inao mpango kabambe wa kuhami, kulinda na kuhifadhi mfumo mzima wa familia au kuujenga upya popote ulipokuwa umebomolewa kabisa.

Sawa na Islam, nidhamu lazima ifundwe kwa kusadikisha na kuelewesha kupitia kila aina ya shughuli za kijamii, na mabaki yaliyopotea lazima yarudishwe.

## Kutenganisha Jinsia

Watu katika nchi za Magharibi hawauelewi kabisa mfumo wa kijamii wa Islam kuhusiana na *purdah*

ambayo inaonekana kama ni ubaguzi kati ya jinsia mbili. Kutokuelewa huku kwa kiasi fulani kunatokana na matumizi mabaya ya mafundisho ya kweli ya Islam katika sehemu nyingi za nchi za Kiislamu na dhima hasi ya vyombo vya habari vya nchi za Magharibi. Imekuwa ni kanuni kwa vyombo vya habari vya nchi za Magharibi kuuhusisha Uislamu na ubaya wa tabia popote utokeapo, lakini wanajizuia kuhusisha tabia za Kiyahudi, Kikristo, Kibudha au Kihindu na dini zao.

Amri ya Islam ya kutenganisha bila shaka haitokani na ufinyu wa fikra wa zama za zamani za giza. Kwa kweli, swala la uzinzi au vinginevyo katika jamii, halina uhusiano kabisa na kuendelea au kurudi nyuma kwa zama husika. Jamii katika zama zote za historia ama zimepanda kwenye kilele au zimeporomoka kwenye mabonde ya mitikisiko ya kijamii au kidini.

Dhana ya ukombozi wa mwanamke sio kabisa muelekeo wa kimaendeleo katika jamii ya binadamu. Kuna ushahidi wenye nguvu kwamba zamani sana na pia katika zama za karibuni za historia ya binadamu wanawake kama tabaka wameshika nafasi zenye madaraka makubwa katika jamii ya binadamu katika sehemu tofautitofauti za dunia.

Uhuru wa kujamiiana kusiko na miiko kati ya jinsia za kiume na kike katika jamii siyo jambo jipya na geni. Tamaduni zimekuja na kutoweka. Bombwe za tabia zimedumu kupembeza kutoka mtindo mmoja kwenda

mwingine. Mielekeo lukuki ya kijamii imekuwa ikianguka na kutuama ikiwa katika bombwe tofautitofauti lakini kila mpopotoo wa nelubini unaifanya ipite kwenye majaribio na miundo mipya. Lakini bado, hakuna muelekeo uliowahi kubaki ambao kwao tunaweza kuhukumu kiuhakika kwamba katika historia yote, jamii ilibadilika kutoka mtengano kuwa ya kizinzi au kutoka hali ya wanawake kuwekewa mipaka kuwa, kwa kulinganisha, hali ya wanawake kukombolewa na kuwa huru.

## Mapambazuko ya Zama Mpya kuhusu Haki za Wanawake

Ni muafaka sana hapa kutupia macho kwenye zile zama za giza katika historia ya Arabia wakati Islam inazaliwa, kwa agizo la Kimbingu, kama sisi Waislamu tunavyoamini, au kama wanavyoweza kusema wasio Waislamu kwamba ni kwa mafundisho binafsi ya Muhammad[saw]. Na yaweje maoni ya baadhi ya wanatheolojia, katu mafundisho ya Islam kuhusiana na utengano kijinsia, hayawakilishi tabia za Waarabu hata kidogo.

Mtazamo wa jamii ya Arabia kwa wakati ule kuhusiana na wanawake ulikuwa na mkanganyiko wa ajabu sana. Kwa upande mmoja, ngono huru, mchanganyiko huria baina ya wanaume na wanawake na karamu za mvinyo zenye ghasia, wanawake na nyimbo vilikuwa ndio vipendwavyo na jamii ya Arabia. Kwa upande

mwingine, kuzaliwa kwa binti kulionekana kuwa ni jambo la aibu na fedheha kubwa. Hata baadhi ya Waarabu wenye majigambo wamesimuliwa kwamba walikuwa wakiwazika binti zao wachanga kwa mikono yao wenyewe ili kukwepa utwezo huo.

Wanawake walichukuliwa kuwa ni kama mali inayohamishika na walinyimwa haki ya kuwapinga waume zao, baba au wanafamilia wengine wa kiume. Hata hivyo, si mara zote kanuni hii ilikuwa ikitumika. Ilikuwa inatokea mara chache, mwanamke mwenye sifa za uongozi zilizojipambanua alikuwa anashika dhima ya muhimu katika shughuli za kabila. Islam ikabadilisha yote hayo, siyo kama matokeo endelevu ya asili ya mivutano ya kijamii, bali kama msuluhishi wa maadili. Mfumo wa kijamii uliamrishwa kutoka juu, ambao haukuwa na mahusiano na nguvu za kawaida, ambao unaipa jamii sura.

Kwa kupitia mafundisho ya utengano, uhuru wa kingono ukasitishwa mara moja. Amri kuhusu mahusiano ya wanamume na wanawake ikawekwa kwa msingi wa kanuni za kina za kimaadili. Wakati huo huo hadhi ya wanawake ikanyanyuliwa kwa kiwango cha juu kiasi kwamba hawakuchukuliwa tena kuwa ni bidhaa isiyo na msaada. Walipewa mgawo sawa katika masuala ya maisha. Wakati ambapo hapo kabla waligawanywa kama sehemu ya mali ya kurithi, sasa wanaweza kurithi sio tu mali za baba zao, bali pia

waume zao, watoto na ndugu wengine wa karibu. Sasa walikuwa wanaweza kuwapinga waume zao na kubishana nao. Walikuwa wanaweza kujadiliana nao, na bila shaka, walikuwa na haki kamili za kukataa. Walikuwa sio tu wanaweza kuachika bali waliweza pia kujikhului kutoka kwa waume zao kama wangependa kufanya hivyo.

Kama mama, wametendewa kwa heshima kubwa katika Islam ambayo ni vigumu kupata mfano wake katika jamii zingine duniani. Ilikuwa ni Mwanzilishi Mtukufu[saw] wa Islam ambaye alisimamia haki za wanawake kwa kutamka kwa agizo la Kimbingu, kwamba 'Pepo iko chini ya miguu ya mama zenu.'

Sio tu kwamba alikusudia ahadi itakayotimizwa katika maisha baada ya kifo, bali pia kwa pepo ya kijamii ambayo wameahidiwa watu wanaoonyesha heshima kubwa na staha kwa mama zao, na wanajitolea kwa dhati kuwaridhisha na kuwapa kila faraja inayowezekana.

Fundisho la utengano ni lazima lieleweke katika muktadha huu. Halikuwa ni matokeo ya ubora wowote wa wanaume bali ulikusudiwa kujenga utukufu wa nyumba; kuleta kuaminiana kwa hali ya juu kati ya mume na mke; kuleta ukadiri kwenye haja za msingi za binadamu; na kuziweka pamoja na kuziwekea nidhamu ili, badala ya kufunguliwa zikiwa ni shetani mwenye

nguvu katika jamii, zifanye kazi nzuri, kama vile nguvu asili zinavyofanya kazi kwa pamoja.

Utengano unaeleweka vibaya kabisa unapodhaniwa kuwa ni kuwawekea vizuizi wanawake wa jamii ya Kiislamu wasishiriki kikamilifu katika nyanja zote za shughuli za kibinadamu. Hiyo sio kweli. Dhana ya utengano katika Islam ieleweke tu katika muktadha wa hatua za kulinda utukufu wa hadhi na heshima ya wanawake katika jamii ili hatari za kuvuruga malengo haya zipunguzwe na kuwa katika kiwango cha chini kabisa.

Michanganyiko huru ya jinsia zote mbili na mambo ya kisirisiri kati ya wanawake na wanaume yanazuiliwa kwa nguvu zote. Wanaume na wanawake wote wanashauriwa kujizuia sio tu kutupiana macho ya tamaa, bali pia kujizuia na ile migusano ya macho na ya kimwili ambayo inaweza kupelekea kwenye mshawasha usiodhibitika. Wanawake wanategemewa wajifunike kiheshima na wanashauriwa wasijiweke katika namna ya kuvutia nadhari isiofaa kutoka kwa wanaume watukutu. Matumizi ya vipodozi na urembo hayakatazwi lakini yasitumike wakati wa kwenda nje ili kuvuta nadhari. Tunaelewa fika kwamba kwa sununu ya sasa ya jamii duniani kote, fundisho hili linaonekana kuwa kali kiasi, zuivu na halichangamshi. Lakini, uchunguzi wa kina wa mfumo mzima wa kijamii wa Islam unaweza kumfanya mtu akubali kuwa maoni haya

ni miropoko isiyo na umakini. Kwa hiyo fundisho hili, ni lazima lieleweke kuwa ni sehemu muhimu ya hali nzima ya mazingira ya kijamii ya Islam.

Dhima waliyonayo wanawake katika mfumo wa kijamii wa Islam bila shaka siyo ya vimada lakini pia siyo ya jamii iliyofungiwa ndani ya kuta nne za nyumba zao, wakizuiliwa kuleta maendeleo na wakinyimwa kuta nne za mwanga wa elimu. Picha hii mbaya ya mfumo wa kijamii wa Islam inachorwa na maadui wa ndani au wa nje wa Islam au na wasomi ambao kabisa hawaelewi njia ya maisha ya Islam.

Kitu pekee, ambacho Islam haitaidhinisha, ni kuwageuza wanawake kuwa vitu vya kuchezea, wanyonywe au waachwe wateseke na ufidhuli wa wanaume. Islam haifagilii mielekeo ya aina hiyo dhidi ya wanawake.

Kwa sababu tu jamii kwa ujumla imekuwa ni yenye kuhitaji mambo mengi zaidi na zaidi, ni ukatili tu dhidi ya wanawake kama inalazimisha kwamba ni lazima daima wawe angalifu kuhusu wanavyoonekana, wajihi wao na jinsi wanavyovaa na wanavyojipodoa. Miili ya kike siku zote imekuwa ikionyeshwa. Hata kwa ajili ya kuuza kikorokoro cha chakula au cha mahitaji a kila siku, kama vile sabuni ya kufulia, kunahitaji tangazo lenye umbo la kike. Maisha bandia, ya kimitindo na ghali yanaonyeshwa kuwa ni ya lazima kwa mwanamke kupata ndoto zake. Jamii ya aina hiyo haiwezi kubaki isiyoyumba, tulivu na maridhawa kwa muda mrefu.

Sawa na Islam, wanawake ni lazima wakombolewe dhidi ya kunyonywa na kufanywa dhima yao ni vyombo tu vya kujistarehesha. Ni lazima wajipatie muda zaidi wa kutekeleza majukumu yao ya nyumba zao na kizazi kijacho cha binadamu.

**Haki Sawa kwa Wanawake**

Unasikia mengi kuhusu ukombozi wa wanawake na haki za wanawake n.k. Islam inazungumzia kanuni yenye msingi mpana, ambayo inatosheleza hali zote:

وَلَهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ ۚ وَلِلرِّجَالِ عَلَيْهِنَّ دَرَجَةٌ ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٢٨﴾

*Nao (wanawake) wanayo haki sawa na ile iliyo juu yao kwa sheria; (yaani, wanawake wana haki zile zile kwa wanaume, kama vile wanaume walivyo na haki kwa wanawake. Hivyo kuna usawa kamili na hakuna tofauti yoyote iwayo katika haki za msingi za wanadamu kati ya wanawake na wanaume) na wanaume wana daraja moja zaidi kuliko wao, na Allah ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.*[23]

Katika sehemu nyingine ya aya ya Kurani Tukufu, inasemwa:

الرِّجَالُ قَوَّامُونَ عَلَى النِّسَاءِ بِمَا فَضَّلَ اللَّهُ بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ وَبِمَا أَنْفَقُوا مِنْ أَمْوَالِهِمْ ۚ

*Wanaume ni walinzi wa wanawake kwa sababu Allah amewafadhili baadhi yao kuliko wengine, na kwa sababu ya mali zao wanazozitoa.*[24]

Kutokana na neno la Kiarabu *Qawwaamuun* (walinzi waliowajibishwa kuzitunza familia zao kwenye njia sahihi), baadhi ya maulamaa (madaktari wa dini) wenye mawazo ya wasomi wa karne zilizopita hivi karibuni wanahitimisha na kudai ukuu wa wanaume dhidi ya wanawake wakati kinachorejelewa kwenye aya hiyo ni kule tu kupiku ambako mkimu familia anako juu ya wategemezi wake. Kwa mantiki hiyo, mlinzi anakuwa katika nafasi nzuri zaidi kutumia nguvu ya kimaadili kwa anaowalinda ili wadumu kubaki katika njia sahihi. Kuhusiana na haki za msingi za binadamu, halirejelei kwa namna yoyote kwa wanawake kutokuwa sawa au kwa ukuu wa wanaume juu ya wanawake. Sehemu ya mwisho ya aya inarejelea kwenye upiku uliotajwa hapo juu na unaifanya iwe bayana dhahiri shahiri kwamba licha ya upiku huu, haki za msingi za wanawake ziko sawa kabisa na zile za wanaume. Neno la Kiarabu *wa* litafsiriwe 'licha ya ukweli kwamba' au 'wakati' na kwa muktadha huu inaonekana kuwa ndio tafsiri pekee iliyo sahihi.

## Mitala

Katika nchi za Magharibi ni kawaida sana kumkabili msemaji kuhusu somo la Islam kwa swali linalouliza hivi: *Je, Islam inamruhusu mtu kuoa mara nne na kuwa na wake wanne wakati mmoja?* Nimekuwa na uzoefu mkubwa mno katika kuhutubia mikutano mingi ya wazi na maalum ya wasomi katika nchi za Magharibi.

Ninakumbuka ni kwa nadra sana ambapo swali hili halikuulizwa.

Mara nyingine hutokea mwanamke akasimama, na, bila shaka, kwa heshima na taadhima, akauliza kimaasumu kama Islam inaruhusu wake wanne au la. Ni dhahiri, kila mmoja analijua jibu lake; lakini, labda, hiki ndio kipengele pekee cha Islam kinachojulikana kwa mapana kiasi hicho katika nchi za Magharibi. Kipengele kingine kinachojulikana sana ni ugaidi, lakini ugaidi hauhusiani chochote na Islam.[25]

Usawa gani huu kati ya wanaume na wanawake unaoletwa na Islam ambapo mwanamume anaruhusiwa kuwa na wake wanne wakati mwanamke anapaswa kuwa na mume mmoja tu? Huu ni muundo mwingine wa swali lilelile, ambalo ninaamini linatumika tu kama hila ya kufuta maono yoyote mazuri kuhusu Islam, ambayo yanaweza kuwa yamejengwa na msemaji. Katika mihadhara isiyo rasmi sana ambako nidhamu haitiliwi maanani sana, swali hilo linashika asili ya dhihaka kuliko ile ya swali jepesi.

Miongo mingi iliyopita wakati nikiwa SOAS (Kitivo cha Uchunguzi wa nchi za Mashariki na Afrika) Chuo Kikuu cha London, mwanafunzi mmoja wa Kipakistani alikerwa na mwanafunzi mwenzake wa Kiingereza kwa swali hilo hilo tena na tena na kwa namna fulani haikushindwa kuvuta kicheko. Siku moja, ninakumbuka, pengine aliudhiwa sana, na mara akamgeukia na

kumuuliza yule kijana wa Kiingereza: Kwa nini mnatupinga sisi kuwa na *four mothers* (mama wanne) wakati hamna kipangamizi cha nyinyi kuwa na *forefathers* (baba wanne, vivo hivyo japo neno limechezewa) *(lilitakiwa liwe four fathers. Neno alilotumia forefathers maana yake ni mababu, mfasiri*). Mchezo wa maneno kwenye neno 'four' (nne) ambao vizuri sana ulimgeuzia kibao mchokozi yule.

Inavyoonekana, ulikuwa ni utani, lakini ukilichunguza kwa ukaribu, utagundua ni zaidi ya utani, kwani unarejea kwenye hali ya kusikitisha iliyotapakaa katika jamii nyingi na inatupatia hali stahiki kwa kulinganisha fikra ya Islam na ile ya jamii ya kisasa. Sio tu ni jambo la mabaraza holela ya wanafunzi lakini hata wanajamii wenye mawazo makini na waheshimiwa sana hawaoni kuwa ni jambo baya na la utovu wa nidhamu kuonyesha dhihaka juu ya upinzani wao dhidi ya amri hii.

Sio zamani sana, nilipokea barua kutoka kwa Jaji mwandamizi wa huko Frankfurt, ambaye binafsi ninamjua kuwa ni mwenye busara sana, muwazi, mwenye heshima zake na mwenye nia njema. Yeye pia, alipinga ruhusa ya Islam kuhusu mitala ya wake wanne na hakuweza kujizuia na tashwishi ya kutumia maneno makali aliyoyaficha kwenye dhihaka isiyo ya kiadilifu, ambayo angalau mimi niliwaza hivyo. Kwa sekunde chache niliwaza kurudisha zawadi ya utani wake kwa utani wa *forefather*, lakini busara ilinikataza.

Jibu fupi nililompa kwa muhtasari ni kwamba ruhusa hii iliyotolewa na Islam ya kuoa zaidi ya mara moja siyo ruhusa ya jumla bali kuwepo kwa ruhusa ya namna hii kunafungamana na hali za aina fulani ambapo inakuwa ni lazima kulinda mambo yote mawili; afya ya jamii na haki za wanawake.

Kurani Tukufu ni kitabu cha mantiki. Kwa hivyo, kisingeweza kuwaagiza Waislamu wapate kisichowezekana. Mungu Amewaumba wanaume na wanawake idadi yao ikiwa takriban inalingana — kukiwa na ongezeko kidogo au punguko kidogo hapa na pale. Inawezekanaje dini ya mantiki kama Islam, ambayo mara kwa mara inasisitiza kwamba hakuna ukinzani kati ya Tendo la Mungu na Neno la Mungu, ihubiri kitu ambacho dhahiri shahiri si asili na sio halisi, ambacho, kama kikijaribiwa, kitaleta hali mbaya ya kukosa usawa, shida zisizoweza kutatulika na mikanganyiko. Fikiria nchi ndogo yenye wanaume milioni moja waliofikia umri wa kuoa na takriban idadi hiyo hiyo ya wanawake. Kama ruhusa hii ingechukuliwa kuwa ni amri ya kufuatwa neno kwa neno la sheria na wote, basi si zaidi ya wanaume 250,000 wangeoa wanawake milioni moja na wanaume 750,000 wangeachwa hawana wake.

Zaidi ya hayo, miongoni mwa dini zote duniani, Islam imesimama wima katika kusisitiza ndoa kwa kila mwanamume na mwanamke. Kurani Tukufu inauelezea uhusiano kati ya mume na mke kuwa kiasili msingi

wake ni upendo na unaleta chemchem ya amani kwa kila mmoja.

وَالْمُحْصَنٰتُ مِنَ الْمُؤْمِنٰتِ وَالْمُحْصَنٰتُ مِنَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ مِنْ قَبْلِكُمْ اِذَآ اٰتَيْتُمُوْهُنَّ
اُجُوْرَهُنَّ مُحْصِنِيْنَ غَيْرَ مُسٰفِحِيْنَ وَلَا مُتَّخِذِيْٓ اَخْدَانٍ ؕ

*Na wanawake wema katika waaminio na wanawake wema katika wale waliopewa Kitabu kabla yenu (ni halali kwenu), mtakapowapa mahari zao, mkifunga nao ndoa, bila kufanya uzinzi, wala msiweke mahawara wa siri.*[26]

Wakati huo huo, Kurani Tukufu inakataa useja ikiuita kuwa ni desturi tu iliyobuniwa na watu.[27] Hakuna cha kupata kwa mtu kujifungia mbali na dunia au kwa kujiadhibu kwa kujinyima haja za asili. Sheria ya ndoa imeimarishwa vizuri katika Islam, lakini muda hauniruhusu kutoka nje ya mada na kujadili mahitajio mbalimbali ya kuwachagua wachumba, marekebisho yaliyopo na kanuni za talaka n.k.

Tukirudi kwenye mitala, ni dhahiri ukiichunguza Kurani Tukufu utakuta ya kwamba hali maalumu ya kipindi baada ya vita ndiyo inayozungumziwa. Ni kipindi ambacho jamii inabakiwa na idadi kubwa ya yatima na wajane wabichi na mpatanisho wa idadi ya wanawake na wanaume unatibuliwa sana. Hali kama hiyo ilitokea Ujerumani baada ya Vita Kuu ya pili ya dunia. Kwa kuwa Islam haikuwa ndiyo dini kuu ya Ujerumani, Ujerumani iliachwa haina ufumbuzi wa tatizo hilo.

Mafundisho makali ya Kikiristo ya mke mmoja hayakuleta nafuu yoyote. Matokeo yake, watu wa Ujerumani walilazimika kukumbana na athari hizi za ukosefu wa mpatanisho wa idadi ya wanawake na wanaume. Kulikuwa na idadi kubwa ya mabikira, maseja wa kike wenye majonzi na wajane wabichi ambao haikuwezekana kamwe kuolewa.

Ujerumani haikuwa nchi pekee katika bara pana la Ulaya kukumbana na matatizo hayo makubwa ya kijamii yanayowiana na hatari za kutisha kabisa. Ilikuwa ni changamoto kubwa sana kwa jamii ya nchi za Magharibi baada ya vita kuweza kuzuia wimbi na kudhibiti kupanuka kwa mporomoko wa maadili na uzinzi, ambao ulistawi wenyewe tu kwa ukunjufu kutokana na hali halisi ya ukosefu wa mpatanisho wa idadi ya wanawake na wanaume.

Kama ambavyo inaweza kuonekana bayana na kila mtu muadilifu jibu pekee kwa masumbuko yote hayo ya kutatanisha ni kuruhusu wanaume kuoa zaidi ya mara moja. Hili halipendekezwi kama utatuzi wa kutoshelezea haja zao za kimwili bali kukidhi mahitajio halisi ya idadi kubwa ya wanawake. Kama suluhisho hili lenye mantiki sana na liwezekanalo likikataliwa, mbadala pekee uliobaki kwa jamii ni kusawijika kwa kasi kuwa jamii yenye upotofu unaoongezeka na yenye kutoa uhuru.

Nasikitika! Hilo ndilo linaonekana kuwa chaguo lililochukuliwa na nchi za Magharibi.

Unaporudia kuzichunguza kwa uhalisi zaidi bila jazba fikra hizo mbili, huwezi kushindwa kuona kwamba sio swala la usawa baina ya wanaume na wanawake bali ni chaguo tu kati ya kuwajibika na kutokuwajibika.

Islam inaruhusu ndoa zaidi ya moja kwa sharti kwamba mwanamume akubali changamoto za shida zitakazojitokeza katika hali mbalimbali na agawe haki kamili na kwa usawa kwa mke wa pili, wa tatu na wa nne.

وَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تُقْسِطُوا فِي الْيَتَامَىٰ فَانكِحُوا مَا طَابَ لَكُم مِّنَ النِّسَاءِ مَثْنَىٰ وَثُلَاثَ وَرُبَاعَ ۖ
فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تَعْدِلُوا فَوَاحِدَةً أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ۚ ذَٰلِكَ أَدْنَىٰ أَلَّا تَعُولُوا ﴿٣﴾

*Na kama mkiogopa kwamba ninyi (kama jamii) mtashindwa kufanya uadilifu katika mambo yahusuyo mayatima baada ya matukio ya vita, basi oeni wanawake wa chaguo lenu wawili au watatu au wanne. Lakini mkiogopa kuwa hamwezi kufanya uadilifu, basi (oeni) mmoja tu, au wale ambao mikono yenu ya kuume imewamiliki; Hii ndiyo njia ya karibu zaidi kwa ajili yenu ili kuepukana na kutokufanya uadilifu.*[28]

Mbadala wake ni mbaya zaidi. Idadi kubwa ya wanawake wanaoachwa bila ya ndoa hawawezi kulaumiwa kwa kujaribu kutongoza na kutamanisha wanaume wenye wake katika jamii ambazo si za kidini sana. Hata hivyo, wanawake ni binadamu pia. Wana

mihemuko yao na haja zisizo kidhiwa. Wakati kiwewe cha kisaikolojia cha vita kimezidisha haja ya kutafuta mtu wa kumuelekea, maisha bila uhakika wa ndoa na nyumba, bila ya kuwa na mwenzi kimaisha na bila matumaini ya kupata watoto ni maisha ya kipumbavu. Mategemeo ya baadae ni matupu na giza kama yalivyo ya sasa.

Kama wanawake wa aina hiyo hawatakaribishwa kisheria na kuwazoesha katika misingi ya kanuni ya 'maafikiano', inaweza kuleta vurumai kwenye utulivu wa jamii. Kwa vyovyote vile, kiharamu watachangia wanaume wale wale wa wanawake walio kwenye ndoa. Matokeo ya hayo lazima yatakuwa ni upuuzi. Uaminifu utagawanyika. Wanawake walioolewa wataanza kutowaamini waume zao. Shaka itaongezeka. Kuongezeka kwa kutokuaminiana kati ya mume na mke kutatikisa misingi ya nyumba nyingi. Kwa wanaume wasio waaminifu kuishi na hisia za makosa na hatia kutazalisha matatizo zaidi ya kisaikolojia na muelekeo wa kufanya makosa zaidi. Dhana bora ya upendo na utii itakuwa miongoni mwa vitu vya mwanzo kuathirika. Mahaba yataanza kupoteza mvuto na kuporomokea kwenye ghururi za kawaida tu zipitazo.

Wale wanaozungumzia usawa katika kila nyanja wanasahau kwamba swala la usawa linakuwa halina maana katika mambo yale ambayo wanaume na wanawake wameumbwa tofauti.

Ni wanawake tu wanaoweza kuzaa watoto. Ni wao tu wanaoweza kupitia zaidi ya miezi tisa ya kunururisha mbegu ya uzazi wa binadamu kwa ajili ya siku za usoni. Ni wanawake tena ambao wanaweza kulea watoto wao, angalau katika kipindi cha awali cha uchanga na utoto, ambapo hakuna mwanamume angeweza kuthubutu. Kwa sababu ya uhusiano wa kidamu wa muda mrefu na wa ndani kwa ndani kabisa na watoto wao, ni wanawake ambao wana muungano wenye nguvu zaidi wa kisaikolojia na watoto ikilinganishwa na wanaume.

Kama mifumo ya kijamii na kiuchumi itapuuzia tofauti hii ya kimaumbile kati ya mwanamume na mwanamke na tofauti zinazowiana katika dhima ya jinsia hizo mbili katika jamii, basi mfumo wa aina hiyo wa kijamii na kiuchumi ni lazima utashindwa kuleta hali nzuri ya usawa. Zaidi ni kutokana na tofauti hizi za kimaumbile kati ya mwanamume na mwanamke ambapo Islam inapendekeza dhima tofauti zinazowiana na kila jinsia.

Mwanamke ni lazima kadiri inavyowezekana aepushwe na jukumu la kutafuta chakula kwa ajili ya familia. Kimsingi, wajibu huu ni lazima uangukie kwenye mabega ya wanaume. Hata hivyo, hakuna sababu ya kuwazuia wanawake kutoa mchango wao katika kusukuma gurudumu la uchumi ikiwa wenyewe wanajisikia kuwa huru kufanya hivyo yaani bila kuacha majukumu yao ya msingi ya kuendeleza kizazi cha

binadamu, kutunza familia na wajibu unaoambatana nao. Hiki ndicho hasa Islam inachokipendekeza.

Tena, wanawake kwa ujumla wana umbo dhaifu linaloonekana kuwa laini. Lakini, cha kushangaza, Mungu Amewajaalia uwezo wa ushupavu ndani ya miili yao. Sifa hizi kimsingi ni kutokana na kuwepo kwa nyongeza ya nusu ya kromosomu katika seli zao, ambazo ndizo zinahusika na tofauti kati ya mwanamume na mwanamke. Bila shaka hizo zimewekwa ili kuweza kuhimili changamoto ya ziada waliyowekewa wakati wa ujauzito, kujifungua na kunyonyesha. Hata hivyo, nguvu hii isiyodhihirika haimfanyi mwanamke kuwa na nguvu na ushupavu zaidi kwa nje. Wasitwishwe kazi ngumu kwenye nyanja za uzalishaji uchumi kwa sababu tu ya kutaka usawa au sababu nyingine yoyote. Hii inahitaji pia kwamba watendewe kwa upole zaidi na wema. Wanawake ni lazima wawe na mzigo hafifu zaidi wa kubeba katika maisha ya kila siku na wasilazimishwe kubeba mzigo sawa na wanaume katika shughuli za umma.

Kinachojitokeza kutokana na maelezo haya ni wazi kwamba kama jukumu la kutunza nyumba ni eneo maalumu la uwajibikaji ambalo anaweza kupewe mwanamume au mwanamke, ni dhahiri mwanamke anastahili zaidi kuliko mwanamume kutekeleza majukumu ya aina hiyo. Kwa kuongezea, kiasili

wanawake wamepewa jukumu la kulea watoto. Jukumu la aina hiyo linaweza kubebwa kiasi tu na mwanamume.

Ni lazima wanawake wapewe haki ya kubaki zaidi nyumbani kuliko wanaume; kama, kwa wakati huo huo, wanaepushwa na jukumu la kuhemea kwa ajili ya maisha yao, muda wao uliopo ni lazima utumike kwa manufaa yao wenyewe au kwa manufaa ya jamii kwa ujumla. Hivyo ndivyo ilivyozaliwa dhana ya *"nafasi ya mwanamke ni nyumbani."* Hakuna swala la wao kuzuiliwa au kufungiwa kwenye kuta nne za nyumba. Hakuna namna yoyote ile Islam inaweza kuingilia haki za wanawake kwenda nje kwa muda wao huru kufanya kazi yoyote au kushiriki kufuatilia chochote chema kilicho ni chaguo lao, kwa sharti, narudia, kwamba hawahatarishi masilahi na haki za kizazi cha usoni cha binadamu walichokabidhiwa. Na ndio maana pamoja na sababu zingine Islam inakataza kwa nguvu zote miingiliano iliyokithiri au kuchanganyikana kiholela kwa jinsia tofauti. Hivyo Islamu inapopondekeza kwamba nyumba ndio makao ya shughuli za mwanamke ni jambo la busara sana na linatatua kwa vitendo matatizo ya maovu mengi ya zama za sasa. Pale wanawake wanapohamishia shauku kwenye kuwa mbali na nyumba inakuwa ni hasara kwa maisha ya kifamilia na kutelekeza watoto.

Kujenga maisha ya kifamilia yanayozunguka kwa kumtegemea mama, kunahitaji uimarishaji wa

mahusiano mengine ya kidamu na kurejeshwa mvuto halisi wa ukoo na ujamaa, undugu na urafiki. Ingawa kila familia inaweza kuishi kivyake, dhana hii ya familia kubwa zaidi ya ukoo inaungwa mkono na kukuzwa na Islam kwa sababu nyingi, baadhi yao ni kama zifuatazo:

1. Inaepusha kutokea kwa utovu wa urari katika jamii.
2. Kama upendo adhimu na mahaba yangekuzwa katika familia kati ya makaka na madada, baba na mabinti, mama na watoto wa kiume nk, ingepelekea kiasili kwenye kuimarisha na kuhifadhi familia madhubuti. Muungano huu wa kiasili unaimarishwa zaidi na mfumo wa undugu unaoizunguka ukiwa katika hali ya undugu halisi na ukaribu baina ya mashangazi, wajomba, wapwa wa kike, wapwa wa kiume, mabinamu, wajukuu na mababu na mabibi. Njia mpya za kutafuta upendo na furaha maridhawa, zinazotokana na kujisikia mwanandugu, zitafunguka kwa walio kwenye mfumo huu mkubwa zaidi wa familia.
3. Familia kama taasisi katika hali za namna hiyo ni vigumu kuvunjika. Kuwa ndani ya nyumba moja kama familia hakutakuwa tena kusiko na maana kama, kwa ujumla, tuonavyo siku hizi. Wanafamilia wataendelea kuvutwa kwenye nguzo kuu ya wazee wa familia; shughuli nyingi

za kifamilia zitazunguka penye mhimili huu. Hakutakuwa na watu wapweke, waliosahaulika, wenye huzuni na kutupwa darini au katika chumba kilicho chini ya ardhi cha nyumba kama makorokoro yaliyokosa matumizi.

Hii hasa ndio dhana ya Islam ya nyumba na familia, ambayo inachukuliwa kuwa ni kizio kikuu katika jamii. Zaidi ni kutokana na tofauti hii kifikra ambapo tunaona siku hizi katika jamii za kisasa duniani matukio mengi mno ya kutelekezwa kwa wazee, wazazi walemavu wanaoonekana kuwa ni mzigo kwa familia.

## Kuwatunza Wazee

Jukumu la kuwatunza wazee taratibutaratibu linahamia kwa serikali. Kuwatunza wazee kunaleta mzigo mkubwa kwenye uchumi wa nchi. Kwa kiasi chochote kile serikali itakachokuwa hiyari kukitumia, haiwezi kuwanunulia amani na kuridhika. Hisia mbaya sana za kuwa umetupwa, umeachwa na kutelekezwa, na maumivu makali sana ya utambuzi wa chumba upweke kipanukacho cha ndani kwa ndani ni matatizo yasiyoweza kutatuliwa na wengi. Kudhania kwamba ndugu wa mbali hata siku moja atatunzwa na familia iliyobaki kumekuwa kusikowezekana kabisa kufikirika.

Katika jamii za aina hiyo, haja ya nyumba za wazee inakua kadiri siku zinavyopita. Lakini, siyo kila siku inawezekana kwa serikali kutenga fadha za kutosha kuwahudumia kwa haja za chini kabisa za maisha ya

staha. Maradhi ya kimwili ni rahisi zaidi kuyatibu au kuyapunguza, lakini lindi la kiwewe cha kisaikolojia wanachoteseka nacho wazee wengi wa jamii za kisasa, ni vigumu zaidi kukitibu.

Katika nchi ambazo wengi ni Waislamu, hata kama maadili yamefifia kiasi gani, hali hii iliyotapakaa katika jamii zingine za kisasa, haifikiriki. Inachukuliwa kuwa ni soni na fedheha kuwatendea watu wazima na wazee bila heshima na kutowajali kiasi hicho. Ni swala la aibu kwa Wailsamu wengi kuitupia serikali majukumu ya ndugu wazee hata kama serikali iko tayari kuwatunza.

Kwa hiyo, dhima ya mwanamke Mwislamu kwa nyumba na familia yake haiishii pale watoto wanapobaleghe. Anaendelea kuwa amebanwa sana kabla na baadae. Ni shauku yake ya wema na ubinadamu na uwezo wake wa asili kuwaangalia wale wanaohitaji kutunzwa, amabayo inakuja kuwaokoa wazee katika jamii. Wanabaki kuwa na thamani na heshima kama kabla na kuendelea kuwa sehemu muhimu ya familia. Mama anafanya sehemu kubwa ya kazi ya kuwaangalia na kuwapa upendo, sio kama sulubu na uchushi, bali kama dhihirisho hai na asilia la udugu wa kibinadamu. Hivyo, atakapozeeka anakuwa na uhakika kabisa jamii ya aina hiyo haitamtupa wala haitamtelekeza kama masalio ya zamani.

Bila shaka, kuna ‘isipokuwa’ katika kila jamii; na kuna mabaki makuukuu ya zamani yanayoonekana kuwa ni

mizigo sumbufu katika baadhi ya familia za Waislamu zinazoishi chini ya athari za mielekeo ya kisasa. Lakini kwa ujumla, jamii za Waislamu zina nyumba chache za wazazi waliotelekezwa kulinganisha na jamii zingine.

Hii inanikumbusha utani mmoja, ambao unaweza ukawafanya watu wengine wacheke, lakini ukawafanya wengine watoe machozi. Siku moja mtoto aliona, akajisikia uchungu sana na masumbuko, kutendewa vibaya kwa babu yake kulikofanywa na baba yake. Taratibutaratibu alihamishwa kutoka kwenye chumba cha ndani chenye kila kitu na raha kupelekwa kwenye chumba kidogo zaidi kisichofaa sana mpaka mwishoni ilipoamuliwa kumpeleka babu kwenye chumba cha mtumishi kilicho uani. Wakati wa masika yenye baridi kuliko kawaida, yule babu alilalamika kuwa chumba chake kina baridi sana na mfarishi wake kuwa mwembamba mno usioweza kumletea joto na raha. Baba akaanza kutafuta blangeti ya ziada kutoka kwenye lundo la matambara ya zamani ya hovyohovyo. Alipoona hivyo, yule mtoto akamgeukia baba yake na akamuomba: Tafadhali usimpe babu matambara yote. Nibakizie baadhi ili niweze kukupayo utakapozeeka.

Katika dhihirisho hili maasumu la kero ya mtoto yamekusanyika masumbuko yote makali ya kizazi kizee katika zama hizi.

Katika jamii za Waislamu, ni mara chache kukuta isipokuwa hizo, kama ilivyo mara chache na inakuwa

mara chache zaidi kukuta isipokuwa katika jamii za kisasa miongoni mwa ndugu katika kuwatendea wazee. Waislamu wanafundishwa:

وَ قَضٰى رَبُّكَ اَلَّا تَعۡبُدُوۡۤا اِلَّاۤ اِيَّاهُ وَ بِالۡوَالِدَيۡنِ اِحۡسَانًا ؕ اِمَّا يَبۡلُغَنَّ عِنۡدَكَ الۡكِبَرَ اَحَدُهُمَاۤ اَوۡ
كِلٰهُمَا فَلَا تَقُلۡ لَّهُمَاۤ اُفٍّ وَّلَا تَنۡهَرۡهُمَا وَقُلۡ لَّهُمَا قَوۡلًا كَرِيۡمًا ﴿٢٣﴾ وَاخۡفِضۡ لَهُمَا جَنَاحَ الذُّلِّ مِنَ
الرَّحۡمَةِ وَقُلۡ رَّبِّ ارۡحَمۡهُمَا كَمَا رَبَّيٰنِىۡ صَغِيۡرًا ﴿٢٤﴾

*Na Mola wako Ameagiza kuwa msimwabudu ye yote ila Yeye tu, na kufanya wema kwa wazazi; kama mmoja wao au wote wawili wakifikia uzee pamoja nawe, katu usiwaambie neno lo lote lenye kuashiria kwamba umechukia wala usiwakemee, bali zungumza nao kwa maneno ya ukarimu. Na uwainikie bawa la unyenyekevu kwa huruma. Na useme: Mola wangu, Uwarehemu kama walivyonilea katika utoto.*[29]

Aya hizi zinahusika sana na somo hili. Baada ya Umoja wa Mungu, binadamu ni lazima, kwa kutumia fikra zao za upendo, mahaba na wema watoe aula ya kwanza kwa wazazi wao ambao wamefikia umri mkubwa na mgumu.

Zaidi ya hayo, aya hizo zinazungumzia hali ambapo tabia ya mzazi mmoja wao au wote wawili inakuwa ya majaribu sana na wakati mwingine ya kuchukiza. Katika kuijibu hiyo, lisitoke kwenye midomo hata dhihirisho dogo la ikirahi au kutoridhia. Kinyume chake, watendewe kwa heshima kubwa.

Msisitizo juu ya uhusiano bora kabisa kati ya kizazi kimoja na kingine, unahakikisha kwamba hakuna nyufa zinazotokea baina ya vizazi. Nyufa hizo daima zinachachawiza upelekaji wa maadili ya kiutamaduni. Kwa hiyo, falsafa ya kijamii ya Islam inafundisha kwamba kizazi chochote kisiruhusu ufa kutokea kati yake na kizazi kinachoondoka na kati yake na kizazi kijacho. Nyufa baina ya vizazi hazitakiwi kabisa katika Islam.

Kama ilivyokwisha semwa hapo kabla, dhana ya familia katika Islam haiishii kwa ndugu wa nyumba moja. Aya ifuatayo inawaagiza Waislamu watoe mafao sio tu kwa wazazi wao, bali pia kwa wana ukoo, ndugu na jamaa ambao wanatajwa baada ya wazazi, kwa kufuata hitari, ili hisia zao za hadhi zisijeruhiwe na upendo miongoni mwao unakuzwa.

وَاعْبُدُوا اللّٰهَ وَلَا تُشْرِكُوْا بِهٖ شَيْـًٔا وَّبِالْوَالِدَيْنِ اِحْسَانًا وَّبِذِي الْقُرْبٰى وَالْيَتٰمٰى وَالْمَسٰكِيْنِ وَالْجَارِ
ذِي الْقُرْبٰى وَالْجَارِ الْجُنُبِ وَالصَّاحِبِ بِالْجَنْۢبِ وَابْنِ السَّبِيْلِ ۙ وَمَا مَلَكَتْ اَيْمَانُكُمْ ۗ اِنَّ اللّٰهَ لَا
يُحِبُّ مَنْ كَانَ مُخْتَالًا فَخُوْرَا ۙ﴿٣٦﴾

*Na mwabuduni Allah wala msimshirikishe na cho chote, na wafanyieni hisani wazazi na pia jamaa za ukoo, na yatima na maskini na jirani miongoni mwa jamaa, na jirani ambaye si jamaa, na rafiki aliye kando (yako), na msafiri, na wale iliyowamiliki mikono yenu ya kuume; bila shaka Allah hampendi Mwenye kiburi, ajivunaye.*[30]

Kurani Tukufu inatamka kwamba ni lazima uwe muangalifu kuhusiana na wema kwa wazazi wako.

Kama jamii ya kisasa itajifunza somo kutokana na amri hizi, matatizo mengi wanayokumbana nayo leo hii na ambayo yanatia dosari kwenye jamii iliyoendelea, yatatoweka. Hakuna nyumba za wazee zitakazohitajika, isipokuwa kwa wazee ambao, kwa bahati mbaya, hawana ndugu wa karibu wa kuwaangalia. Lakini katika jamii ya Kiislamu, upendo kati ya wazazi na watoto unasisitizwa mara ka mara kiasi kwamba inakuwa haiwezekani kwa mtoto kuwatelekeza wazazi wake watakapozeeka ili ajipatie starehe.

## Kizazi Kijacho

Kuhusiana na kizazi kijacho, Kurani Tukufu inaielimisha jamii kwa namna ya kipekee. Inafundisha kwamba ili kupata uhusiano bora kabisa kati yako na watoto wako, ni lazima sana kwamba uhusiano kati yako na mke wako uwe pia mzuri kabisa.

Kuhusiana na jambo hili, aya iliyonukuliwa hapo kabla,[31] inayowazungumzia walezi (Qawwaamuuna), inaweka jukumu zito sana kwenye mabega ya mume. Kama tabia yake hailekei kuleta hali bora kwa ajili ya afya ya maisha ya kifamilia, atashindwa katika dhima yake ya kutenda kama mlinzi (*Qawwaam*). Ni lazima ikumbukwe kwamba mfano bora kabisa wa *Qawwaam* alikuwa ni mwenyewe Mwanzilishi mtukufu[saw] wa Islam. Hakuwa mkali,

dikteta wala kwa namna yoyote ile kero au aliyezidi katika kuonyesha madaraka kwenye uhusiano na familia yake. Kuwadumisha katika njia sahihi lilikuwa jukumu zito, lakini namna alivyolitekeleza jukumu hili kunatoa mfano hai bora kabisa kwa zama zote zijazo kwa wale wote wanaotaka kuchunguza na kuelewa maana halisi ya kivumishi *Qawwaam*.

Katika Hadithi maarufu, Abuu Huraira[ra] anasimilia kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema:

> *Mbora kabisa wa Waaminio katika masuala ya imani ni ambaye tabia yake ni bora kabisa; na walio bora miongoni mwenu ni wale wenye tabia njema kwa wake zao.*[32]

Kama wazazi kweli wanataka watoto wao wawe miongoni mwa jamii ya wachaMungu, ni lazima wakumbuke kwamba uhusiano baina ya waume na wake utakuwa na mchango mkubwa katika kujenga au kubomoa khulka za watoto wao.

Kurani Tukufu inafundisha:

وَ الَّذِیۡنَ لَا یَشۡہَدُوۡنَ الزُّوۡرَ ۙ وَ اِذَا مَرُّوۡا بِاللَّغۡوِ مَرُّوۡا کِرَامًا ﴿۷۳﴾ وَ الَّذِیۡنَ اِذَا ذُکِّرُوۡا
بِاٰیٰتِ رَبِّہِمۡ لَمۡ یَخِرُّوۡا عَلَیۡہَا صُمًّا وَّ عُمۡیَانًا ﴿۷۴﴾ وَ الَّذِیۡنَ یَقُوۡلُوۡنَ رَبَّنَا ہَبۡ لَنَا مِنۡ
اَزۡوَاجِنَا وَ ذُرِّیّٰتِنَا قُرَّۃَ اَعۡیُنٍ وَّ اجۡعَلۡنَا لِلۡمُتَّقِیۡنَ اِمَامًا ﴿۷۵﴾

*Na wale ambao hawashuhudii uwongo, na wanapopita penye upuuzi, hupita kwa heshima. Na wale ambao wanapokumbushwa Aya za Mola wao hawaziangukii*

*kwa uziwi na upofu. Na wale wanaosema: Mola wetu! Utupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho, na Utujaalie kuwa viongozi kwa wamchao (Mungu).*[33]

Dua hii ina haiba ya kipekee na imejaa busara nyingi. Mapatna wote wawili katika ndoa wanafundishwa kuombeana na kuwaombea watoto wao kwamba Mungu daima Awape kinai ya kina na furaha itokayo miongoni mwao, wao kwa wao na pia kutoka kwa watoto na kuwafanya watoto wao kuwa watangulizi na viongozi wa kizazi cha wacha Mungu, kiadilifu.

Inamtaka mtu kulitekeleza fundisho hili binafsi yake kumuwezesha kuelewe kikamilifu umuhimu wa aya hii. Kama unakitaka kitu fulani kimashaka mashaka, hiyo inaweza isiathiri matendo yako vya kutosha, lakini kama ukifanya maombi kwa dhati kwa ajili ya hicho, basi matendo yako ni lazima yataathiriwa na maombi hayo. Kwa mfano, wapo wengi miongoni mwetu wanaotamani kuwa wakweli lakini ni mara chache tu tamaa hii inatafsiriwa kivitendo. Wale wanaomuomba Mungu kwa dhati kwamba Awafanye wawe wakweli, wanaathirika zaidi katika matendo yao kutokana na maombi yao kuliko wale wanaotamani tu kitu bila udhati. Jitihada ya kweli inafanywa katika kunyoosha tabia ya mtu iwe nzuri zaidi. Mtu atakuwa anafanya mzaha sana baada ya maombi hayo kama atamtendea

mke wake na watoto kwa namna isiyopatana na maombi yake.

Ikiwageukia makhsusi kizazi kipya na haki zao na wajibu wao, Kurani Tukufu inaonya:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنْظُرْ نَفْسٌ مَا قَدَّمَتْ لِغَدٍ ۖ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٩﴾

*Enyi mlioamini! Mcheni Allah, na mtu aangalie aliyoyatanguliza kwa ajili ya kesho, na mcheni Allah; hakika Allah Anazo habari za mnayoyatenda.*[34]

Kurani Tukufu inawaonya wazazi kwamba kama watashindwa kutekeleza wajibu wao kwa watoto wao na kuacha nyuma kizazi, ambacho hakishikiki katika tabia zake, basi wazazi watawajibika mbele ya Mungu. Tena, wazazi wanaonywa wasiwaue watoto wao kwa maana kwamba wazazi wanakuwa wanahusika na kuwa ndio sababu kwa namna fulani katika kuharibu tabia zao.[35]

Sio tu watoto wake mwenyewe bali kwamba kizazi kipya chote lazima kitendewe kwa upendo, wema na heshima ni neno la nguvu la ushauri lililotolewa na Mtume Mtukufu[saw] wa Islam:

أَكْرِمُوا أَوْلَادَكُمْ

*Daima kuweni wema kwa watoto wenu.*[36]

Mtu hana budi kuona kwamba hiki ndicho hasa kinachotakiwa na dunia ya kisasa leo hii. Kuna

majadiliano makali yanayoendelea Uingereza, siku hizi, kuhusiana na uwezekano wa kutunga sheria itakayowafanya wazazi wawajibike kiniaba, katika macho ya sheria, kwa makosa yatakoyotendwa na watoto wao na hivyo wakiwa ni wahalifu waadhibiwe kwenye mahakama za watoto. Inahisiwa kwa nguvu kwamba kama wazazi wangetekeleza wajibu wao kuwaadabisha watoto wao kwa umakini zaidi, kungekuwa na makosa machache zaidi yaonekanayo katika mitaa ya Uingereza. Lakini swali ni je kwa kiasi gani hatua za adhabu na za kibano zinaweza kuongeza ubora wa jamii ambapo hakuna usuli wa maadili ya kidini yanayofanya kazi katika kila nyanja za maisha?

## Mambo ya Ufujaji na ya Kipuuzi Yamekatazwa

Kurani Tukufu inaendelea kulijenga somo hili la jamii kwa kutamka:

وَالَّذِيْنَ هُمْ عَنِ اللَّغْوِ مُعْرِضُوْنَ ۙ﴿۴﴾

*Na ambao katika upuuzi ni wajiepushao.*[37]

Wale wenye busara, wanajitanibu na upotezaji wa nguvu zao kufuatilia mambo yasio na faida wala maana.

Kutafuta muda kwa ajili ya burudani nyepesinyepesi si vibaya wala hakukatazwi katika Islam. Lakini kama burudani hiyo inaanza kuweka athari hasi kwenye jamii kwa ujumla, bila shaka haishauriwi. Zaidi ya hivyo, kama badala ya kuwa ni fursa ya kutoa kani za maisha, burudani yenyewe ikawa jambo, itashutumiwa kuwa

*Laghw* (upuuzi na ufujaji) kwa istilahi za Kurani. Kama burudani inaanza kuingilia shughuli za kila siku za kutafuta maisha au inachukua sehemu kubwa ya muda wa mtu ambao ungeweza kutumika vizuri zaidi vinginevyo, nayo pia itahesabiwa kuwa upuuzi sawa na neno la kiarabu *Laghw*.

Luninga zimeleta faida nyingi kwa jamii. Lakini watoto wanakaa siku nzima macho yao yakiwa yamegandishwa kwenye televisheni. Baada ya kurudi toka kazini, kina baba wanaendelea kukaa mbele ya televisheni bila kujali kipindi gani cha TV kiko hewani. Kwa kufanya hivyo, wanapuuza majukumu yao kwa watoto wao, wake zao, marafiki na jamii kwa ujumla. Kwa kweli TV imekuwa hizaya ya kisasa. Muda mwingi sana unapotezwa katika zama hizi katika kuangalia TV kiasi kwamba itakuwa ni vigumu sana na changamoto kwa mtu kujaribu kupima faida na hasara zake. Lakini hilo halitoshi.

Kwa kuonyesha filamu za jinai, TV aghlabu inatoa taswira ya jinai kwa namna ambayo, badala ya kuleta hisia za kuiepuka katika mioyo ya watoto, inafanya kinyume. Hata kwa vipindi maalumu kwa watoto, ni kawaida sana kuona mastaa wakisababisha uharibifu kwa kubuni maajabu ya kierevu yanayotibua amani nyumbani. Vipindi hivyo viwe vinachekesha au kuburudisha kiasi gani, ni wazi kabisa havielimishi. Bila shaka, watoto wengi watukutu wanazalishwa kwa

kuangalia vipindi vya aina hiyo. Mtoto anakuwa akiwa na uwezekano wa kuwa mhalifu.

Katika vipindi vya wakubwa, njia za kivumbuzi za kufanya makosa zinafundishwa bila uangalifu wowote. Maisha ya kupumzikapumzika ya starehe na michezomichezo kuonyesha jinsi maisha yanavyopaswa kuwa yanachorwa kwa kutamanisha sana kiasi kwamba inaacha taswira potofu akilini. Nasikitika ni kidogo sana wanachobaini kuhusu umbali kati ya uwezo wa kubuni na uhalisi na kati ya yaweje na yakoje.

Utafutaji wa starehe za kipuuzi uliokatazwa na Kurani Tukufu sio jambo dogo au lililofanywa bila mpango kama ambavyo wengi wangelichukulia hivyo. Njia hii na nyingine nyingi za burudani zinachangia sana kuleta hali ambapo kiwango cha kukata tamaa kinazidi kupanda. Mtu anashangaa ni lini hali ya kukifu itapatikana.

## Udhibiti Tamaa

Kurani Tukufu inataka udhibiti wa tamaa: wivu usiruhusiwe kuzaa tamaa zisizo na mipaka zisizoridhika.

Fundisho hili lina ujumbe muhimu sana kuhusiana na adabu na upunaji wa tamaa. Islam, bila shaka, sio dini ya ukwepaji au ukaataji wa kitawa au kujinyima raha ambapo mtu anatakiwa kuachana na haja zake zote za asili ili kupata *Nirvana* au kuokolewa kwenye utumwa

wa tamaa. Sawa na falsafa ya *Nirvana,* ni tamaa, ndiyo inayotugandisha kwenye maada na kutufanya tuwe watumwa wa dunia. Jibu rahisi ni kujizuia tamaa zote.

Islam inaikataa falsafa hii kwa kuwa imebuniwa na binadamu, haina uasilia na isiyotosha kutatua matatizo. Dhana ya *Nirvana* iko karibu zaidi na ufu kuliko amani. Islam ina ufumbuzi tofauti kabisa wa kutoa.

Kuua tamaa, sio jibu, sawa na Islam, la kutatua utata wa maisha. Miongoni mwa hatua nyingi zilizopendekezwa ili kuleta amani ya jamii ni agizo kwamba mtu ni lazima aziadabishe na kuzifupisha tamaa zake na daima kuzichunga. Vinginevyo, itakuwa ni jambo lisilowezekana kwa mtu yeyote kupata amani kwa kuzitosheleza tamaa. Kama ilivyosemwa hapo kabla, tamaa daima zinakuja kwa kasi zaidi kuliko mtu anavyoweza kuzifuatilia. Hata zionekane ndogo kiasi gani, hatua hizi zina uwezekano wa ufanisi na ni za muhimu. Kwa mfano, Kurani Tukufu inasema:

وَلَا تَمُدَّنَّ عَيْنَيْكَ إِلَىٰ مَا مَتَّعْنَا بِهِۦٓ أَزْوَٰجًا مِّنْهُمْ زَهْرَةَ ٱلْحَيَوٰةِ ٱلدُّنْيَا لِنَفْتِنَهُمْ فِيهِ ۚ وَ
رِزْقُ رَبِّكَ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ ﴿١٣١﴾

*Wala usivikodolee macho yako Tulivyowafaidisha watu wengi miongoni mwao: ni mapambo ya maisha ya dunia, ili Tuwajaribu kwavyo; na riziki ya Mola wako (Akupayo) ni bora mno na iendeleayo sana.*[38]

Kurani Tukufu inakataza dhana mbaya kwa wengine, au kuwa mdadisi na mdukizi au kusengenya:

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيۡنَ اٰمَنُوا اجۡتَنِبُوۡا كَثِيۡرًا مِّنَ الظَّنِّ اِنَّ بَعۡضَ الظَّنِّ اِثۡمٌ وَّ لَا تَجَسَّسُوۡا وَ لَا يَغۡتَبْ بَّعۡضُكُمۡ بَعۡضًا ؕ اَيُحِبُّ اَحَدُكُمۡ اَنۡ يَّاۡكُلَ لَحۡمَ اَخِيۡهِ مَيۡتًا فَكَرِهۡتُمُوۡهُ ؕ وَ اتَّقُوا اللّٰهَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ تَوَّابٌ رَّحِيۡمٌ ﴿۱۳﴾

*Enyi mlioamini! Jiepusheni kufanya shuku kwa wingi, maana shuku pengine inakuwa dhambi, wala msipeleleze, wala baadhi yenu wasiwatete wengine; je, mmoja wenu anapenda kula nyama ya nduguye aliyekufa? La, hampendi: Na Mcheni Allah, bila shaka Allah ni Mwenye kupokea toba, Mrehemevu.*[39]

## Kujenga Uaminifu na Kutokiuka Amana na Mikataba

Katika jamii ya Kiislamu, ujengaji wa uaminifu una nafasi ya muuhimu sana. Kutokiuka amana na mikataba ya kimataifa kunafikiriwa kuwa ni msingi wa dhana ya umoja katika jamii ya Kiislam. Waaminio wanaelezwa katika Kurani Tukufu kuwa ni wale:

وَالَّذِيۡنَ هُمۡ لِاَمٰنٰتِهِمۡ وَعَهۡدِهِمۡ رٰعُوۡنَ ۙ﴿۹﴾

*Na ambao kwa amana zao na ahadi zao ni waangaliao.*[40]

## Kuondoa Maovu — Jukumu la Wote

Jukumu la kuelimisha watu halijaachiwa serikali bali ni la watu wenyewe kufanya matendo mema na kujiepusha na maovu.

Katika jamii zilizoendelea zaidi, ni jukumu la wasomba taka kukusanya takataka kutoka majumbani na mitaani

kwa ajili ya kuzitupa. Katika nchi masikini zaidi, kina mama wanatupa tu lundo la takataka barabarani mpaka mitaa inakuwa imechafuka kwa takataka na inakuwa tena haifai kama njia za kupita. Bila shaka ni jukumu la wenye nyumba kuzisafisha nyumba lakini ni lazima kuwe na mfumo fulani wa kutunza usafi katika mitaa na njia za kupita.

Inasikitisha kwamba ingawa nchi za Magharibi zimejifunza umuhimu wa hili jukumu la kijamii la kutunza sehemu zinazopitiwa na watu mara kwa mara katika hali ya usafi, bado hazijatambua haja kubwa sana ya kuwa na jukumu la kuitakasa jamii dhidi ya taka jinai za watu ambazo kila siku zinatiririka kutoka majumbani kuelekea mitaani na sehemu za kukaa watu.

Islam inalishughulikia swala hili kwa upana. Himizo la msingi ni kwa wazee wa familia kupunguza taka za jamii ili mema zaidi kuliko maovu yanachangiwa kwenye jamii. Pili, Islam inaliweka jukumu kwa jamii, kwa mtu mmoja mmoja na pia kwa pamoja, kuwa jihadi dhidi ya maovu, sio kwa msaada wa upanga na sheria zuizi, bali zaidi kwa maonyo ya kudumu, ushauri na wosia wa busara. Maonyo na ushawishi kwa subira ni chombo kizuri kabisa, sawa na Kurani Tukufu, kuisafisha jamii dhidi ya maovu ya kijamii:

وَ لۡتَكُنۡ مِّنۡكُمۡ اُمَّةٌ يَّدۡعُوۡنَ اِلَى الۡخَيۡرِ وَ يَاۡمُرُوۡنَ بِالۡمَعۡرُوۡفِ وَ يَنۡهَوۡنَ عَنِ الۡمُنۡكَرِ ؕ وَ
اُولٰٓئِكَ هُمُ الۡمُفۡلِحُوۡنَ ﴿۱۰۵﴾

*Na liwepo miongoni mwenu kundi linaloita kwenye kheri na kuamuru kutenda mema na kukataza maovu, na hao ndiyo watakaostawi, (yaani jamii hizo ndizo zitakazodumu[2]).[41]*

Isihitimishwe kutokana na aya iliyotajwa hapo kabla kwamba utaratibu wa Islam kuhusiana na utunzaji wa afya na ustawi jamii kabisa hauhusishi serikali na dola halina wajibu katika hilo. Bila shaka, maeneo ya sheria na utekelezaji wake ni haki ya serikali. Lakini nilichokuwa najaribu kukisisitiza ni ukweli tu kwamba sawa na Islam, vyombo vya dola pekee havitoshi kuzimisha, kukataza au kupunguza sana uhalifu. Pale tabia za kihalifu zinaporuhusiwa kukua na kumea majumbani na katika jamii kwa ujumla, kitu pekee ambacho serikali inaweza kukifanya ni kuzifuta tu dalili zinapojitokeza. Mzizi wa maovu umezama sana kwa mkono mrefu wa sheria kuweza kuufikia. Ni kazi ya msingi ya familia, viongozi wa dini na viongozi wa maoni ya umma katika kila jamii kuondoa maovu.

Kwa kuizingatia aya hii na nyingine nyingi za namna yake, Mtume Mtukufu[saw] aliwahi kutamka watu wa kabla yenu waliishia kupata majonzi kwa sababu waliziasi mamlaka na walivuka mipaka. Hawakujizuia

[2] Neno *muflihuun* hapa linaweza pia kufasiriwa kuwa wale wenye uwezo wa kuhimili.

wao kwa wao dhidi ya udhalimu walioutenda. Kisha akaendelea:

> Hakika, Wallahi, ni lazima muamrishe mema na kukataza maovu; zuieni mkono wa mhalifu na kumshawishi afanye kwa haki; mjengeni imara katika haki, vinginevyo Allah Ataihusisha mioyo ya baadhi yenu na mioyo ya wengine na Atawaalani kama Alivyowalaani.[42]

Sawa na Mtume[saw], moja ya ishara kubwa ya kuporomoka kwa kaumu ni kwamba wanapoteza ujasiri wa kuonyesha kutoridhishwa kwao kunapotokea mambo ya aibu na tabia mbaya zinaonyeshwa hadharani. Mtume Mtukufu[saw] anaonyesha mfanano kati ya jamii hiyo na wasafiri kwenye merikebu katika Hadithi ifuatayo:

> Nu'maan ibn Bashir anasimulia kwamba Mtume Mtukufu[saw] alisema: Mfano wa wale wanaozingatia mipaka ya Allah na wale wasioijali ni kama wasafiri kwenye meli ambao wanapiga kura kuamua kina nani wakae sehemu ya juu ya meli na kina nani wakae sehemu ya chini na wakajipanga sawa na matokeo hayo. Wale waliokuwa sehemu ya chini walipitia kwa wale wa juu kila mara walipohitaji kuchota maji. Hivyo wakawaambia wale wa juu: Kama tungetoboa tundu katika sehemu yetu basi tusingelazimika kuwasumbua-sumbua. Sasa kama wale wa juu wangewaacha

wale wa chini kutekeleza mpango wao, wote kwa pamoja wangehilikishwa, lakini kama wangewazuia kutekeleza hivyo, wote wangesalimika.[43]

Nionavyo kihuzuni kisa hiki kinahusikana kwa kiwango kikubwa na jamii za kisasa za dunia hii.

## Mahimizo na Makatazo

Baadhi ya Aya kutoka kwenye Kurani Tukufu juu ya majukumu mengine ya kijamii, ambayo huhamasisha amani ni:

وَعِبَادُ الرَّحْمٰنِ الَّذِيْنَ يَمْشُوْنَ عَلَى الْاَرْضِ هَوْنًا وَّ اِذَا خَاطَبَهُمُ الْجٰهِلُوْنَ قَالُوْا سَلٰمًا ﴿٦٣﴾

*Na watumishi wa Rahmani ni wale wanaotembea ardhini kwa unyenyekevu, na wajinga wakisema nao husema: Amani;*[44]

وَ اِذَا حُيِّيْتُمْ بِتَحِيَّةٍ فَحَيُّوْا بِاَحْسَنَ مِنْهَآ اَوْ رُدُّوْهَا ؕ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ حَسِيْبًا ﴿٨٦﴾

*Na mnaposalimiwa kwa maamkio, basi itikieni kwa yaliyo bora kuliko hayo, au mrejeshe hayo hayo; hakika Allah Anafanya hesabu ya kila kitu.*[45]

وَلَا تُصَعِّرْ خَدَّكَ لِلنَّاسِ وَلَا تَمْشِ فِي الْاَرْضِ مَرَحًا ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُوْرٍ ﴿١٩﴾ وَ
اقْصِدْ فِيْ مَشْيِكَ وَاغْضُضْ مِنْ صَوْتِكَ ؕ اِنَّ اَنْكَرَ الْاَصْوَاتِ لَصَوْتُ الْحَمِيْرِ ﴿٢٠﴾

*Wala usiwafanyie watu chuki, wala usitembee katika nchi kwa maringo; hakika Allah Hampendi kila ajivunaye, ajifaharishaye. Na ushike mwendo wa katikati, na uteremshe sauti yako; bila shaka sauti ya punda ni mbaya kuliko sauti zote.*[46]

Mwenendo, ambao Islam inajaribu kuujenga miongoni mwa Waislamu, wenyewe ni kikwazo kwa kukua kwa tabia mbaya na uovu. Islam huleta ardhi yenye afya, ambayo huzuia ukuaji wa vijidudu vya magonjwa na magugu. Lengo hili hufanikishwa kwa maelezo ya kina sana na mafundisho timilifu ya mahimizo na makatazo, ambayo yanafikia idadi ya mamia. Kiini cha kati cha mafundisho haya kinafanana na karibia dini zote. Badala ya kutilia mkazo tofauti za kiitikadi kati ya dini moja na nyingine, naweka baadhi yake mbele yenu pamoja na marejeo husika (sura:aya) ya Kurani Tukufu.

**Mahimizo**

Kuepuka zinaa: 17:33; 23:6–8; 24:31, 34, 61; 25:69; 33:36; 70:30–32.

Usafi: 2:223; 4:44; 5:7; 22:30; 74:5–6.

Kuzuia hasira: 3:135.

Ushirikiano: 5:3.

Ujasiri: 2:178; 3:173–175; 9:40; 20:73–74; 33:40; 46:14.

Kutenda mema: 2:196; 3:135; 5:94; 7:57.

Kuhimiza mema na kukataza mabaya: 3:111.

Kushindana katika kutenda mema: 2:149.

Kurejesha amana kwa uaminifu: 2:284; 4:59; 23:9; 70:33.

Kuwalisha wenye njaa: 76:9; 90:15–7.

Usamehevu: 2:110; 3:135,160; 4:150; 5:7,90; 14:8; 39:8, 67; 46:16.

Kutoa ushahidi wa kweli: 4:136; 5:9; 25:73.

Kuwatendea wema watumishi: 4:37.

Kuwatendea wema majirani: 4:37.

Kuwatendea wema jamaa: 2:178; 16:91; 30:39.

Shukrani: 2:153, 173, 186, 244; 3:145; 5:7, 90; 14:8; 39:8, 67; 46:16.

Unyenyekevu: 6:64; 7:14, 56, 147:16:24, 30; 17:38; 28:84; 31:19–20; 40:36.

Uadilifu/Haki: 5:9; 6:153; 16:91; 49:10.

Kupatanisha baina ya watu: 4:115; 49:10.

Subira/Uvumilivu: 2:46, 154, 156, 178; 11:12; 13:23; 16:127–128; 28:81; 29:61; 39:11; 42:44; 103:4.

Kufanya bidii: 13:23; 41:31–33.

Taqwa: 2:223; 5:7; 9:103, 108; 24:22; 33:34; 74:5; 87:15; 91: 10–11.

Kujizuia Nafsi: 4:136; 7:202; 18:29; 30:30; 38:27; 79:41–42.

Uaminifu wa moyo: 39:3–4; 98:6; 107:5–7.

Ukweli: 4:136; 5:120; 9:119; 17:82; 22:31; 25:73; 33:25, 36, 71; 39:33.

Kuepuka Unibafsi: 2:208, 263; 11:52; 59:10; 64:17; 76:9–10; 92:20–21.

**Makatazo**

Uzinifu: 17:33.

Kiburi: 2:35, 88; 4:174; 7:37

Kusengenya: 49:13.

Majisifu: 57:24.

Udhalilishaji: 49:12.

Dhihaka: 49:12.

Kukata tamaa: 39:54.

Wivu: 113:6.

Ubadhirifu: 7:32; 17:27–28.

Kufuata kile ambacho mtu hana elimu nacho: 17:37.

Maringo: 17:38; 23:47; 31:19.

Kutoa pungufu: 83:2–4.

Kuitana majina mabaya: 49:12.

Ubahili: 4:38; 47:39; 57:2–5; 59:10; 64:17.

Hiana: 4:106,108; 8:28, 59.

Dhana mbaya: 49:13.

Kusema uongo: 22:31; 25:73.

Kuiba: 5:39.

Islam inawaalika viongozi wa dini zote kuungana mikono katika jihadi ya kuhamasisha na kustawisha wema na kukataza matendo maovu.

Kama hili lingetendeka, dunia ingekuwa na hali bora zaidi.

## Kupinga Ubaguzi wa Kimbari

Kati ya laana zote ambazo zimetapakaa zama za sasa, ubaguzi wa kimbari ndio ambao unashikilia hatari

kubwa zaidi kwa amani ya dunia. Kurani Tukufu inawakumbusha sio tu Waislamu bali pia watu wote:

يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوْا رَبَّكُمُ الَّذِىْ خَلَقَكُمْ مِّنْ نَّفْسٍ وَّاحِدَةٍ وَّخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا
رِجَالًا كَثِيْرًا وَّنِسَآءً ۚ وَاتَّقُوا اللّٰهَ الَّذِىْ تَسَآءَلُوْنَ بِهٖ وَالْاَرْحَامَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيْبًا ۝٢

*Enyi watu! mcheni Mola wenu ambaye Amewaumbeni kutoka katika nafsi moja, na Ameumba kutoka katika nafsi ile nafsi mwenziwe, na kutoka katika nafsi hizo mbili Akaeneza wanaume wengi na wanawake; na Mcheni Yeye bilkhususi kwa kuziheshimu fungamano za kidugu; hakika Allah ni Mlinzi juu yenu.*[47]

Hakuna yeyote aliye na ubora zaidi ya wengine. Vivyo hivyo Kurani Tukufu inasema:

يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ اِنَّا خَلَقْنٰكُمْ مِّنْ ذَكَرٍ وَّاُنْثٰى وَجَعَلْنٰكُمْ شُعُوْبًا وَّقَبَآئِلَ لِتَعَارَفُوْا ؕ اِنَّ اَكْرَمَكُمْ
عِنْدَ اللّٰهِ اَتْقٰىكُمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَلِيْمٌ خَبِيْرٌ ۝١٤

*Enyi watu! kwa hakika Tumewaumbeni katika kiume na kike, na Tumewafanyeni mataifa na makabila ili mjuane; hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Allah ni yule amchaye zaidi katika ninyi. Kwa yakini Allah ni Mjuzi, Mwenye habari.*[48]

na

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا يَسْخَرْ قَوْمٌ مِّنْ قَوْمٍ عَسٰۤى اَنْ يَّكُوْنُوْا خَيْرًا مِّنْهُمْ وَلَا نِسَآءٌ مِّنْ نِّسَآءٍ
عَسٰۤى اَنْ يَّكُنَّ خَيْرًا مِّنْهُنَّ ۚ وَلَا تَلْمِزُوْۤا اَنْفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَزُوْا بِالْاَلْقَابِ ؕ بِئْسَ الِاسْمُ
الْفُسُوْقُ بَعْدَ الْاِيْمَانِ ۚ وَمَنْ لَّمْ يَتُبْ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الظّٰلِمُوْنَ ۝١٢

*Enyi mlioamini! Watu wasicheke watu wengine huenda wakawa bora kuliko wao; wala wanawake kwa wanawake huenda wakawa bora kuliko wao. Wala msiwasingizie watu wenu wenyewe, wala msitushane kwa majina ya kupanga. Ni jambo baya sana kujichumia sifa mbaya baada ya kuungama kuikubali imani; na wale wasiotubu hao ndio wadhalimu.*[49]

Kwa muonekano, jamii ya sasa yaelekea kuwa inaachana na ubaguzi wa rangi na inakuwa na ufahamu zaidi wa madhara yanayohusiana nao. Lakini ikiwa mtachunguza suala hili kwa uangalifu zaidi na kwa kina, mtagundua kwamba ubaguzi unapatikana kila mahala.

Tatizo moja kubwa ni ainisho la ubaguzi. Neno hili laweza kuonekana tofauti katika mazingira tofauti. Ni vigumu kuchora mipaka ya mwisho kati ya ubaguzi, kuthamini ubora wa kimatabaka au kidini, ukabila, ufashisti, ubeberu na utaifa. Matendo ya kutisha kabisa na yasiyo ya kibinadamu waliyotendewa Wayahudi kwa mikono ya Wakristo huko Ulaya ya Magharibi kwa miaka zaidi ya elfu moja yaweza kuchukuliwa kuwa ni mambo yaliyozikwa zamani, lakini unyama waliotendewa Wayahudi hivi karibuni katika miaka ya 1930 na 1940 kwa mikono ya Manazi bado ni mbichi mno katika fahamu zetu kuweza kusahaulika. Kwa hiyo wakati tunaposikia neno ubaguzi wa kimbari, mawazo yetu yanajielekeza kwenye kupinga Uyahudi na historia

ndefu ya kutendewa vibaya kwa Wayahudi kwa mikono ya Wasiokuwa Wayahudi.

Huu bila shaka, ni uelewa finyu sana wa ubaguzi wa kimbari .... Ni finyu mno kiasi kwamba maana nyinginezo za taswira hiyo hiyo zinatuponyoka kuzizingatia. Ni nadra mno kwetu kusimama na kufikiria juu ya wenye msimamo mkali miongoni mwa Wayahudi ambao wanawaangalia wasiokuwa Wayahudi kwa mtazamo hasi ule ule wa kutisha ambao wao wenyewe waliwahi kuwa walengwa.

Lakini hayo sio yote. Kuna mengi zaidi katika ubaguzi wa kimbari kuliko yanayofikiwa na jicho. Ubaguzi wa kimbari ingawa hautambuliki wazi wazi kuwa ndiyo yenyewe, unakuwapo chini ya mafichamo mbali mbali, utaifa ukiwa ni mmojawapo. Tena, udini, ukabila na ukanda ni mifano michache tu ambamo ubaguzi wa kimbari unakutwa ukiwa kazini kwa majina tofauti. Ubaguzi wa watu weupe dhidi ya wasio weupe vile vile ni aina za ubaguzi wa kimbari, lakini sio haki kuwalaumu watu weupe tu kwa ubaguzi dhidi ya watu wasio na rangi sawa na yao au maumbile. Upo pia ubaguzi wa watu weusi, ubaguzi wa watu wa manjano na ubaguzi wa watu wale ambao hawawezi kupambanuka kwa rangi kuwa weupe, weusi au wa njano bali wapo kati na kati ya rangi hizo.

Msingi wa ubaguzi wa kimbari ni ubaguzi wa kitabaka. Labda hili ndilo ainisho bora zaidi la ubaguzi wa

kimbari. Kila watu wanapoanza ubaguzi dhidi ya tabaka jingine la watu kwa kulinda maslahi ya tabaka lao, ubaguzi wa kimbari unakunjuka na kuinua kichwa chake chenye sura mbaya na sumu; busara haitumiwi kudhihirisha chuki kama hiyo; sifa binafsi za watu hazizingatiwi; bali sheria huwa kwamba wote ni wa namna moja.

Sio karne nyingi zilizopita, nusu tufe ya Magharibi iligawanyika zaidi baina ya pande ya Ukristo na ya Uislamu. Jukumu lolote lililochukuliwa na Wayahudi katika zama za ubaguzi mkali dhidi ya mashariki ya Waislamu kwa kiasi haliko wazi. Kinachojuilikana hata hivyo, ni ukweli kwamba Wayahudi walikuwa ni sehemu ya Ulaya ya Kikristo, ambayo iliyachukia na kutoyaamini mataifa ya Kiislamu kuzunguka Mediterania na waliogopa kuenea kwa Uislamu kuelekea Magharibi.

Katika kipindi hicho cha chokochoko nzito kati ya Wakristo na Waislamu, kulikuwako na jambo la nyongeza ambalo ni ubaguzi wa kimbari kwa msingi wa tofauti za rangi, katika wakati huo, Waislamu wa Indonesia, Malaysia, China na India walikaa pembeni kabisa na hawakujali kilichokuwa kinaendelea. Ugomvi ulionekana kuwa zaidi kuhusika na Waturuki na Waarabu kwa upande mmoja dhidi ya Ulaya ya Kikristo yote kwa upande mwingine.

Ingawa historia hii yaelekea kuwa imezikwa na kusahaulika, naweza kuiona ikiinua kichwa chake tena. Matatizo ya binadamu kamwe huwa hayafi kwa kudumu hata yaonekane yamazikwa katika kina kirefu kiasi gani. Tukirejea kwenye zama hizi, kwa kuwa dunia iligawanyika pande mbili na mataifa mawili yenye nguvu kubwa pamoja na wenzi wao, ilikuwa ni muhimu kwa faida ya Magharibi kutoamsha maswala kama haya au kuruhusu yaamshwe. Lakini tangu kuchomoza kwa kipindi kipya cha mahusiano ya mashariki na magharibi, usiku wa giza kutoka zama za kale nao pia unakaribia kutupa miali ya kivuli chake cha kichimvi.

Kuna hatari ya kweli ya kufufuka kwa uadui wa kihistoria baina ya Wakristo na Waislamu na baina ya siasa na dini katika mazingira haya mapya yaliyoletwa na mabadiliko makubwa yaliyotokea USSR na Ulaya Mashariki. Hii yaweza kupepelewa zaidi na tamaa binafsi zilizofichika za pande zote mbili. Nahofia kwamba katika hali hii, viongozi wa pande zote wa Wakristo na Waislamu wanaelekea kuchukua jukumu la kufanya uchimvi katika kuzidisha ugumu wa mambo na kuharibu zaidi matumaini ya amani na utangamano kati ya Waislamu na Wakristo. Hili likitokea kwa hakika litakuwa na faida kwa Israeli. Haiyamkiniki kwamba Israeli itakuwa mtazamaji tu asiyeguswa na kuhusika na haya.

Halafu tena, kuna mistari gawanyishi ya kisiasa na kiuchumi ambayo inazalisha aina mpya ya ubaguzi wa kimbari, yaani ubaguzi wa kimbari wa kaskazini tajiri na kusini iliyo maskini, na Magharibi na Mashariki ambayo yaelezeka vizuri kwa:

*Mashariki ni mashariki na magharibi ni magharibi*

*Na kamwe hizi mbili hazitokutana.*

Urafiki na maridhiano ya hivi karibuni baina ya mataifa yenye nguvu kubwa yaweza kufufua malumbano ya kihistoria ya kidini na kisiasa na uadui baina ya Ulaya ya Kikristo na Mashariki ya Uislam. Haitapaswa kabisa kuwa jambo la kushangaza ikiwa Mashariki na Magharibi zitasogea mbali mbali zaidi kutokana na ubeberu mpya na ubaguzi wa kimbari utakaowakumba wengi zaidi ambao ni lazima uzaliwe kutoka kwenye maridhiano ya hivi karibuni baina ya mataifa yenye nguvu kubwa.

Kwa mujibu wa matumizi ya neno yaliyokubaliwa kimataifa, naweza kuonekana kuvuka mipaka ya maana ya ubaguzi wa kimbari na kuipanua kufikia maeneo ambayo hayajulikani kuhusiana na ubaguzi wa kimbari. Lakini mtazamo wangu unatokana na uchunguzi huru na wa kina zaidi wa tashwishi za kibinadamu, ambazo huzaa ubaguzi wa kimbari. Kadri ambavyo nguvu za tashwishi zitabaki kuwa zile zile, kama uiite tabia mbaya ya binadamu inayoonekana kwa jina la ubaguzi wa

kimbari au uiite kwa jina jingine la kiungwana na kistaarabu, kimsingi maradhi ni yale yale.

Ubaguzi wa kimbari, katika maana pana zaidi, inabidi ueleweke kuwa ni ubaguzi wa kundi kinyume na mazingatio ya haki kamili na kutendeana kwa usawa.

Kuyeyuka kwa haraka kwa mtengano kati ya makundi ya Amerika na kunatuingiza kwenye kipindi kipya kabisa ambamo tunaelekea kwenye mafungamano mapya katika dunia zaidi kuliko kutoweka kwa migawanyiko. Kadiri migawanyiko ya kiitikadi inavyofifia, migawanyiko ambayo imeshatambulika katika pande mbali mbali katika mahusiano ya kimataifa ni lazima itaongezeka na kuonekana dhahiri zaidi. Mgawanyiko wa tangu azali kati ya Ulaya Magharibi na Marekani na nchi za Mashariki ulipunguzwa mpaka ukawa sio muhimu na wa nafasi ya pili katika kipindi cha uadui mkubwa baina ya Ubepari na Usoshalisti. Hili kwa kuwa halipo tena sasa, mgawanyiko wa mashariki na magharibi utajitokeza tena kuwa ndio mstari muhimu zaidi wa kugawa baina ya mataifa yaliyoendelea ya magharibi na yasiyoendelea ya mashariki.

Nchi zilizokombolewa za Ulaya ya mashariki pamoja na Urusi zitasogea pole pole na hatimae kuungana na nchi za kibepari na kufuata misimamo ile ile ya kibepari juu ya nchi za ulimwengu wa tatu. Ingawaje uadui mpya utazuka kutokana na kugombea kuyashika na kuyatawala masoko ya nje, kwa ujumla, Magharibi

itatokezea kuwa nguvu kubwa zaidi ya kisiasa na kiuchumi kuliko hapo kabla na hatimae italimeza kundi la Mashariki. Hii italeta nafuu zaidi na kuweka mkazo kwenye mgawanyiko wa tangu zamani kati ya Ulaya Magharibi na Marekani na nchi za Mashariki. Ongezea hapo, kuzaliwa kwa usoshalisti wa kimamboleo, ambapo mataifa yatachukua nafasi ya watu binafsi na makundi ya watu binafsi. Mgawanyiko baina ya wenye vyote na wasio na chochote utaongezeka. Kwa hiyo msuguano utakuwa, sio kati ya matajiri wa taifa moja na harakati zao na maskini wa taifa jingine. Kwa miaka kadhaa inayokuja mgawanyiko huu angamizi waweza kuwekwa chini ya udhibiti na kukosa makali, lakini hatimae mapambano makubwa hayawezi kuepukwa daima.

Nina hofu kubwa kwamba tunaingia katika zama mpya ya ubaguzi wa kimbari wa dunia nzima wa kuchukiza sana kabisa, ambao waweza kusaidiwa zaidi na kutiwa nguvu na kundi la uongozi wa kisiasa wa Wazayoni. Kama Benjamin Beit-Hallahmi wa chuo kikuu cha Haifa na mtunzi wa *"Israel Connection: Whom Israel Arms and Why"*[3] achukuliwe kiuhalisia, na kama ushahidi aliouonesha wa falsafa iliyojengeka vizuri na iliyoainishika vizuri ya Wazayoni, uchukuliwe kuwa ni jambo la kweli jambo hili linatia kifundo kibaya mno katika mlolongo wa matarajio ya kupatikana amani ya dunia.

[3] Kimechapishwa 1988 na I.B. Tauris & Co. Ltd, London.

Picha ifuatayo ya jukumu lililotekelezwa na ambalo bado kutekelezwa na Israel katika maswala ya dunia inajitokeza:

David Ben-Gurion, baba wa taifa la Israel, alisema January 1957:

> *"Kwa muono wa uwepo wetu na usalama, urafiki wa nchi moja ya Ulaya una thamani zaidi kuliko maoni ya watu wote wa Asia. (Medzini, 1976; uk.. 175). uk. 5*

".... Haja ya Israel ya kurejesha ujogoo wake dhidi ya Waarabu imekuja kushabihiana na lengo la Amerika la kuzuia kuporomoka kwa Ubeberu. uk. 205.

> "Kitu ambacho kinapendwa na mtu wa kisasa wa mrengo wa kulia ni Israeli — yenye nguvu kubwa, kali, yenye silaha aina ya "Uzi" na ikiuwa wenyeji wenye ngozi nyeusi katika ushindi dhidi ya nguvu za siasa kali ya ulimwengu wa Tatu. Hivi ndivyo majenerali wa Agentina, Makanali wa Paraguay, mabrigedia wa Ki-Afrikana walivyokuja kuwapenda Waisrael uk. 218.

> "Fikra mpya ya 'tokomeza Ulimwengu wa Tatu' inayoendelea Amerika tangu miaka ya 1970 ilifungamanishwa na Israeli, na waasisi wake kama Daniel Patrick Moynihan na Jean Kirkpatrick wameichukulia Israel kuwa ni mshirika na mtiaji shime.

"Vladimir Jabotinsky, kiongozi wa mrengo wa kulia wa Uzayoni kabla ya vita Kuu ya II, alikuwa wazi kabisa juu ya ushirikiano kati ya Uzayoni na Ubeberu... Uzayoni unayo nia isiyotingishika kubakisha Mediterania nzima kwenye mikono ya Ulaya ... Katika kila mzozo baina ya Mashariki na Magharibi, daima tutakuwa upande wa Magharibi. Kwa kuwa Magharibi imeonyesha ustaarabu bora zaidi kuliko Mashariki katika miaka elfu moja iliyopita baada ya kuharibiwa kwa Ukhalifa wa Baghdad na Wamongolia ... na sisi leo ndio washikiliaji maarufu zaidi wa ustaarabu huo ... Hatuwezi kamwe kuusaidia mwendeleo wa Waarabu ambao kwa sasa unapingana nasi, na tunafurahishwa ndani ya moyo na kila janga liupatalo mwendeleo huu. (Brenner, 1984 uk. 75–77) uk. 227

Wazo la ukombozi kwa kundi la Ulimwengu wa Tatu linatishia msingi wa Uzayoni. Dhana za haki za binadamu ni hatari mno kwa mfumo wa kisiasa wa Israel ... Dhuluma iliyofanywa kwa Wapalestina ni bayana mno na inagusa mno hisia kiasi haiwezi kujadiliwa kwa uwazi na mjadala wowote kuhusu nini Israel imekuwa ikifanya katika Ulimwengu wa Tatu bila shaka utapelekea kwenye kuangaliwa kwa haki za Wapalestina... Wao (Waisrael) ni wepesi kuulaumu ulimwengu wote kwamba ni mnafiki pale maswala ya haki za binadamu na haki

ulimwenguni yanapojadiliwa. Katika hilo wanafanana mno na watu weupe wa Afrika ya Kusini. uk. 236–237.

"Kutoka Manila katika Ufilipino mpaka Tegucigalpa katika Hondurasi mpaka Windhoek katika Namibia, askari wa Israel wamekuwa wakihusika katika vita endelevu, ambayo kwa kweli ni vita ya dunia. Na ni adui gani Israel inapigana naye? Ni watu wa Ulimwengu wa Tatu ambao hauwezi kuruhusiwa kushinda mapinduzi yake. uk. 243.

Matarajio ya hali ya baadae ya Israel yanaonekana kuwa mazuri iwapo tu ulimwengu wa Waarabu, na Ulimwengu wa Tatu wote unaobaki, utaendelea kuwa umegawanyika na mdhaifu. Badiliko lolote katika picha hii litaleta balaa. uk. 247.

Kile ambacho Israel imekuwa ikipeleka nje ya nchi yake ni falsafa ya mkandamizaji, namna ya kuiona dunia ambayo imefungwa kwenye ukandamizaji uliofanikiwa. Kinachopelekwa nje ya nchi sio tu teknolojia, silaha, na uzoefu, sio tu ujuzi bali pia aina fulani ya mtazamo wa kifikra. uk. 248.

Inatumainiwa sana kwamba dhidi ya ukelele huu wa vita ya Uzayoni, sauti ya kundi tulivu zaidi la viongozi wa Israel litashinda. Kati ya waandishi wote wa Israel ambao wanaweza kusemwa kuwa na mtazamo nafuu na hoja makini, Harkabi anaonekana kuwa mfano halisi. Sio

tu hakubaliani na mtazamo wa kutumia nguvu ya kijeshi katika mambo ya siasa wa wazayoni wenye msimamo mkali bali pia kwa dhati kabisa analiona hilo kuwa ni kujiua wenyewe kwa hatima ya mwendeleo wa Uzayoni. Maoni yaliyoelezwa na Harkabi hayakubaliwi sawa sawa na wanafalsafa na wanazuoni wengine wa Kiyahudi. Harkabi, kwa mfano, anashika mtazamo ambao ni wenye hekima na wenye mantiki zaidi juu ya tatizo hili. Hususan, pendekezo lake la "ardhi kwa amani" linafungua mlango wa tumaini kwa Waarabu.

Ninaamini kwa dhati kwamba ubaguzi na juhudi yoyote ya kuwagawa binadamu kwa msingi wowote inaweza kutoa manufaa ya muda mfupi kwa baadhi ya watu, lakini hatimae madhara yake yatakuwa mabaya kwa wote waliohusika. Katika hali hii iliyopo hivi sasa, islam inao ujumbe chanya sana na jukumu fumbuzi la kutekeleza.

Islam inakataza ubaguzi wa kimbari na chuki ya kitabaka kwa kauli thabiti kabisa. Kusababisha machafuko kwa namna yoyote kumekatazwa. Aya za Kurani Tukufu zilizonukuliwa mapema ni chache kati ya nyingi juu ya somo hili.

Mwenendo wa Mtume Mtukufu[saw] wa Islam unaelezwa kuwa ni Mwangaza wa Mungu ambao sio wa Mashariki wala wa Magharibi, yaani ni wa kila upande sawa sawa.

اَللّٰهُ نُوْرُ السَّمٰوٰتِ وَ الْاَرْضِ ؕ مَثَلُ نُوْرِهٖ كَمِشْكٰوةٍ فِيْهَا مِصْبَاحٌ ؕ اَلْمِصْبَاحُ فِيْ زُجَاجَةٍ ؕ اَلزُّجَاجَةُ كَاَنَّهَا كَوْكَبٌ دُرِّيٌّ يُّوْقَدُ مِنْ شَجَرَةٍ مُّبٰرَكَةٍ زَيْتُوْنَةٍ لَّا شَرْقِيَّةٍ وَّ لَا غَرْبِيَّةٍ ۙ يَّكَادُ زَيْتُهَا يُضِيْٓءُ وَ لَوْ لَمْ تَمْسَسْهُ نَارٌ ؕ نُوْرٌ عَلٰى نُوْرٍ ؕ يَهْدِي اللّٰهُ لِنُوْرِهٖ مَنْ يَّشَآءُ ؕ وَ يَضْرِبُ اللّٰهُ الْاَمْثَالَ لِلنَّاسِ ؕ وَ اللّٰهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيْمٌ ۙ﴿۳۶﴾

*Allah ni nuru ya mbingu na ardhi; mfano wa nuru Yake ni kama kishubaka kilichomo taa: taa ile imo katika tungi: tungi lile ni kama nyota ing'aayo, inayowashwa katika mti uliobarikiwa wa mzeituni, usio wa mashariki wala wa magharibi; ni karibu mafuta yake kung'aa ingawa moto haujayagusa — nuru juu ya nuru — Allah Humwongoza kwenye nuru Yake Amtakaye, na Allah Hupiga mifano kwa watu; na Allah ni Mjuzi wa kila kitu.*[50]

Zaidi ya hapo ametambulishwa kuwa:

رَحْمَةً لِّلْعٰلَمِيْنَ ﴿۱۰۸﴾

*Rehema (na chanzo cha baraka) kwa ulimwengu wote (na kwa wanadamu wote).*[51]

Ninashangazwa kuona Wanazuoni wengi wa Kiislam, wenye mawazo ya kizamani, ambao kimakosa wameitwa 'wakereketwa' wanakubaliana na mtazamo kwamba Waislamu lazima wapambane na wasio Waislamu katika vita ya silaha na kubakia vitani na wao mpaka ama waangamizwe au wakubali Islam. Islam, kama inavyokutikana katika Kurani Tukufu, haina uhusiano wowote uwao na fikra hii potovu na fisadi juu

ya 'vita takatifu.' Kwa kuwa aya nyingi zimenukuliwa katika kipengele kinachoshughulika na amani ya kidini, hakuna haja ya kuzirudia.

Hebu nihitimishe kwa kusisitiza kwamba Islam kwa ukweli inafundisha na kupendekeza njia za kuwaleta wanandamu pamoja kupitia mchakato wa amani kwa lengo la kuleta amani duniani na kuwaunganisha wanadamu wote.

Kwa kadiri mtazamo wa Mwanzilishi Mtukufu[saw] wa Islam unavyohusika, nukuu zifuatazo kutoka hotuba ya mwisho (Ijulikanayo kama hotuba ya Maagano) aliyoitoa kabla ya kifo chake mbele ya umati mkubwa zaidi kupita wowote ambao alipata kuuhutubia yapasa itoshe:

> "Enyi watu, nisikilizeni. Kwani sijui kama nitasimama mbele yenu tena katika bonde hili na kuwahutubieni kama ninavyowahutubieni hivi sasa. Maisha yenu na mali zenu zimefanywa salama na Mwenyezi Mungu katika mashambulio ya nyinyi kwa nyinyi mpaka siku ya hukumu. Mwenyezi Mungu Amemteulia kila mmoja sehemu katika urithi. Hakuna 'wasia' utakaokubaliwa sasa utakaokwenda kinyume na haki za mrithi mwenye kustahili. Mtoto mwenye kuzaliwa katika nyumba yoyote atachukuliwa kama mtoto wa baba wa nyumba hiyo. Yeyote atakayekana ubaba huu, kwa mtoto huyu atastahili adhabu chini ya sheria ya Islamu. Yeyote atakayenasibisha uzawa wake kwa

baba ya mtu mwingine, au kwa uongo anadai mtu mwingine kuwa bwana wake, Mwenyezi Mungu, Malaika wake na wanadamu wote watamlaani.

"Enyi watu, mna haki kwa wake zenu, lakini wake zenu vilevile wana haki kwenu. Haki zenu kwao ni kwamba waishi maisha ya utawa na wasishike njia zinazoweza kuleta fedheha kwa mume mbele ya watu wake... Lakini kama wake zenu hawafanyi jambo la aina hii, na mwenendo wao si wa namna inayoweza kuleta fedheha kwa waume zao, basi wajibu wenu ni kuwapatia chakula na nguo na makazi, sawa na hali ya maisha yenu. Kumbukeni hamna budi kuwatendea wake kwa wema. Mwenyezi Mungu Amewapeni nyinyi kazi ya kuwatunza. Mwanamke ni mnyonge na hawezi kulinda haki zake yeye mwenyewe. Mlipowaoa Mwenyezi Mungu Aliwateueni nyinyi kuwa wadhamini wa haki hizo. Mliwaleta wake zenu majumbani mwenu chini ya sheria ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, msiitumie vibaya amana ambayo Mwenyezi Mungu Ameiweka mikononi mwenu.

"Enyi watu, bado mnao baadhi ya wafungwa wa vita. Hivyo basi, ninawanasihini kuwalisha na kuwavisha katika namna ile ile mnayojilisha na kujivisha wenyewe. Kama wakifanya jambo lolote baya ambalo hamwezi kusamehe, basi watoeni kwa

mtu mwingine. Wao ni sehemu ya viumbe vya Mwenyezi Mungu. Kuwapa maumivu au shida haiwezi kuwa haki.

"Enyi watu, ninayowaambieni, lazima msikilize na kukumbuka. Waislam wote ni ndugu. Nyote nyinyi mko sawa. Wanadamu wote wawe wa taifa au kabila gani na wawe wa daraja gani katika maisha, ni sawasawa. Alipokuwa akisema hivi Mtume[saw] (Akinyanyua mikono yake na kuunganisha vidole vya mkono mmoja na vya mwingine aliongeza). Kama vilivyo sawa vidole vya mikono miwili, hivyo ndivyo binadamu walivyo sawa. Hakuna mwenye haki yoyote au fadhila yoyote juu ya mwingine. Nyote mko kama ndugu. Enyi watu, Mungu wenu ni Mmoja na mzazi wenu ni mmoja. Mwarabu hana ubora wowote juu ya asiye Mwarabu, kama ambavyo asiye Mwarabu hana ubora wowote juu ya Mwarabu. Mtu mweupe hana ubora kwa njia yoyote juu ya mweusi na kwa namna hiyo hiyo mtu mweusi hana ubora wowote juu ya mweupe, isipokuwa kwa kiwango kile tu anachotekeleza wajibu wake kwa Mungu na kwa wanadamu wenzake. Anayeheshimiwa zaidi miongoni mwenu mbele ya Mungu ni yule aliye mcha-Mungu zaidi miongoni mwenu...

"Basi kama ambavyo mwezi huu ni mtukufu, ardhi hii ni yenye heshima na siku hii i tukufu ndivyo

> Mwenyezi Mungu Alivyofanya maisha, mali na heshima ya kila mwanadamu kuwa tukufu. Kutoa maisha ya mtu yeyote au kutwaa mali yake, au kumwondolea heshima yake, ni udhalimu na ni kosa kama kuondoa utukufu wa siku hii, mwezi huu, na nchi hii. Ninalowaamuruni leo halikusudiwi kwa leo tu. Linakusudiwa kwa nyakati zote. Mnatazamiwa kulikumbuka na kulitekeleza mpaka mwondoke dunia hii na kwenda katika ulimwengu mwingine kukutana na Muumba wenu...
>
> "Niliyoyasema leo kwenu myafikishe mpaka pembe zote za dunia. Asaa wale wasioweza kunisikia wakafaidika nayo zaidi kuliko wale walionisikia".[52]

Kifungu hicho cha maneno kina nguvu sana na kinajieleza chenyewe. Lakini kimahsusi, cha kuzingatia ni ukumbusho wa Mtume Mtukufu[saw] wa Islam, kwamba sote tu wana wa baba mmoja. Ukweli huu una maana ya dhahiri kwamba dini mbalimbali hazipaswi kuruhusiwa kuugawa udugu wa ulimwengu mzima wa wanadamu ulitokona na mzazi mmoja.

## Marejeo

---

[1] Sura 30: Al-Rum: 42

[2] Sura 103: Al-'Asr: 2–4

[3] Sura 57: Al-Hadid: 21

[4] Sura 24: Al-Nur: 40

[5] Sura 23: Al-Mu'minun: 38

[6] Sura 17: Bani-Isra'il: 50

[7] Sura 23: Al-Mu'minun: 83

[8] Bukhari, Kitabur Riqaq, Babun fil 'Amali wa Tuulihi

[9] Tirmidhi

[10] Sura 74: Al-Muddaththir: 43–47

[11] Sura 2: Al-Baqarah: 285

[12] Sura 17: Bani-Isra'il: 37

[13] Albert Einstein

[14] Sura 59: Al-Hashr: 23–25

[15] Sura 67: Al-Mulk: 2–5

[16] Matthew 7: 16–18

[17] Sura 14: Ibrahim: 25–26

[18] Sura 14: Ibrahim: 27–28

[19] John: 1:1

[20] Sura 11: Hud: 124

[21] Sura 7: Al-A'raf: 55

[22] Sura 16: Al-Nahl: 91

[23] Sura 2: Al-Baqarah: 229

[24] Sura 4: Al-Nisa': 35

[25] Angalia Murder in the Name of Allah cha Mtunzi wa kitabu hiki

[26] Sura 5: Al-Ma'idah: 6

[27] Kwa mfano angalia Sura 57: Al-Hadid: 28

[28] Sura 4: Al-Nisa': 4

[29] Sura 17: Bani-Isra'il: 24–25

[30] Sura 4: Al-Nisa': 37

[31] Sura 4: Al-Nisa': 35
[32] Tirmidhi, Kitabun Nikah, Babu Haqqul Mar'ati 'ala Zaujiha
[33] Sura 25: Al-Furqan: 73–75
[34] Sura 59: Al-Hashr: 19
[35] Mfano Sura6: Al-An'am: 152
[36] Sunan Ibni Majah, Abwabul Adab, Babu Birrilwalidi wal Ihsani Ilal Banati
[37] Sura 23: Al-Mu'minun: 4
[38] Sura 20: Ta-Ha: 132
[39] Sura 49: Al-Hujurat: 13
[40] Sura 23: Al-Mu'minun: 9
[41] Sura 3: Al-'Imran: 105
[42] Sunan Abu Da'ud, Awwalu Kitabil Malahimi, Babul 'Amri wan Nahyi
[43] Bukhari, Kitabus Sharikah, Babun Hal Yuqra'u fil Qismati wal Istihami fihi
[44] Sura 25: Al-Furqan: 64
[45] Sura 4: Al-Nisa': 87
[46] Sura 31: Luqman: 19–20
[47] Sura 4: Al-Nisa': 2
[48] Sura 49: Al-Hujurat: 14
[49] Sura 49: Al-Hujurat: 12
[50] Sura 24: Al-Nur: 36
[51] Sura 21: Al-Anbiya': 108
[52] Sihah Sitta, Tabari, Hisham, Khamis and Baihaqi

Na mfano wa wale wanaotoa mali zao kwa kuitafuta radhi ya Allah na kujiimarisha wenyewe, ni kama mfano wa bustani iliyo mahali pa juu, ikaifikia mvua kubwa na ikaleta matunda yake maradufu; na kama haifikiwi na mvua kubwa, basi hata umande (huitoshea); na Allah Anayaona mnayoyatenda.

- Kurani Tukufu, 2:266

א

Watu wamepambiwa huba ya matamanio ya wanawake na watoto na marundo ya dhahabu na fedha, na farasi wanaotunzwa, na wanyama na mashamba; hayo ni matumizi ya maisha ya dunia; na kwa Allah ndiko kwenmye marudio mazuri.

- Kurani Tukufu, 3:15

# SURA YA TATU

# AMANI YA KIJAMII NA KIUCHUMI

Dini ya Islam ina ushauri pia kuhusu masuala mtambuka ya kijamii na kiuchumi. Kama mafundisho haya yatekelezwe, yatageuza siku zetu za kawaida kuwa nyakati zenye uzuri wa kipekee.

## Uadilifu wa Kiuchumi katika Ubepari, Ujamaa na Uislamu

Haki ya kiuchumi ni kauli mbiu nzuri sana. Wakati ambapo jitihada zimefanyika kuihodhi ili wengine wasiipate, kauli hiyo hiyo mbiu hutumika katika jamii ya kibepari yenye uchumi wa soko huru na pia hutumika katika itikadi ya usoshalisti wa kisayansi ya uyakinifu pembuzi: zote mbili huzungumzia uadilifu. Lakini, kwa kuomba radhi inavyostahili, ni lazima nieleze mfadhaiko wangu kwamba zote zimeshindwa kuitendea haki kikamilifu kanuni hii ya uadilifu wa kiuchumi yenye thamani sana, ila mengi juu ya hili yatafuata baadaye.

Dhana ya uadilifu kamili katika dini ya Islam imeshinda zote na imeenea kote. Inatosheleza jiha zote za mafundisho ya Kiislam. Lakini haiishii hapo, Islam inapiga hatua moja zaidi.

Katika usoshalisti wa kisayansi, juhudi ilifanyika kusawazisha ardhi ya kiuchumi kikamilifu na kisahihi

kabisa kiasi kwamba kunakuwa hakuna miinuko na mabonde yanayobaki. Kama ardhi ya aina hii ikitiwa maji itapata mgawo wake sawasawa. Kunakuwa hakuna suala la madai yoyote ya wasiojiweza wala hofu ya aina yoyote kwa matajiri kutoka kwa tabaka la wanyonge katika jamii kwamba watawapora mali zao za ziada.

Katika jamii ya kibepari wanazungumzia zaidi fursa sawa, viwanja tambarare vya kuchezea na uchumi huria kuliko ugawaji sawa wa mali. Hivyo, daima kunakuwa na uwezekano wa kudai haki na pia kuundwa kwa makundi shawishi kama vile vyama vya wafanyakazi n.k, vinavyodai vingi iwezekanavyo kutoka serikalini au kwa mabepari wengine kwa ajili ya waajiriwa na vibarua ambao daima wanaishi na hisia za kunyimwa.

Ikiwa usoshalisti wa kisayansi utekelezwe kikamilifu, hakutakuwa na haja itakayobaki kwa tabaka lolote la jamii kudai haki. Ama jamii itakuwa tajiri vya kutosha kuweza kugawanya mali ya umma kiusawa sawa na mahitaji, au itakuwa maskini kiasi kwamba itashindwa kuwatimizia mahitaji yao ikimwacha kila mwananchi akigawana umaskini kiusawa. Kwa vyovyote itakavyokuwa, itaishia tu kuwa ni jamii ambamo madai hayatakuwa na dhima yenye maana.

Kwa upande mwingine, mfumo wa kibepari huongozwa na mahitaji. Tabaka la jamii lenye bahati ndogo ni lazima lipewe haki ya kueleza kutoridhika kwake na fursa huru ya kusikilizwa. Ndiyo maana kunakuwa na haja ya

uundwaji wa makundi shawishi na migomo, migogoro ya kikazi, kufungia nje, n.k.

Islam inajenga mazingira ambapo serikali na matajiri daima husisitizwa kwamba ni kwa faida yao wenyewe kustawisha mfumo wa kiuchumi wenye usawa. Vilevile huhimizwa daima kuchunga haki za wengine. Dhaifu kwa maskini wasinyimwe haki zao za msingi za kiuchumi kama vile uhuru wa kujichagulia ajira, fursa sawa ya kupatikana kwa nafasi na mahitaji ya msingi ya maisha. Kukosekana kwa mwelekeo huu maalumu kumesababisha tayari shida, mateso na vurugu nyingi katika historia ya juhudi za binadamu katika kupambana na maisha. Ndiyo maana, Islam hutilia mkazo mkubwa zaidi katika kutoa badala ya kupokea au kulimbikiza. Serikali na matajiri ni lazima wachunge daima kusije kukawepo na tabaka lolote linalonyimwa haki ya msingi ya kibinadamu ya kuishi vizuri. Dola halisi ya Kiislam ingetambua haja na kuchukua hatua mwafaka za kuitimiza. Kabla huzuni haijageuka kuwa vilio na malalamiko na kabla haja haijahatarisha amani na utengamano, chanzo cha huzuni ni lazima kiondolewe na haja itimizwe.

Katika muktadha huu Islam inaonekana kana kwamba inafungamana na jamii za kijamaa, lakini kwa kweli kufanana huku ni kwa juujuu tu. Islam hutimiza lengo lake lakini si kwa njia zilezile za kimabavu kama zilivyoelekezwa katika usoshalisti wa kisayansi. Muda

hauniruhusu nieleze kwa urefu namna ambavyo Islam hufanya bidii kutimiza lengo hili adhimu, lakini kwa kifupi tunaweza kusema kwamba jinsi Islam inavyoshughulikia jambo hili ni tofauti na ile falsafa ya uyakinifu pembuzi isiyovutia na isiyotumia tafakuri. Mfumo wa ujamaa wa Kiislam hufungamana sana na kanuni za asili za ufahamu wa binadamu.

Pamoja na mambo mengine, Islam hujenga mazingira ambapo madai ya haki za mtu yaacha nafasi ya kujali haki za wengine. Kiwango cha kutambua na kujali mateso ya wanadamu wenzako hunyanyuliwa kufikia daraja ambapo wanajamii kwa ujumla hujali zaidi wanawajibika nini kwa jamii kuliko jamii inavyowajibika kwao.

"Mlipe mwajiriwa zaidi kuliko haki yake" ni ukumbusho wa Mtume Mtukufu[saw] wa mara kwa mara kwa wafuasi wake. "Mpatie malipo yake kabla jasho lake halijakauka. Msiwakalifishe watumishi wenu kwa kuwapa kazi msizoweza kuzifanya nyinyi wenyewe. Kadiri iwezekanavyo, walisheni watumishi wenu kile kile mnacholisha familia zenu. Wapatieni mavazi kama ya kwenu. Msivuke mipaka dhidi ya wanyonge kwa namna yoyote, vinginevyo mtawajibika mbele ya Mungu. Ili msije mkamezwa na majivuno yasiyo na msingi yafaa wakati fulani mkae meza moja na watumishi wenu na kuwahudumia."[1]

## Kutoa katika njia nzuri hata kwa dhiki

Hadhi ya utu hutiliwa mkazo sana katika nyanja zote za maisha. Aya zifuatazo za Kurani Tukufu hubainisha kanuni ya kimaadili kuhusiana na mahitaji ya maskini na wenye shida na namna yanavyoweza kutimizwa.

Zawadi ya msamaha kutoka kwa Mungu ni kwa:

الَّذِيْنَ يُنْفِقُوْنَ فِي السَّرَّآءِ وَ الضَّرَّآءِ وَ الْكٰظِمِيْنَ الْغَيْظَ وَ الْعَافِيْنَ عَنِ النَّاسِ ؕ وَ اللّٰهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِيْنَ ۚ﴿۱۳۵﴾

*Ambao hutoa katika (hali ya) faraja na dhiki, na wazuiao ghadhabu na kuwasamehe watu; na Allah Hupenda wafanyao ihsani.*[2]

## Kutoa katika kuwasaidia maskini

Dhana ya sadaka ielewekavyo duniani kwa ujumla ina maana mbili. Kwa upande mmoja, hutoa sifa kwa tabia nzuri za mtoaji wa sadaka. Na kwa upande mwingine hujenga taswira ya kuaibisha kama sio ya kufedhehesha kwa mpokeaji. Kitendo chenyewe tu cha kupokea sadaka humshusha hadhi yake. Islam hugeuza kabisa dhana hii.

Uchanganuzi wa kuvutia umefanyika katika aya ifuatayo ya Kurani Tukufu unaoeleza sababu kwa nini baadhi ya watu ni maskini sana na wengine ni matajiri:

وَفِيْٓ اَمْوَالِهِمْ حَقٌّ لِّلسَّآئِلِ وَالْمَحْرُوْمِ ﴿۱۹﴾

*Sehemu moja ya mali zao huwa ni haki ya aombaye msaada, ombaomba, na ya yule pia asiyeweza kuomba, fukara.*[3]

Kwa kawaida jambo linalokosewa ni matumiza ya neno *hak* linalomaanisha haki, ambalo linaeleza kwa upana na urefu kuhusu mwenendo wa mtoaji sadaka na vilevile mtazamo wa mpokeaji sadaka. Mtoaji hukumbushwa kuwa mali anayowapatia maskini kwa kweli haikuwa ya kwake. Ni lazima jambo fulani halijakaa vema katika iktisadi ambapo baadhi ya watu wanaachwa kuwa mafukara au wanalazimishwa kuomba ili kuishi. Katika mfumo wa kiuchumi ulioshamiri vizuri ufukara usiwepo. Hakuna haja ya kweli ya mtu kuomba ili aishi. Ujumbe unaofikishwa kwa apokeaye sadaka kwamba hakuna haja ya yeye kuona aibu wala kuteseka na hali yoyote ngumu kwani kwa hakika Mwenyezi Mungu Amempa haki ya msingi ya kuishi vizuri na kwa heshima. Kwa hiyo, chochote anachopatiwa na aonekanaye kama mfadhili wake ni haki yake ambayo kwa namna fulani ilihawilishiwa kwa mfadhili.

Kama ilivyoelezwa kabla, mafundisho ya Mwenyezi Mungu yana uhusiano wa moja kwa moja na asili ya binadamu. Amri yoyote inayoweza kutibua usawa katika jamii husawazishwa kwa hatua rekebishi.

## Shukurani

Katika hali iliyozungumziwa hapo juu, bila shaka imo hatari ya asili kwamba baadhi ya watu wasingetoa

shukurani kwa wafadhili wao. Badala ya kuonesha shukurani kwa fadhila yoyote waliyopata kutoka kwa wengine wanaweza wakaishia kusema kwamba kile alichotupatia kilikuwa ni haki yetu. Hakuna haja hata kidogo kwa sisi kumtolea shukurani mtu kama huyu. Kama mwelekeo huu ungekuzwa basi ingekuwa ni kwa kupoteza hulka stahifu na za adabu.

Ikimgeukia mpokeaji wa fadhila, Kurani Tukufu mara kwa mara humkumbusha wajibu wake wa kushukuru na kuonesha shukurani zake hata wa fadhila ndogo kabisa iliyooneshwa kwake. Mwaminio huambiwa mara kwa mara kwamba Mwenyezi Mungu Hampendi mtu asiyeshukuru, kwa mfano:

إِنْ تَكْفُرُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنْكُمْ ۖ وَلَا يَرْضَىٰ لِعِبَادِهِ الْكُفْرَ ۖ وَإِنْ تَشْكُرُوا يَرْضَهُ لَكُمْ ۗ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۗ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ مَرْجِعُكُمْ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ۚ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ٨

*Mkikufuru, basi Allah hana haja nanyi, lakini Haridhii kufuru kwa watumishi Wake; na kama mkishukuru, hayo Atawaridhieni; wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine; kisha marudio yenu ni kwa Mola wenu, basi Atawaambieni yale mliyokuwa mkifanya. Bila shaka Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.*[4]

Akisisitiza zaidi umuhimu wa tabia ya kutoa shukurani, mwanzilishi mtukufu[saw] wa Islam aliwanasihi waumini:

مَنْ لَمْ يَشْكُرِ النَّاسَ لَمْ يَشْكُرِ اللَّهَ

Asiyewashukuru watu hawezi kutoa shukurani kwa Mwenyezi Mungu pia.[5]

Maana yake ni kwamba asiyewashukuru binadamu wenzake, hata kama akitoa shukurani kwa Mwenyezi Mungu, shukurani zake hazitakubaliwa na Mungu. Kwa hiyo adabu, heshima na shukurani hazipingwi na ujumbe uliomo katika aya iliyotangulia ya Kurani Tukufu.[6] Ni ujumbe wa kimya tu kwa mpokeaji fadhila kwamba asiteseke na hali yoyote ngumu na heshima yake ibaki haijavunjika. Hitimisho litakuwa kwamba kutoa shukurani hakuko dhidi ya heshima ya binadamu bali, kinyume chake, huinyanyua zaidi.

Ikimwelekea mfadhili, Islam hukazia mawazo ya aina tofauti kabisa. Huchukuliwa kuwa ni kinyume cha adabu na mwenendo mwema kupokea shukurani kana kwamba ni stahiki yako. Dhana hii hupatikana duniani kote kama sehemu ya silika nzuri, lakini ipo tofauti ya msingi kati ya tabia hii ya duniani kote na mafundisho ya maadili ya Kiislam. Islam humwagiza mfadhili kuwatumikia wanadamu kwa dhamira bora na sharifu zaidi kuliko kutimiza tu matamanio ya kawaida au kupata umaarufu kwa matendo ya ukarimu. Mara kwa mara Islam humkumbusha binadamu kutenda matendo mema kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ili kupata radhi na fadhila Zake tu.

Kutokana na hii ni wazi kwamba Mwislamu halisi anapomsaidia chochote maskini yeyote, kwa kweli

hafanyi hivyo kwa ajili yake mwenyewe au mtu mwingine, bali kwa ajili pekee ya kumridhisha Muumba Wake Aliyemjaalia awali vitu vyote alivyokuwa navyo.

Kwa mwangaza wa kanuni hii, chochote anachowapatia wengine ni kwa kuonesha shukurani zake kwa Mola wake na si kwa ajili ya kumfadhili mtu yeyote. Asili ya dhana hii iliyotukuka ni mojawapo kati ya aya za mwanzo za Kurani Tukufu iwakumbushayo waumini:

وَمِمَّا رَزَقْنٰهُمْ يُنْفِقُوْنَ ۙ۝٣

*Kutoka yale Tuliyowapa hutoa sehemu katika njia Yetu.*[7]

Kwa hiyo, Mwaminio wa kweli huwa hakatai kushukuriwa kwa kuona huruma tu bali anaamini kwa dhati ni kwamba kama kuna yeyote anayepaswa kushukuriwa ni Mwenyezi Mungu pekee wala si yeye. Waislamu wanaofahamu fika maana halisi ya imani, hufadhaika sana kama misaada yao ikishukuriwa. Kurani Tukufu inasema:

وَ يُطْعِمُوْنَ الطَّعَامَ عَلٰى حُبِّهٖ مِسْكِيْنًا وَّ يَتِيْمًا وَّ اَسِيْرًا ۝٩ اِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللّٰهِ لَا نُرِيْدُ مِنْكُمْ جَزَآءً وَّ لَا شُكُوْرًا ۝١٠

*Na huwalisha chakula kwa mapenzi Yake, maskini na yatima na mfungwa, ingawa wao wenyewe ni wahitaji wasema: Tunawalisheni kwa ajili ya radhi ya Allah tu, hatutaki kwenu malipo wala shukurani.*[8]

Kuwalisha watu pekee hakutoshi, bali watakiwa kuwapatia chakula ilhali wewe mwenyewe unaifahamu

maana ya njaa na taabu, na unashirikiana nao katika mateso yao bila kutarajia kuzawidiwa au kushukuriwa.

Uzuri wa aya hii unang'ara sana. Kama waumini wangefundishwa kuonesha mkao wa kujifaragua na kusimanga kwa kukataa tu kupokea shukurani na kujitia upole, kungekuwa na kila uwezekano kwamba hiyo ingezidisha unafiki. Tusemapo, 'usijali', kwa hakika tunafahamu moyoni kwamba kwa kusema hivyo sifa zetu zinaongezeka machoni pa mfadhiliwa.

Fundisho la Kiislam lina utukufu zaidi. Mfadhili hufundishwa kwamba hatakiwi kuuza bidhaa zake mara mbili kwa sehemu tofauti. Kitendo kizuri kinaweza kutendwa ili kupata radhi ya Mwenyezi Mungu ama kusifiwa na watu. Kwa mujibu wa aya hii hatutakiwi kuwa na nia zote mbili kwa wakati mmoja.

Mja halisi wa Mwenyezi Mungu anapomwambia mwenye shida kwamba nia yake hasa ni kumridhisha Mungu, wakati huo huo jambo hili linamkumbusha kwamba Mungu ndiye Mfadhili wake Mkuu. Hivyo, hisia yoyote ya udhalili iwezayo kupatikana huondolewa mbali.

## Fadhila Hazizawadiwi na Binadamu

Katika Islam, kuwa na adabu kwa wengine kusiwe ni tabia ya kujionesha inayotokana na maadili ya ustaarabu tu, bali hutakiwa kujikita katika imani juu ya Mungu. Sadaka zitolewazo kwa maskini zitolewe bila kuwa na

nia moyoni ya kupata chochote baadaye kutoka kwa mfadhiliwa.

وَلَا تَمْنُنْ تَسْتَكْثِرُ ﴿۶﴾

*Wala usiwafanyie ihsani ili upate zaidi.*[9]

Fadhila inapokuwa imeishafanywa kwa yeyote, Islam inamtaka mfadhili kuisahau kabisa kana kwamba halijatukia lolote. Kuonesha kiburi au masimbulizi juu ya mema kwachukuliwa kama kutilifisha na kuvunja heshima ya yale matendo mema. Kinyume cha hayo, mwamini halisi hutenda kama ilivyobainishwa katika aya zifuatazo ambazo zinalinganisha kwa upana tabia nzuri na mbaya:

مَثَلُ الَّذِيْنَ يُنْفِقُوْنَ اَمْوَالَهُمْ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ كَمَثَلِ حَبَّةٍ اَنْۢبَتَتْ سَبْعَ سَنَابِلَ فِيْ كُلِّ سُنْۢبُلَةٍ
مِّائَةُ حَبَّةٍ ؕ وَاللّٰهُ يُضٰعِفُ لِمَنْ يَّشَآءُ ؕ وَاللّٰهُ وَاسِعٌ عَلِيْمٌ ﴿۲۶۱﴾ اَلَّذِيْنَ يُنْفِقُوْنَ اَمْوَالَهُمْ فِيْ
سَبِيْلِ اللّٰهِ ثُمَّ لَا يُتْبِعُوْنَ مَآ اَنْفَقُوْا مَنًّا وَّلَآ اَذًى ۙ لَّهُمْ اَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۚ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَ
لَا هُمْ يَحْزَنُوْنَ ﴿۲۶۲﴾ قَوْلٌ مَّعْرُوْفٌ وَّ مَغْفِرَةٌ خَيْرٌ مِّنْ صَدَقَةٍ يَّتْبَعُهَآ اَذًى ؕ وَاللّٰهُ غَنِيٌّ
حَلِيْمٌ ﴿۲۶۳﴾ يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تُبْطِلُوْا صَدَقٰتِكُمْ بِالْمَنِّ وَالْاَذٰى ۙ كَالَّذِيْ يُنْفِقُ مَالَهٗ رِئَآءَ
النَّاسِ وَلَا يُؤْمِنُ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ ؕ فَمَثَلُهٗ كَمَثَلِ صَفْوَانٍ عَلَيْهِ تُرَابٌ فَاَصَابَهٗ وَابِلٌ فَتَرَكَهٗ
صَلْدًا ؕ لَا يَقْدِرُوْنَ عَلٰى شَيْءٍ مِّمَّا كَسَبُوْا ؕ وَاللّٰهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْكٰفِرِيْنَ ﴿۲۶۴﴾

*Mfano wa wale wanaotoa mali zao katika njia ya Allah, ni kama mfano wa punje moja itoayo masuke saba, katika kila suke punje mia. Na Allah humzidishia Amtakaye; na Allah ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua. Wale wanaotoa mali zao katika njia ya Allah kisha hawafuatishii*

*waliyoyatoa masimbulizi wala udhia, wao wana ujira wao kwa Mola wao, wala haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika. Kauli njema na msamaha ni bora kuliko sadaka inayofuatishwa na udhia; na Allah ndiye Mkwasi, Avumiliaye. Enyi mlioamini, msiharibu sadaka zenu kwa masumbulizi na udhia, kama yule anayetoa mali yake kwa kuwaonyesha watu, wala hamwamini Allah na siku ya Mwisho. Basi hali yake ni kama hali ya mwamba juu yake udongo, kisha ikaufikia mvua kubwa na ikauacha mtupu; hawatakuwa na uwezo juu ya chochote katika wanavyovichuma; na Allah Hawaongozi watu makafiri.*[10]

Vivi hivi,

وَأَمَّا السَّآئِلَ فَلَا تَنْهَرْ ﴿١٠﴾

*Wala usimkaripie aombaye.*[11]

## Kuombaomba

Hata ombaomba hutakiwa kutendewa kwa heshima. Usimkaripie ombaomba. Ingawa kuomba msaada hakuhimizwi lakini haki ya kuomba ikiwa ni lazima inalindwa. Sio hii tu, bali mtu yeyote haruhusiwi kuvunja heshima ya wale walioshurutishwa kuomba msaada.

Mwanzoni mwa Islam, licha ya ukweli kwamba heshima binafsi hata ya ombaomba ililindwa kikamilifu, jamii kwa ujumla ilielewa vizuri kuwa kutokuomba bila shaka

ni bora kuliko kuomba. Mwanzilishi Mtukufu (saw) wa Islam akisisitiza jambo hili alisema:

اَلْيَدُ الْعُلْيَا خَيْرٌ مِّنَ الْيَدِ السُّفْلٰى

*Mkono wa atoaye ni bora kuliko mkono wa apokeaye msaada.*[12]

Matokeo yake ni kuwa Waislamu wengi waliona ni heri kufa na umaskini kuliko kuomba msaada ili kuishi. Ili kuwatimizia mahitaji yao Kurani Tukufu inaikumbusha jamii kwa ujumla kwamba miongoni mwenu wako watu wanaojitahidi katika njia ya Allah wasioweza kujinasua na umaskini:

لِلْفُقَرَآءِ الَّذِيْنَ اُحْصِرُوْا فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ لَا يَسْتَطِيْعُوْنَ ضَرْبًا فِي الْاَرْضِ ۫ يَحْسَبُهُمُ الْجَاهِلُ
اَغْنِيَآءَ مِنَ التَّعَفُّفِ ۚ تَعْرِفُهُمْ بِسِيْمٰهُمْ ۚ لَا يَسْـَٔلُوْنَ النَّاسَ اِلْحَافًا ؕ وَمَا تُنْفِقُوْا مِنْ خَيْرٍ
فَاِنَّ اللّٰهَ بِهٖ عَلِيْمٌ ﴿۲۷۳﴾

*Sadaka hizi ni kwa ajili ya watu maskini waliozuiwa katika njia ya Allah na wasioweza kutembea huko na huko katika ardhi; mjinga huwadhania kuwa ni matajiri kwa sababu ya kujizuia kuomba. Unawafahamu kwa alama zao; hawaombi watu kwa kung'ang'ania. Na mali yoyote mnayotoa, basi kwa yakini Allah Anaijua.*[13]

Kanuni hii hueleweka waziwazi kutokana na aya ifuatayo:

مَآ اَفَآءَ اللّٰهُ عَلٰى رَسُوْلِهٖ مِنْ اَهْلِ الْقُرٰى فَلِلّٰهِ وَلِلرَّسُوْلِ وَلِذِى الْقُرْبٰى وَالْيَتٰمٰى وَالْمَسٰكِيْنِ وَ
ابْنِ السَّبِيْلِ ۙ كَيْ لَا يَكُوْنَ دُوْلَةًۢ بَيْنَ الْاَغْنِيَآءِ مِنْكُمْ ؕ وَمَآ اٰتٰىكُمُ الرَّسُوْلُ فَخُذُوْهُ ۗ وَمَا نَهٰىكُمْ

عَنْهُ فَانْتَهُوا ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۖ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ۝٧

*Mali Aliyoleta Allah kwa Mtume Wake kutoka kwa watu wa vijijini ni kwa ajili ya Allah, na Mtume, na jamaa zake na mayatima na maskini na msafiri; ili isiwe inayorudia baina ya matajiri wenu tu. Na anachowapeni Mtume basi pokeeni, na anachowakatazeni basi jiepusheni; na Mwogopeni Allah; kwa yakini Allah ni Mkali wa kuadhibu.*[14]

Mtume Mtukufu[saw] wa Islam pia alitaja kanuni hii katika Hadithi ambayo sehemu yake ni:

عَنْ حَكِيمِ بْنِ حِزَامٍ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ اَلْيَدُ الْعُلْيَا خَيْرٌ مِّنَ الْيَدِ السُّفْلَى، وَابْدَأْ بِمَنْ تَعُولُ وَخَيْرُ الصَّدَقَةِ عَنْ ظَهْرِ غِنًى . وَمَنْ يَّسْتَعْفِفْ يُعِفَّهُ اللهُ، وَمَنْ يَّسْتَغْنِ يُغْنِهِ اللهُ

Hakim Ibn Hizam[ra] anasimulia: Mtume Mtukufu[saw] alisema: Mkono wa juu ni bora kuliko mkono wa chini (yaani anayetoa msaada ni bora kuliko anayeupokea). Mtu hutakiwa kuanzia na jamaa zake katika kutoa msaada. Kitu bora kilichotolewa kama sadaka ni cha mtu tajiri anachotoa katika kilichobaki baada ya kutimiza mahitaji yake. Anayejiepusha na kuomba mali kama msaada kwa wengine, Allah Atamjaalia na kumsaidia asilazimishwe kuomba watu, na Allah Atamfanya awe anajitegemea.[15]

Kuna hadhi kubwa zaidi utoapo huduma yaani kutoa sadaka na kuwatumikia wengine, badala ya kuwa katika upande wa kupokea sadaka au msaada.

## Nini kinachotakiwa kutolewa kama sadaka?

Mbali na namna ya utoaji, unachotoa ni muhimu pia. Ukitoa kitu ambacho mwenyewe unaona aibu kukipokea kwa mwingine hakiwezi kuhesabiwa kama sadaka kwa mujibu wa Kurani Tukufu. Zaidi ingekuwa mithili ya kukitupa kitu kwenye pipa la taka.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اَنْفِقُوْا مِنْ طَيِّبٰتِ مَا كَسَبْتُمْ وَمِمَّآ اَخْرَجْنَا لَكُمْ مِّنَ الْاَرْضِ ۠ وَلَا تَيَمَّمُوا
الْخَبِيْثَ مِنْهُ تُنْفِقُوْنَ وَلَسْتُمْ بِاٰخِذِيْهِ اِلَّآ اَنْ تُغْمِضُوْا فِيْهِ ۭ وَاعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ غَنِيٌّ حَمِيْدٌ ﴿٢٦٨﴾

*Enyi mlioamini, toeni katika vitu vizuri mlivyovichuma, na katika vile tulivyowatoleeni katika ardhi, wala msikusudie (kutoa) vilivyo vibaya, ambavyo ninyi wenyewe msingevipokea isipokuwa mach o yenu yakiwa yameinamishwa chini kwa huzuni na aibu, na jueni kwamba Allah ni Mkwasi, Asifiwaye.*[16]

لَنْ يَّنَالَ اللّٰهَ لُحُوْمُهَا وَلَا دِمَاۗؤُهَا وَلٰكِنْ يَّنَالُهُ التَّقْوٰى مِنْكُمْ ۭ

*Nyama zao hazimfikii Allah wala damu zao, lakini unamfikia utawa wenu.*[17]

## Kutoa kwa Dhahiri na kwa Siri

Islam huruhusu namna zote mbili; kutoa kwa dhahiri au kwa siri. Kurani Tukufu hufundisha:

وَمَآ اَنْفَقْتُمْ مِّنْ نَّفَقَةٍ اَوْ نَذَرْتُمْ مِّنْ نَّذْرٍ فَاِنَّ اللّٰهَ يَعْلَمُهٗ ؕ وَمَا لِلظّٰلِمِيْنَ مِنْ اَنْصَارٍ ﴿٢٧١﴾
اِنْ تُبْدُوا الصَّدَقٰتِ فَنِعِمَّا هِيَ ۚ وَاِنْ تُخْفُوْهَا وَتُؤْتُوْهَا الْفُقَرَآءَ فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ؕ وَيُكَفِّرُ
عَنْكُمْ مِّنْ سَيِّاٰتِكُمْ ؕ وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرٌ ﴿٢٧٢﴾

*Na chochote mtoacho katika njia ya Allah au nadhiri mnazoweka basi hakika Allah Anajua; na kwa wadhalimu hawatakuwako wasaidizi. Kama mkitoa sadaka kwa dhahiri ni vizuri; na kama mkitoa kwa siri na kuwapa mafakiri, basi huo ni ubora kwenu; na Atawaondoleeni sehemu ya maovu yenu; na Allah Anazo habari za yale mnayoyatenda.*[18]

## Wajibu wa Kijamii

Katika Islam, huzingatiwa sana kwamba wale walio madarakani wawe makini kwa manufaa ya watu kiasi kwamba kusiwe na haja ya kuunda makundi shawishi.

Kwa mujibu wa Kurani Tukufu, mtawala husisitizwa kuwajibika na kuulizwa mbele ya Mwenyezi Mungu kuhusiana na hali halisi ya watu walioko chini ya himaya yake au wale aliopewa dhamana yao. Twasoma katika Hadithi moja ya Mwanzilishi Mtukufu[saw] wa Islam:

كُلُّكُمْ رَاعٍ وَكُلُّكُمْ مَسْئُوْلٌ عَنْ رَعِيَّتِهٖ

*Kila mmoja wenu ni kama mchungaji wa kondoo, aliyeaminishwa na jukumu la kuwachunga kondoo. Ndiyo maana mtaulizwa.*[19]

Hadithi hii hutaja uhusiano mbalimbali ambapo mtu anaweza kuwa msimamizi wa watu wengine. Kwa mfano, mtawala kwa watumishi, mama ambaye ni mlezi wa nyumba na baba ambaye ni mkuu wa familia, ambao wote wawili huwajibika kwa familia nzima. Pia, mwajiri ambaye huwajibika kwa waajiriwa chini ya uangalizi wake na kadhalika. Kila mara Mtume Mtukufu[saw] alirudia: Kumbukeni mtawajibishwa na mtaulizwa.

## Mfano katika historia ya mwanzo ya Islam

Siku moja Hadhrat Umar[ra] Khalifa wa pili wa Islam, wakati wa usiku alikuwa akipita kwenye mtaa katika vitongoji vya Madina. Ilikuwa ni kawaida yake kutembea mitaani asitambulike ili aone mwenyewe moja kwa moja kile kinachoendelea kwa watu walio chini ya mamlaka yake. Alisikia katika nyumba moja watoto wakilia ambao walionekana kuwa katika uchungu fulani. Udadisi wake ulibainisha kwamba kulikuwa na takriban watoto watatu wakikaa karibu na moto ambao juu yake kuna maji yakichemka ndani ya birika au chungu na mama yao alikuwa amekaa pamoja nao. Akauliza, nini kimetokea? Mama akajibu: 'Wanangu wana njaa. Sina cha kuwalisha. Kwa ajili ya kuwatuliza tu nimetia maji na mawe kwa kiasi katika birika au chungu ili ichukuliwe kama chakula kinapikwa. Hicho ndicho unachoona.'

Kwa uchungu mwingi na sikitiko, Hadhrat Umar[ra] mara moja akarudi ofisini kwake. Akachukua unga, siagi,

nyama na tende na kuzitia kwenye mfuko. Akamwambia mtumwa aliyesimama karibu kumsaidia kumtwika mfuko mgongoni. Mtumwa akamuuliza Hadhrat Umar[ra] kwa mshangao kwamba kwa nini alitaka kubeba mzigo yeye mwenyewe na akaomba kwamba aruhusiwe kubeba mfuko badala yake. Hadhrat Umar[ra] akajibu, leo unaweza kabisa kubeba mzigo huu ila nani atanibebea mzigo wangu siku ya Kiyama? Alimaanisha kwamba siku ya Kiyama yule msaidizi wake hawezi kuulizwa badala yake kuhusu utekelezaji wa majukumu yake. Ni lazima atekeleze mwenyewe. Hii ilikuwa namna ya kafara aliyojilazimisha Hadhrat Umar[ra] kwani alifikiri mwenyewe ni mhusika wa mateso na taabu ya yule mama maskini na watoto wake. Aliona mji wote na mambo mengine yaliyouzunguka kwa kweli ni wajibu wake na ni kama amana ambayo mwenyewe anatakiwa kuitimiza.

Ni muhali kwa mkuu wa serikali yoyote kuiga kama alivyofanya Hadhrat Umar[ra] lakini bila shaka kwa namna zote yeye ni mfano bora. Mfano huu unatakiwa kuigwa na jamii zote za zama hizi duniani kote. Ikiwa serikali zinajali mateso ya watu, wale walioko madarakani watalizimika kuchukua hatua tatuzi hata kabla watu wenyewe hawajalalamikia mateso yao na hisia za kuonewa. Hii haitakuwa kwa sababu ya hofu ya malalamiko bali ni kutokana na sauti ya ndani ya nafsi zao.

## Mipaka mipana ya utoaji

Kurani Tukufu hupanua wigo wa kile kinachotolewa katika njia ya Allah kwa mapana na marefu. Sentensi moja inajirudia mara kwa mara ndani ya Kurani Tukufu ambayo ni vigumu kupatikana sehemu zingine, ni:

وَمِمَّا رَزَقْنٰهُمْ يُنْفِقُوْنَ ۝

*Na waumini halisi hutoa katika njia Yetu kutoka katika yale Sisi Wenyewe Tuliyowajaalia.*[20]

Kauli hii hukusanya kila uwezo, kipawa na pia bila shaka aina zote za mali na mahusiano na mafungamano ya wanadamu. Vilevile hubeba maadili kama heshima, amani, starehe na kadhalika. Kwa kifupi, kila kitu kinachoweza kufikiriwa kimo ndani ya mawanda ya maneno ya Kiarabu *wa mimmā razaqnāhum.*

Aidha, la kustaajabisha ni namna neno *min* lilivyotumika hapa ambalo maana yake ni sehemu au chochote katika kitu fulani. Neno hili limerahisisha agizo hili ili liweze kuzingatiwa na watu wote. Aya hii haimaanishi kwamba mnatakiwa kutoa katika njia Yetu kila Tulichowapa au sehemu yake maalumu. Bali maana yake ni hii kwamba mnatakiwa kutoa chochote katika yale Aliyowapa Allah. Dhana ya '*kitu chochote*' ni pana kiasi kwamba hata wanyonge wasioweza kutoa mali maridhawa angalau wanaweza kushiriki katika mchango kadiri wawezavyo. Islam hufanya bidii katika ukuzaji wa mazingira haya ya huduma za jamii.Upande mmoja yanahusu tabia ya mtu

katika jamii na upande mwingine yanahusu mienendo yake ya kiuchumi.

Ni vigumu sana na muhali kutofautisha kati ya mema na mabaya katika jamii ambapo watu wote wanaelekea zaidi kuhodhi na wanahusika na faida yao tu. Yawezekana kabisa jamii ya aina hii kuingilia haki za wengine badala ya kubaki katika mipaka yake.

Upande mwingine, jamii ambayo daima hukumbushwa na kufundishwa kuwapa wengine zaidi hata kuliko haki zao ni mbali kabisa na kunyang'anya haki zao. Katika hali kama hii, unyanyasaji hauwezi kutokea.

## Kuwatumikia Wengine

Msingi wa dhana ya Islam ya kutumikia wengine umebainishwa vizuri na kikamilifu katika aya moja isemayo:

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ ۗ وَلَوْ
آمَنَ أَهْلُ الْكِتَابِ لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ ۚ مِنْهُمُ الْمُؤْمِنُونَ وَأَكْثَرُهُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿١١٠﴾

*Enyi Waislamu! Ninyi ni umati bora mliotolewa kwa ajili ya manufaa ya watu wote, mnaamuru yaliyo mema na mnakataza maovu, na mnamwamini Allah. Na kama watu wa Kitabu wangaliamini ingalikuwa bora kwao; kati yao wako waaminio, na wengi wao ni wavunjao amri.*[21]

Mtabakia kuwa umati bora maadamu mtakuwa na moyo wa kutumikia wengine. Mkishindwa kuwatumikia

wengine, hamtakuwa na haki ya kujivunia ubora wa Islam na umma wa Waislamu.

## Uharamu wa kunywa pombe na kucheza kamari

Mtu akizungumzia ulevi kwa kawaida anafikiria madawa ya kulevya. Kuna maana nyingine ya ulevi katika mawanda mapana ambayo ni nadra sana kuhusishwa na neno lenyewe. Ninamaanisha namna jamii inavyoona aina za starehe kama vile pombe na kamari. Zote mbili haziashirii uzuri kwa amani na manufaa ya jamii.

Mchezo wa kamari umerasimishwa takribani katika nchi zote zilizostawi duniani. Katika baadhi ya nchi za Ulimwengu wa Tatu ambapo mchezo huo haujarasimishwa kwa kiwango kikubwa lakini unapatikana katika ngazi zote kama kazi binafsi kwa muda mfupi. Ulevi wa pili ni kunywa pombe ambao jamii za dunia nzima zimesumbuliwa nao sana.

Kurani Tukufu huharamisha kucheza kamari na kunywa pombe:

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِنَّمَا الْخَمْرُ وَ الْمَيْسِرُ وَ الْاَنْصَابُ وَ الْاَزْلَامُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطٰنِ
فَاجْتَنِبُوْهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُوْنَ ﴿٩١﴾ اِنَّمَا يُرِيْدُ الشَّيْطٰنُ اَنْ يُّوْقِعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةَ وَ الْبَغْضَآءَ فِي الْخَمْرِ وَ
الْمَيْسِرِ وَ يَصُدَّكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللّٰهِ وَ عَنِ الصَّلٰوةِ ۚ فَهَلْ اَنْتُمْ مُّنْتَهُوْنَ ﴿٩٢﴾

*Enyi mlioamini! bila shaka vileo na kamari na masanamu (ya kuabudu) na mishale (ya ramli) ni uchafu wa kazi ya Shetani. Basi jiepusheni nayo, ili*

*mpate kufaulu. Hakika Shetani anataka tu kuunda uadui na bughudha kati yenu kwa njia ya vileo na kamari na kuwazuilieni kumkumbuka Allah na kusali. Basi je, mtaacha?*[22]

Mtume Mtukufu[saw] alisema pombe kuwa:

أُمُّ الْخَبَائِثِ

*Mama ya maasi yote.*

Ulewi wa aina zote mbili umetapakaa kotekote duniani kiasi kwamba ni vigumu kuzitenganisha. Pande za Mashariki na Magharibi haziungani kidhahiri, lakini kwa kiasi kikubwa sana pande za Mashariki na Magharibi na vilevile Kaskazini na Kusini zimekwishaungana tayari katika kuzielekea kamari na pombe.

Kunywa pombe na kucheza kamari zote mbili ni maovu ya kijamii na kiuchumi. Kila siku kiasi ambacho hutumika kwa kunywa pombe katika Uingereza kinaweza kutosheleza chakula cha wingi wa watu wa Afrika wanaotaabika na njaa kwa majuma mengi. Hata hivyo, katika nchi za Afrika na mabara mengine yaliyoshikwa na ufukara, pombe haichukuliwi kama anasa ambayo watu hawamudu kuilipa. Mamilioni ya Waafrika huwa wanaweza kupata vileo kirahisi hata kama wanashindwa kujikimu mahitaji ya msingi ya maisha au kuwasomesha watoto. Kusini mwa India ambapo kwa sababu ya umaskini vileo

vilivyotengenezwa kiwandani havipatikani kwa wote, divai ya kienyeji hutumika badala yake. Kwa hali yoyote umaskini huwa unapunguza kwa kiasi fulani kutapakaa kwa 'mama ya maovu yote'. Ikiwa mapato kwa kila mtu yanaongezeka vilevile matumizi ya vileo pia huongezeka. Hakuna anayejali jambo hili mpaka mwenyewe anakuwa mlevi sugu.

Hapa mtu anaweza akafikiria kuwa kwa sababu gani vileo na kamari zinachukuliwa kama matatizo ya zama hizi ingawa kwa kweli vitu hivi ni vya zama za kale tangu historia ya binadamu ifahamike. Naam, vileo na kamari vilipatikana katika zama na sehemu zote duniani na zinaweza kuchukuliwa kama matatizo ya kila zama kwa sababu haviwezi kupitwa na wakati.

Kiuchumi, mchezo wa kamari huchukiza zaidi kuliko kileo. Katika kamari fedha huuzwa kwa mwingine bila kusababisha uchumi usonge mbele. Mfano wake ni kama fedha zinavyobadilishwa katika taasisi za kubadilishia fedha bila ya mabadilishano muhimu ya bidhaa. Kwenye kamari fedha huzunguka mikononi mwa watu bila kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na uzalishaji wa mali. Ni kweli katika taasisi za kubadilishia fedha, faida ya kiuchumi inapatikana japo kwa kiasi tu lakini katika mchezo wa kamari faida hiyo haipatikani kabisa. Katika biashara huria na ukuzaji wa viwanda, fedha haziwezi kuzunguka mikononi mwa watu bila kupata faida inayochangia uchumi. Katika biashara, mara nyingi

mabadilishano ya fedha hufaidisha washiriki wote. Haiyumkiniki wafanyabiashara wengi aghlabu kupata hasara. Katika kamari, kwa kawaida mara zote wengi wa washiriki hupoteza. Lakini kasino zinafilisika nadra sana. Maelfu ya watu hupata hasara kwa faida ya wachache tu. Thamani pekee wanayoipata baada ya kupoteza mali ni msisimko wa taharuki na hatimaye wanajikuta wakiwa wameshindwa bao. Halafu wanaanza tena kuweka dau wakiona uwezekano mdogo wa kufidia hasara na wanaendelea mpaka mfadhaiko na wasiwasi unazidi sana kushinda furaha ya taharuki iliyopatikana awali. Mateso ya akili na huzuni havibaki kuwa tatizo la mtu mmoja tu bali zinaanza kuathiri vibaya mahusiano ya kifamilia. Katika matabaka ya chini ya jamii hata mahitaji ya lazima ya wanafamilia husahauliwa kabisa kutokana na mchezo wa kamari. Kurani Tukufu pamoja na kuharamisha vileo na kamari inakubali kwamba zinaweza kabisa kuwa na manufaa kwa kiasi lakini kwa hakika mara zote madhara yake hushinda manufaa yake:

يَسْـَٔلُوْنَكَ عَنِ الْخَمْرِ وَ الْمَيْسِرِ ؕ قُلْ فِيْهِمَآ اِثْمٌ كَبِيْرٌ وَّ مَنَافِعُ لِلنَّاسِ ۫ وَ اِثْمُهُمَآ اَكْبَرُ مِنْ نَّفْعِهِمَا ؕ وَ يَسْـَٔلُوْنَكَ مَا ذَا يُنْفِقُوْنَ ۬ؕ قُلِ الْعَفْوَ ؕ كَذٰلِكَ يُبَيِّنُ اللّٰهُ لَكُمُ الْاٰيٰتِ لَعَلَّكُمْ تَتَفَكَّرُوْنَ ۙ﴿۲۲۰﴾

*Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema: Katika hivyo mna dhambi kuu na manufaa kwa watu pia, lakini dhambi yao (hasara) ni kubwa zaidi kuliko manufaa*

*yao. Na wanakuuliza watoe nini. Sema: Vilivyo vizuri. Hivi ndivyo Allah Anavyowabainishieni Aya ili mpate kutafakari,*[23]

Mjadala huu unaweza ukazuka kuwa namna ya kujifurahisha na hela zako haitakiwi kumhusu mtu mwingine yeyote. Yampasa kila mtu afurahie atakavyo na jamii haina haki ya kujiingiza katika mambo ya binafsi kiasi kwamba mtu anaambiwa namna ya kutumia pato lake.

Lakini hili pia likumbukwe kuwa mafundisho ya kidini hutolewa kama miongozo na maonyo tu. Hatua dhibiti katika dunia hii hazina nafasi katika mafundisho ya dini yoyote isipokuwa katika baadhi ya makosa ya jinai yaliyofanywa dhidi ya watu ambayo yanastahiki adhabu hata kwa mtazamo usio wa kidini. Kama vile mauaji, uporaji, utapeli, uharibifu na unyang'anyaji wa haki. Zaidi ya hayo kwa mtazamo wa dini kuna makosa mengine ya kijamii yanayoangamiza jamii kwa jumla. Ndiyo maana adhabu ya makosa haya huwa haitolewi kwa mtu mmoja mmoja bali jamii yote huteseka. Na kwa hakika hukumu hutolewa kwa mujibu wa sheria pana za kijamii. Si jambo la kushangaza kwamba baada ya muda mfupi matumizi ya vileo na kamari hugeuka kuwa maangamio kwa jamii nzima.

Aidha, inaendelea kuwa vigumu zaidi kugharimia jamii za aina hii na sehemu kubwa ya mali ya umma huendelea kupotea bure. Katika hali kama hii watu

hukata tamaa. Makosa ya jinai huendana sawa na ulevi na kamari. Mateso na huzuni za watu wengi hutokana na ulevi na kamari na hivyo ndivyo mshikamano kati ya familia huharibika. Matokeo yake ya lazima ni kuvurugika kwa mfungamano baina ya wanafamilia na kuvunjika kwa uhusiano baina ya mume na mke.

Ulevi una madhara ya kifedha na vilevile ya kijamii kama yalivyotajwa katika jarida la *Scientific American*. Mbali na machafuko nyumbani kuna matukio ya ubakaji wa watoto, maharimu na watu wengine kwa sababu ya kutokuona aibu katika kuvuka mipaka kutokana na athari ya ulevi na hali yake ya hatari.

Takwimu za vifo vya watu:

- Kupungua kwa miaka kumi katika matarajio ya muda wa kuishi wa walevi.
- Kuongezeka kwa idadi ya vifo maradufu katika wanaume kuliko kawaida na mara tatu zaidi kuliko kawaida katika wanawake.
- Kuzidi kwa walevi katika kujiua mara sita kuliko kawaida.
- Kileo ni sababu kuu ya vyanzo vinne vya kifo katika watu wenye umri kati ya miaka 25 na 44 ambavyo ni ajali za barabarani (asilimia 50), mauaji (asilimia 60), kujiua na ugonjwa sugu wa maini kutokana na pombe.

Hasara ya kifedha kila mwaka:

- Hasara ya mazao — Billioni $ 14.9
- Gharama ya matibabu — Billioni $ 8.3

| | |
|---|---|
| • Hasara katika ajali | Billioni $ 4.7 |
| • Hasara katika kuteketea kwa moto | Billioni $ 0.3 |
| • Hasara ya mashambulio makali | Billioni $ 1.5 |
| • Gharama itumikayo na jamii ili kupinga mambo yaliyotajwa juu | Billioni $ 1.9 |
| • Hasara kwa jumla ya matumizi mabaya ya ulevi | Billioni $ 31.6 |

Katika jamii nyingi duniani ulevi, kamari, muziki, dansi na aina nyingine za starehe huchukuliwa kama matendo yasiyo na madhara. Huwa zinaelezwa kama sehemu muhimu za tamaduni mbalimbali. Ingawa namna za utekelezaji hutafautiana katika jamii moja na nyingine lakini vipengele vya msingi ni vile vile. Tukiachana na sanaa ya uchongaji nakshi, uchoraji n.k, mambo mengi yaliyotajwa hapo awali hayabaki bila ya kudhuru utamaduni wa jamii bali yanakera vikali na wakati mwingine yanalemaza na kuvunja uti wa mgongo wa jamii. Jamii huwa haiwezi kudhibiti mwelekeo wake bali kwa kawaida ulevi, kamari, muziki, dansi n.k zinavuta macho ya watu. Kwa kasi zinawaathiri vibaya vijana kiasi kwamba wanaanza kufuata kawaida ya watu bila kutafakari.

Kwa kuona jamii za aina hii mtu anaweza akaelewa kwamba kufuata starehe na kujitia kabisa katika matamanio ya nafsi ndiyo shabaha ya uumbaji wa binadamu.

La hasha kwa mujibu wa mafundisho ya Islam.

إِنَّ فِيْ خَلْقِ السَّمٰوٰتِ وَ الْاَرْضِ وَ اخْتِلَافِ الَّيْلِ وَ النَّهَارِ لَاٰيٰتٍ لِّاُولِي الْاَلْبَابِ ﴿۱۹۰﴾ الَّذِيْنَ
يَذْكُرُوْنَ اللّٰهَ قِيٰمًا وَّ قُعُوْدًا وَّ عَلٰى جُنُوْبِهِمْ وَ يَتَفَكَّرُوْنَ فِيْ خَلْقِ السَّمٰوٰتِ وَ الْاَرْضِ ۚ رَبَّنَا مَا
خَلَقْتَ هٰذَا بَاطِلًا ۚ سُبْحٰنَكَ فَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿۱۹۱﴾

*Kwa hakika katika uumbaji wa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana ziko Ishara kwa wenye akili; Ambao humkumbuka Allah wakiwa wima na wakikaa na wakilala kibavu na huutafakari uumbaji wa mbingu na ardhi: Mola wetu, Hukuviumba hivi bure; utukufu ni Wako, basi Utuepushe na adhabu ya Moto.*[24]

Kauli hii imetolewa na Kurani Tukufu ili kuwasifu waja wa Allah wenye busara. Ambao baada ya kutafakari juu ya mambo ya uumbaji wa maisha, hukiri kwa moyo mmoja kwamba lazima kuna shabaha ya uumbaji, hauwezi kuwa bure.

Aya hizi za Kurani Tukufu hukumbusha furaha ilivyooneshwa katika kauli ya Archimedes alipoguta *Eureka*! *(nimegundua*).

Kwa hiyo, hizi ni hali mbili tofauti kabisa. Kwa mujibu wa Kurani Tukufu binadamu ameumbwa ili kutimiza shabaha njema ya kufuata njia inayomwongoza kwa Muumba wake. Kwa kuchukua maana hii pana ya ibada, Kurani Tukufu inasema:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْاِنْسَ اِلَّا لِيَعْبُدُوْنِ ﴿۵۶﴾

*Sikuwaumba majinni na watu ila wapate kuniabudu.*[25]

Kwa kuchunguza aina zote za starehe, huenda watu hawaoni madhara kiasi kinachosababisha kuipiga marufuku hata aina moja. Hususani katika jamii zenye uhuru usio na mipaka watu hawawezi kuelewa sababu ya Islam kuwa dini iliyo na mawazo makali yasiyovutia. Sivyo, Islam si dini ambayo haivutii kama inavyoonekana kwa juujuu. Kwanza, watu wenye silika nzuri hupata ladha ya hali ya juu katika matendo mema yaliyochukuliwa kwa nje kama hayana ladha. Pili, wale waliozidi kujaaliwa na upendo halisi wa Allah, huongezeka katika utakaso wa hali ya juu kiasi kwamba ladha za kidunia kwao zinaonekana duni, zenye thamani ndogo, zisizo na maana na za muda mfupi. Tatu, katika mawanda mapana, jamii isiyokuwa na kawaida ya kutafuta starehe haiwezi kamwe kuingia hasarani. Katika uchambuzi wa mwisho, inabainika kuwa sio tu mabadilishano ya thamani bali hali ya furaha kubwa na matamanio ya nafsi kupata starehe kupita kiasi zinabadilishwa na amani, utulivu, usawa, usalama zaidi, uungwana na kutoshelezeka ambazo ni bora zaidi kama zawadi kuliko zote.

Wakati mazingira haya mawili ya kijamii yanapolinganishwa kwa ujumla wake, sio vigumu kabisa kuelewa kwamba kwa nadra sana mti wa mapenzi ya Mungu na kunyenyekea kwake waweza kustawi katika mazingira ya jamii inayoishi kwa starehe. Bila shaka, kuna hali zisizo za kawaida lakini hali hizo

haziwezi kuchukuliwa kama kanuni. Mazingira haya mawili ni tofauti kabisa.

## Marejeo

---

[1] Vyanzo mbalimbali vya Hadithi za Mtume[saw]
[2] Sura 3: Al- 'Imran: 135
[3] Sura 51: Al-Dhariyat: 20
[4] Sura 39: Al-Zumar: 8
[5] Tirmidhi, Kitabul Birri Was Silati 'An Rasulillahi, Babu Ma Ja'a Fishshukri Liman Ahsana Ilaika
[6] Sura 39: Al-Zumar: 8
[7] Sura 2: Al-Baqarah: 4
[8] Sura 76: Al-Dahr: 9–10
[9] Sura 74: Al-Muddaththir: 7
[10] Sura 2: Al-Baqarah: 262–265
[11] Sura 93: Adh-Dhuhaa: 11
[12] Bukhari, Kitabuz Zakat, Babun La Sadaqata illa 'An Zahri Ghinan
[13] Sura 2: Al-Baqarah: 274
[14] Sura 59: Al-Hashr: 8
[15] Bukhari, Kitabuz Zakat, Babun La Sadaqata illa 'An Zahri Ghinan
[16] Sura 2: Al-Baqarah: 268
[17] Sura 22: Al-Hajj: 38
[18] Sura 2: Al-Baqarah: 271–272
[19] Bukhari, Kitabun Nikah, Babun Al-Mar'atu Ra'iyatun fi Baiti Zaujiha
[20] Sura 2: Al-Baqarah: 4
[21] Sura 3: Al- 'Imran: 111
[22] Sura 5: Al-Ma'idah: 91–92
[23] Sura 2: Al-Baqarah: 220
[24] Sura 3: Al- 'Imran: 191-192
[25] Sura 51: Al-Dhariyat: 57

Allah Hufuta riba na Hukuza sadaka, na Allah hampendi kila aliyethibitika kuwa kafiri na mtenda dhambi mkuu.

- Kurani Tukufu, 2:277

א

Siyo! Bali ninyi hamuheshimu mayatima, Wala ninyi hamhimizi juu ya kulisha maskini. Nanyi mnakula urithi kwa ulaji wa pupa, Na ninyi mnapenda mali kwa pendo la kupita kiasi.

- Kurani Tukufu, 89 : 18 - 21

# SURA YA NNE

# AMANI YA KIUCHUMI

## Falsafa za Uchumi wa Kibepari, Kijamaa na Kiislam

Mpangilio wa uchumi wa Kiislam hautokani na ubepari wala ujamaa. Falsafa ya uchumi wa Kiislam ni ya kisayansi pasipo kukosa busara. Imewekewa nidhamu isiyo na vikwazo vingi. Falsafa ya uchumi wa Kiislam inaruhusu umiliki binafsi wa mali na uanzishwaji wa biashara ila haihamasishi uroho na ulimbikizaji mali kwa walio wachache na kuacha sehemu kubwa ya jamii ikigeuka kuwa fukara, watwana na watumwa wanaotumikia mfumo wa kinyonyaji ulio dhalimu na unaokosa huruma. Kuna tofauti tatu za msingi zinazotofautisha falsafa ya kiuchumi ya ubepari, ujamaa na Uislam.

## Ubepari

Kwenye mfumo wa ubepari fedha huzawadiwa kwa riba. Kwa asili inakubalika kimsingi ya kwamba mtaji una haki ya kukua. Katika mfumo wa kibepari riba ndiyo msingi unaoleta nguvu ya kuhodhi fedha zinazosambazwa kama nishati ya kuwashia mtambo unaoufanya uzalishaji uzunguke. Kwa ufupi riba ni kichocheo kinachofanya fedha ziendelee kuzunguka.

## Ujamaa

Kwenye ujamaa, ingawa hakuna kichocheo cha riba kuweza kuzungusha na kuendelea kujizungusha kwa fedha ili ziweze kuzalisha, serikali ndiyo inayohodhi fedha. Hivyo hakuna haja ya motisha.

Katika mfumo huru wa biashara, haijalishi kama mtu ametoa au hajatoa riba, jambo la muhimu ni mtu kujiona mmiliki binafsi wa fedha kunakozalisha hamasa na msukumo wa kutaka kukuza kwa kasi ya haraka iwezekanavyo kipato chake. Ikiwa mtu atatakiwa kulipa riba kwa fedha aliyokopa, kiwango cha riba kinakuwa ni kipimo kinachofanyakazi kama dirisha linalosaidia kuona na hivyo kufuatilia ulinganifu wa ukuaji au upunguaji wa kipato. Katika mfumo wa uchumi wa kijamaa msukumo huu unakosekana kwa sababu wale wanaoshughulika na fedha hawazimiliki na hakuna namna ya kufanya ulinganifu unaomfikisha mtu kwenye maamuzi yanayotokana na kuona kiwango cha ukuaji kama ni chenye manufaa kibiashara au la.

Kwenye mfumo wa ujamaa kunakuwa na umiliki wa nguvu wa fedha zote za nchi kunakofanywa na serikali yenyewe ambako kunaufanya utaratibu wa riba uonekane hauna haja yoyote na usio na maana kabisa. Tatizo ni pale unapokosekana msukumo wa aina yoyote wa kupata faida zaidi ya riba inayotakiwa kulipwa kunakosababisha kukosa kabisa motisha na kuondoa kabisa uwajibikaji.

Ingekuwa fedha zote zilizo kwenye mzunguko katika nchi ya kijamaa zithaminishwe kwa kuangalia kiasi cha riba ambacho kingeweza kupatikana kama fedha hizo zingewekwa benki, hiyo ingetupa hali halisi ya upande mmoja wa picha. Upande mwingine ungejitokeza kwa kufanya tathmini ya kiuchumi kwa misingi ya faida na hasara. Bila shaka ingepita kwenye ugumu tofauti kama vile kufanya tathmini ya mishahara n.k ila kama wataalam wa mambo ya kifedha wakune vichwa juu ya jambo hili, vizuizi kama hivyo vinaweza kutafutiwa ufumbuzi. Kulinganisha mambo haya mawili kungetuonesha mambo kadhaa mazuri yanayo-wezekana.

Inawezekana sana kwa kufanya hivi wahalifu halisi wa kushuka kwa ubora wa maisha wangeng'amuliwa vizuri zaidi. Hata bila kufanya zoezi kubwa kama hilo, haioneshi kuwa ni kazi ngumu kuzing'amua sababu za kushuka kwa ubora wa maisha. Ninaamini ya kwamba kwa sababu serikali inakuwa ndiye bepari inajinyima utaratibu wa ufuatiliaji ili kujihadhari na hatari inayosababishwa na uharibifu, upotevu na kuboronga kunakotokana na namna mtaji wa umma unavyoendeshwa. Hii ni kwa sababu serikali haina majukumu ya kufanya ya kifedha na hivyo inaweza hata kutumia mtaji huo pasipo uwajibikaji wowote. Hiyo ndiyo hali iliyotapakaa pamoja na hatari zake za asili. Ukosefu wa msukumo binafsi na kutokuwepo mfumo wa tahadhari juu ya faida au hasara inayotokana na

matumizi ya fedha inaharibu kabisa uwiano wa juhudi inayofanyika na matokeo yanayopatikana. Pia kiwango cha uharibifu kinazidi kuongezeka.

Halafu hakuna ukaguzi unaowekwa kwenye sera inayosimamia ugawanyaji wa fedha. Kwa mfano hakuna kipimo kwa serikali za kijamaa kinachoweza kuamua kiwango halisi cha ukuaji wa uchumi ikilinganishwa na uchumi wa soko huria unaotumiwa na upande mwingine wa ulimwengu. Tatizo jingine linaloongezeka kwa nchi za kijamaa ni matumizi makubwa kwa ajili ya ulinzi, udukuzi na uendeshaji wa vyombo vya sheria ndani ya nchi zao. Mambo mengine yakiwa sawa, ulinzi na usalama pekee huchukua sehemu kubwa ya matumizi yasiyo na utaratibu. Haya na mambo mengine kama hayo husababisha matumizi mazito katika uchumi. Bila shaka kwa muktadha huu hatima ya kuanguka kwa uchumi inaweza tu kucheleweshwa lakini haiwezi kuepukwa kabisa.

## Dhana ya Kiislamu

Wakati ujamaa hautoi motisha yoyote kwa anaejihusisha moja kwa moja kwenye shughuli za uzalishaji mali, Islam inatoa motisha licha ya kukataza riba. Islam inaondoa riba bila kushirikiana na matatizo maalum yanayoukumba ulimwengu wa kijamaa. Pasipo riba inayovuta mtaji kwenye njia zisizozalisha mali, Islam yazuia mtaji usiotumika. Kuzuia huku ni kwa sura ya 'kodi' inayofahamika kama Zaka. Zaka haitozwi

kutokana na mapato au faida bali hutozwa mtaji wenyewe.

Utofauti upo bayana sana. Katika jamii za kibepari fedha hukusanywa kwenye mikono ya wachache. Kwa sababu ya uroho fedha huongezeka kwa malimbikizo ya riba na huzungushwa tena kwenye mfumo wa uchumi kwa kazi maalum iliyoelekezwa kupata faida kubwa zaidi ya kiwango cha riba kilichopo. Kwenye Uislamu kwa kuchelea kupungua kidogo kidogo kwa fedha zisizozunguka kutokana na kulipa Zaka, yeyote mwenye ziada ya akiba yake analazimika kuitumia kupata faida itakayoziba pengo linalotokana na kulipa Zaka.

Kwa mujibu wa Uislamu, jibu la matatizo ya kiuchumi yanayoukabili ulimwengu haliwezi kupatikana kwenye ujamaa wala ubepari. Si rahisi kulifafanua somo hili kwa sasa ila kutakuwa na mada itakayoangalia ukosefu wa ulinganifu wa kiuchumi uliosababishwa na ubepari ili kupata maarifa yatakayosaidia baadae.

## Sifa Nne za Jamii ya Kibepari

Alama zinazoitambulisha jamii isiyo na usawa zimeelezwa bayana katika aya zifuatazo za Kurani Tukufu.

كَلَّا بَل لَّا تُكْرِمُونَ الْيَتِيمَ ﴿١٧﴾ وَلَا تَحَاضُّونَ عَلَىٰ طَعَامِ الْمِسْكِينِ ﴿١٨﴾ وَتَأْكُلُونَ التُّرَاثَ أَكْلًا لَّمًّا ﴿١٩﴾
وَتُحِبُّونَ الْمَالَ حُبًّا جَمًّا ﴿٢٠﴾

*Siyo! Bali ninyi hamuwaheshimu mayatima, Wala ninyi hamhimizi juu ya kuwalisha maskini. Nanyi mnakula*

*urithi kwa ulaji wa pupa, Na ninyi mnapenda mali kwa pendo la kupita kiasi.*[1]

Kwa ufupi alama za jamii yenye ukosefu wa usawa zimebainishwa kuwa ni:

1. Kutowatendea kwa heshima mayatima
2. Ulishwaji wa maskini hauchagizwi
3. Kujitwalia urithi wa wengine
4. Ulimbikizaji mali usiokoma

## Hatima ya Ubepari ni Maangamio

Pasi na kuunga mkono falsafa ya kijamaa, Islam inakataa baadhi ya mambo ya kibepari kwa sababu:

أَلْهَىٰكُمُ التَّكَاثُرُ ﴿١﴾ حَتَّىٰ زُرْتُمُ الْمَقَابِرَ ﴿٢﴾ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٣﴾

*Yamekughafilisheni mashindano yenu ya kujilundikia mali. Kiasi ya kwamba mmeyazuru hata makaburi. Tahadharini karibuni mtajua.*[2]

## Mpangilio wa Kiuchumi wenye Mabadiliko

Unyonyaji wa wananchi maskini zaidi kupitia ubepari uliojikita kwenye riba uliosababisha maasi kwa wenye kuamini ujamaa ni kama jambo lililopitwa na historia. Ila ikichunguzwa kwa kina itabainika ya kwamba haya ni kama mabadiliko tu ya mitindo ya mavazi.

Ulimwengu kwa ujumla umegawanyika kwa matajiri na maskini kulikosababishwa na unyonyaji unaofanywa na nchi zilizoendelea za kibepari. Hali hii ikijumuishwa na

kurejea kwa kasi kwenye ubepari kunakofanywa na nchi zenye majuto za Ulaya ya Mashariki, mtu hupigwa na butwaa kwa kuona kiasi kikubwa zaidi cha damu kitakachofyonzwa kutoka kwenye nchi zilizodhoofishwa zisizo na hata damu za ulimwengu wa tatu. Ila inaonekana ya kwamba wanyonya damu wa kibepari ni lazima tu wachote damu zaidi.

Ni dhahiri kwamba zama zimekwisha za mapambano baina ya miamba miwili yenye mitazamo ya kiuchumi inayohasimiana ya kibepari na kijamaa. Mfumo wa kiuchumi uliofuata misingi ya ki-Marx na Lenin imeshindwa kufua dafu mbele ya jukwaa la mahitaji ya kibinadamu. Upande mwingine kinachoitwa uchumi huria wa Magharibi unaonekana kushangiliwa kwa ushindi dhahiri. Kwa kuizuia China, nchi za Ulaya ya Mashariki bado zinajitahidi kupunguza ukali wa machungu ya maumivu ya kundi kubwa la wasio nacho katika nchi zao kwa kisingizio cha uhuru mpya walioupata.

Pengo la kiuchumi baina ya Magharibi na Mashariki sio kubwa kuliko lile lililopo baina ya Kaskazini na Kusini. Nchi za Ulimwengu wa Kwanza za Kaskazini zimegawika katika uwanda mwingine unaoanzia nchi za Uulimwengu wa Tatu za Afrika na Amerika ya Kusini. Ingawa ikiangaliwa tofauti ya kiuchumi pengo baina ya Amerika ya Kaskazini na ile ya Kusini inaleta maumivu, ukweli ni kwamba hakuna ukaribu wowote wa pengo la

kiuchumi baina ya Ulaya na Afrika. Kijiografia Afrika imekaribiana mno na Ulaya, lakini kupitia vipimo vya kiuchumi Afrika ndiyo iliyojitenga mbali zaidi na Ulaya.

Hali ya kujiona salama ambayo nchi maskini ziliwahi kuipata kutokana na uhasama baina ya nchi zenye nguvu, na kama kulikuwa na fursa yoyote ya kujinufaisha kwa nchi masikini sana kutokana na kuyeyuka kwa vita baridi, hali hizo zote zitapotea haraka sana. Badala yake kutakuja kuwa na ushindani mkubwa wa kweli baina ya nchi za Merikani, Urusi na Ulaya nzima wakigombea kuteka, kumiliki na kujihakikishia masoko ya nchi za Ulimwengu wa Tatu.

Japan haitaendelea kubaki kuwa mshindani pekee wa Marekani. Kuna Ulaya mpya inayochomoza kutokana na kuimarika haraka kwa Jumuiya ya Ulaya na ushiriki unaotarajiwa wa nchi za Ulaya Mashariki kwenye soko pana la pamoja utasababisha ushindani mkali zaidi kwa Marekani kuliko inaoupata sasa kutoka kwa mahasimu wake wa nchi za Ulaya.

Makundi ya mamilioni ya watu wa Ulaya Mashariki na Urusi wana matarajio makubwa na wanataka kwa nguvu zote kuboresha hali ya viwango vyao vya ubora wa maisha. Kurekebisha masoko yaliyojifunga pekee hakutatosheleza mahitaji makubwa ya nchi hizi yanayoongezeka kadiri muda unavyokwenda. Kuna ulazima kwa masoko ya nje kusaidia upanukaji na ukuaji wa viwango vya hali njema za maisha ya

wananchi wa Ulaya Mashariki na Urusi  kunakoweza kutimizwa na Jumuiya ya Ulaya, Marekani na Japan. Mategemeo ni hafifu kwa nchi za Ulimwengu wa Tatu kuweza kufikia fursa za masoko haya na hasa kwa watu wa bara la Afrika walio na bahati ndogo.

Wanasiasa wa nchi za ulimwengu ulioendelea kiuchumi na kisiasa wanajali zaidi mapinduzi ya kiuchumi wa kibepari yanayotokea mashariki ya mbali  — Japani, Korea ya kusini, Formosa, Hong Kong na Singapore na inaonekana umbali baina ya Mashariki ya Mbali na Magharibi umeshapunguzwa kwa kiunganishi kilichoegemezwa kwenye vichwa vya nchi nyingi maskini za bara la Asia – Indonesia, Malesia, Kambodia, Tailandi, Bama, Bangladeshi, India, Sirilanka na Pakistani.

Inawezekana pia kwamba ili kukabiliana na changamoto inayoongezeka ya uchumi mkubwa wa Japan na katika kuweka kipimo cha uchumi wake unaopanuka kwa kasi, nchi nyingine za Mashariki ya Mbali zisingependelea tena kuwa wanufaika wa teknolojia na fedha kutoka Marekani. Kwa upande mwingine inawezekana Marekani ikaegemea zaidi kwa marafiki zake wa Mashariki ya Mbali ili kuweza kukabiliana barabara na changamoto mbalimbali kutoka Japan na nchi zenye uchumi mkubwa zaidi za Muungano wa Ulaya. Hii inatabiri hali mbaya ya maisha ya mwanadamu kwani

inaweza hatimaye kuzima kabisa ndoto za kupata amani kwa sababu ya mwelekeo mpya ulio tofauti kabisa na mweleko uliozoeleka wa falsafa zinazohasimiana za kibepari na kijamaa.

Ni mapema mno kutabiri namna mabadiliko ya huko Ulaya Mashariki na Urusi yatakavyoathiri ulinganifu wa uchumi ulimwenguni na kama urejeaji wa nchi za Ulaya Mashariki kwenye mfumo wa ubepari utakuwa kwa ukamilifu au wa kiasi, kwa taratibu au kwa kasi? Lolote likitokea, jambo moja halina shaka ya kwamba mabadiliko haya yataendelea kuathiri vibaya zaidi hali ya uchumi wa nchi za Ulimwengu wa Tatu. Hali hiyo haitadumu kwani tayari ulimwengu unaelekea kwenye msiba mkubwa.

Islam inao ushauri kwa nchi ambazo kwa sasa zinaufurahia sana ubepari uliosimama kwenye msingi ulio mtupu ndani wa riba. Nchi hizi hatimaye zitajikuta zikiporomoka chini na kupasuka vipande vipande. Kile kinachoitwa ushindi uliopatikana hivi karibuni wa ubepari dhidi ya ujamaa hakuleti amani ya kudumu. Falsafa zenyewe za kibepari zitakuja kuzaa mashetani wenye nguvu watakaopata maumbile mapevu kwa haraka bila ya washindani kutoka kwenye Ujamaa. Hatimaye Volkano ya ubepari itakuja kulipuka kwa mshindo ambao ulimwengu wote utatingishika, kutetemeka na kusambaratika.

## Mfumo wa Kiuchumi wa Kiislamu

Kuhusiana na mfumo wa jamii unaoshauriwa na Islam, mfumo wa uchumi wa Kiislam unaanza kwa kauli ya msingi kwamba vitu vyote vilivyomo mbinguni na ardhini vimeumbwa na Mwenyezi Mungu Ambaye Amemjaalia mwanadamu mali na uwezo mbalimbali kama dhamana tu. Akiwa mdhamini mwanandamu ataulizwa namna alivyoitumia dhamana hii. Hali yote ya kupata au kukosa mali imewekwa kuwa njia ya majaribio ili wale wanaokumbuka juu ya kuulizwa kwao watofautishwe na walioamua kuwa sugu wakikumbuka kwa nadra sana shida za wanadamu wengine.

Kurani Tukufu mara kwa mara inatukumbusha kwamba:

وَلِلّٰهِ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۗ وَاللّٰهُ عَلٰى كُلِّ شَیْءٍ قَدِیْرٌ ﴿١٩٠﴾

*Na ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Allah; na Allah ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.*[3]

Halafu Kurani inafundisha ya kwamba ikiwa kila kitu kimetengenezwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya wote, baadhi ya vitu ni lazima vigawiwe miongoni mwa watu.

اَمْ لَهُمْ نَصِیْبٌ مِّنَ الْمُلْكِ فَاِذًا لَّا یُؤْتُوْنَ النَّاسَ نَقِیْرًا ﴿٥٣﴾

*Ama wanayo sehemu ya ufalme? Basi hapo wasingaliwapa watu hata sawa na tundu la kokwa ya tende.*[4]

وَاللّٰهُ فَضَّلَ بَعۡضَكُمۡ عَلٰى بَعۡضٍ فِى الرِّزۡقِ‌ۚ فَمَا الَّذِيۡنَ فُضِّلُوۡا بِرَآدِّىۡ رِزۡقِهِمۡ عَلٰى مَا مَلَـكَتۡ
اَيۡمَانُهُمۡ فَهُمۡ فِيۡهِ سَوَآءٌ‌ ؕ اَفَبِنِعۡمَةِ اللّٰهِ يَجۡحَدُوۡنَ ﴿٧٢﴾

*Na Allah Amewafadhilini baadhi yenu kuliko wengine katika riziki. Lakini wale waliofadhiliwa hawarudishi riziki zao kwa wale iliowatamalaki mikono yao ya kuume ili wawe sawa katika (riziki) hii. Basi je, wanazikataa neema za Allah?*[5]

Wajibu wa mwanandamu ni kuitendea na kuitekeleza dhamana hii kwa haki na uadilifu mkubwa.Katika sehemu nyingine Kurani Tukufu inaeleza kwamba:

اِنَّ اللّٰهَ يَاۡمُرُكُمۡ اَنۡ تُؤَدُّوا الۡاَمٰنٰتِ اِلٰٓى اَهۡلِهَا ۙ وَاِذَا حَكَمۡتُمۡ بَيۡنَ النَّاسِ اَنۡ تَحۡكُمُوۡا بِالۡعَدۡلِ‌ ؕ
اِنَّ اللّٰهَ نِعِمَّا يَعِظُكُمۡ بِهٖ‌ ؕ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ سَمِيۡعًۢا بَصِيۡرًا ﴿٥٩﴾

*Hakika Allah Anawaamuruni kuzirudisha amana kwa wanaozistahili, na ya kwamba mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu; bila shaka mawaidha Anayowatoleeni Allah ni mazuri sana; Hakika Allah ndiye Asikiaye, Aonaye.*[6]

Juu ya ukweli kwamba mali ni chanzo cha majaribio imeelezwa ndani ya Kurani Tukufu kama ifuatavyo:

اِنَّمَاۤ اَمۡوَالُـكُمۡ وَاَوۡلَادُكُمۡ فِتۡنَةٌ‌ ؕ وَاللّٰهُ عِنۡدَهٗۤ اَجۡرٌ عَظِيۡمٌ ﴿١٦﴾

*Bila shaka mali zenu na watoto wenu ni jaribio na kwa Allah kuna ujira mkubwa.*[7]

Kuna msingi muhimu katika umiliki (wa mali) kwa mujibu wa Islam; nao ni kuondolewa kwa baadhi ya

rasilimali kutoka katika umiliki wa watu binafsi na kuwekwa kwenye umiliki wa wanadamu wote. Hivyo rasilimali kama za madini na mazao ya bahari haziwezi kuwa mali binafsi ya mtu yeyote au kundi lolote la watu.

**Zaka**

Zaka ni moja ya nguzo tano za Kiislam — nyingine zikiwa ni kushuhudia ya kwamba hakuna Mungu ila Allah na Muhammad[saw] ni mjumbe Wake; kusali; kufunga saumu ya Ramadhan; na kuhiji katika nyumba ya Allah iliyoko Makka. Kurani Tukufu inaamrisha ya kwamba:

وَ اَقِيْمُوا الصَّلٰوةَ وَ اٰتُوا الزَّكٰوةَ وَ اَطِيْعُوا الرَّسُوْلَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُوْنَ ۝٥٧

*Na simamisheni Sala na toeni Zaka na mtiini Mtume, ili mrehemewe.*[8]

Kwa Kiarabu neno Zaka lina maana ya kukitakasa kitu. Na katika mazingira ya kuifanya Zaka kuwa ni kodi ya lazima itamaanisha mali iliyotakaswa tena halali kwa waaminio iliyobaki baada ya kutoa zaka.

Kwa kawaida Zaka hutozwa kwa kiwango cha 2.5% ya mali iliyofikia kiasi maalum kilichopangwa ambayo wamiliki wamekaa nayo kwa zaidi ya mwaka mmoja. Ingawa mengi yameshasemwa kuhusiana na kiwango au asilimia ya kodi hii lakini hakuna ushahidi wowote wa kiwango maalum cha asilimia kilichotajwa ndani ya Kurani Tukufu. Na kwa hoja hii ninatofautiana na fikra za kulazimisha zinazokosa ushahidi za wanazuoni wa

zama za kati. Ninaamini ya kwamba suala la kiwango cha asilimia ya zaka kitabaki kuwa huru na kitatathiminiwa kutokana na hali ya uchumi wa nchi husika.

Zaka ikiwa ni kodi inayotozwa kwa mali iliyofikia kiasi maalum kilichowekwa, ni yumkini kwamba matumizi yake yatafanywa kwa baadhi tu ya mambo maalum yaliyoainishwa. Matumizi hayo yameainishwa kwenye aya ifuatayo ya Kurani Tukufu:

إِنَّمَا الصَّدَقَٰتُ لِلْفُقَرَآءِ وَالْمَسَٰكِينِ وَالْعَٰمِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِي الرِّقَابِ وَ
الْغَٰرِمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ وَابْنِ السَّبِيلِ ۖ فَرِيضَةً مِّنَ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٦٠﴾

*Sadaka ni kwa mafakiri tu na maskini na wanaozitumikia na waungiwao mioyo yao na (kwa kuwakomboa) wafungwa na wenye deni na katika njia ya Allah na msafiri. Ni faradhi kutoka kwa Allah; na Allah ni Mjuzi, Mwenye hekima.*[9]

Hazina imepewa jukumu la kulisimamia agizo hili. Katika historia ya awali kabisa ya Uisalmu, Makhalifa wawili wa mwanzo Hadhrat Abu Bakar[ra] na Hadhrat Umar[ra] walikuwa mashuhuri kwa uwezo wao binafsi wa kuhakikisha sadaka inagawiwa na kuwafikia wanaostahili kwa haraka. Utawala wao ulijulikana kwa kuwa nchi ya kwanza yenye mipango kabambe ya kutoa huduma za jamii bure. Mfumo huu uliendelea kufanya kazi kwa karne kadhaa ukiwa na mafanikio makubwa

hasa katika kipindi chote kilichojulikana kama utawala wa Waabbasia.

Kama ilivyoelezwa kwamba mvuto wa Zaka unachukua nafasi ya madhumuni maovu ya riba. Ukiangalia namna mfumo wa zaka unavyofanya kazi, utakuta tofauti nyingi zikijitokeza baina ya nidhamu ya kiuchumi ya Kiislam na mifumo mingine ya kiuchumi. Sifa na tabia za uchumi ulio tofauti kabisa huanza kujitokeza.

Katika mfumo wa Zaka bila kujali kuwa fedha ni nyingi au kidogo kwa ujumla hakuna fedha itakayokaa bure ikaweza kuhimili muda mrefu kama haitajiongeza kwa haraka zaidi ya kiwango kinachotozwa Zaka. Hivyo ndivyo hasa Zaka inavyosongesha mbele uchumi wa taifa halisi la Kiislam.

Fikiria katika mazingira ambayo mtu mwenye mtaji mdogo unaomfanya asiweze kujishughulisha moja kwa moja kibiashara na hakuna benki za kumkopesha ili aweze kurudisha mkopo kwa riba. Ikiwa mtaji wake huo ni mkubwa kuliko kiasi kile kinachotakiwa kutozwa Zaka, wakusanyaji wa mapato watabisha hodi mlangoni kwake kila mwaka wakidai asilimia ya Zaka kutoka kwenye mtaji wake. Watu watakaokumbana na hali kama hii katika jamii watakuwa na njia mbili tu za kufanya; ama kila mtu ataingiza fedha yake kwenye shughuli yoyote ili apate faida binafsi au watajiunga pamoja wachanganye mitaji yao ili waanzishe biashara ndogo au kubwa.

Hii inasaidia sana kukuza uzalishwaji wa ushirikiano wa kibiashara na ubunifu wa kampuni ndogo za kibiashara au kuwa na hisa kwenye makampuni makubwa kwa kufuata utaratibu wa kawaida wa kupata faida na hasara. Kampuni kama hizo hazitadaiwa chochote na taasisi za kifedha ambako wangetakiwa kulipa madeni makubwa yanayosababishwa na riba. Kwa nadharia ya kawaida kama ilinganishwe mzigo unaobebwa na kampuni kama hizi na ule unaobebwa na makampuni ya aina kama hiyo yanayoendeshwa kwenye uchumi wa kibepari, itagundulika ya kwamba kampuni hizi zitakuwa zikifanya kazi katika mazingira na hali ya unafuu kabisa hasa kwenye vipindi vya misukosuko ya kibiashara na mkwamo wa kiuchumi. Kwa biashara au kiwanda kinachopitia kipindi kigumu cha kushuka kwa biashara tena kwenye uchumi wa kibepari, kushuka kwa uzalishaji wake kunakotokana na kupungua kwa mahitaji ya bidhaa kunaweza kuisukuma biashara au kiwanda hicho karibu sana na kufilisika kwa sababu ya madeni. Riba itakayotakiwa kulipwa wakati wa kulihudumia deni itaendelea kuongezeka bila huruma mpaka haitawezekana tena kampuni za kibiashara kama hizo kendelea kuwepo.

Kwa upande mwingine ikiwa uchumi utaendeshwa kwa misingi ya Kiislam, kupungua kwa fursa za kukuza biashara na kiwanda kutapelekea biashara hiyo kupita kwenye hali ya kutokuzalisha. Na hivyo ndivyo hali ya asili ya ulimwengu inavyohakikisha uwepo wa uhai kwa

anayefaa zaidi kuishi katika kipindi cha hali ngumu na madhoruba. Ikiwa nguvu inayotumika inapungua, mazao ni lazima nayo yapungue isije ikatumika nguvu ya akiba inayotunza uhai. Mfumo wa kifedha wa Kiislam unaweza kuhimili zaidi misukosuko na changamoto za mdororo wa uchumi kwa kuwa hauna mzigo wa kupindukia wa kuhudumia madeni.

## Makatazo Ya Riba

Mfumo wa kiuchumi wa Kiislam unaendeshwa bila ya riba kabisa. Hata hivyo hakuna ushahidi wa kihistoria au wa nyakati hizi ya kwamba kwa matokeo ya kutojihusisha na riba shetani wa mfumuko wa bei amewahi kucharuka na akazipaisha bei juu bila udhibiti. Katika nyakati tulizo nazo tunayo fursa nzuri ya kulinganisha kuwepo au kutokuwepo kwa viwango vya riba kunavyoathiri mfumukobei.

Serikali ya China katika kipindi cha Mao Tse Tsung ilifanya majaribio mengi katika uchumi. Baadhi ya majaribio hayo yalionyesha matokeo mazuri sana na baadhi hayakufanya vizuri. Lakini kipindi chote cha utawala wa Mao Tse Tsung riba haikuruhusiwa kufanya kazi yoyote iwe ndani ama nje ya nchi. Katika kipindi hicho chote hakukuwa na mwongezeko wa maana katika mfumukobei. Ukweli ni kwamba katika kipindi hicho kiwango cha uzalishaji kiliongezeka kwa ujumla na bei za bidhaa zilianza kushuka.

Kama hali hii ilinganishwe na taifa la Israeli, nchi ambayo huenda ikawa ndiyo ya kibepari zaidi ulimwenguni ambako kiwango chake cha mfumukobei kimekuwa miongoni mwa viwango vikubwa kabisa kufikiwa duniani ukiachilia mbali nchi za Amerika ya Kusini na vioja visivyo vya kawaida vya mfumukobei vilivyojitokeza katika nchi za Ulaya hasa Ujerumani baada tu ya vita. Hata hivyo hizo hazikuwa siku za kawaida. Ukweli ni kwamba ukiachilia mbali mambo mengine kazi kubwa ya riba kwenye uchumi wowote ule si nyingine bali kuongeza mfumukobei.

## Viwango vya juu vya Riba nchini Uingereza

Mjadala mkali uliopo nchini Uingereza juu ya faida na hasara ya kuwa na viwango vya juu vya riba unatoa mfano wa kuvutia kufanya uchunguzi. Kwa muda mrefu serikali ya chama cha Conservative imeacha riba ikiwa kwenye kiwango cha juu cha kupindukia huku serikali ikieleza sababu kubwa kuwa ni kupambana na matumizi binafsi na kufanya hivyo ni katika kudhibiti mfumukobei. Tayari uchumi unalalama na kukoroma kutokana na shida zilizosababishwa na sera hiyo ya serikali.

Mambo kadhaa tunaweza kujifunza kutokana na utafiti huu. Pamoja na mambo mengine utafiti huu unatuonyesha jambo muafaka juu ya maamuzi yenye nguvu ya kiuchumi yanayofanywa kwa misingi ya nadharia ambayo yenyewe ni ya mashaka.

Dhana kwamba kupandishwa kiwango cha riba kutapunguza mfumukobei inaonekana kuwa ndiyo sababu pekee inayohalalisha udumishwaji usio wa kawaida wa viwango vya juu vya riba.

Uchunguzi wetu juu ya kinachoendelea nchini Uingereza tunafahamu kwamba haijawahi kutokea kiwango cha riba ikawa ndiyo sababu hasa ya msingi kwenye mlolongo wa kupanda kwa mfumukobei. Ni lazima kulikuwa na ukosefu wa usimamizi thabiti wa maeneo mengi tu yanayochangia katika uchumi ambayo ikiambatanishwa pamoja na dosari ya sera yenyewe ya uchumi kwa ujumla imesababisha kwa kiasi fulani kupanda kwa kiwango cha mfumukobei tunakokuona sasa. Kupandishwa viwango vya riba kumesaidia tu kuvuruga mawazo ya watu yasijikite kwenye sababu za msingi kwa kisingizio rahisi cha kupunguza mfumukobei. Kwenye hatua za mwanzo mkakati huu unaweza kuonyesha kipimo cha mafanikio ya kupambana na mfumukobei lakini tayari kwa sasa mkakati huu umesababisha vipengele vyenye nguvu kufanya kazi vitakavyopelekea kujitokeza athari za daraja la pili. Nchi itatupwa katika hali isiyofikirika ya mdororo wa uchumi huku ukosefu wa ajira ukiongezeka.

Haiwezekani kuamini kwamba jopo la wataalaamu wa serikali ya Conservative halipati ushauri kutoka kwa wachumi wabobevu, wataalamu wa fedha wazoefu,

wataalamu wa Benki Kuu na wataalamu wengine. Kwa vyovyote kutakuwa na sababu za makusudi za ucheleweshwaji wa muda mrefu wa upunguzaji wa viwango vya juu vya riba kwa maelezo mabovu eti ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa nchi katika kupunguza mwenendo wa mfumukobei. Sio kwamba kisiasa muda wa kupunguza viwango vya riba haujawa muafaka kwa serikali? Huenda ikacheleweshwa mpaka karibu kabisa na uchaguzi mkuu ujao, ambapo unafuu wa kupunguza viwango vya riba watakaoupata watu wa ngazi zote za jamii utawapa sifa za kisiasa Wahafidhina. Kama jambo hili lifanyike mapema sana, athari za hatua ya pili — nilizoziashiria tayari — zinaweza kuanza kujitokeza na kuficha kabisa mafanikio ya muda mfupi yatokanayo na unafuu unaopatikana kwa kupunguzwa kwa viwango vya riba.

Baadhi ya vipengele vinavyoweza kuuachia huru mtindo huu usiofaa ni hivi vifuatavyo:

1. Kiwango cha juu cha riba sio tu kimekaba sana uwezo wa kufanya matumizi kwa wananchi bali kimeathiri mshipa mkuu unaoleta damu safi kwa viwanda.

2. Bila shaka kiwango kikubwa cha riba kimewaumiza wananchi wengi wa Uingereza wanapotaka kupata huduma muhimu. Waliokopa fedha nyingi kwa ajili ya nyumba bila shaka walijitathmini na kufanya hesabu zao vizuri kabla

ya kuchukua mikopo hiyo kwa dhamana ya nyumba zao. Walijibana kadiri ya uwezo wao kuhakikisha wanajenga uwezo wa kulipa mkopo kwa kubana matumizi yao ya kila siku. Watu hao tayari walishajizoesha kujinyima kwa kufanya matumizi yasiyo ya lazima kwa sababu hawakuwa na njia mbadala isipokuwa kulipa madeni yao. Bila shaka wakopaji wa mikopo ya nyumba wa Uingereza hawakusababisha mwenendo wa muongezeko wa mfumukobei. Kinyume chake kundi hili ndilo lililoadhibiwa vikali na sera ya serikali ya kukomesha kupanda kwa mfumuko wa bei inayosemwa ni kwa manufaa ya umma. Thamani ya nyumba za watu hawa imeshuka kwa kasi na hivyo kuwaacha kwenye mtanziko usio na ufumbuzi kwa kuwa hawana uwezo wa kulipa zaidi na hawawezi kupata wanunuzi wa nyumba zao kwa bei ambayo itawawezesha kulipa deni.

3. Mfumukobei ni suala gumu. Hotuba hii haikusudii kutumia muda mrefu kwenye jambo hili ingawa kwa sababu zitakazobainishwa baadaye nitaomba uvumilivu kutoka kwa wasikilizaji.

Pamoja na mambo mengine Mfumukobei unaweza kuwepo ikiwa watu wana fedha nyingi wakati upatikanaji wa bidhaa ni hafifu. Kwa kawaida watu

wakiwa na fedha nyingi hutaka kufanya matumizi mengi wakati bidhaa ni chache. Hivyo kunakuwa na haja au mshawasha wa kununua vitu vingi ilhali bidhaa chache tu ndizo zilizopo kuweza kununuliwa. Kwa uchumi wa Kiingereza hali hii haikujitokeza. Fedha nyingi zilizokuwa kwenye mzunguko zilikuwa zikiviwezesha viwanda vya Waingereza kwa kiwango kikubwa katika kuongeza bidhaa kwa walaji walioko kwenye soko lake la ndani. Pamoja na hilo kulikuwa na unafuu uliotokana na upunguzwaji wa kodi na viwango vizuri vya ubadilishanaji wa sarafu ya Pauni kwenye masoko ya nje. Thamani ya Pauni ya Uingereza iliwafanya wanunuzi wa nje wazipende bidhaa za Uingereza hali ambayo iliongeza mauzo kwa viwanda vyake ambavyo tayari vilikuwa vikisaidiwa na walaji wa soko lao imara la ndani.

Kilichokuwa kimetegemewa ni kushuka kwa bei ya bidhaa za viwandani. Kuongezeka kwa uzalishaji kungepunguza gharama kubwa za uzalishaji na gharama ndogo zingeweza kubebwa na bei ya kuuzia bidhaa hizo viwandani. Kwa sababu ya uzalishaji mkubwa kuongeza faida kidogo tu kwenye bidhaa kungewafanya wazalishaji wawe na nafasi ya kutosha kupunguza bei za bidhaa kwa walaji.

Viwango vya juu vya riba vilivyodumu kwa muda mrefu vimegeuza ukuaji wa kawaida wa uchumi wa Kiingereza kwa kutaka tu umaarufu wa baadaye. Wakati

hali ya masoko ya nje ambayo yameshaanza kuponyoka itakuwa vigumu kuyarejesha tena.

Mabadiliko yanayoendelea barani Ulaya yanauongezea damu zaidi uchumi mkubwa wa Ujerumani Magharibi au Ujerumani kwa ujumla. Madhara mabaya yaliyoelezwa kwa kifupi hapo juu yanaweza kuupeleka pabaya uchumi wa Uingereza.

Serikali iliyoko madarakani inaweza isifanikiwe katika hila yake ya kupunguza viwango vya riba kwa wakati ule wanaoutaka na hivyo serikali ijayo, na kama itaendelea kuwa ya chama cha Conservative, itarithi matatizo makubwa kutoka serikali iliyopita inayotokana na chama chao.

Kwenye haya yote linajitokeza fundisho muhimu sana kwa watunga sera wote ulimwenguni. Fundisho hilo ni kwamba riba inapokuwa ni chombo cha kudhibiti uchumi wa nchi huwa inachezea dhana nzima ya uchumi wa soko huria. Hakuna uchumi unaoendeshwa kwa fedha yenye harufu ya dhana inayohusiana na riba unaoweza kuelezwa kwa uhakika kabisa kuwa ni uchumi huria ikiwa serikali husika ina nguvu na mamlaka yote ya kuongeza au kupunguza viwango vya riba.

Mfumo wa uchumi wa Kiislam hautoi fursa ya serikali kutengeneza mipango ya kinyonyaji kama hii.

## Madhara Mengine ya Riba

Bila shaka itafaa kutaja mambo mengine machache yanayohusiana na riba. Kiwango cha riba kinachotozwa pale benki zinapoazimana fedha ili kukidhi shughuli zao za muda mfupi hulipwa kutokana na jumla ya amana zote zilizowekwa na wala haitozwi kutoka kwenye amana zilizo kwenye akaunti binafsi za wateja. Licha ya kwamba kuna kuongezeka kwa fedha, lakini faida ya riba inayopatikana kutokana na amana ni ndogo kuliko thamani halisi ya fedha. Ingawa kwa muda mfupi viwango hubadilika badilika mwisho wa siku amana inapata faida iliyo chini ya kiwango cha mfumukobei. Kwa upande mwingine kama kiwango hicho cha fedha kingewekezwa kwenye biashara nyingine kuna uwezekano mkubwa kwamba ingezalisha faida kubwa inayoakisi hali halisi.

Kwenye jamii zinazovutiwa na riba, wenye fedha wako tayari kukopesha bila hata kutaka kujua uwezo halisi wa mkopaji kulipa deni. Hata hivyo wapo wakopaji wachache tu wanaoweza kujitathmini kwa makini juu ya uwezo wao wa kulipa deni. Walio wengi hawajatambua ya kwamba kukopa kwa wakopeshaji mapapa wafananao na shylock — ambao wako radhi hata kiuzwe kipande cha mwili wa mtu kwa ajili ya fedha — na taasisi kubwa za fedha na benki, ni sawa na mtu kujikopesha mapato yake binafsi ya baadae. Tabia ya kukopa inamhamasisha mtu aishi maisha yaliyo nje ya kipato chake halisi yanayopelekea kwenye kufanya

matumizi makubwa ambayo yatamfanya baadae apoteze uwezo hata wa kulipa madeni. Jamii kama hizo zinasababisha kuongezeka ghafla uzalishaji katika hali isiyokuwa ya uhalisia.

Inafaa pia kueleza zaidi tena kinagaubaga kwa mifano madhara yanayotokana na uchumi unaoendeshwa kwa riba.

Katika jamii ambamo kushindana na majirani katika kuhodhi vitu vya kifahari vya kisasa inakuwa ni tamaa isiyotulizika, tamaa hiyo kwa kiasi kikubwa hushawishiwa kupitia matangazo yanayoelezea mitindo mbalimbali ya vifaa hivyo. Umma huonyeshwa maisha ya kifahari ya matajiri kwa kuonyeshwa mitindo mipya ya samani za ndani pamoja na nyumba za kifahari zilizonakshiwa na kuwekwa vifaa vya kisasa jikoni na maliwatoni kwake.

Katika jamii kama hizo watu wenye uwezo mdogo wanahadaiwa bila kupenda kwa kuwataka waishi tofauti na hali zao halisi. Watu hawa hulazimika kupoteza fedha kupitia kadi zao za mikopo ili waweze kutosheleza hamu za nafsi zao. Hii ni dhahiri kwamba wananunua zaidi kuliko vipato vyao. Kama fedha hizi zingelipwa bila hata riba ingekuwa sawa tu na kufanya matumizi makubwa kwa sasa ili kubana matumizi ya baadae ya kipato chako.

Ukichukuliwa mfano wa mtu mwenye kipato cha Dolla 1,000 kwa mwezi na anakwenda kufanya manunuzi ya

gharama kwa fedha za mkopo zinazofikia Dolla 40,000 uwezo wake wa kurudisha mkopo utatokana na akiba yake ya kila mwezi. Ikiwa matumizi yake halisi kwa mwezi ni Dolla 600 ina maana anaweka akiba ya Dolla 400. Bila ya riba itamchukua miezi 100 kulipa mkopo wa Dolla 40,000 aliouingiza kwenye matumizi aliyoyafanya kwa muda mfupi sana. Mtu huyu alichokifanya ni kujikopesha mwanzoni tu fedha zake za miezi 100 (miaka 8 na miezi 4). Faida aliyoipata ni kukidhi haraka yake na kutimiza shauku ya moyo wake badala ya kusubiri kwa miaka takribani minane ijayo.

Ikiwa atatakiwa kulipa riba kwa deni lake la Dolla 40,000 hali yake ya kifedha itakuwa mbaya zaidi ya kilichoelezwa hapo juu. Kwa kiwango cha riba ya 14% mkopo wake unaotokana na kipato chake utakuwa mkubwa sana. Hii itapunguza uwezo wake wa kulipa na kuongezeka sana kipindi cha kuendelea kulipa deni hilo. Mtu huyo atataabika akisubiria kwa zaidi ya miaka 20 akiadhibiwa kwa haraka yake huku akilipa Dolla 500 kila mwezi zitakazompelekea kulipa jumla ya Dolla 120,000 pamoja na riba.

Hasara  anapata mkopaji na sio mkopeshaji. Mkopeshaji ni sehemu ya mfumo wa kimabavu wa kinyonyaji unaomhakikishia kubaki na fedha nyingi hata kama kuwe na mfumukobei au hasara kwenye mkopo wenyewe.

Ukiongeza suala la mfumukobei, hali ya mkopaji huyu inazidi kudidimia. Uwezo wake wa kufanya matumizi utakwenda chini sana kwani kama ilikuwa ni vigumu kuishi kwa Dolla 600 kwa mazingira ya mfumukobei haitawezekana aendelee kutumia kiasi hicho kadri siku zinavyokwenda. Wapo wachache wenye bahati wanaopata nyongeza ya mishahara yao kila mwaka inayolingana na kiwango cha mfumukobei.

Kuonyesha hali mbaya zaidi katika jamii ya watu wanaopenda raha haiwezekani waendelee kuvumilia muda mrefu wakibaki kwenye nidhamu eti kwa dhiki waliyoipata wenyewe baada ya kipindi kifupi cha kufanya matumizi yao ya kifahari. Wao wataendelea kukopa fedha zaidi zitakazoongeza matumizi maradufu ya uwezo wa vipato vyao. Hatimaye kwa miongo kadhaa mtu huyu ataendelea kujiweka rehani benki na taasisi nyingine za kifedha kwa dhamana ya kipato chake wakati deni likiongezeka linaloambatana na matatizo.

Kwa ujumla, uchumi wa namna hiyo unaelekea kwenye mkwamo mkubwa kwa sababu haiwezekani kuendelea bila kikomo kuweka rehani mapato ya baadae kabla ya kukumbana na kizingiti cha mporomoko wa kifedha unaotokana na matumizi mabaya yanayosababisha kuongezeka kwa kiwango cha mfumukobei. Ukipambana na mfumukobei kwa kuongeza viwango vya riba kwa mategemeo ya kudhibiti matumizi

inapelekea kuanzisha mlolongo wa mambo utakaokufikisha kwenye mdororo wa uchumi.

Hali hii ni mbaya kwa nchi na ikiwa mambo yanayofanana yanasababisha mdororo wa uchumi kwa nchi nyingi duniani, itapelekea mdororo wa uchumi wa dunia ambao ni tishio kwa mwanadamu unaotoa fursa pana zaidi ya vita vya dunia na maangamizi mengine makubwa.

Kufilisika huanza kuongezeka, biashara husimama, viwango vya ukosefu wa ajira hupanda ghafla na biashara za nyumba huanza kuporomoka. Hatima ya yote ni kuvurugika kwa mambo katika kila eneo kunakochangia kukuza ukosefu wa kazi, udanganyifu na uhalifu. Ikiwa haya yanatokea, yasimshangaze yeyote, hasa kwa watetezi wakubwa wa ubepari.

Katika jamii za kibepari hali haikomei tu kwa mtu kukopeshwa zaidi ya uwezo wake wa kulipa, bali huenda mbali zaidi kwenye kuathiri mustakabali wa sekta nzima kwa sababu ya kutaka matokeo ya kipato cha muda mfupi. Mwanzoni viwanda vyote nchini hufaidika kwa kiasi kikubwa — jambo linalosaidia katika kushusha bei za bidhaa za ndani. Uhamishaji wa fedha kwa kumpa mtu binafsi kupitia mkopo siyo tu kunamwongezea uwezo wa kufanya matumizi bali kunaleta athari kwenye mfumo wa uzalishaji. Kuongezeka kwa mahitaji kunakotokana na watu kuwa na fedha za mikopo husababisha uzalishaji mkubwa

unaoufanya bei za bidhaa kushuka na hivyo kuzipa nguvu za ushindani katika masoko ya nje. Haya yote yanaonekana mazuri na yenye manufaa lakini baada ya haya itakuja kujilaumu na kasumba inayotokana na mazoea ya maisha rahisi.

Jamii inapokosa ustahimilivu unaoambatana na matumizi makubwa yasiyoendana na kipato halisi hupelekea jamii hiyo kwa ujumla kudaiwa na mabenki wakati uwezo wake wa kufanya matumizi ukipungua taratibu na hatimaye kukoma kabisa. Ili kuendelea kuwepo viwanda vitalazimika kujitahidi kuangalia zaidi masoko ya nje. Hali kama hiyo kwa nchi yenye wigo mdogo katika ujenzi wa uchumi itafikiwa na hatima yake ya kiuchumi mapema zaidi wakati ile yenye wigo mpana inaweza kuchelewea kidogo kukutana na mgogoro unayoikabili.

Hebu na tuigeukie Marekani kuangalia mambo yanakuwaje huko. Hakuna shaka kwamba Marekani ni nchi yenye soko kubwa zaidi la ndani kuweza kutoshelezwa na viwanda vyake. Hata baadhi ya wataalamu wa masuala ya uchumi wanaamini kwamba hata kama Marekani ijitenge na Jumuiyya ya Kimataifa, ukubwa wa soko lake la ndani unatosha kuvihakikishia viwanda vyake kuendelea kufanya kazi. Wataalamu hao wa uchumi wameshindwa kutilia maanani vipengele vingine vinavyoweza kusaidia kuangalia hali halisi ya kiuchumi. Mfano ulioelezewa hapo juu kama ukitumika

katika mazingira ya Marekani, utaanza kuona ya kwamba hakuna ufumbuzi mwingine wenye busara unaoweza kutolewa minghairi ya ule uliotolewa. Ni suala la muda tu ila njia ni ile ile kwani Marekani ina nakisi kubwa kwenye bajeti yake na inadaiwa madeni yanayofikia trilioni za dola. Kama nchi, Marekani imeshafanya matumizi zaidi ya uwezo wake na wananchi wake wako kwenye deni kubwa na uwezo wake wa kufanya matumizi kama taifa lazima upungue, ama mikopo ya nyumba itafilisika. Ni suala tu la ukubwa wa uchumi wake linalosababisha kuchelewa lakini kanuni za msingi za asili zisizoepukika zitafanya kazi bila ya upendeleo kwenye mazingira yanayofanana.

Katika majira ya joto madimbwi na mabwawa hupata joto la kawaida haraka sana sawa na mazingira, wakati maziwa huchelewa kidogo. Kadhalika bahari ndogo hupata joto haraka zaidi kuliko kubwa ingawa zote zinapita kwenye majaaliwa yaleyale. Inachukua muda mrefu zaidi kwa bahari ya Pasifiki kupata joto na inapofikia hali hiyo tayari majira ya baridi huwa yameshafika katika nchi nyingi zinazopakana na bahari hiyo kubwa, ndiyo maana hali ya hewa inakuwa ni joto la wastani kuliko maeneo yanayopakana na bahari ndogondogo. Hivyo ndivyo ilivyo hata katika ulimwengu wa bahari za uchumi. Kwa uhakika kabisa falsafa yenyewe ya kutumia fedha ya mkopo imepindika kiasi ambacho ni wendawazimu kutegemea matokeo ya haki tena yaliyonyooka.

Kuna kipengele kingine muhimu cha kukiangalia kwa makini. Endapo sekta fulani au uchumi wa nchi unafikia hatua ya kubanwa kabisa, nchi maskini na zisizoendelea zinakabiliwa na hatari kubwa ya kuathirika na cheche zinazotokana na mlipuko wa hali ya uchumi wa nchi zilizoendelea. Hatihati huanza kwa uharaka wa viongozi wa kisiasa wa nchi zenye viwanda kutaka kuuza bidhaa nyingi ili kuviokoa viwanda vyao na kulinda viwango vya ubora wa maisha ya watu wao. Hivyo viongozi hao hukabiliwa na matatizo ya aina mbili: 1. Watu wanakuwa wamezoea starehe na raha za kisasa. 2. Ili viendelee kuwepo, viwanda vinawasisimua watu kwa vifaa na matoleo mapya ya kisasa zaidi vikiwaliwaza majumbani mwao.

Hakuna serikali ya kisiasa inayoweza kuhimili ikiwa wananchi wanaendelea kudai viwango bora vya maisha. Uchumi unatakiwa ulindwe kwa gharama yoyote ile.

Ni wazi kwamba nchi za Ulimwengu wa Tatu ndizo zitakazonyonywa damu zaidi kuliko hata kabla ili kuweza kulinda viwango nadharia vya maisha katika nchi zilizoendelea. Ziko changamoto mpya zinazozikabili nchi zinazoendelea kama vile kuutengeneza upya uchumi wa jumuiyya ya Kikomunisti ya Kisovieti ya Jamhuri ya watu wa Urusi (USSR) na Ulaya ya Mashariki, mahitaji makubwa ya kuimarisha masoko ya nje ya nchi zinazochipukia kwenye ubepari zilizokuwa za kijamaa; na bado vyombo

vya habari vya Kimagharibi vinaumiza matamanio na matarajio ya mafukara kutoka nchi za kijamaa na zile za Ulimwengu wa Tatu. Mambo haya yote yakiwekwa pamoja hayaonyeshi kuleta mabadiliko yenye ubora kwenye uso wa dunia.

## Riba Inavyohatarisha Amani

Jambo hili muhimu limewekewa onyo kali sana kwa mwanadamu ndani ya Kurani Tukufu tangu miaka 1400 iliyopita. Ikionya juu ya maangamizi makubwa ya mwanadamu yatakayoletwa na uchumi unaotegemea riba utakaomtawala mwanadamu.

اَلَّذِيْنَ يَاْكُلُوْنَ الرِّبٰوا لَا يَقُوْمُوْنَ اِلَّا كَمَا يَقُوْمُ الَّذِيْ يَتَخَبَّطُهُ الشَّيْطٰنُ مِنَ الْمَسِّ ؕ ذٰلِكَ
بِاَنَّهُمْ قَالُوْٓا اِنَّمَا الْبَيْعُ مِثْلُ الرِّبٰوا ۘ وَ اَحَلَّ اللّٰهُ الْبَيْعَ وَ حَرَّمَ الرِّبٰوا ؕ فَمَنْ جَآءَهٗ مَوْعِظَةٌ مِّنْ
رَّبِّهٖ فَانْتَهٰى فَلَهٗ مَا سَلَفَ ؕ وَ اَمْرُهٗٓ اِلَى اللّٰهِ ؕ وَ مَنْ عَادَ فَاُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ النَّارِ ۚ هُمْ فِيْهَا
خٰلِدُوْنَ ﴿٢٧٥﴾ يَمْحَقُ اللّٰهُ الرِّبٰوا وَ يُرْبِي الصَّدَقٰتِ ؕ وَ اللّٰهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ كَفَّارٍ اَثِيْمٍ ﴿٢٧٦﴾ اِنَّ الَّذِيْنَ
اٰمَنُوْا وَ عَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ وَ اَقَامُوا الصَّلٰوةَ وَ اٰتَوُا الزَّكٰوةَ لَهُمْ اَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۚ وَ لَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَ
لَا هُمْ يَحْزَنُوْنَ ﴿٢٧٧﴾ يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اتَّقُوا اللّٰهَ وَ ذَرُوْا مَا بَقِيَ مِنَ الرِّبٰوٓا اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿٢٧٨﴾
فَاِنْ لَّمْ تَفْعَلُوْا فَاْذَنُوْا بِحَرْبٍ مِّنَ اللّٰهِ وَ رَسُوْلِهٖ ۚ وَ اِنْ تُبْتُمْ فَلَكُمْ رُءُوْسُ اَمْوَالِكُمْ ۚ لَا
تَظْلِمُوْنَ وَ لَا تُظْلَمُوْنَ ﴿٢٧٩﴾ وَ اِنْ كَانَ ذُوْ عُسْرَةٍ فَنَظِرَةٌ اِلٰى مَيْسَرَةٍ ؕ وَ اَنْ تَصَدَّقُوْا خَيْرٌ لَّكُمْ اِنْ
كُنْتُمْ تَعْلَمُوْنَ ﴿٢٨٠﴾

*Wale wanaokula riba, hawatasimama ila kama anavyosimama yule ambaye Shetani humpoozesha kwa kumshika. Hayo ni kwa sababu wamesema, Biashara ni kama riba tu; hali Allah ameihalalisha biashara na*

> *kuiharimisha riba. Na aliyefikiwa na mawaidha kutoka kwa Mola wake, kisha akajizuia, basi yake ni yale yaliyokwisha pita, na shauri lake ni kwa Allah. Lakini anayerejea (kula riba), basi hao ndio watu wa motoni, humo watakaa. Allah Hufuta riba na Hukuza sadaka, na Allah Hampendi kila aliyethibitika kuwa kafiri na mtenda dhambi mkuu. Hakika wale walioamini na kufanya vitendo vizuri na kusimamisha Sala na kutoa Zaka, wao watapata ujira wao kwa Mola wao, wala haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika. Enyi mlioamini! mcheni Allah, na acheni yaliyobakia katika riba, ikiwa mmeamini. Na kama hamtafanya (hivyo), basi fahamuni mtakuwa na vita kutoka kwa Allah na Mtume Wake; na kama mkitubu, basi mtapata rasilmali zenu; msidhulumu wala msidhulumiwe. Na kama mdaiwa ana dhiki, basi (mdai) angoje mpaka amefarijika; na kama ninyi (mnaodai) mkiacha kama sadaka, ni bora kwenu, ikiwa mnajua.*[10]

Onyo la Mwenyezi Mungu juu ya vita lililomo kwenye aya hizi linamaanisha kwamba kanuni ya maumbile inayotawaliwa na Mwenyezi Mungu itaziadhibu jamii za kibepari pale ambapo yale yaliyojadiliwa hapo juu yatamfikisha mwanadamu kwenye hatima ya kukosa haki ya kiuchumi na vita. Fujo na vita ni matokeo ya unyonyaji na unyang'anyi wa haki za wanyonge. *Na kama hamtafanya hivyo basi fahamuni mtakuwa na vita kutoka kwa Allah na Mtume wake* inamaanisha taifa

linaloendeleza riba halitakwepa kuishia kwenye hali ngumu ya mataifa kushikiana silaha.

Muda hauruhusu kueleza kila jambo linalohusiana na riba. Lakini katika Kurani Tukufu kila aya inayokataza riba inafuatiwa na onyo la vita — jambo linaloonyesha uhusiano wa karibu baina ya riba na vita. Wanaofahamu historia ya Vita ya Kwanza na ya Pili ya Dunia watakumbuka ya kwamba ubepari sio tu ulifanya kazi ya hatari ya kuvianzisha bali na kuvidumisha kwa muda mrefu.

## Makatazo ya Kujilimbikizia Mali

Uislamu unakataza kila aina ya unyonyaji pamoja na mbinu zisizoleta usawa kama vile kuhodhi mali, fedha, bidhaa au vifaa kunakosababisha bei kupanda na hatimaye kuleta mfumukobei. Kurani Tukufu inaeleza;

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِنَّ كَثِيْرًا مِّنَ الْاَحْبَارِ وَ الرُّهْبَانِ لَيَاْكُلُوْنَ اَمْوَالَ النَّاسِ بِالْبَاطِلِ وَ
يَصُدُّوْنَ عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ؕ وَ الَّذِيْنَ يَكْنِزُوْنَ الذَّهَبَ وَ الْفِضَّةَ وَ لَا يُنْفِقُوْنَهَا فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ۙ
فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ اَلِيْمٍ ﴿۳۴﴾ يَّوْمَ يُحْمٰى عَلَيْهَا فِيْ نَارِ جَهَنَّمَ فَتُكْوٰى بِهَا جِبَاهُهُمْ وَ جُنُوْبُهُمْ
وَ ظُهُوْرُهُمْ ؕ هٰذَا مَا كَنَزْتُمْ لِاَنْفُسِكُمْ فَذُوْقُوْا مَا كُنْتُمْ تَكْنِزُوْنَ ﴿۳۵﴾

*Enyi mlioamini! bila shaka wengi katika makasisi na wamonaki wanakula mali za watu kwa batili na kuwazuilia njia ya Allah. Na wale wakusanyao dhahabu na fedha wala hawazitoi katika njia ya Allah, basi wape habari za adhabu iumizayo. Siku (mali yao) itakapochomwa ndani ya moto wa jahanamu na kwayo*

*vitachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao; haya ndiyo mliyoyakusanyia nafsi zenu basi onjeni (adhabu ya) yale mliyokuwa mkiyakusanya".*[11]

Zaidi ya hayo lakini Uislamu unatoa uhuru wa mtu binafsi kujipatia fedha kwa njia yoyote halali inayoendana na maadili ya mwenendo wa uchumi wa Kiislam. Hivyo upo uhuru na haki kwa watu kumiliki mali na kuanzisha biashara binafsi.

Katika kutengeneza uchumi wa nchi serikali nyingi zinaangalia zaidi kile ambacho mtu amechuma tu. Kodi hutozwa kwenye mauzo, faida iliyotokana na biashara pamoja na kodi ya mapato yanayotokana na mishahara. Baada ya kutekeleza hivyo hakuna uingliliaji tena katika mambo ya kifedha ya mtu. Kwa ujumla wigo wa maslahi ya taifa umeishia upande wa mapato tu, lakini namna mtu anavyotumia kipato alichochuma au ameweka akiba wala sio jambo hasa linaloshughulika nalo serikali nyingi. Mtu akipenda anaweza kupoteza fedha au mali aliyonayo au anaweza kuishi maisha ya kifahari apendavyo au licha ya utajiri wake mtu anaweza kuchagua kuishi maisha ya kujihini. Imekuwa sio kazi ya serikali kutaka kujua mtu atazifanyia nini fedha zake.

Hata hivyo eneo hili dini huingilia kwa namna ya kumuonya na kumshauri mtu. Katika muktadha wa dini mtu haelekezwi tu namna ya kupata kipato chake cha

kila siku bali humuongoza pia njia zinazofaa ili aepukane na zile zisizofaa kutumia kipato alichopata. Sheria nyingi zinazohusiana na matumizi zipo katika msingi wa miongozo ya kimaadili na kiroho. Kwa mfano Uislamu unakataza matumizi ya ulevi, kamari na anasa zinazoendana na hizo. Makatazo haya hayakusudii kudhibiti bajeti ya matumizi bali ni matokeo ya mafundisho ya kiroho ya dini yenye maadili. Kwenye uchumi wa kibepari makatazo kama haya yanaonekana ni kuingilia faragha na haki ya mtu kufanya matumizi atakavyo. Mtazamo huu si mpya kwa mwanadamu.

Kurani Tukufu inatueleza kwamba kaumu zilizostaarabika za zama zilizopita zilikuwa na mtazamo kama huu dhidi ya dini. Mitazamo hiyo ilisababisha mijadala juu ya haki ya dini kuingilia mambo binafsi ya watu. Miongoni mwa Manabii wa kale ni Hadharat Shuaib[as] ambaye alijaribu kuwaelimisha watu wa Midiani namna bora ya kutumia utajiri wao na mambo wanayotakiwa kujiepusha nayo; alishutumiwa na watu wake kama ifuatavyo:

قَالُوْا يٰشُعَيْبُ اَصَلٰوتُكَ تَاْمُرُكَ اَنْ نَّتْرُكَ مَا يَعْبُدُ اٰبَآؤُنَآ اَوْ اَنْ نَّفْعَلَ فِيْٓ اَمْوَالِنَا مَا نَشٰٓؤُا ؕ
اِنَّكَ لَاَنْتَ الْحَلِيْمُ الرَّشِيْدُ ﴿٨٨﴾

*Wakasema: Ewe Shuaibu, je, Sala yako inakuamuru tuyaache waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu, au tuache kufanya tupendavyo katika mali zetu? Bila shaka wewe ndiwe mpole sana, mwongofu.*[12]

## Kuishi Maisha Rahisi na ya Kawaida

Uislamu unapendelea kuishi maisha ya kawaida. Islam inakataza ubadhirifu ingawa inahimiza kufanya matumizi kama ilivyoelezwa katika aya zifuatazo za Kurani Tukufu;

وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ وَلَا تَبْسُطْهَا كُلَّ الْبَسْطِ فَتَقْعُدَ مَلُومًا مَّحْسُورًا ﴿٣٠﴾

*Na wala usiufanye mkono wako ufungiwe shingoni mwako kwa ubahili uliokithiri, wala usiukunjue wote (kwa ubadhirifu mkubwa); usije ukaishia katika hali ya kulaumiwa na kujuta.*[13]

وَآتِ ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ وَالْمِسْكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ وَلَا تُبَذِّرْ تَبْذِيرًا ﴿٢٧﴾ إِنَّ الْمُبَذِّرِينَ كَانُوا إِخْوَانَ
الشَّيَاطِينِ ۖ وَكَانَ الشَّيْطَانُ لِرَبِّهِ كَفُورًا ﴿٢٨﴾

*Na umpe ndugu haki yake, na maskini na msafiri, wala usitapanye (mali yako) kwa ubadhirifu. Hakika watumiao kwa ubadhirifu ni ndugu za mashetani; na Shetani ndiye asiyemshukuru Mola wake.*[14]

## Matumizi Kwenye Sherehe ya Ndoa

Utofauti wa sherehe za ndoa kwa familia za kitajiri na zile za hali ya chini ni eneo nyeti linaloweza kusababisha taharuki na maumivu ya moyo kwa wazazi maskini wenye mabinti waliofikia umri wa kuolewa.

Uislamu unakataza sherehe za ndoa za kifahari zilizojawa na matumizi makubwa ya kujionesha. Tangu mwanzo, historia ya Uislamu inaonyesha ya kuwa

sherehe za ndoa zimekuwa zikifanywa kwa namna rahisi sana na kuwafanya walio wengi walione tukio la ndoa kuwa ni la kawaida sana.

Mpaka hivi sasa bado sherehe rasmi ya ndoa imebaki kimsingi kuwa ni ya kawaida tena isiyo na gharama kwa wote, matajiri na maskini licha ya ukweli kwamba sherehe nyingi za ndoa za Waislam wenye uwezo zimeathiriwa na mila, tamaduni na desturi za jamii zao. Mila na tamaduni hizo kwenye sherehe za ndoa zimesababisha kuingizwa kwa mambo mengi ya uzushi na ubunifu. Ndoa (Nikah) mara nyingi hutangazwa msikitini ambako wote matajiri na maskini hukusanyika. Wakiwa katika hali inayofanana kwa vile msikiti ni nyumba ya ibada na wala siyo sehemu ya kuoneshana ufahari.

Juu ya maandalizi ya sherehe ya ndoa na mambo mengine ya furaha Waislam hasa matajiri wameonywa vikali kwamba sherehe yoyote ambayo maskini hawajaalikwa imelaaniwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo kwenye mjumuiko wa matajiri waliovalia maridadi, utawakuta maskini hohehahe wakiwa huru wakichanganyika na matajiri — njia kubwa ya kuwakumbusha matajiri wajibu wao na sherehe hiyo ikiwapa maskini fursa ya kula vyakula vizuri vinavyotumiwa na matajiri.

## Kuridhia Mialiko ya Wenye Hali ya Chini

Matajiri na wale wenye hadhi katika jamii wamesisitizwa mno kuitikia mialiko ya watu wenye hali ya chini sana wanapowaalika majumbani mwao. Naam, si lazima kwa tajiri ambaye alishajipangia mipango yake na anajaribu kupambana na changamoto mbalimbali zinazomkabili; lakini huu ulikuwa ni utaratibu wa kawaida wa Mwanzilishi Mtukufu[saw] wa dini ya Kiislam kuitikia mialiko ya watu wa hali ya chini sana. Kwa wale wote wanaompenda na kujinasibisha nae kwa kuwa ni Kiongozi wao Mtukufu hujisikia fahari sana wanapolitekeleza fundisho hili. Ingawa kwa jamii ya leo tajiri akikubali mialiko yote ya namna hii hatakuwa na kazi nyingine ya kufanya zaidi ya hiyo, lakini bado umuhimu wa kula pamoja na mtu wa hali ya chini uko palepale na ubora wa fundisho hili unaweza kuwa umeheshimiwa na kuenziwa kwa kuitikia baadhi ya mialiko ya namna hii.

Tumeishasema hapo awali ya kwamba pombe na kamari vimekatazwa. Kwa hiyo matumizi ya anasa kwenye sherehe na furaha yameondolewa. Fundisho hili la jumla linalokataza matumizi ya vitu vya kifahari na maisha ya hali ya juu halihusiki tu kwa ajili ya sherehe za ndoa bali linahusika kwenye maeneo yote ya shughuli za mwanadamu. Uzuri wa fundisho hili halikuwekwa litekelezwe kwa kulazimisha bali linachochewa kwa maneno ya ushauri na upendo.

## Ulaji Chakula kwa Kiasi

يَٰبَنِيٓ ءَادَمَ خُذُواْ زِينَتَكُمۡ عِندَ كُلِّ مَسۡجِدٖ وَكُلُواْ وَٱشۡرَبُواْ وَلَا تُسۡرِفُوٓاْۚ إِنَّهُۥ لَا يُحِبُّ ٱلۡمُسۡرِفِينَ ٣١

*Enyi wanadamu, shikeni mapambo yenu wakati wa kila Sala; na kuleni na kunyweni wala msipite kiasi; hakika Yeye Hawapendi wapitao kiasi.*[15]

Muda hauniruhusu kupambanua juu ya haja ya kusaidia mapambano dhidi ya njaa yanayohitimishwa kwa hatua muhimu sana ya kuepusha umwagaji wa chakula. Hata hivyo jambo hili nitalirejea kwa uchache huko mbeleni.

## Ukopaji wa Fedha

Kuhusiana na kukopa fedha kwa ajili ya mahitaji ya msingi, Uislamu mara kwa mara umesisitiza kwa haja za dharura kutolewa mkopo huo bila riba. Wenye uwezo wawasaidie wenye kuhitaji msaada wa kifedha. Iko wazi kwamba mkopi asipoweza kulipa deni kwa muda uliowekwa kwa sababu ya hali yake ngumu basi apewe muda zaidi. Ndugu wa karibu wanaweza kumsaidia mdaiwa kulipa deni lake. Madeni yanaweza kulipwa kutoka kwenye mali ya urithi wa marehemu. Zaka inaweza kutumika kumsaidia mwenye mzigo mkubwa wa madeni. Mdai akisamehe deni ni bora zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Hata hivyo mdaiwa mwenye uwezo wa kulipa deni ni lazima atekeleze ahadi ya kulipa deni kwa wakati na anaweza kuongeza kiasi kidogo kama shukrani. Ni lazima ifahamike ya kwamba kiasi kinachoongezwa si lazima na wala hakijawekewa

kiwango kwani kufanya hivyo itakuwa ni sawa na kuweka riba. Kurani Tukufu inafundisha kwamba:

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْۤا اِذَا تَدَايَنْتُمْ بِدَيْنٍ اِلٰۤى اَجَلٍ مُّسَمًّى فَاكْتُبُوْهُ ؕ وَ لْيَكْتُبْ بَّيْنَكُمْ كَاتِبٌۢ
بِالْعَدْلِ ۪ وَ لَا يَاْبَ كَاتِبٌ اَنْ يَّكْتُبَ كَمَا عَلَّمَهُ اللّٰهُ فَلْيَكْتُبْ ۚ وَ لْيُمْلِلِ الَّذِيْ عَلَيْهِ الْحَقُّ وَ
لْيَتَّقِ اللّٰهَ رَبَّهٗ وَ لَا يَبْخَسْ مِنْهُ شَيْـًٔا ؕ فَاِنْ كَانَ الَّذِيْ عَلَيْهِ الْحَقُّ سَفِيْهًا اَوْ ضَعِيْفًا اَوْ لَا
يَسْتَطِيْعُ اَنْ يُّمِلَّ هُوَ فَلْيُمْلِلْ وَلِيُّهٗ بِالْعَدْلِ ؕ وَ اسْتَشْهِدُوْا شَهِيْدَيْنِ مِنْ رِّجَالِكُمْ ۚ فَاِنْ
لَّمْ يَكُوْنَا رَجُلَيْنِ فَرَجُلٌ وَّ امْرَاَتٰنِ مِمَّنْ تَرْضَوْنَ مِنَ الشُّهَدَآءِ اَنْ تَضِلَّ اِحْدٰىهُمَا فَتُذَكِّرَ
اِحْدٰىهُمَا الْاُخْرٰى ؕ وَ لَا يَاْبَ الشُّهَدَآءُ اِذَا مَا دُعُوْا ؕ وَ لَا تَسْـَٔمُوْۤا اَنْ تَكْتُبُوْهُ صَغِيْرًا اَوْ كَبِيْرًا اِلٰۤى
اَجَلِهٖ ؕ ذٰلِكُمْ اَقْسَطُ عِنْدَ اللّٰهِ وَ اَقْوَمُ لِلشَّهَادَةِ وَ اَدْنٰۤى اَلَّا تَرْتَابُوْۤا اِلَّاۤ اَنْ تَكُوْنَ تِجَارَةً حَاضِرَةً
تُدِيْرُوْنَهَا بَيْنَكُمْ فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ اَلَّا تَكْتُبُوْهَا ؕ وَ اَشْهِدُوْۤا اِذَا تَبَايَعْتُمْ ۪ وَ لَا يُضَآرَّ كَاتِبٌ وَّ
لَا شَهِيْدٌ ؕ۬ وَ اِنْ تَفْعَلُوْا فَاِنَّهٗ فُسُوْقٌۢ بِكُمْ ؕ وَ اتَّقُوا اللّٰهَ ؕ وَ يُعَلِّمُكُمُ اللّٰهُ ؕ وَ اللّٰهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيْمٌ ﴿۲۸۲﴾
وَ اِنْ كُنْتُمْ عَلٰى سَفَرٍ وَّ لَمْ تَجِدُوْا كَاتِبًا فَرِهٰنٌ مَّقْبُوْضَةٌ ؕ فَاِنْ اَمِنَ بَعْضُكُمْ بَعْضًا فَلْيُؤَدِّ
الَّذِي اؤْتُمِنَ اَمَانَتَهٗ وَ لْيَتَّقِ اللّٰهَ رَبَّهٗ ؕ وَ لَا تَكْتُمُوا الشَّهَادَةَ ؕ وَ مَنْ يَّكْتُمْهَا فَاِنَّهٗۤ اٰثِمٌ قَلْبُهٗ ؕ وَ
اللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ عَلِيْمٌ ﴿۲۸۳﴾

*Enyi mlioamini, mnapokopeshana deni kwa muda uliowekwa, basi liandikeni. Na mwandishi aandike baina yenu kwa uadilifu, wala mwandishi asikatae kuandika kama alivyomfunza Allah hivyo aandike. Na aandikishe (mkopi) ambaye juu yake iko dhima, naye amwogope Allah, Mola wake, wala asipunguze chochote ndani yake. Na kama yule ambaye juu yake iko haki ni mpumbavu au mnyonge, au yeye hawezi kuandikisha mwenyewe, basi aandikishe wakili wake kwa adili. Na mshuhudishe*

*mashahidi wawili katika wanaume wenu. Lakini ikiwa hakuna wanaume wawili, basi mwanamume mmoja na wanawake wawili katika wale mwapendao kuwa mashahidi, kama mmoja wao akisahau, mmoja wao amkumbushe mwingine. Na mashahidi wasikatae waitwapo. Wala msipuuze kuliandika, likiwa dogo au kubwa, mpaka muda wake: hayo ndiyo bora mbele ya Allah, na imara zaidi kwa ushahidi, na pia ni karibu ya kuwa msiwe na shaka, isipokuwa iwe biashara iliyohudhuria mnayopeana baina yenu, basi si dhambi kwenu msipoandika. Na shahidisheni mnapouziana. Wala asipate taabu mwandishi wala shahidi, na kama mkifanya hivyo, basi kwa hakika hilo ni kosa kwenu. Na mwogopeni Allah, na Allah Anawaelimisheni; na Allah ni Mjuzi wa kila kitu. Na kama mkiwa safarini au hamkupata mwandishi, basi rehani ikabidhiwe (mdai); lakini kama mmoja wenu ameweka amana kwa mwingine, basi aliyeaminiwa airudishe amana ya mwenzake, na amche Allah, Mola wake, Wala msifiche ushahidi; na atakayeuficha, basi hakika moyo wake ni wenye dhambi. Na Allah Huyajua mnayoyatenda.*[16]

Ni muhimu sana kufahamu ya kwamba aya hizi zimetafsiriwa na kutumika vibaya kabisa na wale waliozifuata fikra za wanazuoni wa karne zilizopita wanaosisitiza ya kwamba ushahidi wa mwanamke mmoja hautoshelezi. Wanasema ili kutosheleza ushahidi kisheria ni lazima kupata ushahidi wa wanawake wawili dhidi ya ushahidi unaojitosheleza wa mwanamume

mmoja. Baada ya kushindwa kabisa kuelewa maana ya aya hizi wamejiingiza kwenye uwongo wa kutengeneza kazi za shahidi mwanamke na mwanamume kwenye fikihi ya Kiislam. Wanadhani ya kwamba Kurani Tukufu inapomtaja mwanamume mmoja kuwa shahidi basi ushuhuda wa wanawake wawili unaweza ukachukua pahala pake, na sehemu ya wanaume wawili kutoa ushahidi ikabadilishwa kwa wanawake wanne na ambapo wanaume wanne watatakiwa kutoa ushahidi wanawake wanane watahitajika kutoa ushahidi huo huo. Wazo hili sio tu limekosa uhalisia bali haliendani kabisa na mafundisho ya Kurani Tukufu na linamfanya mtu aone kero kwa msimamo wa wanazuoni wa karne zilizopita juu ya jambo hili lenye umuhimu wa kipekee kisheria.

Aya hizi zimetaja mambo manne muhimu yafuatayo:-

1. Aya hazihitaji wanawake wote kutoa ushahidi.
2. Jukumu la mwanamke wa pili limeelezwa wazi na limebaki kuwa ni msaidizi.
3. Ikitokea mwanamke wa pili ambaye si mtoa ushahidi ataona sehemu yoyote ya maelezo ya mtoa ushahidi yanapishana na ukweli wa jambo linalojadiliwa anaweza kumkumbusha mtoa ushahidi.
4. Ni jukumu la mwanamke mtoa ushahidi kukubali au kutokubaliana na msaidizi wake. Ushahidi

unabakia kuwa ni wa mwanamke mtoa ushahidi na ikitokea kutokubaliana na mwenzie neno lake ndilo litakalochukuliwa kama ushahidi.

Baada ya kutoka kidogo nje ya mada, twarejea kwenye somo husika. Kurejea makubaliano ya deni na kulifuta kwa kufuata maombi ya mdaiwa mbele ya mashahidi wa mkataba wa mauziano ya bidhaa, kuwa mwaminifu na kuwa na hofu ya Mwenyezi Mungu katika kutekeleza shughuli zake; na wadhamini kutekeleza dhamana yao kwa uaminifu ni sifa muhimu za mikataba katika Islam.

Ifahamike ya kwamba kwenye uchumi ambao hakuna riba kwenye kukopeshana, mkopeshaji hawezi kukopesha fedha zake kwa urahisi. Kwa hiyo uwezo wa jamii kufanya matumizi unabaki kwenye uhalisia wake na hivyo kukomesha tabia ya kufanya matumizi ya kipato cha baadae. Biashara inayoanzishwa katika mazingira ya namna hii ni lazima itaimarika na kustawi hata katika mapito magumu ya hatari za kiuchumi.

Fedha za umma hazitakiwi kuzunguka kwenye anga za wenye nacho pekee bali ni lazima zizunguke kuelekea kwenye uwanda wa watu wa hali ya chini na wasionacho.

Islam inaweka mfumo wa maisha yaliyo rahisi yasiyohamasisha tamaa na ufisadi kiasi cha kuanza kuudhi watu wa matabaka ya chini na kuwasababishia maumivu ya moyo na kuongeza utofauti wa matabaka haya mawili ya jamii.

## Tofauti za Matabaka ya Kiuchumi

Ieleweke vyema kwamba matabaka hujitokeza sio tu kwa sababu ya kujilimbikizia mali kwenye mikono ya watu wachache, la hasha, bali matabaka yanaweza kujitokeza kutokana na mgawanyo wa fedha miongoni mwa wamiliki na wafanyakazi au wamiliki wa ardhi na walimaji / watenda kazi kwenye ardhi hiyo. Ziko sababu nyingi zinazosababisha matabaka kwenye jamii na si rahisi kuzitaja sababu zote na namna zinavyochangia uwepo wa matabaka. Uchunguzi wa jadi ya jamii ya Kihindi unatoa mfano mzuri sana wa uwepo wa matabaka kwa miaka elfu kadhaa. Matabaka haya hayakusababishwa na ugawanaji wa mali bali yalisaidiwa na mambo yaliyotokana na ubaguzi wa rangi, hadhi katika jamii, dini pamoja na siasa. Kuna historia ya muda mrefu inayohusu uvamizi, mapigano ya wenyewe kwa wenyewe, kupambana ili kuishi na kutawala, iliyohifadhiwa kwenye mfumo wa tabaka litokanalo na ukoo, kazi vyeo na kadhalika wa Kihindi, ambayo imesaidia kuweka njia za matabaka mbalimbali.

Max alifahamu vyema hali hii na katika mlolongo wa barua zake alizoziandikia gazeti la *Herald Tribune* la mjini New York alieleza hali ya jamii ya India kuwa haiendani na falsafa ya Ukomunisti. Alikiri ya kwamba uwepo wa mfumo wa tabaka la utawala unaifanya India iwe nchi isiyoweza kubadilika kuwa ya Kikomunisti. Kwa muono wa Kiislam mfumo wa matabaka kwenye jamii unaanza kuumiza pale tu unapokosekana utaratibu

wenye maadili thabiti wa kusimamia namna bora ya matumizi ya fedha. Chukulia mfano wa jamii inayoishi maisha ya kawaida yasiyo na matumizi ya anasa kwenye mavazi, chakula na malazi na hakuna utofauti sana unaojitokeza wa hali ya maisha ya wanajamii hao. Jamii kama hii watu hawapati maumivu bila kujali ni kiasi gani cha mali kinachomilikiwa na watu wachache. Kwa ujumla namna ya kufanya matumizi ndiyo inayoumiza, hasa matumizi yakifanywa pasipo uangalifu tena kwa uharibifu. Ni maisha ya anasa ya mataijiri yanayoambatana na kujionyesha, ufahari na kushindana yanayoleta maumivu. Mambo haya yanapoonwa na mtu anayeishi kwenye maisha ya taabu na kubanwa na umaskini na kupambana na maisha ndipo unapozalika ufa mkubwa usiozibika wa hisia tofauti baina ya makundi haya mawili. Kwa hiyo Uislamu haujazuia kabisa uhuru wa mtu kuchuma mali na kuhifadhi. Badala yake Uislamu unahimiza ukuzaji wa sekta binafsi kuliko hata ya umma. Islam imeweka taratibu za maisha zilizoelezwa kwa ufasaha ambayo kama zitekelezwe zote tena kwa moyo wote, itafanya maisha kwa wote yawe rahisi na yaburudishayo. Inafaa kukomea hapa kwa kuwa falsafa ya uchumi wa Kiislam inayoelezea kipengele hiki ilishajadiliwa.

## Sheria ya Mirathi ya Kiislam

Sheria ya mirathi ya Kiislam inafanya kazi kubwa ya kugawa mali za marehemu kwa wategemezi wake. Mafungu yaliyopangwa ni lazima yagawiwe kwa

wazazi, mke, mume, watoto, ndugu na jamaa wa karibu. Hakuna anayeweza kuwanyima haki zao za kurithi walizopewa na Mwenyezi Mungu isipokuwa kama kuna sababu ya msingi ambayo katika nchi ya Kiislam sababu hiyo itathibitishwa na mahakama na sio mtu mwingine yeyote. Katika Islam mtu anaruhusiwa kuwatolea wasia watu wengine au taasisi anayoipenda mali yake isiyozidi theluthi moja.[17] Njia hizi ndizo zinazosaidia sana katika kuhakikisha mali hairundikani katika mikono ya watu wachache.

Sheria ya mirathi ya Kiislam inaondoa matendo ya kunyima haki za warithi, kama vile inazuia utaratibu wa mali yote ya mzazi kurithiwa na mtoto wa kwanza wa kiume au ugawaji wa mirathi usizingatie uadilifu au uwezo usio na mipaka wa matakwa ya mwenye kutoa wasia. Katika mfumo huu mali zote zinazohamishika na zisizohamishika zitaendelea kugawanywa kupitia kizazi kimoja hadi kingine mpaka kizazi cha tatu au nne, hata urithi wa mashamba makubwa hugawanywa kwenye miliki ndogondogo kiasi kwamba kunakuwa hakuna mfarakano wa kudumu unaotokana na kuhodhi umiliki wa ardhi.

## Makatazo ya Hongo

وَلَا تَأْكُلُوٓا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ وَتُدْلُوا بِهَآ إِلَى الْحُكَّامِ لِتَأْكُلُوا فَرِيقًا مِّنْ أَمْوَالِ النَّاسِ
بِالْإِثْمِ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١٨٩﴾

*Wala msiliane mali zenu kwa batili na kuzipeleka (kama hongo) kwa mahakimu ili mpate kula sehemu ya mali ya watu (wengine) kwa dhambi na hali mnajua.*[18]

Mara nyingine tena yanibidi niache kueleza kipengele hiki ambacho kinajidhihirisha vizuri sana kwa sura ya hongo katika nchi za Ulimwengu wa Tatu, lakini nitakieleza kwenye somo linalohusu utulivu wa mtu binafsi.

**Maadili ya Kibiashara**

Uislamu haukubaliani na ubepari na wala haukatai kabisa ukomunisti, bali unabakiza mambo na mienendo mizuri ya mifumo hii.

Ifuatayo ni mifano ya maadili mema ya kibiashara yaliyofundishwa miaka 1400 iliyopia ambayo mwanadamu ameanza kuyagundua leo:-

1. Mahusiano ya kibiashara ya Kiislam yanategemea uadilifu na uaminifu wa hali ya juu sana.[19]
2. Islam inakataza matumizi ya vipimo vya uwongo na mizani isiyotimia.[20]
3. Wafanyabiashara wamekatazwa kuuza bidhaa zenye kasoro zilizooza au zisizofaa kwa matumizi. Mchuuzi hatakiwi kujaribu kuficha kasoro yoyote ya bidhaa anayoiuza.[21] Ikitokea bidhaa yenye hitilafu au kasoro ameuziwa mnunuzi bila ya yeye kufahamu, mnunuzi anayo

haki ya kurudisha bidhaa hiyo atakapogundua hitilafu au kasoro na kurudishiwa fedha yake.[22]

4. Mfanyabiashara amekatazwa kupandisha bei kwa kumwangalia mteja ingawa maamuzi ni yake ya kuuza kwa bei ya mapatano kwa mteja yeyote. Muuzaji yuko huru kuweka kiwango chochote cha bei anachokiona kinafaa.[23]

5. Islam inakataza ushindani wa kibiashara wa kutengenezwa au upangaji wa bei unaopelekea ushindani usio halisi. Kuongeza bei kwenye mnada kwa kutamka bei isiyoendana au kuahidi kununua kwa bei bandia ili kuwazuia wanunuzi wengine kumekatazwa pia kwa mujibu wa Islam.[24]

6. Islam inapendekeza mauziano ya bidhaa yafanyike sehemu ya wazi na ikiwezekana kuwe na mashahidi, na mnunuzi aelezwe tahadhari za bidhaa anayonunua.[25]

Kwa ufupi Islam imeweka mkakati wa kuhakikisha tofauti kati ya matajiri na maskini inapungua kwa kufanya yafuatayo:

1. Imeweka makatazo kadhaa kama ilivyoelezwa hapo awali kwa mfano unywaji wa pombe na kamari.

2. Katazo la kuhodhi mali na ulimbikizaji wake unaotokana na riba.

3. Kuhamasisha biashara na uwekezaji binafsi
4. Kuchochea mzunguko mpana wa fedha.
5. Kujirudia kwa maonyo, ushawishi na maagizo yanayomnasihi mwanadamu kuwa na mwenendo mwema ili kwa hiari yake aishi maisha yasiyo na makuu yaliyojaa uvumilivu na yaliyo rahisi yanayoendana na mtu wa hali ya kawaida.

Nia kubwa ni kumfanya mwanadamu atambue zaidi hali ya wengine na kupunguza hisia za kikatili na tamaa na kuzifanya zisifanye kazi. Vita takatifu kwa maana halisi ya neno lenyewe ni kujizuia dhidi ya majisifu, unafiki, majivuno na purukushani. Tabia hizi zinapoboreshwa mwanadamu anakuwa mwema na anafanywa kuwa mwenye kujali sana taabu za wengine kiasi ambacho wakati mwingine anahisi haifai kuishi vizuri wakati wengine wakitaabika na kupata riziki yao kwa shida sana, hofu na unyonge.

Kwa kawaida watu wenye utamaduni wa hali ya juu wa kuwa mstari wa mbele katika kujali thamani ya mwanadamu huwa ni wachache kwenye jamii ingawa wanaiamsha jamii kwa kiwango kikubwa sana kutambua mahitaji ya wengine na inakuwa haiwezekani kujiangalia hali zao binafsi na kusahau hali mbaya ya watu wa tabaka la chini kwenye jamii. Hofu yao ya maisha haiwi tena kwa ajili yao tu bali huanza kujifunza kuishi kwa kufikiria haja za watu mbalimbali wanaoishi nao. Jamii haijisikii vizuri bila kushiriki kwa vitendo

kuziondoa dhiki na kuinua viwango vya maisha ya wengine. Mwenendo wa jamii kama hiyo ambayo ni ya watu wachaMungu umeelezwa katika aya za mwanzo za Kurani Tukufu iliyonukuliwa hapo nyuma:

وَمِمَّا رَزَقْنَٰهُمْ يُنفِقُونَ ۝٣

*Na hutoa katika yale Tuliyowapa.*[26]

## Mahitaji ya Msingi

Kwenye sehemu iliyopita iliyozungumzia amani ya kijamii na kiuchumi tumeona namna Uislamu ulivyoleta mapinduzi ya matumizi ya sadaka na kutimiza haja za maskini na wenye mahitaji. Kuhusiana na haki za watu mbalimbali kutoka kwenye mfuko wa taifa Kurani Tukufu imetoa vigezo vya kutathmini kiasi cha fedha zilizohamishiwa kwa matajiri ambazo zilitakiwa kupelekwa kwa wananchi maskini.

وَالَّذِينَ فِيٓ أَمْوَٰلِهِمْ حَقٌّ مَّعْلُومٌ ۝٢٤ لِّلسَّآئِلِ وَالْمَحْرُومِ ۝٢٥

*Na ambao katika mali zao iko sehemu maalumu, Kwa ajili ya aombaye na maskini asiyeomba.*[27]

Aya hizi zinawaeleza matajiri kwa kuwakumbusha kwamba katika sehemu ya utajiri wao iko haki ya maskini na mafukara.

Je tunawezaje kuamua kwamba jamii haikutenda haki kwa kuhamisha haki za maskini kwa matajiri? Kipimo cha kigezo hiki ni kuona baadhi tu ya haki zilizoahidiwa kutolewa.

Kwa mujibu wa Uislamu kuna mahitaji ya msingi manne ya binadamu ambayo ni lazima ayapate. Kurani Tukufu inasema:

إِنَّ لَكَ أَلَّا تَجُوعَ فِيهَا وَلَا تَعْرَىٰ ﴿١١٩﴾ وَأَنَّكَ لَا تَظْمَأُ فِيهَا وَلَا تَضْحَىٰ ﴿١٢٠﴾

*Hakika hutakuwa mwenye njaa humo wala hutakuwa uchi. Na kwa yakini hutapata kiu humo wala hutapata joto.*[28]

Hivyo Uislamu umeweka haki za kiwango cha chini kwa namna ya mkataba wenye mambo manne yanayomaanisha mahitaji ya msingi ambayo serikali inawajibika kuhudumia. Mahitaji hayo ni:

1. Chakula 2. Mavazi 3. Maji 4. Makazi.

Hata katika nchi zilizoendelea kama Uingereza na Marekani bado kuna mamia ya maelfu ya watu wanaokosa pa kulala na wale wanaopita kwenye mapipa ya takataka wakitafuta makombo yawasaidie kuondoa njaa zao.

Mambo yanayoonyesha matendo yasiyovutia kama hayo yanabainisha udhaifu uliopo wa jamii za kibepari na kuibua dalili za maradhi yaliyojificha. Hatima ya tamaa ya mali ni uchoyo na kutojali, na kuhafifisha uwezo wa kujali matatizo ya wengine.

Kuna matukio mabaya zaidi ya hayo tena ya kuogofya yanayotokana na umaskini uliotopea uliopo katika nchi nyingi za Ulimwengu wa Tatu; tatizo ni kwamba jamii

kwa ujumla ni maskini na nchi zenyewe zinaendeshwa katika misingi ileile ya kibepari. Hivyo sio suala la walio wengi kwenye nchi hizo kuwa ni Wakristo, Wayahudi, Wahindu, Waislamu au wapagani bali ni mfumo ambao kimsingi unabaki kuwa ni wenye asili ya kibepari.

Uhalifu unaendelea kustawi na uovu unaongezeka kwenye mitaa wanayoishi watu maskini kwenye nchi zinazoitwa zimeendelea; hizi ni nini kama si dosari kwenye uso wa ubinadamu wenyewe?

Katika bara la Afrika na nchi nyingine yapo maeneo ambayo sehemu kubwa ya jamii inakosa hata maji safi ya kunywa. Ukiweza hata kupata mlo mmoja kamili kwa siku unajiona ni mwenye bahati. Na tatizo la kukosa maji ni la kila siku tena kwa kudumu. Ziko nchi ulimwenguni zilizo na uwezo na njia za kila namna kubadilisha hali yao kwa kipindi cha miaka michache bila wenyewe kupata maumivu. Lakini bado nchi hizo hazijali na wala hazitoi kipaumbele katika kuwekeza rasilimali zao ili kutengeneza hali bora ya mamilioni ya watu wanaopata dhiki kwenye nchi maskini.

Kwa muktadha wa Islam, jambo hili ni muhimu sana. Katika Uislamu taifa haliwajibiki tu kwa shida anazopata mwananchi wake bali jamii katika nchi hiyo ina wajibu wa kutatua shida za binadamu katika jamii yao na jamii nyingine yoyote ile. Kwa maneno mengine taifa linao wajibu wa kujali ubinadamu ambao hauna mipaka ya kitaifa, kidini, kisiasa na rangi.

Ubinadamu ni kuwajibika; hivyo basi mwanadamu anawajibika kwa Mungu. Endapo jamii yoyote inakumbwa na baa la njaa, utapiamlo, au janga jingine lolote asilia ni lazima janga hilo lichukuliwe kuwa ni mkasa wa kibinadamu ambao jamii na nchi zote za ulimwengu zinatakiwa kushiriki katika juhudi za kusaidia kupunguza makali ya janga hilo.

Inaleta fedheha kwamba pamoja na maendeleo yote yaliyofikiwa ya sayansi na teknolojia utokomezaji wa njaa na kiu haujapata msukumo stahiki. Ni lazima kuwe na mfumo kabambe utakaohakikisha kupelekwa kwa haraka na ufanisi rasilimali zote kwenye maeneo yaliyokumbwa na njaa inayotaabisha binadamu ama sehemu yoyote ambayo watu wamepata ufukara na ukosefu wa makazi.

Serikali zina majukumu ya kitaifa na kimataifa. Majukumu katika ngazi ya kitaifa ni pamoja na kutimiza mahitaji ya msingi ya kila raia kwa kuhakikisha kwamba wote wanapata chakula cha kutosha, mavazi na wanapelekewa huduma ya maji na makazi. Wajibu wa serikali kimataifa ni kushiriki kikamilifu katika ukusanyaji wa rasilimali za kushughulikia changamoto za majanga makubwa ya asili au maafa yanayotokana na shughuli za kibinadamu na kuzisaidia nchi ambazo hazina uwezo wa kushughulikia vema migogoro.

Ni jukumu la serikali kuweka mambo yake vyema kwa kuwarudishia mafukara na maskini kile kilicho haki yao.

Kwa hivyo mahitaji ya msingi kama chakula, mavazi, maji na makazi vitawekewa kipaumbele. Serikali ikiweza kuhakikisha upatikanaji wa mahitaji haya ya msingi inakuwa angalau imeshatekeleza wajibu wake wa msingi ingawa jamii kwa ujumla wake inatakiwa itekeleze zaidi ya hapo.

“Mwanadamu hawezi kuishi kwa mkate tu” ni msemo maarufu wenye uzito wa aina yake. Pamoja na mkate huo anahitaji pia maji safi na salama, mavazi yanayofaa na sehemu ya kujihifadhi. Hata kama mahitaji haya yote yajumuishwe pamoja bado hayawezi kukamilisha maisha. Mwanadamu atataka mara zote jambo zaidi ya mahitaji ya msingi ya maisha. Kwa hiyo jamii lazima ijipambanue kufanya jambo lolote zaidi kuondoa yasiyofaa na kuboresha hali ya maisha ya watu wa chini na kuwafanya nao waweze kupata raha wanazozipata wenye nacho.

Haitoshi tu kwa wenye uwezo kuwapa wale wasio na uwezo katika jamii bali ni lazima nao waonje machungu yanayoendana na hali ya kuwa maskini inayowatesa wanadamu wengi. Uwekwe utaratibu utakaowezesha kuchanganyika maskini na matajiri ambapo kwa ridhaa yao watu wa matabaka ya juu ya jamii wanajumuika na wale wa matabaka ya chini ili washuhudie wenyewe hali halisi ya kuishi kimaskini. Islam imependekeza hatua nyingi mbalimbali zinazoyafanya matabaka mbalimbali yasiweze kujiweka

na kufanya mambo peke yao. Hatua hizo zimeelezwa kwa ufupi hapo nyuma.

## Ibada Kama Njia ya Umoja wa Kiuchumi

1. Kwa kuanza na ushuhuda kwamba hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu, inaleta Umoja wa Mungu na viumbe vyake kunakomuunganisha mwanadamu na Muumba wake.

2. Sala tano za kila siku zinazoswaliwa kwa jamaa inaweza kuwa ndiyo njia inayofaa zaidi kuliko hatua nyingine zote juu ya jambo hili. Matajiri, maskini, watoto kwa wakubwa wanatakiwa wote waswalie misikitini pale inapowezekana. Hata kama sio wote lakini sehemu kubwa ya jamii ya Kiislam inajishughulisha katika kutimiza agizo hili. Kwa baadhi ya nchi inaweza kuwa ni asilimia ndogo ya wanaoswali sala tano kila siku na nchi nyingine ikawa asilimia kubwa lakini kwa ujumla ni jambo la kawaida linalofanywa na sehemu kubwa ya Waislam karibu wote. Utaratibu wenyewe wa sala unatoa ujumbe mkubwa sana wa usawa wa binadamu. Anayetangulia kufika msikitini anakaa sehemu anayoipenda na hakuna anayeweza kufikiria kumuondoa hapo hata kama kuwe na mwenye nafasi kubwa kwenye jamii. Wakati wa kuswali wote husimama kwa kugusana mabega. Kwa hiyo aliyevaa kwa

umaridadi na unadhifu anaweza kusimama pamoja na aliyevaa mavazi kuukuu. Mdhaifu aliyekondeana huchanganyika pamoja kila siku na mwenye afya aliyenawiri kwenye ukumbi mmoja ambako ujumbe unaotawala ni “Mungu ni Mkuu”.

Kujionea machoni namna baadhi ya wakazi wanavyoishi kwa mashaka na kukutana nao kila siku huacha athari nzito sana moyoni mwa mtu anayeishi maisha yenye unafuu. Ujumbe unakuwa wa wazi na unamtaka mwenye unafuu wa maisha afanye jambo fulani kubadilisha na kuboresha hali zao vinginevyo ajishushe hadhi mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele yake binafsi.

Fursa ya kukutana huongezeka zaidi kila siku ya Ijumaa ambapo Waislam huswali kwenye msikiti mkuu ambako matajiri wa sehemu moja wanakutana na wale wanaotoka maeneo ya maskini. Wigo hupanuka hata zaidi ya hapo kwenye sherehe mbili zinazofanyika kwa mwaka zinazotanguliwa na ‘Fitrana’ — mfuko unaochangiwa kwa hiyari kuwasaidia maskini.

3. Mwezi wa kufunga kwa Waislam pia unaweka uwanja sawa kwa maskini na matajiri. Tajiri anapata kiu na njaa vikimkumbusha maumivu ya maskini ambaye ni hali ya kawaida kwake kukaa na njaa na kiu.

4. Zaka hupeleka kwa maskini haki zao kutoka kwa wenye nacho.

5. Mwishowe ni nguzo ya tano ya Kiislam, Hija inayoelezewa kuwa ni ibada inayowaunganisha wanadamu wengi zaidi. Mahujaji wanawake wameruhusiwa kuvaa nguo zilizoshonwa kawaida. Mahujaji wanaume hujivika maguo – migolole miwili yenye rangi nyeupe isiyoshonwa iliyo sare kwa tajiri na maskini.

Haiishii hapo tu kwa sababu licha ya matendo ya ibada yaliyoainishwa hapo juu ziko hatua nyingine kadhaa zilizotekelezwa na jamii za Kiislam ambazo zinadumu kupunguza utofauti baina ya matabaka ya jamii na kuleta hali njema inayofaa kuweka mazingira ambayo tajiri anaendelea na utajiri wake lakini pia anawajibika kuhudumia maskini.

Kanuni kama hiyo ilielezwa na Hadhrat Isa[as] aliposema; "Mnyenyekevu atairithi dunia". Inasikitisha sana kuona kwamba licha ya agizo hili la kimaadili, ubepari umeshindwa kabisa kuwajali maskini na watu wanyenyekevu kwenye jamii.

## Majukumu ya Kimataifa

Kurani Tukufu ikizungumzia njia mbadala ya kushika pale yanapotokea majanga yoyote ya asili au baa kubwa linapoikabili jamii (rejea mahitaji ya msingi yaliyotajwa hapo kabla) inaeleza chaguo sahih kwa utaratibu ufuatao:

فَكُّ رَقَبَةٍ ﴿١٤﴾ أَوْ إِطْعٰمٌ فِي يَوْمٍ ذِي مَسْغَبَةٍ ﴿١٥﴾ يَتِيمًا ذَا مَقْرَبَةٍ ﴿١٦﴾ أَوْ مِسْكِينًا ذَا مَتْرَبَةٍ ﴿١٧﴾

*Ni kumpa mtumwa uungwana, Au kumlisha siku ya njaa, Yatima jamaa, Au maskini hohe hahe.*[29]

Kwa maneno mengine uamuzi ulio bora katika kuhudumia waliopatwa na majanga utafanywa kwa mtiririko huu:

1. Msaada ulio wa kweli kabisa kwa mwanadamu ambao unakubalika mbele ya Mwenyezi Mungu umeelezwa hapa. Kipaumbele katika kupewa msaada miongoni mwa wanaohitaji msaada ambao mwanadamu anatakiwa kuwasaidia ni waliodhulumiwa. Msaada wowote unaokwenda tofauti na kanuni hii hauna thamani mbele ya Mwenyezi Mungu. Kwa mtazamo huu, utaratibu wa kisasa wa kutoa misaada ya kifedha inayoambatana na masharti magumu kwa nchi maskini haukubaliki kabisa.
2. Chaguo linalofuata ni kumlisha yatima hata kama anae mlezi anaemsaidia.
3. Na chaguo la mwisho ni kumlisha fukara asiyeweza kabisa kujisaidia.

Licha ya kuwa katika hali ya nafsi ya umoja, aya hizi zinaonesha kuelezea mgogoro mpana sana. Kidokezo cha neno 'yaum' (lenye maana ya siku) na namna aya zinavyoeleza ni wazi juu ya jambo hilo. Katika kufikiria kwa makini aya hizi zinatoa picha halisi ya namna nchi kubwa tajiri na zenye nguvu zinavyozifanyia nchi

maskini zenye haja hasa ya msaada wakati wanapopatwa na madhara ambayo hawawezi kujisaidia. Nchi hizo maskini husaidiwa kwa misaada inayoambatana na masharti magumu hivyo kuharibu nia na madhumuni ya kusaidia wengine. Kidhahiri zinasaidiwa kutolewa kwenye balaa moja kwa kupelekwa kwenye mtego mwingine.

Mfumo mzima unaotumiwa zama hizi kwa ajili ya misaada ya kimataifa yenye masharti magumu umenyambulishwa kwa wepesi kabisa kupitia maneno hayo machache ya Kurani Tukufu. Waumini wameagizwa kutotumia mwanya wa kuwasaidia wasioweza kujisaidia kwa kupunguza machungu kwa watu na nchi maskini wakati huo huo wakiwanyima uhuru wao.

Neno 'yatima' hapa limetumika kwa maana pana kwa kujumuisha mtu au nchi zisizojitegemea. Ziko nchi zinazofanana na yatima mwenye ndugu na jamaa wengi lakini zimetelekezwa na ndugu na jamaa zao. Nchi hizo zisiachwe bila kusaidiwa kwani zinaweza hata kusaidiwa na wengine ambao wana wajibu wa msingi kwao.

Mfano mzuri unaoweza kutajwa hapa ni nchi zenye utajiri wa mafuta. Kama nchi chache tu za Ghuba zingeungana kupunguza madhila makubwa yanayowasumbua wanadamu walio wengi, wangekuwa tayari wameshatatua tatizo la njaa na ukame

linalolikumba bara la Afrika bila hata nchi hizo kupata maumivu yoyote. Kiwango kikubwa cha fedha walizotunza kwenye mabenki na rasilimali walizowekeza kwenye nchi za Magharibi zinazalisha riba na kipato kingine ambacho kingetosha kabisa kumaliza hali ngumu inayowakumba watu wa Afrika. Kwa mujibu wa Islam wao hawana namna yoyote ya kutumia riba kwa manufaa yao binafsi.

Kuhusiana na baa kubwa la njaa, misukosuko na mahitaji yanayotokana na majanga ya matetemeko na mafuriko huko Bangladesh ni mfano mwingine unaofaa kuelezea. Kwa ujumla Dunia imewasusia Wabangladeshi peke yao kadhia hii. Kama kuna msaada wowote unaowafikia ni kidogo usiotosheleza kujinasua kokote kutoka kwenye janga hilo.

Mataifa yenye matatizo kama haya yanatakiwa kuchukuliwa kama yatima kwa maana pana ya neno lenyewe yatima. Mataifa yatima kama haya yanaposuswa na ndugu na jamaa zao linakuwa ni kosa kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu.

Watu wamejijengea tabia hasi ya kumlaumu Mwenyezi Mungu na majanga ya asili yanayosababisha mateso kwa nchi maskini. Ukweli ni kwamba mwanadamu mwenyewe ndiye anaetakiwa kulaumiwa kwa usugu na kutokujali kwake hali za wengine. Kama tuijaze mioyo ya wanadamu kwa sifa ile maalum itakayowafanya

waweze kuumia kwa ajili ya wengine, dunia inaweza kugeuzwa kuwa pepo.

Katika ulimwengu nje ya Uislam, tabia ile ile ya uchoyo ndiyo inayotawala. Kwa mfano nchi kama Ethiopia yenye mahusiano ya karibu na muungano wa Kisovieti msaada hautakiwi kusimamishwa kwa kisingizio cha kuitaka Jumuiyya ya Kisovieti itekeleze wajibu wake kwa kuwa ni mlezi wa Ethiopia. Ikiwa mamilioni ya Waislamu wanakufa kwa njaa nchini Sudan taabu yao isidharauliwe kwa kisingizio kuwa nchi ndugu zao tena zenye uwezo kama Saudi Arabia na nchi nyingine za Kiislam zenye utajiri wa mafuta ndizo zenye wajibu mkubwa wa kuwalisha. Hii ndiyo maana halisi ya maneno ya Kiarabu; "*Yatiman dha maqrabatin*" ikimaanisha yatima, aliye jamaa wa karibu.

Pia aya hii imeelekeza kwamba watu binafsi au mataifa yaliyo kwenye dhiki kutokana na mikwamo ya kiuchumi ni lazima kusaidiwa mpaka pale watakapoweza kusimama wenyewe. Hali hii ndiyo iliyoko kwenye nchi nyingi za Ulimwengu wa Tatu ambazo uchumi wao unaporomoka kwa haraka kwa sababu tu hawapewi kwa wakati misaada yenye uzito unaostahili.

Chaguo la tatu ni "*au Miskinan dha matrabatin*", ambalo linatumika kwenye uchumi ambao umeparaganyika kabisa na mfumo mzima wa uchumi umeanguka. Kwa mujibu wa Kurani Tukufu haitoshi kuwalisha tu watu

kwenye nchi kama hizo. Ni wajibu wa mwanadamu kuchukua hatua zitakazoweza kustawisha uchumi wao.

Kwa bahati mbaya mahusiano ya kibiashara katika zama hizi yanakwenda kinyume chake. Fedha mara zote hutiririka kuelekea kwenye nchi tajiri na zilizoendelea wakati uchumi wa nchi maskini ukiendelea kudidimia kuelekea katika hali ya hatari.

Mimi si mchumi lakini angalau ninafahamu kwa kiasi hiki tu ya kwamba si rahisi kwa nchi za ulimwengu wa tatu kuendelea na mahusiano ya kibiashara na nchi zilizoendelea na wakaweza kuzuia mtiririko wa mali kutoka kwenye nchi zao kuelekea nchi zilizoendelea kwa kuhakikisha wanaweza kulinganisha mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa kwenye nchi hizo dhidi ya yale yanayopatikana kutokana na uingizwaji wa bidhaa kutoka kwenye nchi zilizoendelea.

Jambo jingine la kutafakari ni hili ya kwamba nchi zote zilizoendeela kiuchumi daima zinasisitiza juu ya uboreshaji wa viwango vya maisha. Nchi maskini zinahimizwa kukopa fedha ili ziweze kufikia viwango vinavyoongezeka vya ubora wa maisha vya nchi zilizoendeelea. Teknolojia ya dijitali inaelekeza kwenye maisha mazuri na rahisi hata kama hatima ya mazoea yake yanaweza kumuathiri vibaya mwanadamu kwa kuondokana na sifa yake muhimu ya ugumu na kugangamala. Ikiwa watu wa nchi zilizoendelea wanataka kunenepesha mashavu yao na kuimarisha afya

ya viungo vyao; zitategemewaje nchi zenye uwezo zisaidie nchi maskini zilizobakiwa na tone la mwisho la damu kuondokana na hali ya madhara wakati ikifahamika wazi kiu kubwa ya nchi zilizoendelea kutaka kufyonza damu hiyo ili kudumisha viwango vya ubora wa maisha yao na kuhamishia fedha zote kwenye uchumi wao?

Shindano hili la kiwendawazimu la kupandisha viwango vya ubora wa maisha bila kutofautisha, sio tu linakaba fursa ya kuwepo na kuendelea kwa nchi maskini bali linakaba nchi zenyewe zilizoendelea kwa kukosekana utulivu na kutosheka kwa mioyo. Jamii yote kwa ujumla imejazwa tamaa ya kutaka mahitaji ya bandia na kila mmoja anaishi katika hali ya kutaka vitu vya kisasa vinavyostarehesha. Hii ndiyo hali ya mambo ambayo inaweza kusababisha vita.

Mwenendo kama huu umekatazwa kabisa kwenye Uislam. Uislamu unawaonyesha taswira ya jamii ambayo watu wanaishi kulingana na hali halisi za vipato vyao vinavyowafanya wajiwekee akiba katika siku za shida sio tu kwa ngazi ya mtu na familia yake tu bali hata kwenye ngazi ya taifa.

Kwa nchi maskini zaidi hali hiyo inakuja na msukumo unaoambatana na hatari kwa sababu nchi zilizoendelea zinapokumbana na changamoto mpya za ushindani kutoka katika nchi zinazochipukia kiuchumi na uchumi wao kuanza kukwama zinaanza kuwa na mahusiano

magumu yenye vipingamizi vinavyoziumiza zaidi nchi za Ulimwengu wa Tatu au nchi zile maskini. Hili haliepukiki kwa sababu kwa namna moja au nyingine serikali za nchi tajiri ni lazima zidumishe kiwango fulani cha ubora wa maisha kwa raia wake ambao tayari wameshazoea hali hiyo ya maisha. Hatimaye ubaya wa mambo haya huzidi kuongezeka na kupanuka; na yakifikia kileleni husababisha vita. Ni vita kama hivyo ambavyo Uislamu unataka kuzuia.

## Marejeo

---

[1] Sura 89: Al-Fajr: 18–21
[2] Sura 102: Al-Takathur: 2–4
[3] Sura 3: Al-'Imran: 190
[4] Sura 4: Al-Nisa': 54
[5] Sura 16: Al-Nahl: 72
[6] Sura 4: Al-Nisa': 59
[7] Sura 64: Al-Taghabun: 16
[8] Sura 24: Al-Nur: 57
[9] Sura 9: Al-Taubah: 60
[10] Sura 2: Al-Baqarah: 276–281
[11] Sura 9: Al-Taubah: 34–35
[12] Sura 11: Hud: 88
[13] Sura 17: Bani Isra'il: 30
[14] Sura 17: Bani Isra'il: 27–28
[15] Sura 7: Al-A'raf: 32
[16] Sura 2: Al-Baqarah: 283–284
[17] Sura 4: Al-Nisa': 8–13
[18] Sura 2: Al-Baqarah: 189
[19] Sura 2: Al-Baqarah: 283–284
[20] Sura 83: Al-Tatfif: 2–4
[21] Muslim
[22] Hadith
[23] Bukhari na Muslim
[24] Bukhari na Muslim
[25] Sura 2: Al-Baqarah: 283–284; Muslim
[26] Sura 2: Al-Baqarah: 4
[27] Sura 70: Al-Ma'arij: 25–26
[28] Sura 20: Ta-Ha: 119–120
[29] Sura 90: Al-Balad: 14–17

Hakika Allah Anawaamuruni kuzirudisha amana kwa wanaozistahili, na ya kwamba mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu; bila shaka mawaidha Anayowatoleeni Allah ni mazuri sana; Hakika Allah ndiye Asikiaye, Aonaye.

- Kurani Tukufu, 4:59

# SURA YA TANO

# AMANI YA KISIASA

## Amani ya Kisiasa Inabidi Ichunguzwe Katika Kiwango cha Taifa na Kimataifa

Katika mnasaba wa siasa za nchi, suala la kupewa kipaumbele ni kuwa mfumo upi ni mzuri au mbaya kwa binadamu? Pia inatakiwa tumaizi iwapo kushindwa kwa mfumo wa kisiasa unaoambatana na udhaifu wa asili ndivyo vinavyosababisha mateso na malalamiko ya wananchi au kuna sababu nyingine minghairi ya hizo? Je nani wa kulaumiwa, mfumo wenyewe au wanaouongoza na kuusimamia mfumo huo? Je inawezekana kweli kwa viongozi wa kisiasa waliogubikwa na ubinafsi, ulafi, ulaji rushwa, ingawaje wamechaguliwa kwa njia ya kidemokrasia wakaweza kuwaletea yaliyo mazuri na yenye faida kinyume na madikteta wema mathalan!

Ili kuanzisha na kuhakikisha kuwepo na amani duniani, Islam ina ushauri ufuatao kwa wanasiasa.

Islam inaweka mkazo mkubwa wa usafi wa moyo katika nyanja zote za maisha ya binadamu – na huwezi kuweka siasa kando katika mtiririko huo.

## Hakuna kukataa moja kwa moja kwa mfumo wowote wa kisiasa

Tunaanza kwa kauli ya kwamba hakuna mfumo wowote wa siasa ambao umetajwa na Islam kuwa ni bora kuliko mifumo mingine.

Hapana shaka Kurani Tukufu inazungumzia mfumo wa demokrasia, mfumo ambao viongozi wanachaguliwa na watu, lakini sio mfumo pekee unaopendekezwa na Islam. Na wala si jambo la busara kwa dini iliyoletwa dunia nzima ichague mfumo mmoja wa kisiasa, jambo ambalo haliwezekani kwani mfumo huo mmoja hauwezi kutumika katika sehemu zote duniani.

Demokrasia haijakomaa hata katika nchi zilizoendelea kufikia kiwango cha serikali ambacho ndio shabaha ya demokrasia. Licha ya ukuaji wa ubepari na utengenezaji wa vifaa vya kisasa kabisa, uchaguzi hasa wa kidemokrasia hauwezi kufanyika mahali popote pale. Juu ya hilo ongezea rushwa, Mafia na makundi mengine shawishi. Kwa ujumla mtu atakuwa hajakosea akisema Demokrasia haimo katika mikono salama hata katika nchi duniani zinazoonekana ni za kidemokrasia. Kama ni hivyo, demokrasia inawezaje kuwafaa wananchi wa Ulimwengu wa Tatu? Hivyo kusema demokrasia ya Magharibi inaweza kustawi Afrika, Asia au Marekani ya Kusini ni kutoa madai yasiyokuwa na kichwa wala miguu!

Sawa na maoni yangu, mafundisho ya Islam hayakatai mfumo wowote wa kisiasa duniani, isipokuwa Islam inaacha uamuzi kwa wananchi ambao wataongozwa na historia na utamaduni wa nchi husika kuchagua mfumo unaowafaa. Kinachowekekewa mkazo na Islam sio mfumo wa serikali lakini ni kwa jinsi gani serikali inatimiza majukumu na wajibu wake.

Iwapo mfumo wa utawala unaenda sambamba na mtizamo wa Islam ambao ni kuheshimu amana iliyopewa na inaowaongoza. Mifumo tofauti ya serikali kama ubwanyenye, ufalme, demokrasia na kadhalika, mifumo yote hii inaweza kutumika chini ya Islam.

## Ufalme

Ufalme umeelezwa mara kwa mara katika Kurani Tukufu na hausakamwi kama taasisi.

Nabii wa Israeli anawakumbusha Mayahudi juu ya Talut.

وَقَالَ لَهُمْ نَبِيُّهُمْ إِنَّ اللّٰهَ قَدْ بَعَثَ لَكُمْ طَالُوْتَ مَلِكًا ۚ قَالُوْٓا اَنّٰى يَكُوْنُ لَهُ الْمُلْكُ عَلَيْنَا وَ
نَحْنُ اَحَقُّ بِالْمُلْكِ مِنْهُ وَ لَمْ يُؤْتَ سَعَةً مِّنَ الْمَالِ ۚ قَالَ اِنَّ اللّٰهَ اصْطَفٰهُ عَلَيْكُمْ وَ زَادَهٗ
بَسْطَةً فِي الْعِلْمِ وَالْجِسْمِ ۚ وَاللّٰهُ يُؤْتِيْ مُلْكَهٗ مَنْ يَّشَآءُ ۚ وَاللّٰهُ وَاسِعٌ عَلِيْمٌ ﴿٢٤٧﴾

*Na Nabii wao akawaambia: Hakika Allah amewatoleeni Taluti kuwa mfalme. Wakasema: Anawezaje kuwa na ufalme juu yetu na hali sisi tumestahili zaidi kupata ufalme kuliko yeye, naye hakupewa wasaa wa mali? Akasema: Bila shaka Allah Amemchagua juu yenu na*

*Amemzidishia wasaa wa elimu na mwili. Na Allah Humpa ufalme Wake Amtakaye. Na Allah ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua.*[1]

Ufalme unaelezwa kwa mapana zaidi wakiwemo na watu wenyewe ambao wanaitwa wafalme.

وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ يَٰقَوْمِ ٱذْكُرُوا۟ نِعْمَةَ ٱللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ جَعَلَ فِيكُمْ أَنۢبِيَآءَ وَجَعَلَكُم مُّلُوكًا وَءَاتَىٰكُم مَّا لَمْ يُؤْتِ أَحَدًا مِّنَ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٢١﴾

*Na (kumbukeni) Musa alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! Kumbukeni neema za Allah zilizo juu yenu, Alipowafanya Manabii kati yenu na Akawafanyeni wafalme, na Akawapeni ambayo Hakumpa yeyote katika walimwengu.*[2]

Pia dola linaloundwa au kupanuka kwa mashambulizi halina sifa nzuri kama tunavyoona Malkia Sheba akiwaasa washauri wake.

Uamuzi wa Malkia Sheba unasema.

قَالَتْ إِنَّ ٱلْمُلُوكَ إِذَا دَخَلُوا۟ قَرْيَةً أَفْسَدُوهَا وَجَعَلُوٓا۟ أَعِزَّةَ أَهْلِهَآ أَذِلَّةً ۖ وَكَذَٰلِكَ يَفْعَلُونَ ﴿٣٥﴾

*(Malkia) akasema: Hakika wafalme wanapouingia mji, wanauharibu na wanawafanya watukufu wake kuwa dhalili; hivi ndivyo wanavyofanya.*[3]

Wafalme hapana shaka wanaweza kuwa wazuri au wabaya kama vile vile mawaziri wakuu na maraisi waliochaguliwa na watu wanavyoweza kuwa wazuri au wabaya.

Lakini Kurani Tukufu inataja kundi la wafalme waliochaguliwa na Allah. Mfano, Mfalme Suleiman[as] ambaye si tu alikuwa mfalme kama wanavyoelewa Wayahudi na Wakristo, lakini pia Nabii wa Allah sawa na Kurani Tukufu.

Hii inaonyesha kuwa kuna wakati kofia hizi mbili Utume na kuongoza dola zinavaliwa na mtu mmoja na utawala wa aina hii madaraka yake moja kwa moja yamewekwa na Allah.

Aina nyingine ya dola kwa kupitia madaraka ya Nabii inaelezwa katika Kurani Tukufu. Aya ifuatayo inafafanua ukweli huu.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ أَطِيعُوا۟ ٱللَّهَ وَأَطِيعُوا۟ ٱلرَّسُولَ وَأُو۟لِى ٱلْأَمْرِ مِنكُمْ ۖ فَإِن تَنَٰزَعْتُمْ فِى شَىْءٍ
فَرُدُّوهُ إِلَى ٱللَّهِ وَٱلرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٦٠﴾

*Enyi mlioamini! Mtiini Allah na mtiini Mtume Wake na wale wenye mamlaka juu yenu; na kama mkihitilafiana juu ya jambo lo lote, basi lirudisheni kwa Allah na Mtume, ikiwa mnamwamini Allah na siku ya Mwisho. Hiyo ndiyo heri, nayo ina matokeo bora.*[4]

Tumechagua aya hii sio tu kuonesha aina za dola isipokuwa kusisitiza kuwa sawa na Kurani Tukufu sio kila mara machaguo ya kidemokrasia yanakuwa sahihi. Yaelekea kabisa kuwa wengi wa wapiga kura wanashindwa kufahamu sifa anazotakiwa kuwa nazo kiongozi bora na hupinga kuteuliwa kwake kama yeye

analazimishwa juu yao. Kwa kigezo chochote utakachotumia huyu atalaumiwa kama dikteta.

Udhaifu wa kimsingi katika chaguzi za kidemokrasia ni kuwa watu wanachagua kutokana na hali ya juujuu na tathimini ya haraka na wanashindwa kutambua sifa za msingi za kiongozi aliye bora na ambaye hatimaye atawaletea manufaa.

Inaonekana katika historia ya wateule wa Mwenyezi Mungu, zimekuwepo nyakati ambapo uhai wao wa kisiasa ulihitaji msaada maalum wa Mungu. Katika nyakati kama hizo Mungu huchukua mikononi Mwake jukumu la uteuzi wa mfalme, mtawala au kiongozi. Ingawaje haipaswi kudhaniwa kutokana na hili kwamba watawala au viongozi wote wamechaguliwa na Mungu au kuidhinishwa na Yeye. Fikra hii potofu ambayo ilikuwa maarufu katika zama za kati za mfumo wa Ukristo haikubaliwi na Kurani Tukufu. Kwa mfano Mfalme Richard analalama:

> *Not all the water in the rough rude sea*
>
> *Can wash the balm from an anointed King.*[5]
>
> Sio maji yote ya bahari jeuri iliyochafuka yaweza kuosha marhamu ya mfalme mpakwa mafuta.

## Kuainisha Dhana ya Demokrasia

Dhana ya demokrasia licha ya kuwa chimbuko lake ni kutoka Ugiriki, hivi leo imejengwa kwenye tafsiri aliyoitoa Abraham Lincoln (*ambaye amewahi kuwa Rais wa*

*Marekani*) kuwa Demokrasia ni *Serikali ya watu inayotokana na watu kwa ajili ya watu*. Ni maneno matamu lakini hakuna yanapotekelezwa mahali popote duniani!

Sehemu ya tatu ya ainisho la demokrasia – *kwa ajili ya watu* – ina utata na imejaa hatari tupu. Nini kinaweza kuelezwa kwa kujiamini kabisa kuwa hiki ni *kwa ajili ya watu*? Katika mfumo wa utawala wa wengi kile kinachofikiriwa kuwa *kwa ajili ya watu* kwa hakika ni kwa ajili ya wengi na sio kwa wachache waliobaki.

Katika mfumo wa demokrasia inawezekana maamuzi ya msingi na muhimu yanaweza kuamuliwa kufuatana na wingi wa watu. Lakini ukifanya utafiti utakuta hatimaye huo ulikuwa ni uamuzi wa watu wachache ambao umelazimishwa kwa walio wengi kwa njia ya demokrasia! Kuna uwezekano pia chama tawala kikawa kimepata kura nyingi kidogo hapa na pale. Lakini kama wapiga kura ni wachache siku hiyo, inatia wasiwasi kwamba kweli chama tawala kinaungwa mkono na walio wengi. Hata chama kikipigiwa kura nyingi kwa jumla, kuna mengi yanaweza kujitokeza wakati kiko madarakani. Mawazo ya watu yanaweza kubadilika sana na hivyo serikali iliyo madarakani ikawa haiwakilishi maoni ya walio wengi. Ni dhahiri mabadiliko ya mtizamo na mwelekeo vinajitokeza wakati wananchi wanapochagua watu wengine kwa kuiweka serikali nyingine madarakani.

Hata serikali ikiendelea kupendwa na wapiga kura, upo uwezekano kuwa maamuzi ya msingi yanapofanywa wanachama wengi wa chama tawala rohoni hawakubaliani na maamuzi ila wanayaunga mkono kwa kuyapigia kura ili wasitie kitumbua chao mchanga na waendelee kuaminiwa kuwa ni wakereketwa wa chama.

Ni jambo pia la kuweka maanani kwamba lile linaloonekana kuwa la manufaa *kwa watu*, hubadilika mara kwa mara. Kama maamuzi hayatachukuliwa kutokana na uadilifu wa hali ya juu kile kinachofikiriwa kuwa kizuri *kwa watu* au kinachofikiriwa kizuri na chama kuna hatari ya kubadilika kwa sera mara kwa mara. Kinachoonekana kizuri leo kinaweza kuwa kibaya kesho halafu hicho hicho kibaya kikawa kizuri kesho kutwa.

Kwa mtu wa kawaida jambo hili linaweza kuzua mkanganyiko. Majaribio ya ujengaji wa ukomonisti kwa sehemu takriban nusu karne kulijengwa kwenye kauli mbiu *kwa ajili ya watu*. Sio nchi zote za kijamaa zilikuwa za kidikteta.

Ni vizuri kukumbuka kuwa mstari unaotenganisha baina ya dola za kijamaa na zile za kidemokrasia kwa mnasaba wa usemi wa *serikali inayotokana na watu* ni mwembamba na pengine haupo tu. Mtu anayewezaje kuzilaumu serikali zote za kijamaa duniani kwamba hazijapata madaraka kutokana na watu. Bila shaka katika dola la Kiimla inawezekana kuwaambia wapiga

kura kuwachagua wagombea fulani kwa njia ambayo haiachi nafasi ya kumchagua mtu mbadala. Hata hivyo, ukiondoa  nchi chache za Magharibi, hila nyingine ovu na mbaya zinaweza kutumika kwenye mataifa yenye mfumo wa demokrasia.

Kwa hakika, demokrasia katika nchi nyingi duniani haipewi fursa ya kuchanua na ni muhali uchaguzi kuwa *wa watu*. Uchaguzi unaambatana na uibaji wa kura, vitisho kutoka kwa polisi na njia nyingine za rushwa kwa mtiririko huu demokrasia inachuja na mwisho kabisa hakibaki chochote tunachoweza kukiita demokrasia.

## Islam Inavyoainisha Demokrasia

Sawa na Kurani Tukufu watu wako huru kuchagua mfumo wa utawala unaowafaa. Demokrasia, ufalme, Ubwanyenye, mifumo yote hii inafaa ilmuradi imekubaliwa na watu kama sehemu ya urithi wa jamii yao.

Hata hivyo, inaonekana Kurani Tukufu inapendekeza demokrasia. Waislamu wanashauriwa kuwa na mfumo wa demokrasia ingawaje sio moja kwa moja kama ule wa mtindo wa Kimagharibi.

Islam haitoi ainisho lolote kuhusu demokrasia mahala popote katika Kurani Tukufu. Yenyewe inajishughulisha na kanuni za msingi na kuwaachia watu waamue wao wenyewe. Fuata upate mafanikio au acha njia uangamie.

## Nguzo mbili za Demokrasia sawa na Islam

Kuna nguzo mbili tu za demokrasia sawa na msimamo wa Islam. Nguzo hizo ni:

1. Dhana nzima ya uchaguzi wa kidemokrasia lazima usimame kwenye amana na uaminifu. Islam inafundisha kuwa unapotumia haki yako ya kupiga kura ukumbuke na uwe na yakini kwamba Allah Anakuona na utawajibika kwa uamuzi wako. Wapigie kura wale wenye uwezo wa kutimiza wajibu wao kwa taifa ambao wao wenyewe ni watu waaminifu. Katika fundisho hili imewekwa bayana haki ya kupiga kura kwa wale wanaostahili labda viwepo vizuizi vyenye kuzuia haki yao hiyo isitekelezwe.

2. Serikali lazima zifanye kazi wakati zimesimama kwenye msingi wa uadilifu. Nguzo ya pili ya dhana ya demokrasia katika Islam ni kwamba kila unapofanya uamuzi usimamie kwenye kanuni ya uadilifu. Jambo hilo liwe la kisiasa, kidini, kijamii, kiuchumi, uadilifu katu usiwekwe kando. Hivyo ukereketwa au ufurukutwa wa aina yoyote usiruhusiwe kuathiri mchakato wa uamuzi. Hatimaye uamuzi utakaochukuliwa kwa kuzingatia kanuni hii utakuwa kweli *wa watu, kutokana na watu na kwa ajili ya watu.*

## Kushauriana Kunapewa Kipaumbele

Kiini cha demokrasia kimejadiliwa kinagaubaga katika Kurani Tukufu na kuhusu ushauri kwa Waislam, ingawaje ufalme haujakataliwa kwamba si wa kidini

inavyoonyesha demokrasia imepewa kipaumbele kuliko mfumo wowote mwingine.

Ikieleza mfumo bora kwa ajili ya jamii ya Kiislam, Kurani Tukufu inasema:

فَمَآ اُوْتِيْتُمْ مِّنْ شَيْءٍ فَمَتَاعُ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ۚ وَمَا عِنْدَ اللّٰهِ خَيْرٌ وَّاَبْقٰى لِلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَلٰى رَبِّهِمْ
يَتَوَكَّلُوْنَ ﴿٣٦﴾ وَالَّذِيْنَ يَجْتَنِبُوْنَ كَبٰٓئِرَ الْاِثْمِ وَالْفَوَاحِشَ وَاِذَا مَا غَضِبُوْا هُمْ يَغْفِرُوْنَ ﴿٣٧﴾ وَالَّذِيْنَ
اسْتَجَابُوْا لِرَبِّهِمْ وَاَقَامُوا الصَّلٰوةَ ۠ وَاَمْرُهُمْ شُوْرٰى بَيْنَهُمْ ۠ وَمِمَّا رَزَقْنٰهُمْ يُنْفِقُوْنَ ﴿٣٨﴾ وَالَّذِيْنَ
اِذَآ اَصَابَهُمُ الْبَغْيُ هُمْ يَنْتَصِرُوْنَ ﴿٣٩﴾

*Basi chochote mnachopewa ni posho ya maisha ya dunia; lakini kilichoko kwa Allah ni bora na hudumu zaidi kwa wale walioamini na kumtegemea Mola wao. Na wale wajiepushao na madhambi makubwa na mambo ya aibu na wanapokasirika wao husamehe. Na wale waliomwitikia Mola wao na kusimamisha Sala, na utendaji wao hufanyika kwa kushauriana wao kwa wao, na hutoa katika yale Tuliyowaruzuku. Na wale ambao wanapodhulumiwa wao hulipa kisasi.*[6]

Maneno ya Kiarabu *amruhum shura bainahum* (ambao mambo yao hufanywa kwa kushauriana) inahusu maisha ya kisiasa ya jamii ya Kiislam, ikionyesha bayana kwamba katika mambo ya serikali, uamuzi unafikiwa baada ya kushauriana, ambayo inatukumbusha sehemu moja ya maana ya demokrasia – *serikali ya watu*. Matakwa ya watu ndiyo yanayotawala kwa kupitia njia ya kushauriana.

Sehemu ya pili ya ainisho la demokrasia linahusu '*kwa ajili ya watu*.' Hii hasa inahusu aya ifuatayo:

إِنَّ ٱللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَن تُؤَدُّوا۟ ٱلْأَمَٰنَٰتِ إِلَىٰٓ أَهْلِهَا

> *Hakika Allah Anawaamuruni kuzirudisha amana kwa wanaozistahili.*[7]

Hii ina maana kila utumiapo uhuru wako wa kuchagua viongozi, dawamu iweke amana yako pale inapostahili.

Haki ya watu kuchagua viongozi wao imeelezwa lakini sio kusudio hasa. Mkazo hasa ni jinsi gani mtu atumie haki yake. Waislam wanakumbushwa kuwa hii si suala la binafsi na ukafanya unavyotaka, la hasha! Hili ni suala la amana ya taifa. Katika masuala ya amana hubakiwi na uchaguzi mwingi. Ni lazima uitumie amana hiyo kwa uaminifu, usafi wa nafsi na bila ubinafsi. Amana lazima itue pale inapostahili.

Wasomi wengi wa Kiislam hunukuu aya hii kuonyesha kuwa Islam inaeleza nadharia ya demokrasia kama inavyoelezwa na wanafalsafa wa siasa wa Magharibi, lakini hii ni sehemu tu ya ukweli.

Nidhamu ya mshawara inayotajwa katika Kurani Tukufu haina nafasi katu kwa ajili ya siasa za vyama vya siasa vya kidemokrasia ya Magharibi na wala hairuhusu mfumo, mwenendo na utaratibu wa mijadala ya kisiasa katika mabunge na kumbi za wawakilishi wa watu waliochaguliwa kidemokrasia na watu. Kwa sababu

tumejadili kwa kina kipengele hiki, hakuna haja ya maelezo zaidi.

Ni lazima ikumbukwe kuhusu sehemu ya pili ya uainishi wa demokrasia kwamba kuhusu dhana ya kushauriana, haki ya kupiga kura ni mali ya mpiga kura na kamwe hapatakiwi kuwekwa vipingamizi au vikwazo.

Sawa na kanuni za demokrasia, mpiga kura anaweza kumpigia kura kibaraka, kuiharibu au kuitupa katika kapu la taka badala ya kuweka kura yake kwenye sanduku la kupigia kura. Hatakemewa kwa hilo na wala hatashitakiwa kwa kuvunja kanuni yoyote ya demokrasia.

Sawa na ainisho la Kurani Tukufu, mpiga kura si mmiliki wa kura yake, isipokuwa hiyo ni amana. Kama amana ni lazima aitendee haki amana hiyo na aiweke mahala panapostahili. Lazima awe macho akielewa kuwa atakuwa mwenye kuulizwa mbele ya Allah.

Sawa na mtizamo huu wa Islam, kama chama kinamteua mtu ambaye mwananchi ana imani huyu hawezi kubeba amana ya taifa, mwanachama huyo anatakiwa aachane na chama hicho kuliko kumpigia kura yule ambaye hastahili kubeba amana hiyo. Ukereketwa kwa chama usiingie katika kuchagua kwake.

Amana lazima itumike kwa nia njema. Hivyo kila mpiga kura ashiriki katika kupiga kura wakati wa uchaguzi,

labda kwa sababu moja au nyingine hawezi, kinyume cha hivyo atakuwa ameshindwa kuitumia vyema amana aliyopewa. Dhana ya kususia kupiga kura kama inavyofanyika Marekani ambako nusu ya wapiga kura wala hawajali kwenda kupiga kura haina nafasi asilani katika dhana ya demokrasia katika Islam.

## Mkanganyiko kuhusu Mfumo halisi wa Serikali ya Kiislam

Ni jambo linalopigiwa chapuo na wanazuoni wa siasa za Kiislam wa zama hizi kuwa Islam hasa ndiyo demokrasia. Sawa na falsafa yao ya kisiasa, kwa sababu Allah ndiye Ana uwezo wote, hivyo mamlaka yote yako Kwake.

## Mamlaka ya Kimbingu

Mamlaka yote na yaliyokamilika ni ya Allah. Kurani Tukufu inayaeleza mamlaka hayo katika aya ifuatayo:

فَتَعٰلَى اللّٰهُ الْمَلِكُ الْحَقُّ ۚ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۚ رَبُّ الْعَرْشِ الْكَرِيْمِ ﴿١١٥﴾

*Basi Ametukuka Allah, Mfalme wa haki; hakuna aabudiwaye ila Yeye, Mola wa Arshi yenye heshima.*[8]

Kanuni ya msingi ni kuwa haki zote za kutawala zinamstahiki Allah, kanuni hii imeelezwa katika sehemu nyingi za Kurani Tukufu. Aya hiyo hapo juu ni mmoja wa mifano hiyo.

Katika kuendesha mambo ya kisiasa, utawala wa Allah umeelezwa kupitia njia mbili:

1. Sheria kama inavyochukuliwa kutoka katika Kurani Tukufu, mwenendo wa Mtume Mtukufu[saw] wa Islam na pia kutoka katika Hadithi sahihi zinazonasibishwa naye na Waislamu wa mwanzo ndio zinazoongoza. Zinabeba miongozo muhimu kwa utungaji sheria na hakuna serikali iliyochaguliwa kidemokrasia inayoweza kuingilia matakwa ya Mungu.
2. Hakuna mchakato wa utungaji sheria utakaokuwa halali uwapo kinyume na kanuni iliyosemwa hapo juu.

Kwa masikitiko makubwa, wasomi wa madhehebu mbalimbali hawakubaliani kuhusu sheria. Kwenye hili wasomi wote wanakubaliana utungaji wa sharia ni haki ya Allah na Amekwishaeleza matakwa yake katika Kurani Tukufu iliyoteremshwa kwa mwanzilishi wa Islam.

Kuhusu vipi serikali za Kiislam ziendeshwe, wazo linaloshabikiwa na wengi ni kuwa, mambo ya utawala ya kila siku yanayofanywa na wawakilishi wa watu, hayo kwa hakika ni matakwa ya Allah. Mamlaka ni ya watu waliokabidhiwa uwezo, hivyo mfumo huo ni wa kidemokrasi.

## Umullah

Huu ni msimamo mgando wa hao wanaojiita wahafidhina ambao wao watakubaliana tu na fikra za

Waislam kuhusu mwenendo wa demokrasia kwa sharti ya kwamba wao Mamullah[4] wawe na kauli ya mwisho kuhusu uhalali wa demokrasia sawa na sharia.

Rai hii ikikubaliwa itakuwa imewekwa rehani nguvu na uwezo ule wa Allah na sasa uwezo huo utakuwa mikononi mwa hawa wahafidhina au Masheikh wa dhehebu jingine. Ukifikiria uwezo wa kuogofya waliopewa na ukakumbana na tofauti kubwa iliyopo baina ya masheikh wa madhehebu mbalimbali, hapo ndipo utaelewa hatari kubwa iliyopo. Kuna madhehebu mengi tofauti ya fik'hi nyingi miongoni mwa masheikh. Hata katika dhehebu moja hakuna kukubaliana katika baadhi ya mambo. Tena msimamo wao kuhusiana na vipi hasa matakwa ya Allah yanavyoelezwa katika sheria ya Kiislamu umekuwa ukibadilika katika vipindi tofauti vya historia.

Jambo hili linaleta tatizo kubwa katika ulimwengu wa Kiislam ambao bado unatafuta namna ya kujitambua. Hii inaendelea kuwa wazi zaidi hatua kwa hatua kwa wasomi wa Kiislam kuwa kinachowaunganisha Mamullah ni msimamo mgumu wa pamoja wa kuwa na sheria ya Kiislam.

Mapinduzi ya Iran yameongeza uchu wa Mamullah ambako Suni ndio wengi. Kwa mantiki yao kama Khomein ameweza kwa nini wao washindwe? Fikra zao na njozi ni kufikia kupita alikofikia Khomeini.

---

[4] Tafsiri inayokaribiana: 'Viongozi' wa Kiislam.

Umma umechanganyikiwa. Je utapendelea Neno la Allah na Mtume[saw] Wake au muwe na watu wasiomuamini Allah na wasio na hofu wawaongozeni na kuwatengenezea kanuni? Suala hili ni gumu kwa mtu wa kawaida ambaye anajikuta katika mahangaiko na mshangao. Wengi katika nchi za Kiislam wanaipenda sana Islam na wako tayari kufa kwa ajili ya Allah na heshima ya Mtukufu Mtume[saw] wa Islam, hata hivyo katika tukio lote hili kuna kitu kinachowaacha wamechanganyikiwa, wamehamanika na kujisikia vibaya. Licha ya mapenzi yao kwa Allah na Mtukufu Mtume[saw] wanazo kumbukumbu za serikali zilizomwaga damu ambazo zilikuwa athari za Mamullah au walitumia Umullah wao kwa ajili ya faida za kisiasa.

Kuhusiana na wanasiasa Waislam, wao wamegawanyika na wasiokuwa na uamuzi. Baadhi hawawezi kuzuia kishawishi cha kuungana na Mamullah na kuwasaidia. Wanaendelea kuwa na matumaini kuwa wakati wa uchaguzi ni wao wataochaguliwa na sio Mamullah kutetea Sharia. Umma ungependa zaidi kuwaamini wanasiasa kama walinzi wa sheria kuliko Mamullah. Maisha yatakuwa rahisi na uhalisia zaidi kuliko chini yao hao walinzi wa mbinguni. Wanasiasa wengi wenye kuona mbali wanaona huu ni mchezo mbaya. Ni masikitiko, hawa wanaendelea kupungua haraka. Siasa na unafiki, ukweli na haya, kwa ufupi kila hulka njema ni mithili ya paka na panya au mbingu na ardhi havikutani. Kwa jumla wasomi wanaelekea zaidi

kwenye demokrasia. Wanaipenda Islam lakini wanahofia utawala wa kidini. Hawaoni demokrasia kuwa ni mbadala wa Islam, lakini wanaamini kwa dhati kama falsafa ya kisiasa ni Kurani Tukufu yenye mwelekeo zaidi kwenye demokrasia.

وَالَّذِيْنَ اسْتَجَابُوْا لِرَبِّهِمْ وَاَقَامُوا الصَّلٰوةَ ۖ وَاَمْرُهُمْ شُوْرٰى بَيْنَهُمْ ۖ وَمِمَّا رَزَقْنٰهُمْ يُنْفِقُوْنَ ﴿٣٩﴾

*Na wale waliomwitikia Mola wao na kusimamisha Sala, na utendaji wao hufanyika kwa kushauriana wao kwa wao, na hutoa katika yale Tuliyowaruzuku.*[9]

وَشَاوِرْهُمْ فِى الْاَمْرِ ۚ فَاِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللّٰهِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ الْمُتَوَكِّلِيْنَ ﴿١٦٠﴾

*Na ushauriane nao katika mambo ya kiutawala; na ufungapo nia, basi umtegemee Allah; hakika Allah Anawapenda wamtegemeao.*[10]

Kutokana na hali hii ya vuta nikuvute miongoni mwa makundi, nchi changa za Kiislam kama Pakistan zinajikuta katika hali ya mkanganyiko na kuchanganyikiwa. Wapiga kura kitabia huchukia Mamullah kurejea katika Bunge kwa idadi kubwa kiasi. Hata wakati wa kilele cha kupendwa kwa Mamullah ni asilimia tano hadi kumi ya Mamullah wanaoshinda katika uchaguzi. Wanasiasa licha ya kuahidi kutekeleza Shariah na hivyo kuungwa mkono na Umullah bado wanasiasa wanajikuta katika hali tete. Ndani katika nafsi zao wanaamini kuwa kukubali Shariah ni kinyume na kanuni za uchaguzi wa kidemokrasia.

Kama uwezo wa kutunga sheria umo mikononi mwa Allah, jambo ambalo Mwislamu hawezi kukataa, hivyo basi kimantiki ni Mamullah na watakatifu ambao wana haki ya kuelewa na kutafsiri  Sharia. Katika muktadha huu zoezi la kuchagua watunga sheria ni kazi bure sawa na kutwanga maji kwenye kinu. Hata hivyo wabunge hawatakiwi kuweka saini tu mahali walipoambiwa na Mamullah waweke saini.

Ni jambo la kusikitisha ya kuwa si wasomi wala wanasiasa waliojitahidi kuelewa ni mfumo au mifumo gani ya serikali ambayo Kurani Tukufu imeielezea na kuitambua.

### Utii Uliogawanyika Baina ya Dola na Dini

Hamna kuhitilafiana baina ya Neno la Mungu na kudura ya Mungu. Hakuna msuguano baina ya dola na dini katika Islam. Lakini suala hili halihusu Islam peke yake.

Kuna matukio mengi katika historia ya binadamu ambapo madola mengi yalipambana na suala hili.

Dola la Kirumi, hasa katika karne tatu za mwanzo za Ukristo, liliulaumu Ukristo kwa mgawanyiko wa uaminifu kati ya dola na Ukristo. Madai haya ya dola yalisababisha ukatili wa kinyama kwa Wakristo wa mwanzoni kwa tuhuma za uhaini na kutomheshimu Mfalme.

Mvutano huu baina ya Kanisa na dola umechangia katika kutengeneza na kuipa mwelekeo historia ya

Ulaya. Napoleon Bonaparte, mathalan, alilituhumu Kanisa Katoliki kwa kuwagawa na akasema utii wa kwanza utakuwa kwa watu wa Ufaransa na kwa serikali ya Ufaransa na hakuna Papa wa Vatikani atakayeruhusiwa kuendesha mambo ya Kanisa Katoliki ndani ya Ufaransa na wala Kanisa Katoliki halitaruhusiwa kuingilia katika mambo yake ya nchi.

Katika historia ya hivi karibuni, Jamaat yangu ya Waislam Waahmadiyya katika Pakistan walikumbana na matatizo makubwa kama haya. Athari za Mamullah zilipozidi kuongezeka chini ya hifadhi na ulinzi wa Jenerali Zia-ul-Haq, Dikteta wa kijeshi aliyetawala kwa miaka mingi nchini Pakistan, Waahmadiyya wakawa wahanga wa tuhuma hii kongwe ya utii uliogawanyika. Serikali ya Pakistan chini ya Jenerali Zia-ul-Haq iliwahi hata kudiriki kutoa waraka unaotuhumu Waahmadiyya kwamba hawana utii kwa Islam wala kwa taifa la Pakistan.

Ulikuwa ni ukichaa ule ule wa zamani sasa ukiwashambulia watu wengine. Mvinyo uliendelea kuwa ule ule ingawaje mitungi imebadilika.

Na hivi karibuni sakata la Salman Rushdie, Waislam wengi wa Uingereza na sehemu nyingine za Ulaya walipambana na tatizo kama hilo kwani walituhumiwa kuwa na utii uliogawanyika. Ingawaje sakata hilo halikufikia mahali pabaya mno athari yake kuhusu

mahusiano miongoni mwa wanajamii haiwezi kupuuzwa.

## Je, Dini ndio iwe na Haki Pekee ya Utengenezaji wa Sheria?

Hili ni tatizo linaloikumba dunia ambalo halijafanyiwa utafiti wa kina. Si wanasiasa wala viongozi wa dunia ambao wamefaulu kuchora mstari unaotenganisha dini na dola.

Kuhusu Wakristo inaonesha suala hilo lilikwishapatiwa suluhu wakati Nabii Isa[as] alipotoa jibu la kihistoria kuwajibu Mafarisayo:

> *"Mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari na mpeni Mungu yaliyo ya Mungu".*[11]

Maneno haya machache yamejaa lindi refu la hekima na busara.

Dini na dola ni magurudumu mawili kati ya magurudumu mengi ya gari lililobeba jamii. Kwa hakika hakuna mushkili wowote iwapo kuna magurudumu mawili au manne au manane ili muradi kila gurudumu liko sehemu kusaidia gari liende mbele. Hakuna suala la mgongano au mapambano.

Kuhusu somo hili Kurani Tukufu inafafanua mipaka iliyowekwa katika nyanja zote za maisha. Itakuwa ni kurahisisha mno jambo hili hadi kupoteza maana iwapo itajitokeza fikra kuwa hakuna dini na dola vinapokutana na kusaidiana. Kwa hakika vinalingana lakini katika

vuguvugu la kushirikiana. Hakuna makusudi ya moja kuhodhi madaraka.

Mathalani, sehemu kubwa ya elimu ya hulka njema katika kila dini huwa ni sehemu ya lazima ya sheria za mataifa duniani kote. Katika hili baadhi yao huchukuwa kidogo elimu hiyo ya hulka lakini nchi nyingine huchukua sehemu kubwa. Adhabu inaweza kuwa laini au kali lakini kwa ujumla dini inalaani uhalifu ambao adhabu yake inatolewa na hufuatilika pasipo marejeo kwenye dini. Ingawaje wanaweza kutokubaliana na sheria nyingi za kiserikali, watu wa dini mbalimbali hawapendi kuzozana na serikali juu ya mambo hayo.

Haya yote hayawahusu Waislam na Wakristo tu bali na watu wa dini nyingine duniani kote. Ni dhahiri sheria za dini ya Kihindu za *Manusmarti* ni kinyume kabisa na sheria na sera za serikali ya kisekula (isiyokuwa na dini rasmi ya taifa). Hata hivyo inaonyesha watu wanaendelea kuishi kwa kukubaliana na kuvumiliana. Kama sheria za kidini zingetumika dhidi ya mifumo ya kisiasa inayopatikana katika nchi nyingi duniani ingepelekea umwagaji mwingi wa damu. Ni bahati kwa binadamu kwamba mambo hayako hivyo.

Kuhusiana na Islam hili katu haliwezi kuwa tatizo kwani kanuni na sheria isiyoyumba ya Islam ni kanuni ya uadilifu.

Kanuni hii inabakia kuwa jiwe kuu la pembeni katika mifumo yote ya serikali inayojinasibisha na Islam.

Ni masikitilo kuwa wasomi wa siasa wa Kiislam wana uelewa mdogo kuhusu mbinu za kuendesha serikali. Wanashindwa kutofautisha matumizi ya sheria zinazohusu uhalifu ambazo zinapatikana mahali pote duniani bila harufu yoyote ya dini, na uhalifu ambao ni mahsusi kwa dini. Hivyo ni waumini wa dini husika ambao wanastahili kushitakiwa.

Makundi haya mawili hayakutofautishwa bayana sana. Kuna mahali uhalifu wa kawaida unaweza kugusa dini na hulka na inawezekana uhalifu huo ukagusa desturi za kawaida katika maisha ya binadamu. Kwa mfano, kuiba ni jambo linalolaaniwa na kuna adhabu zinazotolewa kwa kutofautiana. Pia kuna suala la mauaji, ulevi, uvunjaji wa amani, makosa ambayo yanakatazwa na dini nyingi. Baadhi ya dini zina adhabu maalum kwa ajili ya makosa haya.

Tena swali linazuka kwamba serikali ishughulikie vipi makosa kama hayo? Swali hili linaibua zaidi swali jingine la kama Islam kwa vyovyote inatoa jibu la mkato na njia iliyoainishwa vyema kwa serikali ya Kiislam au isiyo ya Kiislam kuifuata. Ikiwa serikali ya Kiislam imetambuliwa rasmi katika Islam, basi maswali mengine muhimu sana yatazushwa kwa mfano uhalali wa serikali yoyote kujiweka chini ya ufuasi wa dini fulani maalum na kuyalazimisha mafundisho ya dini hiyo kwa wananchi wake wote bila kujali kama ni wafuasi wa dini hiyo au la.

Dini zina wajibu wa kuwakumbusha watengeneza sheria kuhusu masuala ya khulka njema. Si lazima utengenezaji wote wa sheria uwe chini ya dini.

Kuwepo kwa madhehebu mengi na tofauti baina ya dhehebu moja na jingine, dini moja na nyingine bila mgongano unaweza kuleta mtafaruku mkubwa katika jamii. Chukua kwa mfano adhabu kuhusu unywaji wa pombe. Ingawaje pombe imekatazwa katika Kurani Tukufu, hakuna adhabu maalum iliyoelezwa kwa ajili ya kosa hilo. Tegemeo pekee ni juu ya baadhi ya Hadithi ambazo hata hivyo zinapingwa na baadhi ya fik'hi. Mahali fulani au nchi fulani adhabu inaweza kuwa hivi na mahali pengine ikawa vile. Kutofahamu sheria kutaenea sana. Mambo ambayo ni sawa kwa Islam ni sawa pia kwa imani nyingine. Sheria kutoka kwenye Talmud zitakuwa hazitekelezeki. Na hivyo inaweza kusemwa kuhusu Ukristo.

Muumini wa dini yoyote anaweza kutekeleza maagizo ya dini yake chini ya sheria za kiserikali. Anaweza kuzungumza bila ya sheria za serikali kumkataza kuzungumza ukweli. Anaweza kusali na kutimiza yote ya kuabudu bila ya kuhitaji kupitishwa kwa sheria maalum na serikali.

Suala hili pia linaweza kutizamwa kutoka upande mwingine wa kuvutia. Kama Islam inakubaliana na rai kuwa pawepo na serikali ya Kiislam nchi ambayo ina Waislam wengi, basi kwa kufuata kanuni ya uadilifu,

Islam lazima ikubali haki ya serikali nyingine kuzitawala kufuatana na wingi wa wafuasi wa dini husika. Hivyo Pakistan lazima ikiri kuwa jirani yake India itatawaliwa na sheria za Kihindu kwani ndio walio wengi nchini India. Hilo jambo likitokea utakuwa msiba mkubwa kwa Waislam wanaoishi India ambao watapoteza haki zao za msingi. Na kama India itatawaliwa na sheria za *Manusmarti* kwa nini nchi ya Israeli inyimwe haki ya kuwatawala Mayahudi na wasio Mayahudi kwa sheria ya Talmudi? Na hili likitokea, maisha hayatakuwa zahama kwa watu wa Israeli tu bali hata kwa Wayahudi wenyewe.

Lakini, dhana hii ya kuwa na madola ya kidini katika nchi kadhaa zinaweza kuwa na nafasi katika Islam, ikiwa Islam itaeleza kuwa katika nchi zenye Waislam wengi, sheria za Kiislam zitumike kwa nguvu za kanuni. Jambo hili litaleta mkanganyiko wa aina yake, kwani kwa upande mmoja wa jina la uadilifu nchi zote zitapewa haki ya kulazimisha sheria ya dini iliyo na wafuasi wengi. Kwa upande mwingine, kila tendo la wana dini walio wengi katika sehemu mbalimbali duniani litalazimishwa kuwa chini ya sheria ya dini ambayo wao hawaiamini. Na hii itakuwa kinyume na dhana nzima ya uadilifu.

Tatizo hili la kutatanisha halijashughulikiwa wala kutatuliwa na wale waumini wa sharia katika nchi hizo zinazojiita za Kiislam. Sawa na uelewa wangu kuhusu

mafundisho ya Islam, mataifa yote ni lazima yaongozwe kwa kutumia kanuni ya uadilifu na kwa kufanya hivyo kila serekali inakuwa serekali ya Kiislam kinadharia.

Sawa na hoja zilizojengwa na tukiwekea maanani dhana kuwa hakuna kulazimishana katika masuala ya imani, dini haitakiwi kuwa na mamlaka ya utengenezaji sheria kuhusu mambo ya kisiasa ya nchi.

## Ujuzi wa Kuongoza Serikali Katika Islam

Utafiti wangu umenidhihirishia pasipo shaka yoyote kuwa Kurani Tukufu inazungumzia juu ya mada ya serikali bila kutofautisha abadan kati ya serikali ya Kiislam na ile isiyokuwa ya Kiislam.

Maelekezo juu ya kuendesha serikali ni yale yale kwa binadamu wote inagawaje wanaambiwa katika Kurani Tukufu ni waaminio. Kurani Tukufu inaeleza juu ya ujuzi wa kuongoza serikali ambao unaweza kutumika kwa Wahindu, Masingasinga, Mabudha, Wakonfyushasi, Wakristo, Mayahudi na Waislamu na kadhalika.

Kiini cha maelekezo hayo kinapatikana katika aya tuliyoinukuu hapo mbeleni na aya nyingine zenye mnasaba huu ambazo tunazinukuu hapa chini.

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتّٰى يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِيٓ اَنْفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا
قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ٦٦

*Siyo, kwa haki ya Mola wako, wao, hawawi wenye kuamini mpaka wakufanye hakimu katika yale waliyohitilafiana kati yao, kisha wasione chuki mioyoni mwao juu ya hukumu uliyotoa, na wanyenyekee kabisa.*[12]

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا كُوْنُوْا قَوّٰمِيْنَ بِالْقِسْطِ شُهَدَآءَ لِلّٰهِ وَ لَوْ عَلٰۤى اَنْفُسِكُمْ اَوِ الْوَالِدَيْنِ وَ
الْاَقْرَبِيْنَ ۚ اِنْ يَّكُنْ غَنِيًّا اَوْ فَقِيْرًا فَاللّٰهُ اَوْلٰى بِهِمَا ۫ فَلَا تَتَّبِعُوا الْهَوٰۤى اَنْ تَعْدِلُوْا ۚ وَ
اِنْ تَلْوٗۤا اَوْ تُعْرِضُوْا فَاِنَّ اللّٰهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرًا ﴿١٣٦﴾

*Enyi mlioamini! Kuweni wakali katika kusimamia uadilifu, mkiwa mashahidi kwa ajili ya Allah, hata kama jambo husika liwe dhidi ya nafsi zenu, au (juu ya) wazazi (wenu) na jamaa wa karibu. Kama akiwa tajiri au maskini Allah Yu karibu nao zaidi wote wawili. Basi msifuate matamanio ili kutofanya uadilifu. Na kama mkipotosha (ukweli) au mkijitenga, basi hakika Allah Anazo habari za mnayoyatenda.*[13]

Hadithi za Mtukufu Mtume Muhammad[saw] ziko bayana kuhusu mada hii. Kila kiongozi aliye madarakani anapimwa ni kwa jinsi gani anavyowatendea walio chini yake na hawa wote wanawajibika moja kwa moja kwa Allah. Lakini kwa sababu mazungumzo haya tayari tumekwisha yazungumza kwa kina, hakuna haja ya kuyarudia.

Kiini cha utafiti huu ni kwamba Islam inazungumzia na kuhimiza serikali isiyoegemea upande wowote, uendeshaji wa serikali ni kwa wote na tofauti za kidini hazipewi nafasi katika uendeshaji wa serikali.

Islam inawaeleza Waislam wafuate utawala wa sheria katika mambo yote ya kidunia.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَ وَأُوْلِي ٱلۡأَمۡرِ مِنكُمۡۖ فَإِن تَنَٰزَعۡتُمۡ فِي شَيۡءٖ فَرُدُّوهُ إِلَى ٱللَّهِ وَٱلرَّسُولِ إِن كُنتُمۡ تُؤۡمِنُونَ بِٱللَّهِ وَٱلۡيَوۡمِ ٱلۡأٓخِرِۚ ذَٰلِكَ خَيۡرٞ وَأَحۡسَنُ تَأۡوِيلًا ٥٩

*Enyi mlioamini! Mtiini Allah na Mtiini Mtume Wake na wale wenye mamlaka juu yenu; na kama mkigombana juu ya jambo lo lote, basi lirudisheni kwa Allah na Mtume, ikiwa mnamwamini Allah na siku ya Mwisho. Hiyo ndiyo heri, nayo ina matokeo bora.*[14]

Lakini kuhusu mahusiano baina ya mwanadamu na Allah uwanja huu ni wa dini pekee na serikali haina haki ya kuingilia uhuru kamili wa fikra na mawazo katika masuala ya imani. Ni haki ya msingi ya binadamu sio tu kuamini chochote akipendacho sana, bali pia kumuabudu Allah au masanamu sawa na mafundisho ya dini yake au mafundisho ya kipagani.

Sawa na Islam, dini haina haki kuingilia mambo yahusikanayo na  serikali pekee, wala serikali haina haki ya kuingilia yale yaliyo sawa kwa dini na serekali. Haki na wajibu vimewekwa bayana mno katika Islam kiasi hiki ya kwamba uwezekano wa kugongana haupo. Aya nyingi zimekwishanukuliwa katika sehemu hii zinazozungumzia amani inayotokana na dini.

Kwa bahati mbaya, kuwa kuna mwelekeo wa serikali za kisekula kurefusha mkono zaidi ya mipaka

inayokubaliwa. Hali kadhalika hali ni hiyo hiyo katika serikali zinazoendeshwa na viongozi wa dini.

Ingawa mtu aweza asikubaliane nao, ila anaweza kuelewa kwa kiasi fulani dhana zinazoegemea upande mmoja za serikali zinazoendeshwa na walioshikilia dini bila akili. Lakini mtu anapoona mtazamo usio wa ukomavu kama huo katika nchi ziitwazo zilizoendelea na katika watu wenye fikra pana wa nchi za kisekula, ni vigumu kuamini. Hili sio jambo la pekee ambalo ni gumu kueleweka katika tabia ya kisiasa ya mwanadamu.

Kwa kadiri siasa zinavyobaki zimeshikamana madhubuti na maslahi ya kitaifa na kuchangia katika falsafa ya taifa, hakuwezi asilani kuwapo kwa kitu kama maadili mema kamili. Kwa kadiri mirengo ya kisiasa inavyotawaliwa na upendeleo wa kitaifa na ukweli, uaminifu, haki na usawa vinaachwa kila inapoonekana vinakinzana na maslahi yajulikanayo ya kitaifa, na Kwa kadiri kufanya hivyo kunavyobakia kukifahamiwa kuwa ndio maana ya mtu kuipenda nchi yake, tabia ya kisiasa ya mwanadamu itabakia kuwa isiyoeleweka, yenye utata na kigeugeu daima.

Kurani Tukufu imeeleza wajibu wa serikali na ule wa wananchi. Baadhi ya wajibu huo umefafanuliwa mwanzoni mwa mhadhara huu, ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa chakula, mavazi, na mahitaji ya msingi ya kibinadamu, kanuni za misaada ya kimataifa, kuwajibika

kwa serikali na wananchi, uadilifu, kuwa na hisia kuhusu matatizo ya wananchi ili wasilazimike kutoa sauti zao ili kudai haki zao.

Katika mfumo halisi wa serikali ya Kiislam ni wajibu wa serikali kuwa macho ili wananchi wasilazimike kugoma, kuwepo migogoro ya viwandani, maandamano, hujuma au sababu yoyote nyingine ya kuwafanya walalamike ili wapate haki zao. Hebu sasa tugeukie kwa ufupi wajibu mwingine.

Kurani Tukufu inaeleza:

وَإِمَّا تَخَافَنَّ مِن قَوْمٍ خِيَانَةً فَانبِذْ إِلَيْهِمْ عَلَىٰ سَوَاءٍ ۚ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْخَائِنِينَ ﴿٥٨﴾

*Na kama ukiogopa hiana kwa watu walioahidiana nawe, basi uivunje (ahadi yao) kama walivyofanya; hakika Allah Hawapendi wafanyao hiana.*[15]

Wale wanaopewa uongozi wasiongoze kwa kusababisha fujo, ghasia, maumivu, bali wajitahidi kusimamisha uadilifu katika nyanja zote za jamii.

أَمَّن يُجِيبُ الْمُضْطَرَّ إِذَا دَعَاهُ وَيَكْشِفُ السُّوءَ وَيَجْعَلُكُمْ خُلَفَاءَ الْأَرْضِ ۗ أَإِلَٰهٌ مَّعَ اللَّهِ ۚ قَلِيلًا مَّا تَذَكَّرُونَ ﴿٦٢﴾

*Au ni nani Anayemjibu aliyedhikika amwombapo na kuondoa dhiki, na kuwafanyeni waandamizi duniani? Je, yuko mungu pamoja na Allah? Ni kidogo mnayoyakumbuka.*[16]

## Mahusiano ya Kimataifa – Kanuni ya Uadilifu Inawahusu Wote Kwa Usawa.

Hata wanasiasa na wale waliobobea katika siasa wa hivi leo wote hao wanahitaji mafunzo ya Islam. Ni imani ambayo jiwe kuu lake la pembeni katika shughuli za kimataifa ni uadilifu.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُونُوا۟ قَوَّٰمِينَ لِلَّهِ شُهَدَآءَ بِٱلْقِسْطِ ۖ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَـَٔانُ قَوْمٍ عَلَىٰٓ أَلَّا
تَعْدِلُوا۟ ۚ ٱعْدِلُوا۟ هُوَ أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ ۖ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ خَبِيرٌۢ بِمَا تَعْمَلُونَ ٩

*Enyi mlioamini! kuweni wasimamizi kwa ajili ya Allah, mtoao shahada kwa adili. Na uadui wa watu usiwashawishini ya kwamba msifanye uadilifu. Shikeni adili, hiyo ni karibu sana na utawa, na Mcheni Allah. Hakika Allah Anazo habari za yale mnayoyatenda.*[17]

Siwezi kudai kuwa nimesoma kila kitu kuhusu dini kuu zote za dunia, lakini si kwamba sijui mafunzo yao.Katika utafiti wangu nimeshindwa kupata maagizo kama haya yanayopatikana katika aya hii. Hata neno uhusiano wa kimataifa ni muhali kukutana nalo. Lakini kama funzo la aina hii linapatikana katika dini nyingine, basi ningeomba kuwaambia kuwa Islam inaunga mkono hilo kwani ni katika funzo hilo ndio kuna chimbuko na ufunguo wa amani ya dunia.

Ulimwengu kwa jumla una wasiwasi juu ya mustakabali wa amani ya dunia. Mabadiliko chanya na ya muhimu katika kambi ya kijamaa na uhusiano baina ya mataifa makubwa maendeleo yote hayo yanaleta matumaini

kidogo. Ulimwengu umo katika shamrashamra na shangwe. Mawazo ya ujumla ya viongozi wa kisiasa ni ya matumaini na ya kushangiliwa kutokana na mabadiliko ya kimapinduzi tunayoona kwa hivi sasa.

Nchi za Magharibi bilhususi zinaonekana kujiamini na kuwa na furaha. Ni vigumu kwa Wamarekani kuzuia furaha yao kwani wanaloliona ni ushindi dhidi ya Ukomonisti, ushindi ambao baadhi wanasema ni ushindi wa wema dhidi ya uovu, na wa kweli dhidi ya uongo.

Haitakuwa mahali pake hapa nikieleza kwa undani hali ya kisiasa ya dunia na matokeo yake. Labda nitatumia saa chache kwenye mada hii katika mkutano wa mwaka wa Uingereza mwisho wa Julai mwaka huu (1990).

## Wajibu wa Umoja wa Mataifa

Mijadala mingi inayohusu mustakabali wa amani duniani sawa na matukio yanayojitokeza kwa hivi sasa ni mingi ila mmoja unahitaji tuupe kipaumbele. Mjadala huo unahusu wajibu wa Umoja wa Mataifa na jinsi gani unavyoweza kusimamia na kuiendeleza kuliko hata siku za nyuma?

Wakati tunaelekea ukingoni mwa vita baridi baina ya nguvu mbili kubwa sana, inasemekana kuna uwezekano hitilafu kati ya mitizamo yao tafauti zikapungua: kupungua utumiaji wa kura za turufu katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, na upo pia uwezekano wa kuwa na sauti katika masuala yote yaliyo tete. Hii

bila shaka inatoa taswira mpya kabisa ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Tatizo pekee mpaka sasa ni China na kujifanya kwake hamnazo, lakini kutokana na matatizo yake sugu ya kiuchumi na ya kisiasa ni rahisi kuihakikishia Uchina kuhusu faida za kukubaliana.

Kama fikra hii na njozi hii itatimia au haitotimia hilo sio tatizo. Ni dhahiri kuwa baraza la usalama na Umoja wa Mataifa viliibuka na kuwa vyombo vyenye nguvu na kuathiri matukio ya dunia na kulazimisha nchi ndogo kusalimu amri kwa mataifa makubwa. Taswira ya namna hii haikuwa ya kufikirika kabla ya kuanguka kwa ukuta wa Berlin. Lakini swali liko pale pale na linajitokeza zaidi kwenye nyanja za siasa kuliko hata hapo kabla, je, Umoja wa Mataifa jukumu lake jipya lenye nguvu nyingi mno za kisheria na kiutawala utaweza kuleta amani duniani.

Naomba radhi kama nitaonekana kuwa nisiye na matarajio mema, lakini jibu langu kujitetea kwa swali hili ni HAPANA! Swali la vita na amani duniani halimo mikononi mwa uhusiano baina ya mataifa makubwa. Ni suala zito na gumu ambalo mizizi yake imo katika falsafa za kisiasa na mtizamo wa kihulka miongoni mwa mataifa yote duniani.

Isitoshe tofauti za kiuchumi na ongezeko la tofauti za kiuchumi baina ya matajiri na masikini ni mambo ambayo yatakuwa na uwezo wa kuathiri matukio yajayo

duniani. Athari za hayo zimekwishaelezwa mwanzoni mwa hotuba hii. Hadi hapo itakapofuatwa na kutekelezwa kanuni ya uadilifu katika mahusiano ya kiuchumi, bei nzuri katika soko, kuacha kunyonya masikini, hakuna anayeweza kuahidi amani. Kama uhusiano wa Umoja wa Mataifa na nchi wanachama haukuelezwa kinagaubaga kuliko hali ilivyo sasa, mustakabali wa amani utaendelea kuwa mashakani.

Kuna haja ya kuwa na mikakati ya kuzuia serikali kuwa katili kwa watu wake. Mikakati hiyo iwe mikononi mwa Umoja wa Mataifa ili kupambana na dhuluma popote inapojitokeza. Mpaka hilo litokee, ni vigumu kufikiria usalama wa dunia.

Ni kwa kiasi gani Umoja wa Mataifa unaweza kuingilia katika kinachoitwa masuala ya ndani ya nchi. Ni swali nyeti lakini la muhimu katika kupata amani ya dunia. Lakini kama mwisho wa yote sera za Umoja wa Mataifa hazitawaliwi na uadilifu, na vigezo havilingani unapotoa uamuzi juu ya baadhi ya mataifa, hapo kuupa Umoja wa Mataifa uwezo mwingi mno wa kuingilia kati mambo ya ndani ya nchi husika unaweza kuzalisha matatizo mengi zaidi kuliko unayoweza kuyatatua. Ni dhahiri suala hili linahitaji utulivu wa hali ya juu na utafiti.

Kilichotokea ni kwamba Urusi pamoja na nchi wafuasi (nchi za Mashariki) zimelazimika kukiri kushindwa kwa ujamaa wa kisayansi katika kuleta maisha bora kwa

Urusi na nchi zilizokuwa katika kambi yake. Hili limeleta taharuki kubwa na mkanganyiko.

Ukungu bado umetanda, hivyo hatuwezi kuona mambo yatakayokuja baadaye. Je itakuwa kushindwa kabisa kwa ujamaa wa kisayansi ukifuatiwa na mbio za kihayawani kuelekea kwenye ubepari kamili au tutakuwa na jaribio jipya la uchumi mchanganyiko? Au kutakuwepo na anguko la utawala wa Kiimla, au serikali ya Kiimla itavunjwa vipande vipande na kupelekea hali ya ghasia kubwa na hivyo kutokuwepo kwa serikali? Au patakuwa na kipindi cha mpito ambapo serikali ya Kiimla ambayo itataka yaishe kwa kukubaliana kuhusu haki za serikali na za mtu ili kadiri wakati utakavyokwenda haki za raia zinasimamishwa tena na haki za binadamu zinahuishwa tena.

Ni muhimu kusubiri matokeo ya mapambano baina ya mawazo ya bwana Gorbachev ya *perestroika* na *glasnost* kwa upande mmoja na wale wahafidhina wa chama cha Kikomonisti. Sawa na ninavyojua wanaofaidi uhondo wa matunda ya Urusi ni matabaka matatu – viongozi wa chama, watumishi wa serikali na wanajeshi. Swali la msingi hapa ni kuwa matabaka haya yatakuwa na wajibu gani katika hali hii ya mapinduzi baridi yanayoendelea kwa hivi sasa?

Swali hili na mengine yanatakiwa yajibiwe kama mtu anataka kuelewa mageuzi haya yatakuwa na athari gani kwa amani ya dunia.

Kupunguza tu mgogoro baina ya wababe wa dunia hakuleti amani wala tija. Kinyume chake kunazuka hofu kubwa hususan katika nchi za Ulimwengu wa Tatu. Wababe hao walikuwa hawaaminiani na ukajengeka wivu ambao uliyapatia kinga mataifa yaliyo dhaifu. Pia ulijengeka uwezo wa nchi masikini kuwa upande huu au upande ule, kuunga mkono Magharibi au Mashariki ambapo hali hii iliwasaidia kidogo kubadili mwenendo wa kisiasa na kuwa na nguvu za mazungumzo na kukubaliana. Lakini hali siyo hiyo kwa hivi sasa. Kuna matumaini gani kwa nchi masikini kuendelea kupumua katika hali ya heshima na uhuru?

Fikra zetu kwenye hatua hii tuliyoifikia zinaenda kwa Umoja wa Mataifa – ngome ya amani na taa pekee ya matumaini ya kuleta mfumo mpya duniani. Angalau mtu anaomba iwe hivyo. Hata hivyo, uchunguzi wa kina ukifanywa, inajitokeza taswira ya kukatisha tamaa, kukandamiza na ya kutisha.

Katika mabadiliko yaliyojitokeza, je Umoja wa Mataifa hautatawaliwa na mbabe mmoja? Hii itafanya nchi masikini na zisizojiweza kuwindwa kama wanavyowindwa wanyama.

Umoja wa Mataifa wa hivi sasa umedhihirisha mara kwa mara kuwa ni chombo sio cha kupigania haki bali kipo kwa maslahi ya kisiasa kwa taifa lolote lililo na nguvu kubwa ya ushawishi. Dhana ya haki na batili haijawahi kuwekewa maanani na Umoja wa mataifa wakati wa

kufanya maamuzi kwa mfumo tulionao wala tusitegemee makubwa wakati ujao. Siasa na diplomasia vimejikita mno katika siasa za kisasa kiasi hiki ya kwamba hakuna nafasi ya uadilifu kuota mizizi na kuishi. Ni ukweli ulio mchungu ambao mtu mwenye kuheshimu ukweli hatoupinga. Ukweli ni kwamba taasisi hii ni uwanja wa mbinu na njama za kidiplomasia, ushawishi wa kisirisiri na hayo yote yanafanywa chini ya mwavuli wa amani ya dunia.

Sawa na Kurani Tukufu dunia inahitaji taasisi ambayo imejiwekea malengo ya kuleta haki. Bila uadilifu sahau kabisa juu ya amani, Mtu anaweza kupigana kwa kisingizio cha kuleta amani, analeta vurugu na mfarakano kwa kisingizio cha amani, lakini kitu pekee anachoweza kupata anayejishughulisha na mambo hayo ni kifo sio amani.

Nasikitika, ni wachache miongoni mwa wanasiasa mahiri duniani wanaoelewa tofauti kati ya kifo na amani.

Vifo vinatokana na kutokuwepo usawa, utawala wa mabavu, na mateso yanayoendeshwa na wenye nguvu. Amani ni mtoto wa uadilifu.

Kurani Tukufu mara nyingi inazungumzia amani sambamba na uadilifu. Amani inaelezwa kuwa sharti la haki (uadilifu).

Katika hali ambayo kuna uhasama kati ya Waislamu wawili au mataifa mawili ya Kiislam, Kurani Tukufu ina ushauri huu:

وَإِنْ طَآئِفَتَانِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ اقْتَتَلُوا فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا ۚ فَإِنْ بَغَتْ إِحْدٰىهُمَا عَلَى الْأُخْرٰى فَقَاتِلُوا الَّتِي
تَبْغِي حَتّٰى تَفِيْٓءَ إِلٰٓى أَمْرِ اللّٰهِ ۚ فَإِنْ فَآءَتْ فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا بِالْعَدْلِ وَأَقْسِطُوا ۖ إِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ
الْمُقْسِطِينَ ﴿١٠﴾ إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ فَأَصْلِحُوا بَيْنَ أَخَوَيْكُمْ وَاتَّقُوا اللّٰهَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿١١﴾

*Na ikiwa makundi mawili katika waaminio wanapigana, basi fanyeni suluhu kati yao; na ikiwa moja la hayo limeruka mipaka dhidi ya lingine, basi piganeni na lile lililoruka mpaka hadi lirudie kwenye uamuzi wa Allah. Na kama likirudi, basi yapatanisheni baina yao kwa uadilifu, na hukumuni kwa haki. Hakika Allah Huwapenda watendao haki. Kwa hakika waaminio ni ndugu, basi fanyeni suluhu baina ya ndugu zenu, na mcheni Allah ili mrehemewe.*[18]

Katika aya hiyo hapo juu, wasio Waislam hawakutajwa kwa sababu iliyo wazi kabisa kwamba hawatarajiwi kufuata mafundisho ya Kurani Tukufu. Hata hivyo aya hiyo ni mfano maridhawa kwa dunia yote kufuata.

Wakati macho ya dunia yanaelekea kwenye Umoja wa Mataifa na Baraza la Usalama kwa matumaini kuwa vyombo hivi viwili vitajishughulisha zaidi katika kutatua migogoro ya kimataifa na hivyo kuifanya dunia mahali salama, hakuna chochote katika historia cha kutuonyesha kuwa kuna matumaini. Ulimwengu ulio ni uwanja wa kushawishi, njama, bidii katika shughughuli

ya kidiplomasia kwa lengo la kuunda makundi shawishi na kujaribu kumshinda mpinzani wako kwa njia yoyote iwayo, mahali ambapo hapana nafasi ya haya wala dhamiri ya binadamu haiwezi kupaingilia, ndio waweza kuitwa Nyumba ya Mataifa japo katika mgongano na mchafukoge. Lakini itakuwa dhihaka kuiita nyumba kama hiyo kuwa Nyumba ya Umoja wa Mataifa. Kama hiyo ndiyo dhana ya umoja basi ningelichagua kuishi katika mataifa ambayo hayana umoja ila yameunganika katika ukweli na haki.

Mapenzi ya kuwa na nguvu za kuteketeza wapinzani na kuwanyamazisha wapinzani, hiyo ni mada ambayo kila taifa linatakiwa liijadili na kuitanzua. Mtu anashangaa pamoja na kushikwa na masikitiko makubwa kwamba mpaka lini nchi wanachama wa Umoja huu adhimu wataendelea kufumba macho yao na akili zao kuhusu hatari inayojitokeza kutokana na namna mambo ya mataifa yanavyoendeshwa kwenye Umoja wa Mataifa?

Amani ya dunia imetundikwa kwenye uzi mwembamba yakiwemo matumaini kwamba haki itatendeka na haki itaonekana kutendeka.

## Marejeo

[1] Sura 2: Al-Baqarah: 248
[2] Sura 5: Al-Ma'idah: 21
[3] Sura 27: Al-Naml: 35
[4] Sura 4: Al-Nisa': 60
[5] Shakespeare
[6] Sura 42: Al-Shura: 37–40
[7] Sura 4: Al-Nisa': 59
[8] Sura 23: Al-Mu'minun: 117
[9] Sura 42: Al-Shura: 39
[10] Sura 3: Al-'Imran: 160
[11] Matthew 22: 21
[12] Sura 4: Al-Nisa': 66
[13] Sura 4: Al-Nisa': 136
[14] Sura 4: Al-Nisa': 60
[15] Sura 8: Al-Anfal: 59
[16] Sura 27: Al-Naml: 63
[17] Sura 5: Al-Ma'idah: 9
[18] Sura 49: Al-Hujurat: 10–11

Wale walioamini na ikatulia mioyo yao kwa kumkumbuka Allah. Sikilizeni! Kwa kumkumbuka Allah mioyo hutulia.

- Kurani Tukufu, 13:29

# SURA YA SITA

# AMANI YA NAFSI

## Mtu kuwa na Amani na Nafsi yake Mwenyewe

Mwishowe, ingawa sio kwa umuhimu, hebu nisisitize kuwa ubora wa sifa na tabia ya mtu mmoja mmoja huchukua dhima kubwa sana katika kuunda jamii ama yenye amani au isiyo na utulivu.

Mpaka sasa tumezungumzia juu ya muonekano na muundo wa majengo ya kidini, ya kijamii, ya kiuchumi na ya kisiasa ambayo Islam inanuia kuyajenga. Kuhusiana na sifa ya matofali yanayohitajika kama vifaa vya kujengea, Islam inasisitiza khulka na mienendo bora ya kila mtu.

Hii ni mada pana iliyoelezwa kwa mapana na marefu ndani ya Kurani Tukufu. Kwa mtazamo wangu, zifuatazo ni tabia muhimu Islam inajitahidi kutilia mkazo kwa kila mwanajamii.

## Kushindana katika Matendo Mema

Kwa mujibu wa Islam, matamanio na malengo yote mawili huongezwa au kuwekewa mipaka kwa kuzingatia maelekezo ya Allah ili ulingano mzuri upatikane. Ni muhali kupata amani ya kijamii pasipo kuwa na ulingano wa namna hii. Islam husisitiza matamanio na malengo yasiyotegemea sana uwezo wa kifedha wa kila mtu au yanayopatikana kwake kirahisi

katika ngazi zote bila gharama au kwa gharama ndogo tu.

Bila shaka kuwa na ari ya kutokeza juu ya watu wengine na kupata sifa ya kipekee ni jambo la kawaida. Lakini matamanio haya ya kawaida ya kupata mafanikio na kuwashinda wengine ni hatari mno yasipodhibitiwa au kuwekewa mipaka. Kwa mfano tabia ya wivu na kwenda kinyume na sheria huvunja moyo wa kushindana kwa uhuru kiasi kwamba jamii nzima huanza kuathirika vibaya badala ya kunufaika na moyo wa ushindani.

Tabia ya kutumia madawa ya kulevya katika michezo ni mfano mdogo tu, lakini ushindani katika tasnia na biashara ya kitaifa na ya kimataifa hutuletea mifano ya kusikitisha sana ya kutokuwepo kwa uwanja sawa.

Namna ya kwenda kinyume na sheria hutofautiana katika nchi za Ulimwengu wa Tatu na nchi zilizostawi zaidi. Rushwa, ughushi, kuvunja ahadi, udanganyifu na ulaghai ni baadhi ya njia zinazotumika waziwazi ili kupata faida ya kiuchumi kwa upesi katika nchi za Ulimwengu wa Tatu. Ndiyo maana mafundisho ya kidini na ya kimaadili yanatakiwa kutumika katika nyanja zote za maisha ya binadamu. Kukosekana kwa mafundisho kama haya kunasababisha matokeo mabaya.

Islam hutuletea maelekezo ya kina yanayohusu uwanja mzima wa namna ya kutendeana katika ushindani. La kusikitisha sana ni kwamba katika nchi za Kiislam

ambapo twasikia mengi kuhusu uenezaji wa Islam na itikadi zake zenye misingi ya kale, lakini hatukutani katu na juhudi za maana ili kufuata taratibu za Kiislam katika tasnia, biashara na mahusiano ya kiuchumi. Bila shaka ni sikitiko la hali ya juu.

Aya ifuatayo ya Kurani Tukufu hutoa kiini cha mafunzo ya Islam katika uwanja huu:

وَلِكُلٍّ وِّجْهَةٌ هُوَ مُوَلِّيهَا فَاسْتَبِقُوا الْخَيْرٰتِ ۗ اَيْنَ مَا تَكُوْنُوْا يَاْتِ بِكُمُ اللّٰهُ جَمِيْعًا ۗ اِنَّ اللّٰهَ عَلٰى كُلِّ شَىْءٍ قَدِيْرٌ ﴿١٤٨﴾

*Na kila mtu anayo shabaha ya mwisho kuielekea inayomwongoza. Sisi Tumewawekea sawa shabaha hii; basi shindaneni katika mema; popote mtakapokuwa Allah Atawaleteni nyote pamoja; kwa yakini Allah ni mweza wa kila kitu Apendacho.*[1]

Katika kauli hii fupi, hekima kubwa imekusanywa na kuwekwa pamoja kwa namna ya kustaajabisha. Huu ni mwongozo kuhusu ushindani wa kila aina katika nyanja zote. Lazima wema uwe na hadhi kubwa kabisa nao uwe shabaha ya mwisho na dhamira halisi ya kila ushindani. Hivyo, tabia ya kukiuka sheria na uchoyo wa aina yoyote huondolewa mbali mara moja.

Muda ungaliruhusu, tungalizama zaidi na kutoa mifano ya kutosha katika mafundisho ya Islam ya kwamba namna ushindani unaweza kuwa bora, safi na wenye kuleta maendeleo. Ni mara chache sana watu wanatambua kuwa utulivu halisi wa moyo kwa kweli

unatokana na mtu kuwa mwema na hautokani na matendo yenye mafanikio ya ajabu yaliyopatikana kwa njia ya udanganyifu au hadaa. Watu kama hawa huwa hawapati amani katika jamii wala ndani ya nafsi yao. Kwa tazamo la haraka wanaonekana kwamba wamefaulu vizuri na kwa hiyo wametulia sana lakini kwa hakika ufaulu huu hauna thamani mbele ya ushindi halisi.

Rafiki mmoja wa karibu wa marehemu tajiri mkubwa wa Pakistani aliwahi kunihadithia kisa cha kushtusha na kuhuzunisha sana. Safari moja alimsifu rafiki yake kwa mafanikio makubwa aliyokuwa nayo. Badala ya kufurahi, jawabu la tajiri huyo lilinishangaza mno. Akafungua vishikizo vya shati lake na akapeleka kiganja chake kifuani kana kwamba alitaka kurarua kifua chake kama mnyama anavyopiga makucha. Akanena: 'Mateso yaliyoje katika mafanikio haya. Mtu angepasua kifua changu na kuona yaliyomo ndani, asingekuta chochote isipokuwa moto unaobimbirika.' Baadhi ya watu wanakiri ukweli huu mgumu, wengine hawakiri lakini hakuna awezaye kwenda kinyume na utu. Mtu anaweza kabisa kurundika mali lukuki na kuwa na starehe na anasa za aina zote katika maisha, lakini ni ukweli usiopingika kwamba kama wapo ni matajiri wachache tu ambao kwa hakika ni wenye furaha na ukinaifu. Hali yao imeelezwa katika Kurani Tukufu kama hivi ifuatavyo:

وَيْلٌ لِّكُلِّ هُمَزَةٍ لُّمَزَةٍ ۙ﴿١﴾ الَّذِىْ جَمَعَ مَالًا وَّ عَدَّدَهٗ ۙ﴿٢﴾ يَحْسَبُ اَنَّ مَالَهٗۤ اَخْلَدَهٗ ۚ﴿٣﴾ كَلَّا
لَيُنْۢبَذَنَّ فِى الْحُطَمَةِ ۖ﴿٤﴾ وَ مَاۤ اَدْرٰىكَ مَا الْحُطَمَةُ ؕ﴿٥﴾ نَارُ اللّٰهِ الْمُوْقَدَةُ ۙ﴿٦﴾ الَّتِىْ تَطَّلِعُ عَلَى
الْاَفْـِٕدَةِ ؕ﴿٧﴾ اِنَّهَا عَلَيْهِمْ مُّؤْصَدَةٌ ۙ﴿٨﴾ فِىْ عَمَدٍ مُّمَدَّدَةٍ ﴿٩﴾

*Maangamizo kwa kila msingiziaji, aliyeikusanya mali na kuendelea kuihesabu. Anadhani ya kuwa mali yake itamdumisha. Hasha! Bila shaka atavurumishwa katika Hutama. Na nini kitakujulisha Hutama ni nini? Ni Moto wa Allah uliowashwa Ambao utairukia mioyo. Hakika huo utafunikwa dhidi yao, katika nguzo ndefundefu.*[2]

Kwa hakika, ridhaa ya kweli itaendelea kumpiga chenga mtu mpaka atimize ari iliyotopea katika maumbile yake ya kutenda mema, kuwa mwema na kuishi vyema.

## Upendo kwa Jamaa na Ndugu

Msisitizo juu ya upendo kati ya jamaa na ndugu ili kujenga mfumo wa kifamilia ulio na mshikamano ni jambo ambalo limekwishazungumziwa katika amani ya kijamii. Hapa linatajwa ili kuonesha haja ya kuboresha kiwango cha ubora wa kila mtu ambaye ana dhima katika jamii kama ile ya tofali. Ubora wa jengo hauwezi kuongezeka bila kuongeza ubora wa tofali.

## Kuwatumikia Wengine

Katika Islam jambo ambalo hutiliwa mkazo ni kupata furaha katika kuwatumikia wengine kuliko kinyume

chake. Sehemu ifuatayo ya aya ya Kurani Tukufu inafikisha ujumbe huu:

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُوْنَ بِالْمَعْرُوْفِ وَ تَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَ تُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ ؕ

*Nyinyi ni umati bora kwa sababu ya kuwatumikia binadamu na mliotolewa kwa ajili ya manufaa ya watu wote, mnaamuru yaliyo mema na mnakataza maovu, na mnamwamini Allah.*[3]

Hii inaonesha kuwa Mwislamu hapewi umuhimu zaidi kuliko wengine bila mantiki fulani. Kuwa kwake Mwislamu hakumaanishi kwamba yeye ni bora kuliko wengine. Ni lazima apate cheo hiki kwa kuwa na faida kwa watu wengine ili ihsani itiririke kutoka kwake kuwaelekea wengine.

Akifafanua maana ya neno 'khair', ambalo linamaanisha bora zaidi na pia bora kabisa, safari moja Mtume Mtukufu[saw] alisema: Mkono wa juu ni bora kuliko mkono wa chini; mkono wa juu hutoa na kutumia, na mkono wa chini huomba na kupokea.[4]

Jambo hili limesisitizwa sana ndani ya Kurani Tukufu na Hadithi za Mtume Mtukufu[saw] kiasi kwamba baadhi ya masahaba wa Mtume Mtukufu[saw] walifikia viwango vya hali ya juu visivyo na mifano katika sifa hii ya kipekee ya binadamu.

Sio tu kwamba walijitahidi kuwatumikia watu wengine bali walisita kupokea au kuomba fadhili kutoka kwao.

Hadhrat Auf ibn Malik Ashja'i anasimulia kwamba safari moja tulikuwa pamoja na Mtume Mtukufu[saw] katika idadi ya watu saba, wanane au tisa alipouliza: Je, hamfungi ahadi pamoja na Mjumbe wa Allah? Kabla ya muda mfupi tulikuwa tumekwishafanya bai'ati kwa hiyo tukajibu: Ewe Mjumbe wa Allah, tayari tumekwishafunga ahadi pamoja nawe. Mtume Mtukufu[saw] akarudia swali lake nasi tukamjibu vilevile na tukaongeza: Ni ahadi gani tunatakiwa kufunga sasa? Akasema, kwamba mtamwabudu Allah na hamtamshirikisha na chochote, kwamba mtasimamisha sala tano za faradhi, na kwamba mtamtii Allah na hamtamwomba mtu yeyote kitu chochote. Kutokea hapo niliona hata kiboko cha kumpigia farasi kilipomwanguka mikononi mwa mtu yeyote kati yao, hakumwomba mtu mwingine amsaidie kukirudisha.[5]

Msisitizo juu ya kuwatumikia wengine si jambo la kawaida lisilovutia bali ni juhudi ili kurekebisha mienendo ya watu na kutilia mkazo kwa binadamu khulka nzuri na maadili ya hali ya juu zaidi. Ikiwa khulka bora zinaendelezwa, watu watalelewa wakiwa wanaona heshima katika kuwatumikia wengine badala ya kupokea tu fadhila na hisani kutoka kwao. Kuwatumikia mahuluku wa Mungu ni nusu ya imani. Mtazamo wa Islam kuhusu kazi njema ni kwamba hii yenyewe ni neema. Jambo hili haliwezi kujadiliwa bali linaweza kushuhudiwa tu.

## Kutafuta Radhi ya Mungu

Katika kukuza maadili mema katika khulka ya binadamu, Islam haiishii hapo tu. Islam huwajengea wafuasi wake uelewa kwamba jambo la msingi na linalotakiwa kupewa umuhimu wa pekee ni kwamba mema ya kila mtu yakubaliwe na Mungu. Msisitizo huu huondoa haja ya kuonesha matendo yake mema ili asifiwe na watu wanaoangalia. Yamtosha kabisa mwaminio halisi kwamba matendo yake yote, ama mema au mabaya, yawe yajulikane kwa Mungu Aonaye sana. Kwa kuzungumzia juu ya hili, Qu'rani Tukufu ina yafuatayo ya kusema:

يَوْمَئِذٍ تُحَدِّثُ أَخْبَارَهَا ﴿٥﴾ بِأَنَّ رَبَّكَ أَوْحَىٰ لَهَا ﴿٦﴾ يَوْمَئِذٍ يَصْدُرُ النَّاسُ أَشْتَاتًا لِّيُرَوْا
أَعْمَالَهُمْ ﴿٧﴾ فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ﴿٨﴾ وَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿٩﴾

*Siku hiyo ardhi itahadithia habari zake, Itakuwa hivyo kwa sababu Mola wako Atakuwa Ameifunulia hivyo. Siku hiyo watu watatoka vikundi vikundi ili waonyeshwe vitendo vyao. Basi anayefanya wema sawa na chembe, ataona umeonekana na Mungu. Na anayefanya uovu sawa na chembe, ataona umeonekana na Mungu.*[6]

Jambo hili litiliwe maanani kwamba hii ni hatua muhimu katika safari ya kuelekea uboreshaji wa kijamii. Hii ndiyo dawa pekee ya kiburi cha binadamu na tamaa yake ya kujionesha na kujivuna.

Mtume Mtukufu[saw] alijumuisha matendo yafuatayo katika maana pana ya sadaka ambayo pia yanastahili malipo kwa Allah:

> Mchango hutakiwa kutolewa na kila kiungo cha mwili wa mtu kila siku jua linachomoza ndani yake. Kuwapatanisha watu wawili ni sadaka. Kumsaidia mtu apande kipando chake au kumwekea mzigo juu yake ni sadaka. Ni sadaka kuondoa njiani chochote kinachowasababishia wapitanjia adha.[7]
>
> Ikiwa Mwislamu anapanda mti, chochote kinacholiwa katika matunda yake ni sadaka kutoka kwake, chochote kinachoibiwa kutoka kwenye mti huo ni sadaka, na chochote kilichochukuliwa kutoka kwenye mti huo ni sadaka.[8]
>
> Jiepusheni na Moto hata kama ni kwa kutoa nusu tende katika sadaka, na kama hii pia isipopatikana, ni kwa kusema jambo jema.[9]
>
> Kama mtu asipokuwa na chochote, inambidi afanye kazi kwa mikono yake kwa ajili ya faida yake mwenyewe na pia atoe sadaka. Na kama hawezi kufanya kazi, inambidi amsaidie maskini asiyejiweza kabisa. Na kama hawezi kufanya hivyo awahimize wengine kufanya wema. Na hata kama hawezi, ajizuie na kutenda maovu. Hii pia ni sadaka.[10]

Hata tonge la chakula unalomlisha mkeo linavuta mapenzi ya Mungu.

## Kuwajali Daima Binadamu Wengine

Islam inasisitiza kutambua na kuhisi shida na mateso ya watu wengine. Tumekwishazungumzia juu ya jambo hili katika sura ya amani ya kijamii na kiuchumi na sura ya amani ya kisiasa. Maelezo mengine hayahitajiki hapa.

## Mawanda Mapana ya Upendo

Islam hupanua wigo wa uwezo wa kila mtu kiasi kwamba asiwapende wanadamu wenzake tu bali awapende viumbe wote wa Mungu. Kama Islam inavyodai kuwa dini ya mwisho kuteremshwa kwa binadamu wote na si kwa kaumu moja tu, hivyo katika hali ya kawaida hutarajiwa kwamba Nabii[saw] wa Islam aelezwe kuwa chanzo cha nuru na baraka kwa binadamu wote. Bali badala yake mtu hushangazwa kusoma kwamba Mtume Mtukufu[saw] ameelezwa katika Kurani Tukufu kama:

رَحۡمَةً لِّلۡعٰلَمِيۡنَ

*Rehema kwa ulimwengu wote.*[11]

Kwa Kiarabu neno *'ālam* linamaanisha dunia au dunia nzima. Lakini neno lililotumika hapa ni al*'ālamīn*, wingi wa *'ālam* (dunia nzima). Ndiyo maana tumetafsiri hapa kama Ulimwengu wote. Mwenye tabia ya kushuku asingeridhika na ukweli wa cheo adhimu kama hiki. Lakini uchunguzi wa kina wa cheo cha utume kwa

walimwengu, ambacho bila shaka alijaaliwa Mtume Mtukufu[saw], hugundua hekima ya cheo cha *Rehema kwa Ulimwengu wote.*

## Dhamira ya Uumbaji wa Binadamu

Kwa mujibu wa dhana ya uumbaji iliyoelezwa na Kurani Tukufu, falsafa ya uumbaji wa Ulimwengu usiokuwa na uhai isingekuwa na maana yoyote isipokuwa kwa upande wa Muumbaji ingechukuliwa kama ni kazi bure, Mungu Apishe mbali. Hivyo nani angalipata kuelewa na kushirikiana katika maarifa na Muumba wa vyote? Hii ingalikuwa sawa na kutokuumba chochote. Shabaha ya uumbaji ilikuwa ni kujenga uelewa na hatimaye kuuboresha, kuupanua na kuongeza ubora wa uelewa huo ili ufikie dhamira ya uumbaji.

Hii sio dhamira ya kawaida nayo inahitaji mjadala mrefu ambao hauna nafasi katika hotuba ya leo. Kwa kuiweka wazi, sehemu husika ni hii kwamba dhamira ya msingi ya uumbaji ilikuwa ni kuumba kiumbe mwenye uelewa wa hali ya juu, ambaye kwa hiari yake alitakiwa ajisalimishe kwa uzuri kamili wa Mungu unaoakisiwa moja kwa moja katika viumbe vyake. Na sio hilo tu, bali awaongoze viumbe wengine wa hadhi ya juu (yaani wanadamu) kupata lengo hilo la msingi la uumbaji, au angalau arahisishe kwa wale wanaotaka kumfuata Mungu miongoni mwao.

Kwa kufikirika, hebu ondoa kwa muda dhamira ya msingi ya uumbaji, mara moja sababu kuu ya uumbaji

na uendelezaji wa ulimwengu itapotea kabisa. Kwa mfano rahisi, dhamira pekee ya kupanda miche ya miti ya matunda, kuitunza, kuimwagilia maji, kuipogoa na kuiendeleza ni kupata matunda. Kama matunda yasingepatikana basi na mti wowote usingekuwepo. Juhudi zote za upandaji na utunzaji wa mti wa matunda zingekuwa bure na hazina maana kama isingekuwepo dhana ya kupata matunda baadaye. Kwa hiyo, mti mzima pamoja na mizizi, shina, matawi, majani na machipukizi vyote vinasaidia kuwepo kwa matunda. Ingawa sehemu zote za mti zinatangulia kuwepo lakini huwajibika kwa lengo lake la msingi. Kwa minajili ya lengo taratibu za uumbaji zenyewe zinaendelea.

Kwa kuzingatia uhusiano uliopo katika dhamira ya msingi ya uumbaji na vitu vilivyopo ulimwenguni, mtu atazamapo mafundisho ya Kiislam anashangaa kugundua kwamba Islam haizungumzii uhusiano baina ya mwanadamu na Mungu tu bali na uhusiano wa mtu na jamii ya wanyama na pia vitu vyote vinavyomzunguka.

Kila kilichopo ni kitakatifu sio kwa sababu ya kuwa bora kuliko binadamu bali kutokana na kuumbwa kwake kwa namna moja ama nyingine, kwa ajili ya binadamu hasa. Hivyo hakuna kitu chochote ulimwenguni kisicho na maana na manufaa au hakipo kwenye ufungamano wa mlolongo wa uumbaji. Hata nyota zilizoko mbali sana zina maana na hushika nafasi katika mpango wa

uumbaji wa binadamu. Jambo hili limezungumzwa mara kwa mara ndani ya Kurani Tukufu kwa namna mbalimbali. Ifuatayo ni baadhi ya mifano:

وَ الشَّمۡسِ وَ ضُحٰىهَا ۪ۙ﴿٢﴾ وَ الۡقَمَرِ اِذَا تَلٰىهَا ۪ۙ﴿٣﴾ وَ النَّهَارِ اِذَا جَلّٰىهَا ۪ۙ﴿٤﴾ وَ الَّيۡلِ اِذَا يَغۡشٰىهَا ۪ۙ﴿٥﴾ وَ السَّمَآءِ وَ مَا بَنٰىهَا ۪ۙ﴿٦﴾ وَ الۡاَرۡضِ وَ مَا طَحٰىهَا ۪ۙ﴿٧﴾ وَ نَفۡسٍ وَّ مَا سَوّٰىهَا ۪ۙ﴿٨﴾ فَاَلۡهَمَهَا فُجُوۡرَهَا وَ تَقۡوٰىهَا ۪ۙ﴿٩﴾ قَدۡ اَفۡلَحَ مَنۡ زَكّٰىهَا ۪ۙ﴿١٠﴾ وَ قَدۡ خَابَ مَنۡ دَسّٰىهَا ﴿١١﴾

*Naapa kwa jua na kwa wakati linapoanza kutoa nuru, Na kwa mwezi unapoliandama, Na kwa mchana unapolidhihirisha, Na kwa usiku unapolifunika, Na kwa mbingu na kwa Yule Aliyeijenga. Na kwa ardhi na kwa Yule Aliyeitandaza, Na kwa nafsi na kwa Yule Aliyeistawisha, Kisha Akaifunulia maovu yake na wema wake; Bila shaka amefaulu aliyeitaksa; Na bila shaka amejihasiri aliyeipotosha.*[12]

وَ سَخَّرَ لَكُمۡ مَّا فِی السَّمٰوٰتِ وَ مَا فِی الۡاَرۡضِ جَمِيۡعًا مِّنۡهُ ؕ اِنَّ فِیۡ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّقَوۡمٍ يَّتَفَكَّرُوۡنَ ﴿١٣﴾

*Na Amewatiishieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini - vyote vimetoka Kwake; bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa watu wanaotafakari.*[13]

وَ سَخَّرَ لَكُمُ الَّيۡلَ وَ النَّهَارَ ۙ وَ الشَّمۡسَ وَ الۡقَمَرَ ؕ وَ النُّجُوۡمُ مُسَخَّرٰتٌۢ بِاَمۡرِهٖ ؕ اِنَّ فِیۡ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّقَوۡمٍ يَّعۡقِلُوۡنَ ﴿١٢﴾

*Na Amewatiishieni usiku na mchana, na jua na mwezi, na (pia) nyota zimetiishwa kwa amri Yake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wenye akili.*[14]

أَلَمْ تَرَوْا أَنَّ اللَّهَ سَخَّرَ لَكُم مَّا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَأَسْبَغَ عَلَيْكُمْ نِعَمَهُ ظَاهِرَةً وَ
بَاطِنَةً ۗ وَمِنَ النَّاسِ مَن يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَلَا هُدًى وَلَا كِتَابٍ مُّنِيرٍ ﴿٢١﴾

*Je! hamwoni ya kwamba Allah Aliwatiishieni vilivyomo mbinguni na ardhini, na Akawakamilishieni neema Zake zilizo dhahiri na za siri? Na wako watu wanaobishana katika (mambo ya) Allah pasipo elimu wala mwongozo wala Kitabu chenye nuru.*[15]

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ ﴿٥﴾

*Bila shaka Tumemwumba mtu kwa rasimu iliyo bora kabisa miongoni mwa rasimu za uumbaji.*[16]

Aya nyingine nyingi na hata baadhi ya sura fupi za Kurani Tukufu zimewekwa kueleza mada hii inayosema binadamu ni kama ulimwengu mdogo aliyepokea athari kutoka kwa namna zote za vitu vilivyoumbwa. Hata nyota iliyoko mbali sana pia imechangia katika huu ulimwengu mdogo wa binadamu.

Uhisiano huu haupo kama mtumishi anavyowajibika kwa bwana wake lakini kama uliopo kati ya bwana na mtumishi wake. Mabwana huwa hawainami wala kunyenyekea kwa wale wanaowatumikia. Hivyo, binadamu huchukuliwa kama bwana wa ulimwengu wote na mtumishi wa mmoja tu aliye ni Mola na Muumba wa ulimwengu.

Falsafa hii hutofautiana kwa kiasi kikubwa na ile ya dini zingine ambazo hazifundishi kuabudu masanamu tu bali

kuabudu na vitu vilivyoumbwa katika namna mbalimbali. Kwa mujibu wa falsafa yao mwezi, nyota, jua, bahari, miti, mvua, radi, hata wanyama kama vile ng'ombe, nyoka na ndege huonekana kama ni bora kuliko binadamu. Binadamu amefundishwa kuviabudu kama miungu kutokana na kuwa bora kuliko binadamu kwa kiasi fulani. Kwa kifupi, binadamu amewekwa katika daraja la chini kabisa huku akifanywa anyenyekee kwa kila kitu ambacho kiliumbwa kumtumikia yeye.

Kwa mujibu wa elimu itokanayo na Islam kuhusu mambo ya kawaida, tunaweza kusema binadamu ni bwana wa vitu vyote vilivyoumbwa. Hivyo, binadamu ana wajibu mkubwa zaidi kuliko vyote kwa Muumba kwa sababu ndiye yeye aliyefaidika na vyote vilivyoumbwa na Mungu; na pia Yeye alimtiishia binadamu kila kitu.

Kwa maneno mengine, binadamu amekombolewa na kila aina ya utumwa kwa kukubali utumwa wa aina moja tu — ambao ni wa Muumba wake tu. Binadamu ndiye mfano halisi wa dhamiri na hisia za ulimwengu mzima. Kila akiinama na kunyenyekea mbele ya Muumba wake, ulimwengu mzima huinama na kunyenyekea ndani mwake. Na kila akimwelekea Muumba wake, tunaweza kusema ulimwengu mzima huelekea kwake.

Kwa mujibu wa Islam, kufahamu fika lengo hili na kurekebisha maisha yako ili kulifikia ndiyo amani kamili.

Aya ya Kurani Tukufu inayonukuliwa mara kwa mara na Waislamu imebeba falsafa hii kwa maneno machache:

قَالُوْٓا اِنَّا لِلّٰهِ وَ اِنَّآ اِلَيْهِ رٰجِعُوْنَ ۝١٥٦

*Hakika sisi ni wa Allah, na bila shaka Kwake tutarejea.*[17]

Ni watu wachache wanaoelewa hapa maana ya kuelekea ni kiroho si kidhahiri. Hii sio kauli ya kawaida tu bali ni ukumbusho juu ya shabaha ya uumbaji wa binadamu. Kama vile samaki huwa hatulii mpaka arudi katika chimbuko lake yaani anapotaga mayai. Vivyo hivyo moyo wa binadamu hautulii mpaka kwa kiroho arejee kwa chanzo cha uumbaji wake. Hii ndiyo maana ya aya ifuatayo:

اَلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَتَطْمَىِٕنُّ قُلُوْبُهُمْ بِذِكْرِ اللّٰهِ ۭ اَلَا بِذِكْرِ اللّٰهِ تَطْمَىِٕنُّ الْقُلُوْبُ ۝٢٨

*Wale walioamini na ikatulia mioyo yao kwa kumkumbuka Allah. Sikilizeni! Kwa kumkumbuka Allah mioyo hutulia.*[18]

## Hakuna Amani bila Mungu

Binadamu hawezi kuwa na amani nafsini mwake wala amani haiwezi kupatikana katika jamii bila njia hii. Hakuna njia nyingine inayoweza kufaa. Ni mapenzi ya Mungu ndiyo jambo la pekee linaloweza kusababisha kutoa heshima kwa Alivyoviumba. Sawa na kiwango

cha ubora wake, kiumbe kinamsogelea Muumba wake na pia muungano baina ya Muumba na viumbe unazidi.

Binadamu huwaheshimu watu wenzake akiwa na lengo la hali ya juu zaidi yaani anawatolea heshima wanadamu wote kutokana na heshima na taadhima Anayostahiki Muumba wake. Ndiyo maana tunaweza kusema kwa hakika ni upendo kwa Mungu uliogeuzwa kuwa upendo kwa viumbe Vyake. Kwa fikra, tukiondoa tu dhana ya Mungu kwa muda, mahusiano ya kibinadamu mara yatageuka kuwa katika hali tofauti kabisa.

Ombwe lililotokana na kutokuwapo kwa Mungu linazibwa haraka na nafsi yenye tamaa ya binadamu. Hii ni falsafa ya kijinga kwamba binadamu huweza kuishi bila Mungu. Kinachofanikishwa na Upagani sio tu kuuawa kwa Mungu mmoja bali kuhuishwa kwa miungu wengi. Kila kiumbe chenye kujitambua kilicho hai ghafla kinachukua nafasi ya kuwa mungu. Ubinafsi, tamaa na kujishughulisha kabisa katika kutimiza matakwa ya nafsi vinaongezeka katika nguvu.

Jamii zinazoundwa na watu wa aina hii, daima zinabaki kuwa na mtazamo binafsi na mwelekeo wa ubinafsi.

Hakuna hekima iliyobaki katika mtu kuwa wa manufaa kwa wengine bila kuwa na tamaa binafsi ya siri. Hakuna pahala pa nje pa marejeo palipobaki katika sura ya Mungu wa Rehema, ambaye pekee ndio kiunganishi na mahala pa makutano kwa aina zote za viumbe.

Huu ndiyo msingi hasa wa falsafa ya Islam. Mtu hawezi kupata utulivu bila kurejea kwa Mungu. Na bila ya utulivu huo, amani katika jamii haiwezi kujengwa. Jitahada zote za kibinadamu kuleta amani kwa njia ya malengo binafsi yaliyofichika, ni lazima zitashindwa kabisa. Kama hakuna Mungu, hakuna amani. Hii ndiyo hekima yenyewe.

Ahsanteni.

## Marejeo

[1] Sura 2: Al-Baqarah: 149
[2] Sura 104: Al-Humazah: 2–10
[3] Sura 3: Al-'Imran: 111
[4] Bukhari, Kitabuz Zakat, Babu La Sadaqatin illa 'an Zahri Ghinan
[5] Muslim, Kitabuz Zakat, Babu Karahatil Mas'alati lin Nasi
[6] Sura 99: Al-Zilzal: 5–9
[7] Bukhari, Kitabul Jihadi was Siyari, Babu man Akhadha birrikabi wa Nahwihi
[8] Muslim, Kitabul Musaqati wal Muzara'ati, Babu Fadlil Gharsi waz Zar'i
[9] Bukhari, Kitabul Manaqib, Babu 'Alamatin Nubuwwati fil Islami
[10] Bukhari, Kitabul 'Adab, Babun Kullu Ma'rufin Sadaqatun Muslim, Kitabuz Zakat, Babu Bayanismas Sadaqati Yaqa'u 'Ala Kulli Nau'imminal Ma'rufi
[11] Sura 21: Al-Anbiya': 108
[12] Sura 91: Al-Shams: 2–11
[13] Sura 45: Al-Jathiyah: 14
[14] Sura 16: Al-Nahl: 13
[15] Sura 31: Luqman: 21
[16] Sura 95: Al-Tin: 5
[17] Sura 2: Al-Baqarah: 157
[18] Sura 13: Al-R'ad: 29